

TWAWEZA KUMWAMINI MUNGU

Siku moja Jimi alimwuliza mtu mmoja anayekana kuwa kuna Mungu endapo alipata kujaribu sana, hata kwa dakika chache tu, kupigana na wazo lisemalo kwamba huenda Mungu yuko.

"Sawa kabisa!" mkana Mungu yule akajibu, akimwacha Jimi na mshangao. "Miaka mingi iliyopita, mimi nilikuwa karibu sana nigeuke na kuwa mtu anayemwamini Mungu. Nilipokiangalia kile kiumbe kidogo sana - lakini - kikamilifu katika kitanda chake kidogo, nilipochungulia na kuviona vidole vile vidogo fahamu za kwanza za kutambua, nilipita katika kipindi cha miezi kadhaa ambayo katika hiyo mimi nilikuwa karibu kabisa niache kuwa mkana Mungu. Kule kumwangalia mtoto yule kulikuwa kumenishawishi karibu kabisa kuwa hapana budi Mungu alikuwa yuko."



1. Kila Kitu Kilichobuniwa Kina Mbunifu Wake

Muundo wa mwili wa kibinadamu unafanya iwepo haja ya kuwako mbunifu wake. Wanasyanshi wanatuambia kwamba ubongo wetu hukusanya na kukumbuka picha elfu nyngi katika mawazo yetu, huyaunganisha matatizo yetu yote na kuyatatua, hufurahia kuona uzuri, huitambua nafasi ya mtu, na kutaka kukuza yaliyo bora ndani ya kila mtu. Chaji za umeme zitokazo katika ubongo huongoza shughuli zote za misuli ya miili yetu.

Kompyuta pia zinafanya kazi kwa njia ya mikondo ya umeme. Lakini ilichukua akili ya mwanadamu katika kuitengeneza hiyo kompyuta na kuiambia la kufanya.

Si ajabu, basi, kwamba mtunzi wa Zaburi alihitimisha kwa kusema kwamba mwili wa mwanadamu unasimulia habari za Muumbaji huyo wa ajabu kwa sauti kubwa iliyo wazi:

"Nakusifu maana nimefanywa kwa namna ya ajabu, matendo yako ni ya ajabu, wewe waniju kabisa kabisa" - (Zaburi 139:14)



Hatuna haja ya kwenda mbali ili kuyaona hayo "matendo" ya Mungu. Umbo la ubongo wetu wenye sehemu nyngi za ajabu na viungo vyetu vingine ni "matendo" ya Mungu, nayo husonda kidole chake kwa yule mbunifu stadi kabisa.

Hakuna pampu yoyote iliyotengenezwa na mwanadamu inayoweza kulinganishwa na moyo wa mwanadamu. Hakuna mtandao wo wote wa kompyuta uwezao kuwa sawa na mfumo wetu wa mishipa ya fahamu. Hakuna mfumo wo wote wa Televisheeni unaofanya kazi yake vizuri kama sauti, sikio, na jicho la mwanadamu. Hakuna kiyoyozi kikuu cho chote (central air conditioning) wala mfumo wa kuipasha joto nyumba uwezao kushindana na kazi inayofanywa na pua, mapafu, na ngozi yetu. Mfumo wenye sehemu nyngi za ajabu wa mwili wa mwanadamu unadokeza kwamba mtu fulani alihuksika katika kuubuni, na Mtu huyo fulani ni Mungu.

Mwili wa mwanadamu ni mfumo kamili wa viungo mbali mbali - vyote vikiwa vinashirikiana, vyote vikiwa vimeumbwa kikamifu. Mapafu na moyo, mishipa ya fahamu na misuli, hiyo yote hufanya kazi za ajabu mno kiasi cha kuwa vigumu kusadikika ambazo hutegemezwa juu ya kazi nyininge zilizo za ajabu mno kiasi cha kutufanya sisi tushindwe kusadiki.

Endapo ungetakiwa kuzipa nambari sarafu kumi kuanzia moja mpaka kumi, na kuziweka mfukoni mwako, na kuzitikisa-tikisa huku na huku, kisha kuzitoa mfukoni mwako na kuziweka tena mfukoni moja moja, je, kuna uwezekano gani kwamba ungefanya hivyo kwa kufuata mfuatano wa nambari zake sawa sawa? Kwa sheria ya mahesabu unayo bahati moja tu katika bilioni kumi ya kuzitoa kwa mpangilio wake kuanzia ya kwanza mpaka ile ya kumi.

Sasa, basi, hebu fikiria ni bahati ngapi tumbo la chakula, ubongo, moyo, ini, arteri, vena, figo, masikio, macho, na meno vingekuwa nazo vikikua vyote pamoja na kuanza kufanya kazi yao kwa dakika ile ile ya wakati mmoja.

Hivi maelezo ya busara kabisa ni yapi kuhusu ubunifu huo wa mwili wa mwanadamu?

"Kisha Mungu akasema, 'Natumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu,'Hivyo Mungu Akamwuumba Mtu Kwa Mfano Wake,..... mwanamume na mwanamke aliwaumba" - (Mwanzo 1:26,27).

Mwanaume na mwanamke wa kwanza wasingeweza kuwa wametokea wenyewe tu. Biblia inathibisha kwamba Mungu alitubuni sisi kwa mfano wake. Alituwaza katika mawazo yake na kutuumba.

2. Kila Kitu Kilichoumbwa Kina Muumbaji Wake

Lakini ushahidi wa kuwako kwake Mungu haufungamani tu na ubunifu wa miili yetu; pia umetandaa huko mbinguni. Acha taa za mjini, angalia juu katika mbingu ya usiku. Wingu lile jeupe kama maziwa lenye nyota, tunaloliita Mkanda wa Nuru (Milky Way) ambalo kwa kweli ni kundi la mabilioni ya majua (galaxy) yanayotoa mwanga mkali wa moto sawa na ule wa jua letu ambaa unaweza kuonekana hapa duniani kwa kupitia katika darubini kubwa zilizopo hapa duniani kama ile darubini iitwayo "Hubble Telescope" iliyo katika anga za juu.

Si ajabu, basi, kwamba mtunga Zaburi alihitimisha kwa kusema kwamba nyota zinamtangaza Muumbaji Mtukufu:

"Mbingu zatangaza utukufu wa Mungu, anga ladhihirisha kazi ya mikono yake" (Zaburi 19:1-3).


Je, hivi sisi twaweza kutoa hitimisho gani la busara kwa kuangalia mpangilio huo unaotatanisha sana na ukubwa wa malimwengu yote?

"Hapo mwanzo Mungu alizumba mbingu na nchi" (Mwanzo 1:1).

"Yeye [Mungu] alikuwako kabla ya vitu vyote; vyote hudumu mahali pale kwa uwezo wake" (Wakolosai 1:17).

Viumbe vyote humshuhudia yule Mungu Mbunifu Mkuu na Muumbaji asiye na Mwisho. Katika maneno haya rahisi, "Hapo mwanzo Mungu," tunalipata jibu la siri ile ya uhai. Yuko Mungu aliyeumba kila kitu.

Wanasayansi wakuu wengi siku hizi wanamwamini Mungu. Dk. Arthur Compton, mwanafizikia mshindi wa tuzo ya Nobel, akitoa maoni yake juu ya fungu hilo la Maandiko, siku moja alisema hivi:
"Kwangu binafsi, imani huanza ninapotambua kwamba yule aliye na akili isiyo na kifani ndiye aliyeyaweka hayo malimwengu na kumwumba mwanadamu. Kwangu mimi si vigumu kuwa na imani hii, kwa maana ni dhahiri kwamba po pote pale palipo na mpango yupo Mungu mwenye akili. Malimwengu yaendayo kwa utaratibu, na kujifunua kwetu hushuhudia



ukweli wa usemi huu adimu mno uliopata kunenwa - 'Hapo mwanzo Mungu"

Biblia haijaribu kumthibitisha Mungu inatangaza kuwako kwake. Dk. Arthur Conklin, mwana biolojia, siku moja aliandika hivi: "uwezekano kwa uhai kutokea kwa ajali ni sawa na uwezekano kwa kamusi kamili kutokea kutokana na mlipuko katika kiwanda cha kuchapisha vitabu".

Twajua kwamba wanadamu hawawezi kutengeneza kitu cho chote bila kutumia kitu kingine. Twaweza kujenga vitu, kuvumbua vitu, kuunganisha vitu, lakini kamwe hatujapata kufanya kitu cho chote bila kuwa na kitu kingine cha kuanzia, awe ni chura mdogo kabisa ua la kawaida kabisa. Vitu vituzungukavyo pande zote hupiga kelele vikisema Mungu ndiye aliyevibuni, Mungu ndiye aliyeviumba, Mungu ndiye anayevitegemeza. Jibu pekee linaloaminika kuhusu chimbuko la malimwengu hayo, dunia hii, na wanadamu - ni Mungu.

3. Mungu Huingia Katika Mahusiano Na Watu Binafsi

Mungu yule aliyezibuni mbingu hizo na nyota, aliyeaumba malimwengu hayo, anatafuta kuwa na uhusiano nasi binafsi. Alikuwa na uhusiano wake binafsi na Musa: "Bwana akasema na Musa....kama vile mtu asemavyo na rafiki yake" (Kutoka 33:11). Mungu Mwenyewe anataka kuingia katika uhusiano nawe na kuwa Rafiki yako. Yesu aliwaahidi wale wanaomfuata, akisema "Ninyi mmekuwa rafiki zangu" (Yohana 15:14).

Sisi sote tumeshughulika sana na wazo hilo la Mungu, kwa kuwa wanadamu kwa asili wanapenda dini. Hakuna mnyama yeoyote ajengaye madhabahu kwa ajili ya ibada. Lakini kila mahali unapowakuta wanaume na wanawake, unawakuta wakiabudu. Ndani ya kila moyo wa mwanadamu kuna ufahamu kuwa Mungu yuko, tamaa ya kuwa rafiki wa Mungu. Tunapoitikia hiyo tamaa yetu na kumpata Mungu, hatuwi na mashaka tena juu ya kuwako kwake na hitaji letu.

Katika miaka ile ya 1990 mamilioni ya wanaomkana Mungu katika nchi ya Urusi waliachana na imani yao hiyo ya kumkana Mungu, kisha wakamgeukia Mungu. Profesa wa Chuo Kikuu cha St. Petersburg alitoa kauli yake inayofanana na maoni yaliyotolewa na wakana Mungu wengi katika Umoja wa Kisovieti iliypota:

"Nimetafuta maana ya maisha katika utafiti wangu wa kisayansi, lakini sikuona kitu chochote cha kutegemea. Wanasyansi wanaonizunguka mimi wanazo hisia hizo hizo za ukiwa. Nilipoangalia ukubwa wa malimwengu katika somo langu la elimu ya nyota, kisha nikaangalia ukiwa uliomo moyoni mwangu, niliona kwamba ni lazima pawe na maana fulani. Kisha nilipoipokea Biblia uliyonipa na kuanza kuisoma, ukiwa katika maisha yangu ukajazwa. Nimeiona Biblia kuwa ndiyo chimbuko la pekee la matumaini kwa nafsi yangu. Nimempokea Yesu kama Mwokozi wangu, nami nimepata amani ya kweli pamoja na kuridhika katika maisha yangu".

Mkristo anamwamini Mungu kwa sababu yeye amekutana naye na kugundua kwamba anayatosheleza mahitaji makubwa sana ya moyo wake. Mungu ambaye Wakristo wamemuona kuwa yuko, anatupatia mtazamo mpya, maana mpya, makusudi mapya na furaha mpya.

Mungu hatuahidi sisi kwamba tutakuwa na maisha yasiyo na taabu, wala mapambano, ila yeye anatuhakikishia kwamba atatuongoza na kutusaidia kama tutakuwa na uhusiano binafsi naye. Na mamilioni ya Wakristo wanaweza kutoa ushuhuda wao kwamba ingekuwa heri kwao kuacha kila kitu kuliko kuyarudia maisha yale yasiyokuwa na Mungu.

Hii ndiyo ajabu kuu kuliko zote kwamba yule Mungu Mwenyezi aliyeabuni, aliyeaumba na kuyategemeza malimwengu hayo anataka kufanya uhusiano na kila mwanaume na mwanamke, kila mvulana na msichana. Daudi alishangaa sana kuhusu jambo hilo alipoandika maneno haya:
"Nikiangalia mbingu, kazi ya vidole vyako, mwezi na nyota



GUNDUA

"ulizozimika huko, mtu ni nini ee Mungu hata umfikirie mwanadamu ni nini hata umjali?" - (Zaburi 8:3,4).

Muumbaji wetu ana "mjali" kila mmoja wetu. Yeye binafsi anakupenda sana wewe kana kwamba wewe ulikuwa ni kiumbe chake cha pekee alichokiumba.

Basi tunaweza kumwamini Mungu:

- (1) Kwa sababu ya ubunifu wake wenye sehemu nyingi katika kila kitu alichokiumba ambacho kinatuzunguka sisi.
- (2) Kwa sababu shauku ile iliyomo ndani yetu juu ya Mungu inatufanya tusiwe na raha mpaka tupatapo pumziko letu ndani yake tena.
- (3) Kwa sababu tunapomtafuta na kumpata, Mungu hutosheleza kila haja tuliyo nayo pamoja na shauku yetu - kikamilifu!

4. Ni Mungu Wa Aina Gani?

Ni jambo la busara tu kwamba Mungu aliye na nafsi yake apende kujifunua mwenyewe kwa viumbe wake kama vile baba atakavyo watoto wake wamjue. Na katika Biblia Mungu anatuambia yeye ni nani, tena anafananaje.

Ni mfano gani alioutumia Mungu katika kuwaumba wanaume na wanawake?

"Hivyo Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba" (Mwanzo 1:27).

Kwa kuwa sisi tumeumbwa kwa mfano wa Mungu, basi, uwezo wetu wa kufikiri na kujisikia, kukumbuka na kutumaini, kutafakari na kuchambua mambo - chimbuko lake lote latoka kwake. Je, tabia kuu ya Mungu ni ipi?

"Mungu ni upendo" (1 Yohana 4:8).

Mungu hufanya uhusiano wake na wanadamu kutokana na moyo wake wa upendo. Hakuna kitu cho chote alichofanya au atakachopata kufanya ambacho hakijasababishwa na upendo wake usio na ubinafsi, ujitoao mhanga.

5. Jinsi Yesu Anavyotufunulia Alivyo Mungu

Katika Biblia Mungu anarudia tena na tena kueleza habari zake Mwenyewe kwamba Yeye ni Baba.

"Je! Sisi sote si watoto wa baba mmoja"?

"Je, sisi sote hatukuumbwa na Mungu yule yule?" Malaki 2:10.

Baadhi ya mababa tuwaonao leo si cho chote, bali hawapendezi. Kuna mababa wasiojali, mababa wanaotukana matusi. Mungu si kama hao. Yeye anajali, ni Baba anayeguswa sana na mambo yetu. Ni Baba apendaye kucheza na mwanawe au binti yake, ni Baba anayewafurahisha sana watoto wake kwa kuwasimulia hadithi kabla hawaenda kulala usiku.

Baba yetu huyo mwenye upendo alitaka kufanya zaidi ya kule kujifunua Mwenyewe kwa njia ya maneno ya Maandiko. Alijua kwamba yule mtu tunayeishi naye ni mtu halisi kuliko yule tunayesikia tu habari zake au tunayesoma habari zake. Kwa hiyo yeye akaja katika dunia yetu kama mtu halisi - yaani, yule mtu Yesu.

GUNDUA

"Kristo mfano wa Mungu asiyonekana" - (Wakolosai 1:15).

Basi kama wewe umemwona Yesu, utakuwa umemwona Mungu. Alijishusha hadhi yake na kuwa sawa sawa na sisi akawa kama sisi - ili apate kutufundisha jinsi ya kuishi na kuwa na furaha, ili kwamba sisi tupate kuona jinsi Mungu alivyo hasa. Yesu ni Mungu aliyeonekana kwa macho. Yeye mwenyewe alisema, "Aliyeniona mimi amemwona Baba" (Yohana 14:9).

Usomapo kisa cha Yesu katika vitabu vinne vya Injili, yaani, vitabu vinne vya kwanza vya Agano Jipya, utagundua picha ya kuvutia sana ya Baba yetu aliye mbinguni. Wavuvi wale wa kawaida tu walizitupa nyavu zao ili kumfuata Yesu, na watoto wadogo wakasongamana kwenda kwake kupokea baraka zake. Aliweza, kumfariji mwenye dhambi aliyeharibika kabisa na kuzivunja nguvu za mnafiki sugu aliyejihesabia haki yeye mwenyewe. Aliponya kila maradhi kuanzia upofu hadi ukoma. Katika matendo yake yote Yesu alidhahirisha kwamba Mungu ni upendo! Alikidhi haja ya mwanadamu kwa namna ambayo hakuna mtu ye yote aliyepata kufanya hivyo kabla yake au tangu wakati wake!

Ufunuo wa Yesu wa mwisho ambao unaonyesha utukufu wa jinsi Mungu alivyo ulitokea pale msalabani.

"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele" - (Yohana 3:16).

Yesu alikuwa sio tu kutupatia maisha yenyе furaha sasa, bali kutupa uzima wa milele pia. Kwa vipindi virefu watu walishangaa, na kutumaini, na kuota ndoto juu ya Mungu. Walionna kazi ya mikono yake mbinguni na katika uzuri wa viumbi vya asili. Kisha pale msalabani, Yesu alikivunjilia mbali kimya cha vizazi vingi, na watu wakajikuta wanautazama ana kwa ana uso wa Mungu, wakimwona yeye kama alivyo hasa - yeye ni upendo, wa milele, tena ni upendo udumuo milele!

Wewe waweza kumgundua Mungu sasa hivi Yesu anapomfunua kwako. Ugunduzi huo utakufanya utoe uthibitisho wako binafsi, ukisema: "Baba, nakupenda!"



TWAWEZA KUIAMINI BIBLIA

Mabaharia waasi maarufu walioizamisha meli ya Kiingereza ilioitwa Bounty waliishia kufanya makazi yao wakiwa pamoja na wanawake, wenyeji wa eneo lile katika kisiwa cha Pitcairn katika Bahari ya Pasifikasi ya Kusini. Kundi lile lilikuwa mabaharia tisa wa Kiingereza, wanaume wa Kitahiti sita, wanawake wa Kitahiti kumi, na msichana wa miaka kumi na mitano.

Mmojawapo wa mabaharia wale alivumbua namna ya kutonesha [kugeuza kuwa mvuke] alkoholi, na baada ya muda mfupi ulevi ukaliharibu koloni lile lilikuwa katika kisiwa kile. Ugomvi kati ya wanaume na wanawake ukageuka na kuwa wa kutumia nguvu.

Baada ya kupita muda fulani mmoja tu kati ya wanaume wale wa kwanza waliofika mle kisiwani ndiye alibaki kuwa hai. Lakini mtu huyo, Alexander Smith, alikuwa ameigundua Biblia katika mojawapo la makasha yaliyochukuliwa kutoka katika ile meli. Alianza kuisoma na kuwafundisha wengine juu ya kile ilichosema. Alipofanya hivyo maisha yake ye ye mwenyewe yakabadilika na hatimaye maisha ya wote waliokuwa katika kisiwa kile.



Wakazi wa kisiwa kile walikuwa wametengwa na ulimwengu wa nje mpaka ilipowasili meli ya Kimarekani ilioitwa Topaz katika mwaka wa 1808. Wafanyakazi katika meli hiyo wakakikuta kisiwa kile kikiwa na jumuia inayokua na kusitawi, bila ya kuwa na pombe kali (wiski), gereza, wala uhalifu. Biblia ilikuwa imekigeuza kisiwa kile kutoka jehanamu ya duniani kwenda katika kielelezo cha vile Mungu atakavyo ulimwengu huu uwe. Na mpaka leo hii kinaendelea kuwa katika hali hiyo.

Je, hivi Mungu bado anaendelea kusema na watu kupitia katika kurasa hizo za Biblia? Bila shaka anafanya hivyo. Ninapoandika haya, naliangalia karatasi la majibu lililotumwa kwetu na mwanafunzi mmojawapo wa kozi zetu za Biblia. Maelezo chini yake yanasema hivi "Mimi nimo gerezani, niko katika orodha ya watu wanaostahili kunyongwa, nimehukumiwa kufa kwa kutenda kosa la jinai. Kabla ya kuchukua kozi hii ya Biblia, nilikuwa nimepotea lakini sasa ninacho kitu cha kutumainia tena nimeupata upendo mpya."

Biblia inao uwezo unaoweza kuyabadilisha kabisa maisha ya watu. Kwa kweli, watu wanapoanza kujifunza Biblia, maisha yao hubadilika kwa namna ya kuvutia sana.

1. Jinsi Mungu Anavyozungumza Nasi Kupitia Katika Biblia

Baada ya kumwumba Adamu na Hawa, yaani, yule mwanaume na mwanamke wa kwanza wa duniani, Mungu alizungumza nao uso kwa uso. Lakini Mungu alipokuja kuwatemeblea baada ya wao kutenda dhambi, je, wale watu wawili walifanya nini?

"Mwanaume yule na mkewe wakasikia sauti ya BWANA MUNGU alipokuwa akitembea mle bustanini wakati wa jua kupunga, nao WAKAJIFICHA ASIWAONE BWANA MUNGU katikati ya miti ya bustani." (Mwanza 3:8).

Dhambi ilikata mawasiliano ya ana kwa ana kati ya mwanadamu na Mungu. Baada ya dhambi kuingia katika ulimwengu huu, je, Mungu aliwasilianaje na watu?



GUNDUA

"Hakika Bwana Mwenyezi hafanyi kitu, bila kuwafunulia watumishi wake manabii nia yake." - Amosi 3:7.


Mungu hakutuacha sisi gizani kuhusu maisha haya tulio nayo na maana yake. Kupitia kwa manabii wake - yaani, watu wale aliowaita Mungu kuwa wanenaji na waandishi wake - wamefunua majibu yake kwa maswali makuu yahusuyo maisha yetu.

2. Ni Nani Aliyeiandika Biblia?

Manabii waliutoa ujumbe wa Mungu kwa kutumia sauti na kalamu zao katika kipindi chao walichoishi, na walipokufa, maandiko yao yaliendelea kuwapo baada yao. Kisha ujumbe huo wa manabii ulikusanywa pamoja chini ya uongozi wake Mungu, na kuwekwa katika kitabu tunachokiita Biblia.

Lakini maandiko yao hayo yanaaminika kwa kiasi gani?

"Zaidi ya hayo, lakini kumbukeni kwamba hakuna mtu ye yote aezaye kufafanua mwenyewe unabii ulio katika Maandiko Matakatifu. Maana hakuna ujumbe wa kiunabii unaotokana na matakwa ya binadamu bali watu walitoa unabii wakiongozwa na Roho Mtakatifu" (2 Petro 1:20,21).



Waandishi wa Biblia waliandika si kwa kufuata mapenzi au tamaa yao, bali kama walivyoongozwa au kuvuviwa na Roho wa Mungu. Biblia ni kitabu cha Mungu!

Katika Biblia hiyo Mungu hutuambia habari zake Mwenyewe, tena hutufunulia makusudi yake aliyo nayo kwa ajili ya wanadamu. Inaonyesha mtazamo wa Mungu kwa mambo yale yaliyopita, kisha inatufunulia mambo ya mbele, ikitueleza jinsi tatizo la uovu litakavyotatuliwa mwishoni na jinsi amani itakavyokuja katika dunia yetu.

Je, hivi Biblia yote ni ujumbe utokao kwa Mungu?

"Maandiko yote, Matakatifu yameandikwa kwa uongozi wa Mungu, na yanafaa kuonya, kusahihisha makosa yao, na kuwaongoza, katika kufundishia ukweli, mtu wa Mungu awe mkamilifu na tayari kabisa kufanya kila kazi njema, waishi maisha adilifu" - (2 Timotheo 3:16,17).

Biblia Takatifu huyabadilisha kabisa maisha ya wanadamu kwa sababu Biblia "yote" ina "pumzi ya Mungu," ni hati iliyovuviwa, ni kitabu cha Mungu. Manabii walisimulia kile walichokiona na kukisikia kwa kutumia lugha ya wanadamu, lakini ujumbe wao ultoka moja kwa moja kwa Mungu. Kwa hiyo, ukitaka kujua maisha haya yana maana gani, soma Maandiko Matakatifu. Kuisoma Biblia kutayabadilisha kabisa maisha yako. Kadiri unavyozidi kuisoma kwa maombi, ndivyo utakavyozidi kupata amani moyoni mwako.

Roho Mtakatifu yule yule aliyewavuvia manabii kuandika, Biblia hiyo, atayafanya mafundisho ya Biblia, injili yake, ifae kuyabadilisha kabisa maisha yako ukimwalika Roho kuwapo wakati unapoisoma hiyo Biblia.

3. Umoja wa Biblia

Kwa kweli Biblia ni maktaba ya vitabu 66. vitabu 39 vya Agano la Kale viliandikwa kuanzia karibu na mwaka wa 1450 K.K hadi 400 K.K, Vitabu 27 vya Agano Jipyä viliandikwa kati ya mwaka wa 50 B.K na mwaka wa 100 B.K.

Nabii Musa alianza kuandika vitabu vitano vya kwanza wakati fulani kabla ya mwaka wa 1400 K.K. Mtume Yohana alikiandika kitabu cha mwisho cha Biblia, yaani, kitabu cha Ufunuo, karibu na mwaka wa 95 B.K. Katika kipindi cha miaka 1,500 kati ya kuandikwa kitabu cha kwanza na cha mwisho cha Biblia,

GUNDUA

walau watu wengine wapatao 38 waliovuviwa walitoa mchango wao. Wengine walikuwa wafanya biasara, wengine wachungaji wa kondoo, wengine wavuvi, wengine askari, matabibu, wahubiri, wafalme - wanadamu toka katika tabaka zote za maisha. Mara nyingi waliishi katika utamaduni na falsafa vilivyohitilafiana.

Lakini hapa ndipo yalipo maajabu ya maajabu yote: Vitabu hivyo 66 vya Biblia pamoja na sura zake 1,189 zenye idadi ya mafungu 31,173 vikiwekwa pamoja, tunaona umoja na mwafaka katika ujumbe vinaoutoa.



Hebu na tuseme kwamba mtu mmoja anagonga mlangoni pako, halafu anapokaribishwa ndani, anaweka kipande cha marumaru chenye umbo la ajabu juu ya sakafu ya chumba chako cha kuongea, halafu anaondoka bila kusema neno lo lote. Wageni wengine wanamfuata, mmoja baada ya mwagine, mpaka takribani watu 40 wanaweka kila mmoja kipande chake cha marumaru mahali pake.

Wa mwisho anapokwenda zake, kwa mshangao wewe unaona jengo zuri limesimama mbele yako. Ndipo wewe unajifunza kwamba sehemu kubwa ya "mafundi hao wanachonga mawe" hawajawahi kuonana kamwe, wakiwa wamekuja, kama walivyofanya, kutoka Amerika ya Kusini, China, Urusi, Afrika na sehemu nyingine za ulimwengu.

Je, wewe ungeamua nini? Ya kwamba mtu fulani alipanga umbo hilo lililojengwa kwa mawe ya kuchonga naye alimtumia kila mtu vipimo sahihi kutokana na kipande chake kile kimoja cha marumaru.

Biblia nzima inatoa ujumbe mmoja unaoshikamana - sawasawa tu na lile jengo la mawe yaliyochongwa ya marumaru. Mtu fulani mmoja mwenye akili alipanga yote hayo, yaani, ni akili za Mungu. Umoja wa kushangaza wa Maandiko Matakatifu unatoa ushahidi wake kwamba ingawa ni wanadamu walioyaandika mawazo yale, yalikuwa yamevuvuviwa naMungu.

4. Waweza Kuiamini Biblia

1. Kuhifadhiwa kwa Biblia ni jambo la ajabu sana. Maandiko yote ya awali ya Biblia yalinukuliwa kwa mkono - muda mrefu kabla ya kuwako mitambo ya kuchapisha vitabu. Waandishi wale walitayarisha nakala za maandiko ya mkono ya asilia na kuzitawanya. Maelfu ya nakala kama hizo za maandiko ya mkono au sehemu zake bado ziko mpaka sasa.

Maandiko ya mkono ya Kiebrania yanayorudi nyuma hadi ule mwaka wa 150 mpaka 200 kabla ya Kristo yalipatikana karibu na Bahari ya Chumvi mnamo mwaka 1947. Ni jambo la kushangaza sana kwamba magombo hayo mawili yenye umri wa miaka elfu mbili yanazo kweli zile zile tunazozikuta katika Agano la Kale la Biblia zinazochapishwa siku hizi. Huu ni ushahidi wenye nguvu unaoonyesha jinsi Neno la Mungu linavyoaminika.

Mitume waliandika kwanza sehemu kubwa ya Agano Jipyka kama nyaraka walizozitura kwa makanisa ya Kikristo yaliyoanzishwa baada ya kifo na ufufuo wake Kristo. Zaidi ya maandiko ya mkono 4,500 ya Agano Jipyka lote au sehemu yake yanapatikana katika nyumba za Makumbusho na maktaba za Ulaya na Amerika. Baadhi yake yanakwenda nyuma hadi karne ile ya pili. Kuyalinganisha maandiko hayo ya mkono ya awali na biblia ya siku hizi, twaweza kuona kwa urahisi kwamba kwa kawaida Agano Jipyka limeendelea pia kubaki bila mabadiliko yo yote tangu lilipoandikwa kwa mara ya kwanza.



GUNDUA

Siku hizi Biblia au sehemu zake zimetafsiriwa katika lugha zaidi ya 2,060 na (dialects). Ni kitabu kinachouzwa sana ulimwengu: zaidi ya Biblia milioni 150 na sehemu za Biblia huuzwa kila mwaka.



2. Usahihi wa Biblia kihistoria ni wa kushangaza sana. Uvumbuzi mwingi wa elimu ya mambo ya kale (akiolojia) umethibitisha kwa namna ya kuvutia sana usahihi wa Biblia. Wanahistoria wamevigundua vibao vya udongo wa mfinyanzi pamoja na majengo ya kumbukumbu ya mawe ambayo yameonyesha majina, mahali, na matukio yaliyojulikana kuhusu siku za nyuma kutokana na Biblia tu.

Kwa mfano, kulingana na Mwanzo 11:31, Ibrahimu na familia yake "wakatoka wote katika Uru... waende katika nchi ya Kanaani." Kwa kuwa ni Biblia peke yake iliyosema juu ya Uru, mabingwa fulani wa Biblia walisema kwamba mji kama huo ulikuwa haujapata kuwako kamwe. Ndipo wachimbaji wa mambo ya kale wakagundua mnara wa hekalu katika nchi ya Iraki Kusini ukiwa na kwenye msingi wake ilioandikwa katika maandishi ya kikabari yaliyokuwa na jina la Uru. Ugunduzi wa baadaye ulionyesha kwamba Uru ulikuwa ni mji mkuu ambao ulikuwa unasitawi wenyewe ustaarabu wa hali ya juu ulikuwa umefikiwa. Sura ya mji ule ilikuwa imesahaaulika ni Biblia peke yake iliyolihifadhi jina lake - mpaka pale koleo ya mwanaakiolojia mmoja ilipouthibitisha ukweli wa kuwako kwake. Na huo Uru ni mmoja tu mionganini mwa mifano mingi ya akiolojia inavyothibitisha usahihi wa Biblia.

3. Kutimia kwa usahihi kabisa kwa utabiri wa Biblia hukuonyesha wewe kwamba unaweza kuitegemea Biblia. Maandiko hayo yana utabiri mwingi wa kushangaza sana wa matukio ya siku za usomi ambayo hivi sasa yanaendelea kutimia mbele ya macho yetu. Tutauchunguza baadhi ya unabii huo wa kusisimua katika masomo ya mbele.

5. Jinsi Ya Kuilewa Biblia

Unapolichunguza Neno la Mungu, weka kanuni hizi mawazoni mwako:


1. Jifunze Biblia ukiwa na moyo wa maombi. Ukiyaendea Maandiko Matakatifu kwa moyo na mawazo yaliyofunguliwa kwa maombi, yatageuka na kuwa mawasiliano kati yako na Yesu (Yohana 16:13-14).

2. Soma Biblia kila siku. Kujifunza Biblia kila siku ni ufunguo wa kupata nguvu katika maisha yetu, ni kukutana na mawazo ya Mungu (Warumi 1:16).

3. Unapoisoma, iache Biblia ijieleze yenye. Uliza: mwandishi huyu wa Biblia alikusudia kusema nini? Kwa kuzingatia kile limaanishacho fungu hilo, twaweza kuitumia kwa akili katika maisha yetu ya leo hii.

4. Soma Biblia kwa kufuata somo. Linganisha andiko na andiko. Yesu alitumia mbinu hii kuthibitisha kwamba ye ye aliwa ndiye Masihi:
"Akaanza kutoka Musa na Manabii wote, akawaeleza katika maandiko yote mambo yaliyomhusu ye ye mwenyewe."

5. Jifunze Biblia ili kupokea uwezo wa kuishi kwa ajili ya Kristo. Neno la Mungu limeelezwa katika Waebrania 4:12 kama upanga mkali ukatao kuwili. Ni zaidi ya maneno tu yaliyo juu ya ukurasa, ni silaha iliyo hai mikononi mwetu ya kupigia na kuyaondolea mbali majaribu yale yanayotushawishi kutenda dhambi.



GUNDUA

6. Sikiliza Mungu anapozungumza nawe kupertia katika Neno lake. Endapo mtu anataka kuujua ukweli wa Bilbia juu ya somo fulani, basi, ni lazima awe tayari kufuata yale inayofundisha (Yohana 7:17), sio yale anayofikiri mtu fulani, au yale yanayokaziwa na fundisho lolote la kanisa lake.

6. Biblia Yaweza Kubadilisha Maisha Yako

"Kuyafafanua maneno yako [Mungu] kwatia nuru, kunampa ufahamu mjinga" - (Zaburi 119:130).

Kujifunza Biblia kutauimarisha "ufahamu" wako, kutakupa nguvu ya kuyashinda mazoea yale yaletayo madhara, na kukuwezesha kukua kimwili, kiakili, kimaadili na kiroho.

Biblia inazungumza na moyo. Inashughulika na mambo yale yanayowapata wanadamu katika maisha yao - yaani, upendo, ndoa, uzazi na kifo. Inaliponya jeraha lenye kina kirefu sana katika tabia ya mwanadamu, pamoja na dhambi na taabu inayotokana nayo.



Neno la Mungu si kitabu cha jamii moja, kizazi kimoja, taifa moja, au utamaduni mmoja. Japokuwa liliandikwa katika nchi ya Masharikiya kati, linawavutia pia wanaume na wanawake wa Magharibi. Linaingia katika nyumba za wanyonge na katika majumba makubwa ya matajiri. Watoto wanazipenda hadithi zake zinazosisimua. Mashujaa wake wanawavutia sana vijana. Wagonjwa, wanaoishi katika hali ya upweke, na wazee wanagundua ndani yake faraja na tumaini la kuwa na maisha bora.

Kwa kuwa Mungu anafanya kazi yake kupertia katika Biblia, basi, inao uwezo mkubwa. Inaivunjavunja hata miyo iliyofanywa migumu dhidi ya hisia zote za kibinadamu, inailainisha na kuijaza na upendo. Tumeona Biblia ikimbadilisha haramia wa zamani na mvuta bangi na kumfanya mhubiri aliye motomoto. Tumeona Biblia ikimbadilisha mwongo na mdanganyaji na kumfanya kuwa mwalimu mwaminifu na mwenye kuheshimika. Tumeona kitabu hicho kikiwanyakua watu wakiwa karibu na kujua wenyewe na kuwapa tumaini la kuanza maisha upya. Biblia inaansha upendo mionganoni mwa maadui. Inawafanya wenye majivuno kuwa wanyenyekevu, na wachoyo kuwa wakarimu. Biblia inatutia nguvu tunapokuwa dhaifu, inatuchangamsha tunapokuwa katika hali ya kukata tamaa, inatufariji tunapokuwa na huzuni, inatuongoza tunapochoka sana. Inatuonyesha jinsi ya kuishi kwa ujasiri na jinsi ya kufa bila hofu.

Kitabu hicho cha Mungu, yaani, Biblia kinaweza kuyabadilisha maisha yako! Utagundua hivyo kwa dhahiri zaidi na zaidi, kadiri unavyoendelea kujifunza miongozo hii ya GUNDUA.

Kwa nini Biblia hiyo iliandikwa kwa ajili yetu? Yesu anatoa jibu: **"Lakini hizi [kweli za Biblia] zimeandikwa; ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini muwe na uzima kwa jina lake" - (Yohana 20:31).**

Sababu kuu kuliko zote kwa nini sisi tunapaswa kuyafahamu Maandiko Matakatifu ni kwamba yamejaa picha zinazomfunua Yesu Kristo na kutuhakikishia sisi uzima wa milele. Kwa kumtazama Kristo katika Biblia nzima, tunabadilika na kufanana naye zaidi. Basi, kwa nini wewe usianze sasa kugundua uwezo huo wa Neno la Mungu uwezao kukufanya wewe kufanana zaidi na Yesu?

JE! MAISHA YANGU YANA MAANA KWA MUNGU?

1. Mungu Aliumba Dunia Kamilifu



Mungu ndiye Muumbaji, mwasisi na mbunifu wa kila kitu kuanzia nyota zinazotoa mlipuko wa mwanga mkubwa kuliko jua na kutoweka (supernovas) hadi mabawa ya kipepeo.

"Kwa neno la BWANA mbingu zilifanyika na jeshi lake lote kwa pumzi ya kinywa chake.... maana yeye alisema, ikawa; na yeye aliamuru, ikasimama" - (Zaburi 33:6-9).

Mungu hana budi kusema tu, kisha vitu vya asili hutii mapenzi yake.

2. Siku Sita Kuifanya Dunia Yetu

"Kwa siku zita BWANA alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba. Kwa hiyo, BWANA akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa" - (Kutoka 20:11).

Muumbaji huyo wa milele, mwenye uweza wote angeweza kuiumba dunia hii kwa dakika moja "kwa pumzi ya kinywa chake." Lakini Mungu alichagua kuchukua siku sita kufanya kazi hiyo dakika sita, au hata nukta sita zingekuwa zinatosha. Sura ile ya kwanza katika Biblia, yaani, Mwanzo 1, inaeleza kile Mungu alichokumba katika kila siku ya juma lile la Uumbaji.

Ni kazi gani bora ya kilele aliyoumba Mungu katika siku ile ya sita?

"Mungu Akaumba Mtu Kwa Mfano Wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba; Mwanaume Na Mwanamke Aliwaumba" - (Mwanzo 1:27).

Juma La Uumbaji

Siku ya Kwanza: Nuru; mfuatano wa mchana na usiku

Siku ya Pili: Anga, hewa ya dunia hii

Siku ya Tatu: Nchi kavu na mimea

Siku ya Nne: Jua na mwezi vikaonekana

Siku ya Tano: Ndege na Samaki

Siku ya Sita: Wanyama wa nchi kavu na mwanadamu

Siku ya Saba: Sabato



Mungu aliamua kuwaumba watu wanaofanana naye ambao wangeweza kufikiri na kujisikia na kupenda. Kila mtu ameumbwa kwa "mfano" wa Mungu.

Kufikia siku ile ya sita, dunia hii ilikuwa imejazwa na mimea na wanyama, ndipo Mungu aksileta kazi yake bora kuliko zote ya uumbaji. Kulingana na Mwanzo 2:7, Mwenyezi aliuumba mwili wa Adamu kwa mavumbi ya ardhi. Basi Mungu alipompulizia "pumzi ya uhai", puanı mwake, mtu akawa "kiumbe hai" - yaani, akawa na uhai. Mungu alimwita Adamu, yule mtu wa kwanza aliyeumbwa kwa mfano wake, neno hilo limaanishalo tu "mtu" na mwanamke yule wa kwanza akamwita Hawa maana yake, "aliye hai" (2:20; 3:20). Muumbaji huyo mweye upendo aliona ipo haja kwa binadamu kuwa na mwenzi.

Wakiwa wametoka wenye afya mkononi mwake Mungu, Adamu na Hawa, wote wawili, walikisi [walirudisha mwanga wa] sura yake. Mungu angeweza kuwaumba wanadamu kama [kikaragosi] roboti wakizurura huku na huku katika ile bustani ya

Edeni na kutosheka na kupaza sauti zao kumwabudu yeye. Lakini Mungu alitaka zaidi ya hilo; yaani, alitaka kuwa na uhusiano wa kweli nao. Maroboti yanaweza kutabasamu, kusema, na hata kuosha vyombo vya kulia chakula, ila hayawezi kupenda.

Mungu alitumba sisi kwa mfano wake, tukiwa na uwezo wa kufikiri na kuchagua, na kukumbuka, kufahamu na kupenda. Adamu na Hawa walikuwa watoto wa Mungu, na kwa namna isiyoelezeka walikuwa wanapendwa sana naye.



3. Uovu Waingia Katika Dunia Hii Kamilifu

Adamu na Hawa walikuwa na kila kitu cha kuwaleta furaha. Walifurahia kuwa na afya kamili kimwili na kiakili, wakiishi katika bustani ile nzuri katika dunia hii isiyo na dosari (Mwanzo 2:8; 1:28-31). Mungu aliwaahidi kuwapa watoto na kufurahia kuona kazi ya mikono yao (Mwanzo 1:28; 2:15). Walikuwa na uzoefu wa kirafiki wa ana kwa ana na Muumbaji wao. Hapakuwa na wasiwasi, hofu, au ugonjwa wo wote wa kuziathiri siku zao zilizowaletea furaha kamili.

Je, dunia hii ilibadilikaje kwa ghafula mno na kuwa mahali pa mateso na misiba? Sura ya pili na ya tatu ya Mwanzo inatusimulia kisa chote juu ya jinsi dhambi ilivyoingia katika dunia yetu. Uzisome kwa nafasi yako. Hapa ni muhtasari mfupi wa mambo yaliyomo katika sura hizo.

Muda fulani baada ya Mungu kuiweka dunia hii kamilifu, yule Shetani akaja katika Bustani ile ya Edeni kumjaribu Adamu na Hawa ili wamwasi Muumbaji wao. Mungu alimwekea yule Shetani mipaka ya mvuto wake kwenye mti mmoja tu katika ile bustani, yaani, kwenye ule "mti wa ujuzi wa mema na mabaya." Kisha akawaonya wale watu wawili, mume na mke, kuwa mbali na mti ule na kutokula kabisa matunda yake, la sivyo, wangekufa.



Lakini siku moja Hawa akazurura kuelekea karibu na mti ule uliokatazwa. Shetani akamshambulia upesi kwa kumwuzia maneno ya kumshawishi. Alidai kwamba Mungu alikuwa amesema uongo kwake na ya kwamba endapo yeye angekula matunda ya mti ule, asingekufa, ila angekuwa na hekima kama Mungu mwenyewe, akijua mema na mabaya. Kwa bahati mbaya sana Hawa, na hatimaye Adamu, ambao walikuwa wanayajua mema tu, wakamruhusu Shetani kuwarubuni, kisha wakalionja lile tunda lililokatazwa - hivyo kukivunja kifungo chao cha imani na utii kwa Mungu.

Mungu alikuwa amefanya mpango kwamba Adamu na Hawa wa "tawale" dunia yetu hii kama mawakili wake wa kazi zile alizoziumba Mungu (Mwanzo 1:26). Lakini kwa kuwa walikosa uaminifu kwa Mungu na kumchagua Shetani kama kiongozi wao mpya, basi, wale watu wawili, mume na mke, wakaipoteza mamlaka yao. Leo hii Shetani anadai kwamba dunia hii ni yake, tena anajitahidi sana kuwanasa watu wa dunia hii.

Mara nyingi sana tunajikuta tukifanya jambo fulani la uchoyo au hata kuwa wakatili wakati tunalotaka kufanya hasa ni kinyume chake. Hivi kwa nini? Kwa sababu huyo adui asiyonekana kwa macho yetu, yaani, huyo Shetani, anafanya kazi yake ili kuwafanya watu washindwe kimaadili.

Unapoisoma sura ya tatu ya Mwanzo, utagundua kwamba dhambi ilimfanya Adamu na Hawa kujificha kwa hofu ili Mungu asiwaone. Dhambi iliathiri uumbaji wote. Miiba ikajitokeza pamoja na maua. Ardhii kaathirika kwa ukame, na kazi ikawa ni mzigo ulemeao. Ugonjwa ukaanza kuwashambulia watu hapa na pale bila kuwa na mpangilio. Wivu chuki, na uchoyo vikazidisha taabu zao. La kutisha mno, pamoja na ile dhambi ikaja mauti.

GUNDUA

4. Shetani Huyo Ni Nani Ambaye Aliiambukiza Dunia Yetu Dhambi?

"Yeye alikuwa MWUAJI TANGU MWANZO; wala hakusimama katika kweli, kwa kuwa hamna hiyo kweli ndani yake. Asemapo uongo, yaliyo yake mwenyewe, kwa sababu yeye ni mwongo na BABA WA UONGO" - (Yohana 8:44).

Kulingana na Yesu, Shetani ndiye mwanzilishi wa dhambi katika dunia hii, yeye ni "baba" wa dhambi na hivyo ni baba wa mauaji na uongo

Thomas Carlyle, mwanafalsafa mashuhuri wa Kiingereza, siku moja alimchukua Ralph Waldo Emerson na kumtembeza kuititia katika baadhi ya mitaa michafu sana iliyoishia mashariki mwa mji wa London. Walitembea pamoja, wakiangalia kimya kimya na kuona umaskini na uovu uliowazunguka pande zote, hatimaye Carlyle akauliza, "Je! unaamini juu ya Shetani sasa?"

5. Je! Mungu Alimwumba Shetani?

La! Mungu mwema asingeweza kumwumba Shetani. Na, hata hivyo, Biblia inasema kwamba Shetani, pamoja na malaika wale aliowadanganya, walipoteza mahali pao mbinguni na kuja katika dunia yetu.

"Kulikuwa na VITA MBINGUNI. Mikaeli na malaika zake wakapigana na yule joka, naye JOKA NA MALAIKA ZAKE akapigana nao. Nao hawakushinda wala mahali pao hapakuonekana mbinguni. Yule joka mkubwa akatupwa chini kwa nguvu - nyoka yule wa zamani, aitwaye Ibilisi au Shetani, audanganyaye ulimwengu wote. Akatupwa kwa nguvu mpaka duniani, na malaika zake wakatupwa pamoja naye" (Ufunuo 12:7-9).



Huyo Shetani aliiingiaje kwanza kule mbinguni?

"Wewe ulikuwa kerubi mwenye kutiwa mafuta afunikaye. Naam nalikuweka hata ukawa juu ya mlima mtakatifu wa Mungu;..... ULIKUWA MKAMILIFU KATIKA NJIA ZAKO tangu siku ile ULIPOUMBWA HATA UOVU ULIPOONEKANA NDANI YAKO" (Ezekieli 28:14,15).

Mungu hakumwumba Shetani, alimwumba Lusifa, malaika mkamilifu, mmojawapo wa malaika wakuu wa mbinguni, aliyesimama karibu na kitu cha enzi cha Mungu. Lakini baadaye alitenda dhambi - "uovu ulionekana ndani" yake. Akiwa amefukuzwa mbinguni, naye akijifanya ni rafiki wa Adamu na Hawa, aligeuka na kuwa adui, mwenye madhara makubwa mno, kwa wanadamu.

6. Kwa Nini Lusifa, Alitenda Dhambi?

"Jinsi ULIVYOANGUKA KUTOKA MBINGUNI, Ewe nyota ya alfajiri (Lusifa), mwana wa asubuhi!..... Nawe ulisema moyoni mwako, "Nitapanda mpaka mbinguni; nitakiinua kitu changu juu kuliko nyota za Mungu..... NITAFANANA NA YEYE ALIYE JUU"- (Isaya 14:12-14).

Kiumbe yule aliyegeuka na kuwa Shetani, zamani aliiwtwa Lusifa, maana yake "nyota ya alfajiri" au "yule anayeng'aa." Ndani ya moyo wa malaika huyo, kiburi na kutaka makuu, mambo hayo, yakaanza kuchukua mahali pa kumwabudu Mungu. Mbegu ya kiburi ikakua mpaka ikawa tamaa isiyotulizika ya kutaka kuchukua mahali pa Mungu.



GUNDUA

Bila shaka Lusifa alikuwa amejitahidi sana kuwashawishi viumbe wale wengine wa mbingu. Ni rahisi kuingiwa na mawazo na kumwona Shetani akibishana na Mungu kwamba alikuwa akizua kitu fulani ili wao wasikipate, na ya kwamba sheria ya Mungu [Amri Kumi] ilikuwa inawabana vibaya mno, na ya kwamba Mungu alikuwa ni mtawala asiyejali. Akamsingizia yule mmoja ambaye tabia yake inaonyesha upendo ni nini.

Vita hiyo ilisuluhishwaje kule mbinguni?

"Moyo wako ukiinuka kwa sababu ya uzuri wako,..... nimekutupa chini" (Ezekiel 28:17).

Kiburi kilimgeuza yule mkuu wa malaika na kumfanya Ibilisi au Shetani. Na ili kuhifadhi amani na umoja ulioko kule mbinguni, yeze pamoja na theluthi moja ya malaika wa mbinguni waliojiunga naye katika maasi yale. Wakapaswa kufukuzwa kule (Ufunuo 12:4, 7-9).

7. Nani Anawajibika Kwa Dhambi?

Kwa nini Mungu hakuwaumba viumbe wasio na uwezo wa kutenda dhambi? Kama angefanya vile, basi, pasingekeuwako na tatizo lo lote la uovu katika dunia yetu. Lakini Mungu alitaka kuwa na watu ambaowangekuwa na uhusiano unaoleta maana. Kwa hiyo "Mungu akaumba mtu kwa mfano wake" (Mwanzo 1:27). Hii maana yake ni kwamba sisi tuko huru, tena tunawajibika. Tunaweza kuamua kumpenda Mungu au kumgeuzia migongo yetu.

Mungu aliwapa malaika wale pamoja na wanadamu wa kila kizazi, tabia ya kiroho na uwezo wa kufanya tabia ya kiroho na uwezo wa kufanya uchaguzi halisi.

"Chagueni wenyewe hivi leo mtakayemtumikia." Joshua 24:15.

Mungu anatoa changamoto kwa viumbe wake aliowaumba kwa mfano wake ili wachague kutenda mema kwa sababu uwezo wao wa kufikiri unawaambia kwamba "Njia ya Mungu ni bora kuliko zote." Kisha kugeukia mbali na makosa kwa sababu uwezo wao wa kufikiri unawaonya dhidi ya matokeo ya uasi na dhambi.



Ni viumbe wale tu walio na uwezo wa kufikiri na kuchagua wawezao kuwa na upendo wa kweli. Mungu alitamani sana kuwaumba watu ambaowangeweza kuijua na kuithamini tabia yake, kuitikia kwa kuonyesha upendo wao kwake, na kujazwa na upendo wake, kwa ajili ya wengine. Mungu alitaka sana kuwashirikisha upendo wake hata akawa tayari kujiingiza katika hatari kubwa mno ya kuwaumba malaika na wanadamu wenye uwezo wa kuchagua. Alijua kwamba uwezekano uliokuwapo kwamba siku moja mmojawapo wa viumbe wake aliowaumba angeweza kuchagua asimtumikie yeze. Shetani alikuwa kiumbe wa kwanza katika malimwengu kufanya uchaguzi wa kutisha. Misiba ilioletwa na dhambi ilianzishwa naye (Yohana 8:44, 1 Yohana 3:8).

8. Msalaba Unafanya Uwezekano Uwepo Wa Kuangamizwa Kwa Dhambi

Kwa nini Mungu hakumwangamiza Lusifa kabla ya ugonjwa wake wa dhambi kuweza kuenea? Lusifa alikuwa amepinga kwa kusema kwamba serikali ya Mungu ilikuwa haina haki. Alikuwa amesema uongo kumhusu Mungu. Kama Mungu angekuwa amemwangamiza Lusifa wakati ule ule, basi, malaika wale wangekuwa wameanza kumtumikia yeze [Mungu] kwa hofu badala ya kumtumikia kwa upendo. Hilo, kwanza kabisa lingekuwa limelivunjilia mbali kusudi la Mungu la kuwaumba viumbe wenye uwezo wa kuchagua.

GUNDUA

Mtu ye yote angewezaje kujua kama njia ya Mungu ilikuwa kweli bora kuliko zote? Mungu alimpa Shetani nafasi ya kuonyesha mfumo wake mbadala. Hii ndiyo maana alipewa fursa [nafasi] ya kumjaribu Adamu na Hawa.

Sayari hii imegeuka na kuwa uwanja wa majoribio ambamo hulinganishwa tabia ya Shetani na aina ya ufalme wake na tabia ya Mungu na aina ya Serikali yake. Nani mwenye haki? Ni nani tuwezaye kumtegemea mwishowe? Lusifa alikuwa mdanganyifu mno, hata imechukua muda kwa viumbwe wa malimwengu kuweza kusadiki kabisa jinsi ilivyo hasa ile njia mbadala iletayo maafa aliyoichagua Shetani. Lakini hatimaye kila mtu atatambua kwamba "mshahara wa dhambi ni mauti" na ya kwamba "karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu" (Warumi 6:23).

Kila kiumbe katika malimwengu hayo wakati ule kitakubali kwamba:-

"Ni makuu, na ya ajabu, matendo yako, Ee Bwana Mungu Mwenyezi. Ni za haki, na za kweli, njia zako, Ee mfalme wa mataifa.... mataifa yote watakuja na kusujudu mbele zako, kwa kuwa matendo yako ya haki yamekwisha kufunuliwa" - (Ufunuo 15:3,4).

Baada ya kila mtu kuielewa tabia ya kufisha ya dhambi na hali ya uharibifu inayoletwa na falsafa ya Shetani, ndipo Mungu anaweza kumwangamiza Shetani pamoja na dhambi. Atalazimika pia kuwaangamiza wale ambaao kwa ukaidi wao wanapinga neema yake na kuing'ang'ania ile njia mbadala aliyoiveka Shetani.



Mungu anahangaika vile vile kulitatua tatizo hilo la dhambi na mateso kama sisi tunavyotaka yeye afanye hivyo. Lakini anangojea mpaka hapo atakapoweza kufanya hivyo kwa msingi utakaoleta matokeo ya kudumu, na mpaka hapo anapoweza kuuhifadhi uhuru wetu wa kuchagua na kuuzuia uovu usipate kutokea tena.

Mungu ameahidi kuiangamiza dhambi milele kwa njia ya kuzitakasa mbingu na dunia hii kwa moto. "kama ilivyo ahadi yake" tunaweza ku "tazamia mbingu mpya na nchi mpya, makao ya wenye haki" (2Petro 3:10,13). Dhambi haitaenea kamwe katika malimwengu kwa mara ya pili. Matokeo mabaya sana ya dhambi yataonekana wazi kabisa kiasi kwamba uasi dhidi ya Mungu utaonekana kuwa ni wa kuchukiza milele zote.

Je, ni nani anayefanya uwezekano uwepo wa kumwangamiza Shetani pamoja na dhambi?

"Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye [Kristo] vivyo hivyo alishiriki katika ubinadmu wao, ili kwa njia ya mauti apate kumharibu yeye aliye na nguvu za mauti - yaani Ibilisi - awaache huru wale ambaao katika maisha yao yote walikuwa wameshikiliwa katika hali ya utumwa kwa hofu yao ya mauti" - (Waebrania 2:14,15).

Pale msalabani malaika pamoja na wale wa dunia zisizoanguka dhambini walimwona Shetani kama alivyo hasa - laghai, mwongo, mwuaji. Pale ndipo alipoidhihirisha tabia yake halisi kwa kuwalazimisha wanadamu kumwua Mwana wa Mungu asiye na hatia. Wakazi wa malimwengu yote walijiona wenyejewa jinsi dhambi isivyo na maana kabisa na ilivyo katili kama vile ilivyo hasa. Msalaba uliyafichua kabisa makusudi ya Shetani, na Mungu atakapomwangamiza Shetani pamoja na wale wanaoendelea kutenda dhambi, wote watakiri kwamba Mungu ni mwenye haki.



Kifo cha Yesu pale msalabani kilifunua wazi mbele ya viumbwe wote walioumbwa kusudi halisi alilonalo Shetani (Yohana 12:31,32). Pia msalaba ule ulimfunua Kristo alivyo hasa - yaani, yeye ndiye Mwokozi wa ulimwengu. Pale Golgotha nguvu ya upendo ilijitokeza wazi kabisa dhidi ya kupenda mamlaka. Msalaba ule ulithibitisha bila shaka lolote kwamba ni ule upendo

GUNDUA



unaojitoa kafara ambao unamsukuma Mungu katika kushughulika kwake kote na Shetani, dhambi, pamoja na wanaume na wanawake wenye dhambi.

Pale msalabani Kristo alionyesha upendo wa Mungu usio na masharti kwa njia iliyokuwa na uwezo wa kuushawishi moyo na kumshinda kabisa Shetani. Vita ilikuwa juu ya nani atakayeitawala dunia hii, Kristo au Shetani? Tena, msalaba ule uliamua hoja hiyo kwa wakati wote. Ni lazima awe Kristo juu ya wote!

Je, umeugundua uhusiano wako na Mwokozi aliyekufa ili kuudhihirisha upendo wake usio na kifani, ambao haubadiliki? Unajisikiaje kuhusiana na huyo mmoja aliyekuja katika dunia yetu kama mwanadamu, na kufa badala yako ili kukuokoa wewe mbali na matokeo ya dhambi? Je, utainamisha chini kichwa chako hivi sasa na kumshukuru Yesu, na halafu kumwomba aingie ndani na kuyatawala maisha yako?.....

MPANGO KWA AJILI YA MAISHA YAKO

Baada ya mchungaji kuzungumza juu ya somo hili, "Kwa nini mimi namwamini Yesu," mwanaume mmoja kijana, aliyevalia vizuri, alimtembelea katika chumba chake cha kusomea na kusema naye kwa mshangao, "Hotuba yako usiku wa leo ilitoka katika Biblia yako. Hebu niambie, kama Yesu alipata kuishi hapa duniani, mbona historia haisemi habari zo zote juu yake?

"Hilo ni swali zuri," mchungaji akajibu alipogeuka na kuchukua vitabu kadhaa na kuviweka chini. "Lakini, kwa kweli, historia inasimulia habari za Yesu Kristo."

"Hizo ningependa kujionea mwenyewe," yule mwanaume kijana akajibu. "Vema, hapa ni barua ya 97 ya kitabu cha 10 cha barua za (Pliny) Ndogo, Balozi wa Roma katika nchi ya Bithinia, jimbo la Asia ndogo ya zamani. Plinio alimwandikia mfalme wa Dola ya Roma Trajani (Trajan), akimwambia habari za matukio katika jimbo lake. Tazama, hapa anaomba ushauri juu ya jinsi anavyopaswa kulishughulikia dhehebu jipya, yaani, Wakristo. Anasimulia habari inayohusu kuongezeka kwao haraka sana na jinsi walivyoimba nyimbo za kumsifu Mungu zilizotungwa kwaajili ya kiongozi wao, yaani, Kristo. Pliny aliiuma barua yake karibu na mwaka ule wa 110 B.K. Barua hiyo iliyoandikwa na Pliny inatoa ushahidi wa kihistoria wa yule mwanadamu, Kristo, na juu ya kuenezwa kwa imani yake katika siku zile za mitume wake."

Akiwa ameshangaa, mwanaume yule kijana alisema, "Hebu niambie zaidi!"



Mchungaji alipoendelea kukipekua kitabu kingine, aliongeza kusema hivi, "Mwanahistoria mwingine, aliyeishi kipindi kile kile kimoja na Pliny, alikuwa ni Tacitus. Katika habari zake za miaka zilizotengwa (Analys), kitabu cha 15, sura ya 44, anasimulia habari za uhasama aliokuwa nao Nero na mateso yake dhidi ya Wakristo wakati mji wa Roma ulipochomwa moto. Tacitus anaeleza kwamba neno hilo "Mkristo" linatokana na jina la 'Kristo.' Anataja kwamba Yesu Kristo, mwasisi wa dini ya Kikristo, alikuwa ameuawa na Pontio Pilato wakili wa Yudea, katika kipindi cha utawala wa mfalme wa Dola Tiberio. Maelezo haya yote anayotupa Tacitus yanalandana kabisa na matukio, majina na mahali palipotajwa katika Biblia."

"Mchungaji, mimi sikujua kabisa mambo hayo kuwa yalikuwamo katika historia ya ulimwengu! mgeni yule akasema kwa mshangao.

Mchungaji yule akaongeza kusema hivi, "Nataka uzingatie kwamba karibu na mwaka wa 180 B.K. Celsus aliandika kitabu akiwashambulia Wakristo, akionyesha kwamba kufikia wakati ule Ukristo ulikuwa ni nguvu iliyopaswa kutambuliwa.

"Kama wewe bado una mashaka, basi, kumbuka kwamba vitabu hivyo vinne vya Injili ni historia iliyosawa na ile ya vitabu hivyo vya kidunia."

Yule mwanaume kijana alipotambua kwamba historia zote mbili, yaani, ile takatifu na ile ya kidunia, zinakubaliana kwamba Yesu alipata kuishi hapa duniani kama mwanadamu, alikwenda zake akiwa ameaminu kwamba Yesu Kristo alikuwa mtu halisi wa kihistoria.

1. Kristo Alikuwako Tangu Milele

Yesu hakuwa tu mtu mwema, alikuwa Mungu pia. Je, ni madai gani aliyoyatoa Yesu mwenyewe kuhusu Uungu wake?

"Kama mngalinijua mimi kweli kweli, mngalimjua na Baba. Tangu




GUNDUA

sasa mnajua, tena mmewona.... Ye yote aliyeniona mimi amewona Baba" - Yohana 14: 7-9.

Ukitaka kujua jibu kwa maswali haya, "Mungu ni nani? Anafananaje?" unapaswa kumtazama tu Yesu, aliyetangaza, akasema, "**Mimi na Baba Tu umoja (Yohana 10:30.)**"

Mungu Baba na Yesu mwanawe wamekuokoa pamoja tangu milele (Waebrania 1:8.) Haukuwako wakati wo wote ule ambapo Kristo hakuwa umoja na baba yake. Baba yake anatoa upendo na ulinzi wake ule ule kwa kila mtu kama aliuonyesha Yesu katika kipindi cha maisha yake ya kibinadamu hapo duniani.

2. Kristo, Kiini Cha Historia Na Unabii



Kwa kuwa kisa cha maisha ya Kristo ni utimizo wa unabii, kisa cha maisha yake kiliandikwa kabla yeye hajazaliwa unabii wa Agano la kale huonyesha kwa kifupi kinachoeleweka wazi maisha yake, kifo chake na ufufuo wake kabla hayajatokea. Agano Jipyä ni kisa cha maisha yake kilichoelezwa kama utimilizo wake. Wakiishi kuanzia miaka mia tano hadi elfu moja na mia tano kabla ya kuzaliwa kwake Kristo, manabii wale wa Agano la Kale waliotoa utabiri mwangi wa pekee kuhusu maisha yake Masihi, na tangu mwanzo kabisa wa kazi yake hapo duniani,
Watu walipoyalinganisha maisha yake na unabii wa Agano la Kale walifikia hitimisho gani?
"Tumemuona yeye aliyeandikwa maisha katika torati na ambaye habari zake manabii pia waliziandika Yesu Nazareth Mwana wa Yusufu" _ (Yohana 1:45).

Mwokozi wetu aliwaelekeza watu kwenye unabii uliotimizwa ili kuthibitisha kwamba yeye ndiye:
"Akaanza kutoka Musa na manabii wote, akawaeleza yote yaliyosemwa juu yake katika Maandiko yote [ya Agano la Kale] kumhusu yeye mwenyewe" - (Luka 24:25-27).

Unabii uliotimizwa unatoa ushahidi unaosadikisha kwamba Yesu ndiye yule Masihi aliyeahidiwa.

3. Maisha Ya Kristo Ni Utimilizo Wa Unabii

Hebu na tuviangalie vifungu hivi vichache vyta unabii huo toka katika Agano la Kale - na kutimizwa kwake katika kumbukumbu za Agano Jipyä.

Mahali Pake Alipozaliwa

Unabii wa Agano la Kale: **"Bali wewe BETHELEHEMU Efrata,... kutoka kwako wewe atanitokea mmoja atakayekuwa mtawala katika Israeli, ambaye matokeo yake yamekuwa tangu zamani za kale, tangu milele"** (Mika 5:2).

Kutimizwa kwake katika Agano Jipyä:

"Yesu alizaliwa BETHELEHEMU ya Yudea" - (Mathayo 2:1).

Kuzaliwa Kwake Na Bikira

Unabii wa Agano la Kale: **"BIKIRA atachukua mimba, atazaa mwana, naye atamwita jina lake Imanueli [Mungu pamoja nasi]"**. - Isaya 7:14.

Kutimizwa kwake katika Agano Jipyä:

"Yusufu, mwana wa Daudi, usihofu kumchukua Mariamu nyumbani kwako kama mkeo, maana MIMBA YAKE NI KWA UWEZA WA ROHO MTAKATIFU. Naye atazaa mwana, nawe utampa jina lake Yesu [BWANA huokoa]" - (Mathayo 1:20-23).



GUNDUA

UKOO WAKE WATOKA KATIKA KABILA LA YUDA,... mpaka atakapokuja yeye anayeimiliki" - (Mwanzo 49:10).

Kutimizwa kwake katika Agano Jipy:

"Maana ni dhahiri kwamba BWANA WETU ALITOKA KATIKA YUDA" -(Waibrania 7:14).

Kukataliwa Kwake

Unabii wa Agano la Kale:

"Alidharauliwa na KUKATALIWA na watu" - (Isaya 53:3).

Kutimizwa kwake katika Agano Jipy:

"Alikuwa kwa wale waliokuwa wake, lakini WALIO WAKE HAWAKUMPOKEA" - (Yohana 1:11).



Kusalitiwa Kwake Na Ujira Aliolipwa Msaliti Wake

Unabii wa Agano la Kale:

"MSIRI WANGU niliyemtumaini, aliyeckula chakula changu, ameniinulia kisigino chake" - (Zaburi 41:9).

"Nikawaambia, "Mkiona vema, nipe ni ujira wangu; kama sivyo, msinipe. Basi wakanipimia VIPANDE THELATHINI VYA FEDHA" - (Zakaria 11:12).

Kutimizwa kwake katika Agano Jipy:

"Wakati huo mmoja wa wale kumi na wawili, jina lake Yuda Iskariote - aliwaendea wakuu wa makuhani na kuwaauliza, 'Ni nini mtakachonipa nikimsaliti kwenu? Wakamhesabia VIPANDE THELATHINI VYA FEDHA" - (Mathayo 26:14,15).

Kifo Chake Msalabani

Unabii wa Agano la Kale:

"WAMENIZUA MIKONO na miguu yangu" - (Zaburi 22:16).

Kutimizwa kwake katika Agano Jipy:

"Walipofika mahali paitwapo FUVU la kichwa, WAKAMSULIBISHA pale" - (Luka 23:33. Angalia pia Yohana 20:25).

Kutoka Kwake Kaburini

Unabii wa Agano la Kale:

"Maana hatukuachia kuzimu nafsi yangu, wala hutamtoa

Mtakatifu wako aone uharibifu" - Zaburi 16:10.

Kutimizwa kwake katika Agano Jipy:

"Yeye mwenyewe akitangulia kuyaona haya, alitaja habari za kufufuka kwake Kristo, ya kwamba roho yake HAKUACHWA KUZIMU, wala mwili wake haukuona uharibifu. Mungu amemfufua huyu Yesu, na sisis sote tu mashahidi wake" - (Matendo 2:31,32).

Ushahidi huo una nguvu kuonyesha kwamba Yesu hakutimiza utabiri mchache tu. Maandiko yahusuyo maisha yake kwa kweli yaliandikwa kabla yake kwa njia ipitayo uwezo wa kibinadamu. Kweli, Yesu ni Mwana wa Mungu.



Baada ya kuuangalia ushahidi huo, tunahitaji kufanya uamuzi wetu kwa njia ya maombi kuhusu nani atakayekuwa Bwana katika maisha yetu. Kama wewe bado hujafanya hivyo, je! utayaweka maisha yako mikononi mwake Yesu?

4. Maisha Yaliyopangwa Na Mungu

Yesu aliishi maisha yaliyopangwa na Mungu, ambayo yameelezwa kwa maelezo machache mamia ya miaka kabla ya kuzaliwa kwake. Siku zote akiwa anautambua ukweli huo, alikuwa mwepesi kutambua maongozi ya Mungu. Kristo alisema:

GUNDUA

"Sifanyi neno lo lote kwa nafsi yangu, ila nanena yale tu aliyonifundisha Baba... kwa sababu nafanya siku zote yale yampendezayo" - (Yohana 8:28,29).

Mungu alipanga maisha ya kibinadamu ya Yesu kabla ya kuzaliwa kwake, tena Mungu anao mpango kwa kila mwanadamu pia. Anajua jinsi kila mmoja wetu anavyoweza kutimiza haja zake zenyekina sana na kujipatia maisha tele.



Ray siku zote hakuwa na hakika kabisa iwapo alitaka kuufuata mpango wa Mungu. Lakini alipokabiliwa na uamuzi mkubwa kuhusu wapi alipaswa kwenda kusoma chuoni, basi, kwa mara yake ya kwanza katika maisha yake aliamua kutafuta uongozi wa Mungu katika suala lile. Aliomba kwa siku kadhaa na kujitahidi kusikiliza jibu la aina fulani. Baada ya muda fulani kupita alionekana amepata sababu zilizo wazi sana kwa nini angepaswa kuchagua chuo B: Chuo Kikuu kisicho na gharama kubwa sana, lakini kikubwa na ambacho hakiendeshwi na mtu fulani mahsusisi. Mara tu baada ya kuanza kusoma pale alifahamiana na Wakristo fulani wa ajabu waliokuwa wamejiunga na chama fulani cha kumtetea Kristo katika eneo lile la kile chuo kikuu. Uzoefu wote aliokuwa nao pamoja nao katika kipindi cha miaka miwili iliyofuata uliyabadilisha maisha yake kabisa.

Ray anapoangalia nyuma leo, anaona kwamba kila wakati alipokuwa amekabiliwa na uamuzi mkubwa na kutafuta uongozi wa Mungu, "Mungu alinifunulia uwanja mpya wa maisha yangu."

Je, unawezaje kuujua mpango wa Mungu kwa maisha yako? Mungu anatoa uongozi wake kwa njia kadhaa:

1. Biblia

Kulingana na mtunga Zaburi, je! ni kitabu gani kinachoyaongoza maisha yetu?

"Neno lako ni taa ya miguu yangu, na mwanga wa njia yangu" - (Zaburi 119:105).

Neno la Mungu huifanya upya mioyo yetu na kutupatia maarifa (Warumi 12:2, Zaburi 199:99). Wakati maalum uliopangwa kwa kujifunza Maandiko na kuomba ndiyo njia bora kuliko zote ya kuyaratibu mambo yenye kipaumbele.

2. Maongozi Ya Mungu Katika Mambo Yanayotupata

Mungu anatuongoza pia kwa mambo yaongozwayo na Mungu mwenyewe. Zaburi 23 huonyesha yeye kama mchungaji mwema. Mchungaji

anawaongoza kondoo wake katika mabonde yenye majani mabichi sana na kupitia katika makorongo yenye miamba. Anao uwezo wa kuwasaidia wale anaowapa maagizo yake ili wanufaikie na kujifunza kutokana na kila jambo linalowapata katika maisha yao. Tunaye mchungaji anayeambatana nasi na kukaa karibu sana kando yetu.

3. Mawasiliano Toka Kwa Mungu Ya Moja Kwa Moja hadi Moyoni

Mungu anatuongoza pia kwa njia ya kuzungumza nasi kupitia katika dhamiri zetu. Roho wake anaweza kuyatia nuru "macho ya mioyo yenu" (Waefeso

1:18). Kadiri tunavyozidi kufanya mazoezi ya kuwasiliana na Mungu ndivyo kadiri anavyoweza kutuongoza sisi. Anaziumba upya hisia zetu za ndani na uwezo wetu wa kufikiri na kuamua ili tupate kuiona wazi hatua inayaofuata ambayo tunahitaji kuichukua.

5. Maongozi Hayo Ni Lazima (Yapatane)?

Naam, yawezekana kudhani kwamba wewe unaishi maisha yanayoongozwa na Mungu wakati wewe unafuata tu mielekeo yako na hisia zako mwenye (Mithali 16:25). Hisia zetu ni lazima zipatane na

mafundisho ya Biblia. Si salama kuamua kwamba ni Mungu anayetuongoza isipokuwa kama maongozi yote matatu yanapatana.

Hebu na tumchukue Jake, kwa mfano. Alikuwa na mke wake mzuri sana na watoto wawili, lakini alifanya uzinzi na mwanamke mwininge. Aliwaambia hivi rafiki zake: P "Mimi nimeliombea jambo hilo, nami najua kwamba hayo ni mapenzi ya Mungu."

Hisia za moyoni za Jake na "maono yake ya ndani" kwa dhahiri yalimpeleka katika njia ile mbaya iliyokwenda chini. Yeye aliwaza kwamba yale yalikuwa ni "maongozi ya Mungu" yaliyompelekea kukutana na mwanamke yule mwininge, wala hakurudi nyuma kuziangalia amri za Biblia dhidi ya uzinzi. Na Biblia hiyo, ambayo ni "sheria na ushuhuda," ndicho kitabu cha mwongozo chenyeye mamlaka, ndiye mwamuzi wa mwisho anayeamua njia sahihi ya kufuata katika utendaji wetu (Isaya 8:20). Kamwe tusiruhusu maoni yo yote au jambo lo lote linaloonekana wazi kuwa ni maongozi ya Mungu kutupeleka mbali na kanuni ya Biblia.

6. Kujikabidhi kwa Mpango Wa Mungu

Shetani alipokuja kumjaribu Yesu kule nyikani, alitoa shauri hili, "Kama wewe ukiachilia mbali kujitoa kwako mhanga kunakokuletea maumivu makali, ambako Baba yako amekupangia wewe, mimi nitakupa dunia hii yote iwe mikononi mwako - pamoja na sifa, mali, na maisha ya raha mustarehe." Shetani akanukuu hata Maandiko katika jitihada yake ya kumfanya Yesu apotee. Lakini kila wakati Yesu alipambana naye na kumsukuma nyuma kwa maneno haya, "Imeandikwa" (Mathayo 4:1-11).



Fundisho moja lenye nguvu tuwezalo kujifunza kutokana na maisha yake Yesu ni utii wake kwa mapenzi ya Baba yake. Hata katikati ya maumivu makali ya kutisha ya Gethsemane, yeye akalia, kasema, "Baba yangu, ikiwezekana, kikombe hiki kiniepuke. Walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe" (Mathayo 26:39). Baada ya ile miaka mitatu ya kazi yake, akiishi siku kwa siku kupatana na mpango wa Baba yake, Kristo alipokuwa akifa maneno yake yalikuwa ni haya: "Imekwisha" (Yohana 19:30). Yesu alikuwa akisema maneno haya hasa, "maisha yangu yaliyopangwa na Mungu sasa yamekamilika na kutimilika."

Unapoanza kuisikia Sauti ya Mungu ikisema nawe kulingana na Neno lake, kupitia katika mambo yale yakupatayo yanayoongozwa na Mungu, na kupitia katika mawazo ya moja kwa moja, unaweza kujifunza kuyakubali maongozi yake hayo kwa moyo wako wote. Wewe pia waweza kuigundua furaha ya maisha yaliyopangwa na kuongozwa na Mungu.

DARAJA KWENDA KWENYE MAISHA YANAYORIDHISHA

Waliikuta mifupa yake kando ya kibanda chake cha muda katika kisiwa kisichokuwa na watu katikati ya Atlantiki. Baharia yule asiyejulikana jina lake alitunza kitabu cha mambo ya kila siku kilichoeleza kwa kinagaubaga mateso mabaya aliopata kwa miezi minne. Alikuwa ametelekezwa pwani ya kisiwa cha Ascension na kundi la manowari za Kiholanzi chini ya kamanda mmoja katika mwaka wa 1725 kwa uhalifu wake fulani uliokuwa haujatajwa. Baada ya muda mfupi kupita, akawa akinywa damu ya kasa ili kuituliza kiu yake kali sana. Mateso ya mtu yule kimwili yalikuwa makali sana, lakini maumivu makubwa zaidi yanaonekana wazi katika kitabu chake cha mambo ya kila siku: yaani, ile hatia yake iligomlemea kabisa.



Aliandika maneno yaliyomtesa sana kama haya: "Ni maumivu yaliyoje yanayowapata wanadamu wanaoziacha njia za haki, wakifurahia kuongeza idadi ya watu waliolaaniwa." Kutengwa kabisa kwa baharia yule katika kisiwa kile cha upweke kulitokana na hisia yake ya kutengwa mbali na Mungu. Hilo ndilo jambo ambalo mwishowe lilionekana kwake kuwa halivumiliki.

Wanadamu wamekuwa wakipambana na kutengwa huko miyoni mwao tangu Adamu na Hawa walipo "jificha BWANA Mungu asiwaone kati ya miti ya bustani" baada ya kula lile tunda lililokatazwa (Mwanzo 3:8). Hisia mpya, ngeni, za kuona aibu, hatia, na hofu zikawalazimisha wale watu wawili, mume na mke, kumkimbia Mungu alipokuja na kuwaita. Hisia zile, kwa bahati mbaya, sasa zinafahamika sana kwetu.



Je, ni kitu gani kinachosababisha utengo huo kati yetu na Mungu?
"Lakini maovu yenu yamewafarakisha ninyi na Mungu wenu; dhambi zenu zimeuficha uso wake msiuone" - Isaya 59:2.

Ufa huo mkubwa unaowatenga wenyewe dhambi mbali na Mungu hautokani na Mungu. Mungu hakutimua mbio kumwacha Adamu na Hawa - wao ndio waliomkimbia yeye.

1. Kukidhi Njaa Yetu Iliyojificha

Kabla dhambi haijaiharibu ile picha, Adamu na Hawa waliufurahia urafiki wao wa karibu sana na Muumbaji wao katika makazi yao yale katika ile Bustani nzuri ya Edeni. Kwa bahati mbaya sana, waliukubali ule uongo wa Shetani kuhusu jinsi ambayo wao wangkuwa na hekima kama Mungu, wakakivunja kile kifungo cha imani kilichokuwapo kati yao na Muumbaji wao (Mwanzo 3).

Baada ya kufukuzwa katika ile Bustani ya Edeni, Adamu na Hawa waliona maisha yao yakizidi kuwa magumu sana kule nje. Kuzaa watoto na kuilima ardhi sasa kukawa ni kwa kutokwa na damu, jasho, na machozi. Uhusiano wao wa karibu sana na Mungu ukavunjika, wakajikuta hawana kinga yo yote dhidi ya tamaa zao zisizotoshelezeka na shauku zao ziwaleteazo maumivu makali - yaani, huo upweke uletwao na dhambi.

Tangu Adamu na Hawa walipotenda tendo lao la uasi la kwanza, "wote" (jamii yote ya mwanadamu) wameanguka na kuwa na mwelekeo ule ule mmoja wa dhambi na kukabiliwa na kifo, yaani, hiyo ndiyo adhabu ya mwisho ya dhambi.

"Kwa hiyo, kama vile dhambi ilivyoingia ulimwenguni kupitia kwa mtu mmoja, na mauti kwa njia

ya dhambi hiyo, na hivyo MAUTI IKAWAFIKIA WATU WOTE, kwa sababu WOTE WAMEFANYA DHAMBI" - (Warumi 5:12).



Sisi sote tunaona njaa kubwa moyoni mwetu kwa kile tulichokwisha kukipoteza, yaani, tunakuwa na shauku ya kupata usalama wa aina fulani amba ni Mungu tu awezaye kutupa. Mara kwa mara sisi tunajitahidi kuikidhi hiyo njaa kwa kuwa walevi wa kununua vitu madukani, au kuwa na mbio za wendawazimu za kutaka kupandishwa cheo kazini, au kwa kuizimisha tu hiyo njaa kwa kutumia alkoholi [pombe], madawa ya kulevya au kwa uzinzi.

Lakini hizo shauku zetu zote ni dalili ya upweke wa kutokuwa na Mungu. Wala hakuna tiba isipokuwa kwa kuuonja upendo wake katika maisha yetu.

"Utanijulisha njia ya uzima, mbele za uso wako ziko furaha tele. Na katika mkono wako wa kuumi. Mna neema milele" - (Zaburi 16:11).

Kuridhika kweli kweli huja tu kama ufa ule uliopo kati yetu na Mungu umejengewa daraja, na sisi tunaweza kuvuka ng'ambo na kuingia mbele zake.

2. Kuziba Ufa Wa Dhambi Na Mauti

Wanadamu sio pekee yao tu wafanywao kuwa wakiwa kutokana na dhambi hiyo. Moyo wa Mungu pia uliumia sana siku ile Adamu na Hawa walipomgeuzia migongo yao. Na bado yeye anaendelea kusikitika kuhusu ile huzuni na misiba inayowapata wanadamu. Mungu anatamani sana kukidhi tamaa zetu zilizo jificha na kutuponya majeraha yetu ya kimaadili. Hakuwa ametosheka kuangalia kwa huruma ng'ambo ya ufa ule uanaotenga sisi mbali naye. Mungu akaazimu kujenga daraja kuvuka ufa ule mkubwa wa dhambi na mauti.

"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asiangamie, bali awe na uzima wa milele. Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye" - (Yohana 3:16,17).

Mungu alimtoea Mwanawe, na Yesu alitoa uhai wake kama kafara ya dhambi, akalipa ile adhabu ya mauti yeye mwenyewe. Maisha yake, kifo chake, na ufufuo wake vikafanya uwezekano uwepo wa kuwasamehe na kuwaokoa wenyewe dhambi bila ya kuihafifisha dhambi, kisha akayaonyesha yale malimwengu tabia halisi ya Kristo na Shetani. Daraja lile lililojengwa kwa mwili wa Kristo ulivunjika na kutoka na damu nyingi linawavuta watu na kuwarudisha nyuma kutoka katika mtego wa dhambi. Upendo unavuka ng'ambo ya ufa huo mkubwa, na kuwawezesha kuvuka ng'ambo na kuingia katika uzima wa milele wale wote wanaoikeni imani yao ndani ya Kristo kama Bwana na Mwokozi wao.



3. Mambo Muhimu Saba Ya Kweli Upaswayo Kuyafahamu Kumhusu Yesu

Mambo hayo saba ya kweli si ya kweli kwa mtu mwengine awaye yote aliyepata kuishi hapa:

(1) Yesu Alitoka Mbinguni. Na Kuja Hapa Duniani Je, Yesu alidai kwamba alikuwako kwa muda gani? "Kabla Ibrahimu hajazaliwa ulimwengu huu, na kusema: "Mimi Niko!" Mimi nimekuwako siku zote. Ingawa Yesu alizaliwa na mama wa kibinadamu.

GUNDUA

Akina Dwight L. Moody, Billy Graham wa karne ile ya kumi na tisa, siku moja walisema hivi juu ya kufanyika mwili kwa Yesu, "Kungekuwa ni kujitolea mhanga kukubwa kwa upande wa Yesu kuja hapa na kubembelezwa katika kitanda kidogo cha fedha cha watoto, kulelewa na malaika, na kulishwa kwa kijiko cha dhahabu. Lakini yule Muumbaji wa mbingu na nchi alikuja hapa na kutwaan mwili wa kibinadamu, na kuzaliwa na wazazi maskini katika zizi la ng'ombe katika mazingira yale mabaya kabisa."



Malaika yule alimwambia Yusufu maneno haya wakati ule wa kuzaliwa kwake Yesu:

"Naye [Mariamu] atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana YEYE ATAWAOKOA WATU WAKE KUTOKA KATIKA DHAMBI ZAO" - (Mathayo 1:21).

Yesu, Muumbaji wa ulimwengu (Yohana 1:1-3,14), kwa hiari yake alitaka kuja katika dhambi na mauti.

(2) Yesu Aliishi Maisha Yasiyo na Dhambi

"Yesu, Mwana wa Mungu,... amejaribiwa kwa kila njia sawasawa na sisi - lakini bila kufanya dhambi" (Waebraania 4:14,15).

Mungu alifanya mengi kuliko kule kusema nasi ili kututaka tutoke katika maisha ya dhambi na kuingia katika maisha yale yanayoridhisha. Kwa kuishi kwake hapa kama mwanadamu, Yesu aliyafanya maisha yake yale yasiyo na dhambi kuwa ya kuvutia sana kuliko hubiri lo lote lile ambavyo lingeweza kufanya.

Shetani, adui yake Kristo alipanga mipango yake mibaya katika kipindi chote cha maisha ya Yesu alioishi hapa duniani ili kumshawishi atende dhambi. I kule nyikani Shetani alianzisha mashambulio yake makali mno dhidi ya unyofu wake (Mathayo 4:1-11). Kule Gethsemane kabla ya kusulubiwa kwake, shinikizo la majoribu lilifikia kiwango chake kikubwa kama kile, Yesu alitoa jasho la damu (Luka 22:44).

Lakini Kristo alisimama imara dhidi ya kila kitu alichomtupia Shetani - "lakini bila kufanya dhambi." Kwa kuwa Yesu aliyapitia matatizo yote ya wanadamu na majoribu yao, anaelewa jitihada zetu tunazofanya. Yeye anaweza "kutuhurumia katika udhaifu wetu" (Waebraania 4:15).



Kwa nini ilikuwa ni lazima kwa Yesu kuishi maisha yasiyo na dhambi?

"Mungu alimfanya Yesu, aliyejekuwa hana dhambi, kuwa dhambi kwa ajili yetu; na badala ya maisha yetu ya dhambi, Yesu anatupa sisi maisha yake yasiyo na dhambi, ili tuweze kuwa bila dhambi ndani yake" (2 Wakorintho 5:21, limefanuliwa).

Yesu aliyashinda majoribu na kuishi maisha yasiyo na dhambi ili atupe sisi hayo kwa kubadilishana na maisha yetu ya dhambi ya zamani.

(3) Yesu Alikufa Kuiondoa Dhambi

Je, ni watu wangapi waliofanya dhambi?

"Kwa sababu WOTE wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu." - Warumi 3:23.

Je, adhabu ya dhambi ni nin?

"Kwa maana Mshahara wa dhambi ni MAUTI; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu" - (Warumi 6:23).

Kwa nini Yesu alikuwa?

"Tazama, Mwana-Kondoo wa Mungu, AICHUKUAYE DHAMBI ya ulimwengu!" (Yohana 1:29).

Sisi sote tumefanya dhambi, tena tunakabiliwa na mauti ya milele, lakini

GUNDUA

Yesu alikufa badala yetu. Akafanywa kuwa "dhambi kwa ajili yetu." Yeye alilipa hiyo adhabu ya mauti kwa niaba yetu. Kifo chake ni zawadi (karama), na hiyo "KARAMA [ZAWADI] ya Mungu ni UZIMA WA MILELE katika Kristo Yesu Bwana wetu" (Warumi 6:23).

Yesu aliyatoa maisha yake makamilifu, ya haki, kama zawadi yake ya upendo kwetu. Upendo kama ule unapita karibu ufahamu wote wa wanadamu. Na kwa sababu ya kifo chake sisi" tu[na] AMANI kwa Mungu" (Warumi 5:1).

(4) Yesu Alifufuka Kutoka kwa Wafu

Kifo cha Yesu pale msalabani hakikuwa mwisho wa kisa chake cha ajabu. Naam, yeye asingeendelea kuwa mfu wakati huo huo kuwa Mwokozi wetu.

"Na kama Kristo hakufufuka, basi, imani yenu ni bure; mngalimo katika dhambi zenu. Na hapo wao nao waliolala katika Kristo wamepotea" - (1 Wakorintho 15:17,18).

Muhammad na Budha wameupa ulimwengu huu baadhi ya zile kweli kuu za kifalsafa. Wameyaongoza maisha ya mamilioni ya watu, lakini hawana uwezo wa Mungu wa kuwapa uzima kwa maana wao bado wanaendelea kubaki katika makaburi yao.



Kwa kuwa Yesu alifufuka kutoka kaburini siku ile ya tatu baada ya kifo chake, je, ni ahadi gani awezayo kuitoa kwetu?

"Na kwa sababu mimi ni hai, ninyi nanyi mtakuwa hai" Yohana 14:19.

Yesu yu hai! Kwa kuwa yeye anao uwezo juu ya mauti, anaweza kutuokoa toka mautini na kutupa uzima ule ambaa ni tele, tena ni wa milele. Ataishi ndani ya mioyo yetu kama tukimkaribisha. Kristo yule aliyefufuka yupo ili kukidhi mahitaji yetu leo.

"Na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari" - (Mathayo28:20).

Wanaume na Wanawake ulimwenguni kote wanabdalishana visa vyao juu ya jinsi Kristo alivyowaokoa kutoka katika mazoea yao mabaya sana na hisia nzito sana za moyoni mwao ziwatiazo kiwewe.

Mmojawapo mionganii mwa wanafunzi wetu wa zamani aliandika maneno haya ya shukrani katika mojawapo ya karatasi zake za majibu: "Mimi nilikuwa mlevi sugu. Siku moja nilipokuwa nimelewa, niliiona kadi mferejini ikitangaza kozi yenu ya Biblia. Niliokota, nikajaza kupata ujuzi wangu wa kwanza wa Kristo. Muda mfupi baada ya kuchukua kozi hiyo ya Biblia, nilitoa moyo wangu kwa Mungu na kuipoteza hamu niliyokuwa nayo kwa wiski. 2

Yesu alipoyatawala maisha ya mtu huyo, nguvu mpya ilimpa uwezo wa kuyashinda mazoea yake yale mabaya. Kwa vile Kristo ni Mwokozi aliyefufuka, anaweza kuwaokoa wote watakaomjia yeye kuomba msaada wake.

(5) Yesu alipaa Mbinguni

Kabla Yesu hajarudi kwa Baba yake baada ya ufufuo wake (Matendo 1:9), alitoa ahadi hii kwa wafuasi wake:

"Msifadhaike mioyo mwenu. Mwaminini Mungu; niaminini na mimi pia nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi;... Ninakwenda kule KUWAANDALIA NINYI MAHALI. Nami.. nitakuja tena na kuwachukua mpate kuwa pamoja nami.... pale nilipo mimi" - (Yohana 14:1-3).



GUNDUA

(6) Yesu Anahudumu Kama Kuhani Mkuu

Daima Yesu anajitahidi sana kutuandalia sisi mahali kule mbinguni.

"Ilimpasa kufananishwa na ndugu zake kwa kila njia, ili apate kuwa KUHANI Mkuu mwenye rehema, mwaminifu katika mambo ya Mungu, ili apate kufanya upatanisho kwa dhambi za watu wake. Na kwa kuwa mwenyewe aliteswa alipojaribiwa, aweza kuwasaidia wale wanojaribiwa"
(Waebrania 2:17-18).

Yesu alikuja katika dunia yetu ili "kufanya upatanisho kwa dhambi za watu wake," na kutuokoa sisi kutoka katika janga la kuwa watumwa wa dhambi. Alikufa kutuokoa sisi ili hatimaye apate kukifutilia mbali chanzo cha dhambi, maumivu na mauti kwa kumwangamiza Shetani.

Yesu kama Kuhani wetu Mkuu alifananishwa na ndugu zake kwa kila njia." Na sasa anaonekana daima mbele zake Baba kwa ajili yetu kama mpatanishi wetu. Yesu yule yule aliywabariki watoto, aliyemrudishia heshima yake mwanamke yule aliyekamatwa akizini, na kumsamehe mwizi yule aliyekuwa anakufa pale msalabani, hivi sasa anaendelea kufanya kazi yake kule mbinguni akituhudumia katika mahitaji yetu, ili "kuwasaidia wale wanaojaribiwa."

(7) Yesu Atarudi Tena

Kabla hajarudi mbinguni, Yesu alitoa ahadi gani?

"Nikienda na kuwaandalia mahali, NITAKUJA TENA na kuwachukua kuwa pamaoja nami ili ninyi pia muweze kuwa pale nilipo mimi (Yohana 14:3).

Yesu anaporudi tena, atatuokoa kutoka katika dhambi, magonjwa, misiba, na mauti, mambo ambayo yanaishambulia sayari hii. Naye atatukaribisha katika dunia mpya iliyojaa furaha ya milele na uzima wa milele.

4. Upendo Usiokoma

Hadithi hii inasimuliwa kuhusu ndoa iliyopangwa katika nchi ya Taiwani kati ya U Long na mwanamke kijana aliyeitwa "Ua la Dhahabu." U Long alipolifunua shela la bibi arusi wake baada ya sherehe ile, alishtuka na kuchukizwa. Uso wake ulikuwa na makovu ya ndui.

Baada ya pale, U Long alikuwa akishughulika na mke wake kwa nadra sana kadiri ilivyowezekana.I alijaribu kadri alivyoweza kumfurahisha; alifanya kazi za nyumbani kwa bidii sana, akitumainia kwamba mume wake hatimaye angeweza kumkubali. Lakini ye ye aliendelea kuwa baridi na kutojali kuonyeshwa kule kote kwa upendo wake [mkewe].

Baada ya miaka kumi na miwili ya ndoa yao ile ya kinafiki, U Long alianza kupoteza uwezo wake wa kuona katika macho yake yote mawili. Daktari akamwambia kwamba angekuwa kipofu kabisa kama asingepandikizwa kioo cha macho. Lakini upasuaji ule ulikuwa wa gharama kubwa, tena palikuwa na orodha ndefu ya watu waliokuwa wakingojea upasuaji huo.

Ua la Dhahabu akaanza kufanya kazi kwa masaa marefu jioni akitengeneza kofia za mikedka ili kujipatia fedha za ziada. Siku moja U Long aliambiwa kwamba kioo cha jicho la mtu mmoja kilikuwa kimepatikana baada ya kutokea ajali. Aliharakisha kwenda hospitalini kufanyiwa upasuaji ule.

Baada ya kupona, ye ye kwa shingo upande aliamua kumwona mke wake ili aweze kumshukuru kwa kuzipata fedha zile. Alipokigeuza kichwa cha mkewe kilichoinama chini ili mkewe apate kumtazama, U Long alihema kwa mshangao. Mkewe akamkazia macho yake akiwa na macho yasiyoona, yaliyo tupu, kioo cha macho yale kikiwa kimeondolewa. Akiwa amezidiwa na jazba, akaanguka miguuni pa mkewe na kulia kwa kwikwi. Hapo ndipo ye ye kwa mara yake ya kwanza alipolitaja jina la mkewe kwa kunong'ona, akasema: Ua la Dhahabu.



Yesu anatamani sana kuwa na uhusiano na wale ambao kwa muda mrefu sana wamekuwa hawamjali. Anatamani kwamba hatimaye sisi tuweze kunong'ona kwa kulitaja jina lake kuwa yeye ndiye Mwokozi wetu. Alijitoa kwa hiari yake sio tu kwa kutoa kafara ya macho yake, bali mwili wake mzima ili apate katuonyesha upendo wake usiokwisha. Upendo wake una nguvu nyingi sana kiasi kwamba Kristo "alikuja ulimwenguni awaokoe wenye dhambi" (1 Timotheo 1:15).

Kafara ile kuu aliyotoa Kristo ilijenga daraja linalopita juu ya kutokujali kwetu, linalofunika mfarakan wetu. Je! hivi wewe umegundua

mwenyewe kwamba yeye anataka kukuvuta juu ya ufa huo mkubwa na kukukumbatia mikononi mwake? Je! utaitikia na kuomba ukisema, "Yesu, nakupenda wewe. Asante kwa kafara yako ya ajabu mno. Ingia moyoni mwangu na kuniokoa sasa - uniokoe kabisa, uniokoe kikamilifu, uniokoe milele"?

YESU

ALIKUJA kama Mungu katika mwili wa kibinadamu.

ALIISHI maisha yasiyo na dhambi kwa niaba yetu.

ALIKUFA kwa ajili ya dhambi zetu.

ALIFUFUKA kutuokoa katika mauti.

ALIPAA kwenda kutuandalia makao yetu kule mbinguni.

ANAHUDUMU kila siku kama Kuhani wetu Mkuu.

ANAKUJA UPESI kutuchukua sisi ili tuwe naye milele.

NAFASI YA PILI YA KATIKA MAISHA

Baada ya kuishi karibu maisha yake yote kama mfuasi wa Budha, mtu wa makamo mmoja katika nchi ya Singapore aliyekuwa amegeuka na kuwa Mkristo aliulizwa swali hili, "Bwana Limu, je, wewe unaona tofauti gani kati ya kuwa mfuasi wa Budha na kuwa Mkristo?

"Hilo ni rahisi," alijibu. "Tangu mimi nimempokea Yesu kama Mwokozi wangu, nina amani nyingi ajabu moyoni mwangu."

Hilo ndilo linalotokea tunapoyaweka maisha yetu ndani ya Kristo.

"Wewe [Mungu] utamlinda katika amani kamilifu, yeye ambaye moyo wake umekutegemea, kwa kuwa anakutumaini" - (Isaya 26:3).

Kuishi maisha ya Kikristo huleta amani kamilifu - hisia kamili ya kuwa na usalama na raha.


Wale walioligundua hili wameiona njia pekee ya kupata nafasi ya pili ya kuishi - yaani, kumpata Yesu!

1. Maana Ya Kupotea

Yawezekana kwa mtu aliye hai kimwili kuwa na kile watu wengine wanachokiita kustarehe, na bado akawa amekufa - yaani, amekufa kiroho.

"NANYI MLIKUWA WAFU KATIKA MAKOSA NA DHAMBI ZENU, ambazo mlizoziente zamani kwa kuifuata kawaida ya ulimwengu huu na kwa kumfuata mfalme wa uwezo wa anga roho YULE [MWOVU] ATENDAYE KAZI SASA katika wana wa kuasi" - Waefeso 2:1,2.

Shetani anamwongoza mtu yule aliyekufa kiroho na kushuka naye kuelekea chini ya ngazi ya dhambi na kutotii. Lakini kweli ile ya ajabu ya injili inasema kwamba Mungu anawapenda watu kama hao. Anawapenda wakiwa wamekufa katika dhambi zao, kisha anawapa ukombozi kamili na wa bure [bila gharama] kutoka katika hatari yao.



"Lakini Mungu ni mwenye huruma nyingi. Alitupenda kwa pendo lisilopimika, hata, ingawa tulikuwa tumekufa kwa sababu ya dhambi, alitufanya hai pamoja na Kristo. Kwa neema ya Mungu ninyi mmeokolewa. Kwa kuungana na Kristo Yesu, Mungu alitufufua pamoja naye, tukatawale pamoja naye mbinguni. Ndivyo alivyopenda kuonyesha kwa watu wa nyakati za baadaye ukuu wa neema yake aliyoitujalia kwa ukarimu katika kuungana kwetu na Kristo Yesu" - (Waefeso 2:2-7).

Mungu alitupenda sisi tulipokuwa hatuna cha kupendeka ndani yetu. Neema yake iliweka ndani yetu maisha mapya ndani ya Kristo. Hatuwezi kujibadilia wenyewe, ila Mungu anaweza. Tunapokuja kwake kwa imani na unyenyekevu, anatupa nafasi ya pili ya kuishi kama zawadi inayotolewa bure.

2. Ni Kutoka Katika Nini Tunahitaji Kuokolewa?

(1) Twahitaji kuokolewa kutoka katika dhambi.

"Wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu" - (Warumi 3:23).

Kusema bila kuficha: sisi hatuishi kulingana na kile tunachoja kuwa ni haki. Mzazi akisongwa sana na matatizo hasira yake inaweza kulipuka na kumwumiza kihisia mtoto wake. Mtu fulani anaweza

GUNDUA

kumkasirikia sana dereva mwingine na kuwa karibu sana kusababisha ajali. Mwanafunzi anaweza kuchukia na kusema maneno mabaya kwa kunong'ona dhidi ya mwanafunzi mwingine. Mfanya biashara anaweza kupanga "kusahau" chanzo fulani cha mapato yake wakati wa kutozwa kodi. "Wote wamefanya dhambi", hiyo ndiyo hali ya wanadamu.

Biblia inaelezaje maana ya dhambi?

"Kila lisilo la haki ni dhambi" - (1Yohana 5:17).

Tunahitaji kuokolewa kutoka katika aina zote za tabia zetu mbaya pamoja na misukumo ya ndani inayotushurutisha kufanya mambo fulani mabaya: kama vile, kusema uongo, hasira inayomfanya mtu atukane watu, tamaa mbaya za mwili, uchungu, kutaja machache tu.



"Kila atendaye dhambi afanya uasi kwa kuwa dhambi ni uasi" (1 Yohana 3:4).

Kwa ajili hiyo, sisi tunahitaji kuokolewa kutoka katika dhambi - yaani, kutoka katika uvunjaji amri [kumi] za Mungu.

(2) Twahitaji kuokolewa kutoka katika uhusiano wetu na Mungu ambao ulivunjika.

"Lakini maovu yenu yamewafarikisha ninyi na Mungu wenu; na dhambi zenu zimeuficha uso wake msiuone" - (Isaya 59:2).

Dhambi ile isiyosamehewa inakata uhusiano wetu na Mungu. Kristo alikuja kuturudishia tumaini letu kwa Mungu, ambalo Shetani alikuwa amelidhoofisha.

(3) Twahitaji kuokolewa kutoka katika mauti ya milele. - adhabu ya dhambi [kuvunja amri Kumi].
"Kwa hiyo kama mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti, na kwa hivyo mauti ikawafikia watu wote, kwa sababu wote wamefanya dhambi" - (Warumi 5:12).

(4) Twahitaji kuokolewa kutoka katika maisha yetu ya dhambi yasiyo na furaha, yaliyo tupu.

Kwa mwenye dhambi, maisha ni kama mtaa uliofungwa mwisho wake.

(5) Twahitaji kuokolewa kutoka katika ulimwengu wenye dhambi.

Ni lazima tuokolewe kutoka katika ulimwengu uliojaa dhambi na athari zake - kama vile, umasikini, huzuni kubwa moyoni, upweke vita, magonjwa na kifo!

3. Ni Nani Awezaye Kutuokoa?

Yesu peke yake aweza kutuokoa sisi.

(1) Yesuaweza kutuokoa sisi kutoka dhambini.

"Naye atazaa mwana nave utamwita jina lake Yesu, maana ye ye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao" - (Mathayo 1:21).

Baniani [Mhindu] mmoja alimwambia rafiki yake Mkristo maneno haya, "Mimi napata mambo mengi katika dini hii ya Kihindu ambayo hayapatikani katika Ukristo, lakini kuna kitu kimoja Ukristo ulicho nacho ambacho dini ya Kibani haina - yaani, Mwokozi." Ukristo ndiyo dini pekee katika ulimwengu huu inayowapa watu Mwokozi.

(2) Yesu anaweza kutuokoa kutoka katika uhusiano wetu na Mungu ambao ulivunjika.

"Mlitengwa mbali na Kristo... mlikuwa hamna tumaini, wala hamna Mungu duniani. Lakini sasa

GUNDUA

katika Kristo Yesu ninyi ambao zamani mlikuwa mbali, mmeletwa karibu kwa damu yake Kristo" - (Waefeso 2:12,13).



Yesu ndiye Rafiki mkamilifu ambaye twaweza kufurahia kuwa na uhusiano naye. Yeye anapenda kijitokeze ndani yetu kile kilicho bora sana. "Kwa damu yake Kristo" maisha yetu ya dhambi yaliyopita yanasaamehewa, na siku-kwa-siku yeye anatupa ukubali wake, nguvu za kushinda dhambi, na maisha yake makamilifu. Tunajua kwamba atakuwa pale kutuinua na kila wakati tunapoanguka. Kwa upande wetu upendo wetu kwake unazaa shauku ya kuishi kwa kufuata njia ile impendezayo yeye.

(3) Yesu anaweza kutuokoa sisi kutoka katika ile mauti ya milele, adhabu ya dhambi.

"Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti [ya milele]; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu" - (Warumi 6:23).

Sisi tu wavunjaji wa sheria yake [amri za Kumi], tumehukumiwa kufa. Yesu anatuokoa sisi kutoka katika mauti ya milele, kisha anatupa uzima wake wa milele.

"Mungu auonyesha dhahiri upendo wake kwetu sisi; tulipokuwa tungali wenyewe dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu" - (Warumi 5:8).

Kwa sababu ya upendo wake usio na mwisho, Yesu "alikufa kwa ajili yetu na kupata mateso kamili ya dhambi zetu, Mungu sasa anaweza kuwasamehe na kuwakubali wenyewe dhambi bila kuihafifisha hiyo dhambi.

(4) Yesu anaweza kutuokoa kutoka katika maisha ya dhambi, yasiyokuwa na furaha.

"Hata imekuwa mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipyta - ya kale yamepita, tazama! Yamekuwa mapya"- (2 Wakorintho 5:17, Philips).

Hatuwezi kujiokea wenyewe kutoka katika dhambi au kuigeuza tabia yetu kwa kujitegemea wenyewe kama vile Simba asivyoweza kuamua awe mwana-kondoo (Warumi 7:18). Dhambi ina nguvu nydingi kuliko nia yetu ya kufanya yale tuyatakayo. Lakini Kristo anaweza kukufanya wewe uwe "imara kwa uweza wake, kwa kazi ya Roho wake katika utu [wako] wa ndani" (Waefeso 3:16). Anafanya kazi yake ili kuondoa tabia zetu ziletazo uharibifu na mahali pake kuweka tabia hizi nzuri: upendo, amani, furaha, upole, uwezo wa kujitawala (Wagalatia 5:22,23). Kristo anaishi maisha yake kuitia ndani yetu, kisha tunapokea uponyaji wa kiroho, tunarejeshwa katika maisha mapya, na kuwezeshwa kuishi maisha hayo mapya.

Harold Hughes alikuwa amepoteza tumaini lake kabisa la kuweza kubadilika kwa wakati uwao wote ule. Alikuwa amejitahidi sana kuacha kunywa pombe mara nydingi sana. Alijua fika kwamba vita yake dhidi ya chupa ya pombe ilikuwa imewaletea maisha ya jehanamu mke wake na binti zake wawili kwa miaka kumi kamili. Basi asubuhi moja yenye baridi kali akaingia katika bafu lake na kuuelekeza mtutu wa bunduki yake kinywani mwake. Kabla hajafyatua risasi, aliamua kwamba ingekuwa heri kwake kumweleza Mungu mambo yake yalivyokuwa. Sala yake ile ikageuka na kumfanya alielewa kwikwi kwa muda mrefu akimsihi amsaidie.

Mungu akamjibu. Harold Hughes akajitoa kabisa kwa Kristo na kupata nguvu za kiroho kumwezesha kulishikilia lile tumaini lake la kubadilika.



GUNDUA

Aliacha kabisa kunywa pombe, akawa mume na baba mwenye mapenzi na wa kutegemewa, kisha akasonga mbele na kujipatia kiti katika Seneti [sehemu ya Bunge] la Marekani. Harold Hughes aligundua uwezo mkubwa kabisa unaoyabadilisha maisha ya watu katika dunia hii - yaani, Yesu!

(5) Yesu anaweza kutuokoa kutoka katika dunia hii ya dhambi.
Miongozo minne ya GUNDUA ifuatayo itaeleza jinsi jambo hilo linavyoweza kufanyika.

4. Tunaokolewa Kwa Kuchukua Hatua Rahisi Tatu

Hatua ya 1. mwombe Kristo aingie na kuishughulikia dhambi katika maisha yako.
Je, sisi tunayo sehemu gani ya kufanya ili kuondokana na maisha yetu haya ya dhambi?

TUBUNI, basi na kumgeukia Mungu, ili dhambi zenu zipate kufutwa kabisa"
- (Matendo 2:38).

Ni kitu gani kinachomwongoza mtu kutubu?
"WEMA WA MUNGU WAKUVUTA WEWE UPDATE KUTUBU" - (Warumi 2:4).
"Huzuni Yenu Iliwaongoza Hata Mkatubu" - (2 Wakorintho 7:9).

Toba ni kuhuzunika tu kwa ajili ya maisha yetu ya dhambi yaliyopita, kisha kugeuka na kwenda mbali na dhambi zetu, tukizikomesha tabia zetu mbaya za zamani, pamoja na mazoea yetu, na mtazamo wetu. Hivyo si huzuni kwa sababu sisi tunaogopa tu ile adhabu, bali ni mwitikio wetu kwa ule "wema wa Mungu" uliomfanya Yesu kufa badala yetu kwa ajili ya dhambi zetu. Tunaikataa dhambi kwa sababu inamwumiza Mungu.

Tunapoyaonja maisha mapya ndani ya Kristo, tungeyasahihisha makosa yetu tuliyofanya zamani kwa kadiri iwezekanavyo (Ezekieli 33:14-16).

Je, sehemu ya Mungu ni ipi katika katuondolea maisha yetu yenye dhambi ya zamani?

Mambo yote mawili, toba na msamaha, ni vipawa vitokavyo kwa Mungu.
"Mungu amemtukuza kwa kumweka mkono wake wa kulia, awe mkuu na Mwokozi ili apate KUWAPA TOBA na MSAMAHWA WA DHAMBI" - (Matendo 5:31).

Nasi tunapotubu, Mwokozi huyo mwenye upendo anatusamehe dhambi zetu, anatusafisha dhambi zetu, na kuzitupa katika vilindi vya bahari.

"TUKIZIUNGAMA dhambi zetu, YEYE NI MWAMINIFU na wa haki, NAYE ATATUSAMEHE dhambi zetu na KUTUSAFISHA na udhalimu wote" - (1 Yohana 1:9. Angalia pia Mika 7:18,19).

Hakuna dhambi ambayo ni ya kutisha sana asiyoweza kuisamehe Mwokozi wetu aliyekufa kwa sababu ya hizo dhambi zetu juu ya msalaba ule wa Kalvari. Mtu yule anayemtumainia Yesu anahitaji tu kumwomba yeeye ili ampe msamaha wake. Kufa kwake Kristo kwa ajili yetu hakuwezi kutupatia sisi msamaha mpaka tuombe kusamehewa. Ni ukweli ulio na busara ndani yake ya kwamba dhambi zetu zilichangia katika kuipigilia ile misumari na kutoboa viganja na nyayo zake Kristo. Na, hata hivyo, Yesu anayo shauku nyingi sana kuliko vile tuwezavyo kuwaza ili tupate kukipokea kipawa chake cha msamaha na upatanisho.

Habari zilimfikia kijana mmoja mwanaume aliyejikuwa ametoroka nyumbani kwao kwamba mama yake alikuwa akifa. Habari zile zikamjaza majuto mengi kuhusu uhusiano wao uliokuwa umevunjika. Akaharakisha kwenda nyumbani, akaingia haraka katika chumba kile na



kujitupa juu ya kitanda cha mama yake. Machozi yakiwa yanabubujika akamsihi amsamehe.

Akamvuta karibu na kunong'ona, "Mwanangu, ningekuwa nimekusamehe zamani sana endapo ungekuwa tu umeniomba mimi."

"Kama wewe umetanga mbali na Mungu - au bado hujamjua - tafadhalii fikiria jinsi Baba yako, akupendaye, aliye mbinguni alivyo na shauku kubwa kukukaribisha nyumbani kwake. Zaidi ya kitu kinginecho chote yeze anataka wewe upokee msamaha wake anaokupa. Yesu anakupenda wewe. Alikufa kwa ajili yako. Siku zote yu tayari kukusamehe wewe. Basi itikia mwaliko wake wa neema unaokutaka utubu. Ungama dhambi zako. Amini naye anafanya hivyo. Mtumainie yeze! Tegemea ahadi zake.

Hatua ya 2. pokea maisha mapya toka kwa Yesu.

Sehemu yako katika kupokea maisha mapya toka kwa Yesu ni kuamini kwamba Yesu amekuokoa kweli kweli. Kubali bila swali ukweli kwamba yeze amekusamehe na kukusafisha, ameyaondoa maisha yako ya dhambi ya zamani, na kukupa wewe maisha mapya kabisa yaliobadilika.

"Bali wote... waliompokea, aliwapa uwemo wa kufanyika watoto wa Mungu" - (Yohana 1:12).

Wewe kama mtoto wa Mungu, unayo "haki" ya kupokea hayo maisha mapya kutoka kwa Yesu. Kama tulivyokwisha kusema, wewe huwezi kuiptaa hiyo kwa kujitegemea mwenyewe - ni zawadi toka kwa baba yako aliye mbinguni! Yesu anatoa ahadi kama hiyo iliyo ya kweli ili kutuondolea wasi wasi na mashaka yetu.

Je, sehemu ya Mungu ni ipi katika kutupa sisi maisha hayo mapya?

"Yesu akamwambia, Amini, amini nakuambia, hakuna mtu awezaye kuuona ufalme wa Mungu asipozaliwa mara ya pili" - (Yohana 3:3).

Kulingana na Yesu, mwenye dhambi aaminiye na kutubu, anazaliwa kabisa na kuwa na maisha mapya. Ni mwujiza amba ni Mungu peke yake auezaye kuufanya. Yeye anaahidi hivi:

"Nami nitawapa ninyi MOYO MPYA, nami nitatia ROHO MPYA ndani yenu; nami nitatoa moyo wa jiwe uliomo ndani yenu, nami nitawapa moyo wa nyama" - (Ezekiel 36:26).

Yesu anaubadilisha moyo wetu - yaani, hisia zetu pamoja na tabia zetu - kisha anakaa "ndani yetu" (Wakolosai 1:27). Maisha hayo mapya si wazo moja tu lililo zuri la kiroho; ni ukweli ulio mkakamavu na imara, ni ufufuo kutoka katika kifo cha kiroho kwenda katika maisha hayo mapya kabisa na uzima.

Hatua ya 3. Uishi kwa ajili ya Kristo kila siku.

Maisha ya Kikristo yanamaanisha kugeuka kila siku kutoka katika kujipenda wenyewe na kuingia katika kifungo na Yesu atupendaye. Tunakua katika maisha hayo mapya kwa kuuimarisha uhusiano wetu na Yesu. Hii ina maana kwamba wakati wetu bora tuutumie pamoja naye, tukijenga mawasiliyanu ya kweli na yaliyo wazi. Mungu ametupa sisi misaada mitano kwa ajili ya kukua kwetu kiroho: Kujifunza Biblia, maombi, kutafakari, kuwa na ushirika pamoja na Wakristo wengine, na kubadilishana uzoefu wetu wa maisha na wengine.

Kuishi ndani ya Kristo hakuna maana kwamba hatuvezi kamwe kufanya makosa. Lakini tunapojikwaa na kutenda dhambi, tunadai msamaha wake Kristo, kisha tunasonga mbele. Tuanaelekea upande fulani, tena tunajua kwamba Kristo, anaendelea kuishi ndani ya mioyo yetu.

Jinsi Tupokeavyo Maisha Mapya Toka Kwa Kristo

1. Tunamwamini yeze na kumpokea kama Mwokozi na Bwana wetu.
2. Tunajenga uhusiano wetu pamoja nao. (kuwa na muda fulani kila siku wa maombi na kusoma Biblia ni jambo la muhimu sana.)
3. Kristo hufanya kazi yake kwa njia ya Roho wake Mtakatifu ili kuziondoa tabia zetu mbaya na kuziweka tabia zake nzuri mahali pake.

5. Furaha Ya Kupewa Nafasi Hiyo Ya Pili

Harold Hughes alipewa vyeo vingi katika kazi yake maarufu kama seneta wa Marekani, lakini kimoja cha maana sana kwake kilikuja muda mfupi tu baada ya kujitoa kwake kwa Kristo.

Jioni moja Harold alikuwa akijifunza Biblia yake akiwa peke yake katika sebule yake alipoguswa na kiwiko kwenye kiwiko chake. Akaangalia juu. Walikuwa ni wale binti zake wadogo wawili, wakiwa wamesimama kimya katika magauni yao ya kulalia usiku. Akawakazia macho kwa dakika moja hivi; walikuwa wamebadilika sana, naye alikuwa amekosa mengi wakati ule alipokuwa akipambana vita dhidi ya chupa ya pombe iliyokuwa ikimletea uharibifu.

Hapo ndipo Carol, mdogo zaidi, aliposema, "baba, tumekuja kukubusu na kukutakia usiku mwema."



Macho ya yule baba yakaingiwa na kiwi muda mrefu mno ulikuwa umepita tangu watoto wale walipokuja kwake na kukumbatiwa naye. Sasa yale macho yao mazuri na maangavu hayakuwa na hofu yo yote. Hatimaye baba yao alikuwa amekuja nyumbani.

Yesu anawapa watu wake nafasi ya pili kweli. Anawachukua wale walio wabaya kupindukia na kuwapa mianzo mipya.

Mwokozi anatamani sana kwamba kila mmoja wetu hatimaye arudi nyumbani. Je, umeukubali huo mwaliko wa upendo wa Kristo anaotoa kwako? Kupokea msamaha na utakaso wa Mungu ni jambo rahisi na la maana sana kama kuinyosha mikono yako na kumkumbatia mtoto ndogo.

Iwapo wewe bado hujamtumainia Kristo kama Mwokozi wako binafsi, basi, unaweza kufanya hivyo sasa hivi kwa kutoa ombi kama hili:

"Baba, nasikitika kwa ajili ya maisha yangu ya dhambi ya zamani. Asante kwa kumtuma Mwanao katika dunia hii kuja kufa badala yangu mimi. Yesu, tafadahli nisamehe dhambi zangu na kuingia katika maisha yangu na kuniokoa. Nataka nipewe nafasi ya pili ya kuishi maisha yangu - nataka kuzaliwa mara ya pili. Naam, zaidi sana, nataka kujenga uhusiano wangu siku-kwa-siku pamoja nawe. Asante kwa kunifanyia mwujiza huo ndani yangu. Katika jina la Yesu, Amina."

Fanya ugunduzi huu wa ajabu: sisi tunapokuja kwake, Yesu hufanya kazi yake ya kutuokoa.

KUHUSU MAMBO YAKO YA BAADAYE

Madaktari Patricia na David Mrazek walikuwa wamelemewa na huzuni kubwa sana katika kazi yao. Kama mabingwa wa magonjwa ya watoto, waliwashughulikia watoto wengi waliokuwa wakiumwa. Lakini waligundua ukweli kwamba baadhi ya watoto walitoka katika hatari yao ya kufisha na kupata nguvu mpya, ambapo wengine waliangamizwa nayo. Kwa nini? Mathalani, kwa nini mtoto mmoja atumie madawa ya kulevyta wakati yule mwingine anakwenda kusoma chuoni? Kwa nini baadhi ya watoto waliotendewa vibaya wanakua na kujitendea vibaya wenyewe, wakati wengine wanakuwa wazazi wazuri?

Akina Mrazek hao walifanya utafiti wao mpana sana ili kupata majibu kwa maswali hayo. Katika uchunguzi wao tabia moja iliyozidi zote ilizidi kujitokeza mionganii mwa watoto wale walionusurika kutoka katika kiwewe chao na kuendelea kuwa na maisha "ulikuwa ni ule mtazamo wa maisha uliojengwa juu ya mwelekeo wa kutazamia kuyaona mambo mazuri siku za mbele na kuwa na matumaini."

Kuwa na tumaini kulileta tofauti ile. Tumaini, kuliko kitu kinginecho chote, linatusaidia sisi kuyashinda mambo ya ajabu-ajabu yanapokuja kwa wingi sana dhidi yetu.

Wanadamu wanalihitaji tumaini sana. Lakini, je! tunalipataje? Tumaini katika ulimwengu wetu huu ni vigumu kuliona - MPAKA tuliangalie kwa mtazamo wa unabii wa biblia. Mwongozo huu wa GUNDUA unauchunguza unabii ule wa maana sana uliowatia tumaini lenye nguvu watu wengi wasio na idadi.

1. Unabii wa Biblia Unaoshangaza

Karibu miaka mia tano hivi kabla ya kuzaliwa kwake Kristo, Mungu aliupa ulimwengu huu mtazamo wa haraka wa mambo ya mbele unaoshangaza sana kuititia kwa nabii Danieli. Mungu alitoa muhtasari wa historia ya ulimwengu huu miaka 2,500 kabla ya kutokea, kuanzia wakati ule wa Danieli mpaka siku zetu hizi.

Unabii huo ulianzia katika ndoto ambayo Mungu alimpa Nebukadreza, Mfalme wa Babeli, yapata mika 2,500 hivi iliyopita. Ndoto ile ilimsumbuwa sana mfalme yule - lakini hakuweza kuikumbuka ndoto ile alipoamka kutoka usingizini! Baada ya wenge hekima wote wa Babeli kushindwa kumsaidia mfalme yule kuikumbuka ndoto yake au kufasiri, kijana mmoja Mwebrania, aliyekuwa kule uhamishoni, kwa jina Danieli, alijitokeza kwenye mandhari ile, akidai kwamba Mungu wa Mbinguni alikuwa na uwezo wa kuzifunua siri zote.



Akiwa amesimama mbele ya mfalme yule, akanena kwa ujasiri, akasema "**Wewe, Ee, mfalme, ultazama, na pale mbele yako ilisimama SANAMU KUBWA** - sanamu kubwa sana, inayong'aa. "Kichwa cha sanamu ile kilitengenezwa kwa dhahabu safi, kifua na mikono yake ni ya fedha, tumbo lake na mapaja yake ni ya shaba nyekundu, miguu yake ni ya chuma, na nyayo zake nusu za chuma na nusu za udongo wa mfinyanzi uliochomwa. "Ulipokuwa ukiangalia, jiwe ilichongwa, lakini si kwa mikono ya wanadamu. Likai piga ile sanamu katika nyayo zake za chuma na udongo na kuivunja vipande vipande. "Ndipo kile chuma, na ule udongo, na ile shaba nyekundu, na ile fedha, na ile dhahabu, vikavunjwa vipande vipande wakati ule ule na kuwa kama makapi juu ya sakafu ya kupepetea wakati wa kiangazi. Upopo ukavipeperusha mbali bila kuacha kitu cho chote mahali pake. Lakini ULE MWAMBA ULIOIGONGA SANAMU ILEukawa mlima mkubwa, UKAIJAZA DUNIA YOTE" - (Danieli 2:31-35).

GUNDUA

Sanamu hiyo, kwa kuitupia jicho mara moja, yaweza kuonekana kana kwamba haina kazi sana kuweza kutupatia sisi tumaini katika nyakati hizi tunazoishi, lakini wewe endelea tu kusoma habari zake.

2. Unabii Watafsiriwa

Baada ya kumsimulia Nebukadreza aliyejewa amevutiwa sana na kile alichokuwa amekiona hasa katika maono yake, nabii Danieli alitoa ufafanuzi wake:

"Hii ndiyo ile ndoto, na sasa tutaifasiri kwa mfalme" - (Danieli 2:36).

KICHWA CHA DHAHABU: Je, ni mamlaka gani ya dunia ambayo Danieli alimwambia yule mfalme kuwa ilionyeshwa kwa mfano wa kichwa cha dhahabu?

"Wewe, Ee mfalme, u mfalme wa wafalme. Mungu wa mbinguni amekupa wewe ufalme na uwe, na nguvu, na utukufu.... WEWE U KICHWA KILE CHA DHAHABU" - mafungu ya 37,38).

Danieli alikuwa anampasha habari hizi mtawala yule wa dola kubwa kuliko zote ulimwenguni: "Nebukadreza, Mungu anakuambia wewe kwamba dola yako, Babeli, imewakilishwa na kichwa hicho cha dhahabu cha hiyo sanamu."



KIFUA NA MIKONO YA FEDHA. Kwa mtazamo wa kibinadamu Babeli ilionekana kama dola ambayo ingeweza kudumu milele. Lakini, je, unabii unasema kitu gani kitatokea baada yake?

"Baada yako, utainuka ufalme ulio mdogo kuliko wako" fungu la 39.



Kwa kutimiza utabiri huo wa Mungu, ufalme ule wa Nebukadreza ulivunjika vipande vipande na kuwa magofu wakati yule Koreshi, Jemedari wa Kiajemi, alipoiangusha dola ile ya Babeli mwaka ule wa 539 K.K. kwa hiyo, kifua na mikono ya fedha huwakilisha Uamedi na Uajemi, dola nyingine yenye nguvu nyingi.



TUMBO NA MAPAJA YA SHABA NYEKUNDU: Sehemu hii ya sanamu ile kubwa ya madini huwakilisha nini?

"Halafu, ufalme wa tatu, ufalme wa shaba nyekundu, utatawala juu ya ulimwengu nzima." - (fungu la 39).

Tumbo na mapaja ya shaba nyekundu ni mfano wa ufalme wa Uyunani (Ugiriki). Iskanda mkuu (Alexander the Great) aliwashinda Waamedi na Waajemi, na kuingiza Uyunani kuwa dola kuu ya tatu ya ulimwengu . ilitawala kuanzia mwaka wa 331 hadi mwaka 168 K.K.



MIGUU YA CHUMA:

"Hatimaye, patakuwa na ufalme wa nne [alisema yule nabii], wenyewe nguvu kama chuma - kwa maana chuma huvunja vitu vyote na kukishinda kila kitu - na kama chuma kisetavyo vitu hivi vyote, ndivyo utakavyovunja-vunja na kuseta zile nyingine zote." - (fungu la 40).

Baada ya kifo chake Iskanda, dola yake ilidhoofika na kugawanyika katika makundi yanayoshindana mpaka hatimaye katika mwaka ule wa 168 K.K, "Dola ya Chuma" ya Roma ikaishinda Uyunani katika vita ya Pydna.

Kaisari Augusto alitawala katika ile Dola ya Roma wakati alipozaliwa Yesu mnamo miaka elfu mbili iliopita (Luka 2:1). Kristo na mitume wake waliishi katika kipindi kile kilichowakilishwa na miguu ya chuma. Giboni, mwanahistoria wa karne ile ya kumi na nane, bila shaka mawazoni mwake alikuwa na unabii wa Danieli, alipoandika maneno haya: "Zile sanamu za dhahabu, au

fedha, au shaba, ambazo zingetumika kuyawakilisha mataifa na wafalme wao, zilivunjwa na kurithiwa na ufalme ule wa chuma wa Roma" - Edward Gibbon, The History of the Decline and Fall of the Roman Empire (John D. Morris and Company), gombo la 4, uk. 89.

Hebu kwa dakika moja tafakari juu ya utabiri huo kwa mtazamo wa kibinadamu. Je, kwa vipi Danieli, aliyeishi katika kipindi kile cha Babeli, angekuwa na wazo lo lote kuhusu dola ngapi zingefuatana moja baada ya nyingine mamia ya miaka katika siku zile za mbele. Sisi tunakuwa na wakati mgumu kukisia soko la biashara litakuwaje juma lijalo! Na, hata hivyo, Babeli, Umedi-Uajemi, Uyunani, na Roma zilifuatana kabisa moja baada ya nyingine, kama vile ilivyotabiriwa - kama watoto wa shule watifi ambao wamesimama katika mstari.

Je, Mungu anayadhibiti mambo yale ya baadaye? Je, tunaweza kuwa na tumaini kwa kutegemea msingi wa mpango wake ule mkuu? Jibu lake ni "Ndiyo!" ivumayo kote.

NYAYO NA VIDOLE VILIVYOCHEANGANYIKA CHUMA NA UDONGO:

Je! kuna dola ya tano ya ulimwengu mzima ambayo ingefuata baada ya Roma?

"Na kama vile ulivyozunga nyayo na vidole vyake kuwa vilikuwa nusu udongo na nusu chuma, hivyo HUO UTAKUWA NI UFALME ULIOGAWANYIKA; hata hivyo, utakuwa na nguvu kiasi fulani za chuma ndani yake, kama vile ulivyoona kile chuma kimechanganyika na udongo wa mfinyanzi. Na chuma na nusu udongo, kadhalika ufalme ule utakuwa nusu yake una nguvu na nusu yake umevunjika" - (Danieli 2:41,42).



Nabii huyo alitabiri, sio juu ya dola ya tano ya ulimwengu mzima, bali juu ya mgawanyiko wa ufalme ule wa chuma wa Roma. Roma ingevunjika katika falme kumi, kama ilivyowakilishwa na nyayo na vidole vya ile sanamu.

Je, jambo hilo lilitokea kweli? Hakika lilitokea. Katika kipindi cha karne ile ya nne na ya tano ya kipindi kile cha Kikristo washambuliaji wa kishenzi (wasiostaarabika) kutoka kaskazini walimiminika kushuka chini kuja katika Dola ya Kiroma iliyokuwa inazidi kupungua nguvu zake, wakaipiga kipigo baada ya kipigo. Hatimaye kumi mionganoni mwa makabila yale yakajipatia sehemu kubwa ya Roma ya Magharibi, na mataifa kumi tofauti yanayojitawala yenye yakaaji marisha katika mipaka ile ya Ulaya. Hivyo vidole vile leo vinayawakilishwa mataifa ya siku hizi ya Ulaya.

Vidole Kumi - Makabila Makuu Kumi Katika Dola Ya Roma Ya Magharibi
Anglo - Saxons Uingereza

Franks Ufaransa

Alemanni Ujerumanı

Lombards Italia

Ostrogoths Wagothi wa Mashariki waliangamizwa baadaye

Visigoths Wagothi wa Magharibi au Hispania

Burugundians Uswis - Switzerland

Vandals Wavandali - Afrika Kaskazini,

waliangamizwa baadaye

Suevi Ureno

Heruli Waharuli - walitoweka baada ya karne chache tu

4. Mtazamo katika Wakati Ujao

Sehemu moja tu ya unabii wa Danieli bado hajatimizwa. Jiwe lile, je! linamaanisha nini ambalo linaipiga ile sanamu nyayoni, na kuisaga tikitiki, kasha ligeuka na kuwa mlima mkubwa unaoijaza dunia nzima?

GUNDUA

"KATIKA SIKU ZA WAFALME HAO [mataifa ya siku hizi ya Ulaya (Magharibi)]. MUNGU WA MBINGUNI ATAUSIMAMISHA UFALME ambao hautaangamizwa kamwe, wala watu wengine hawataachiwa. Utazivunja falme hizo zote vipande vipande na kuzikomesha, lakini WENYEWE UTADUMU MILELE NA MILELE" - (Danieli 2:44).

"Wafalme hao" huwahusu tu wafalme wale waliowakilishwa na nyayo na vidole vya sanamu ile - yaani, watawala wa Ulaya (Magharibi) ya leo, huzionyesha siku zetu. Jiwe lile lililochongwa bila kutumia mikono ya kibinadamu litaipiga hiyo sanamu na kuivunja vipande, kisha litajaza dunia nzima (mafunku ya 34, 35, 45). Yesu atashuka hivi karibuni kutoka mbinguni kuja ku "usimamisha ufalme," huo, yaani, ufalme wake ulioja furaha na amani. Hapo ndipo Kristo, Mwamba wa Kale na mfalme wa wafalme, atakapoitwaa dunia hii milele hata milele!

Kila kitu katika utabiri wa Danieli 2 kimetimia isipokuwa lile tendo la mwisho yaani, kupigwa kwa sanamu hiyo na lile jiwe. Kulingana na ratiba ya Mungu, hivi sasa tunakikaribia kilele kile kikuu, yaani, kurudi kwake Kristo katika dunia yetu. Yesu Kristo, Mwana wa Mungu yu karibu sana kulikomesha hilo pambano la umwagaji wa damu la muda mrefu katika historia ya kibinadamu na kusimamisha ufalme wake wa milele wa upendo na neema.

5. Ndoto Ya Mfalme Na Wewe

Unabii huu hudhihirisha mkono wa Mungu uongozi katika kuinuka na kuanguka kwa mataifa. Mungu anajua yaliyopita, na huo unabii wa Biblia huonyesha wazi kwamba yeze anajua mambo ya baadaye pia.

Kama Mungu anaongoza nyendo za mataifa kwa usahihi mkamilifu kama huo, basi, ni hakika kwamba anaweza kuyaongoza maisha ya kila mtu mmoja mmoja. Yesu alituhakikishia sisi kwamba: "Hata nywele za vichwa vyenu zimehesabiwa zote. Msiogope basi" (Mathayo 10:30-31). Zawadi ya Mungu ya imani inaweza kuwa dawa ya kupunguza wasi wasi na hofu zetu zote. Tumaini analoliamsa ndani yetu linaweza kuwa nanga ya roho zetu (Waebirania 6:19).



Erasmo, mtaalam wa Biblia wa karne ya kumi na sita, alisimulia habari za tukio moja lililotokea wakati wa safari yake baharini, ambayo ilichukua maisha yake yote. Chombo alichokuwa anasafiria kilipwelea wakati wa dhoruba. Mawimbi yenye nguvu yakakipiga, kikaanza kupasuka, hata mabaharia walianza kuingwi na hofu kuu. Abiria walikuwa karibu kupagawa.

Wengi sana walipiga makele wakiomba msaada toka kwa mtakatifu wao mlezi, waliimba nyimbo za kumsifu Mungu, au walimsihi sana Mungu kwa sauti kuu katika sala zao.



Walakini, Erasmo alimgundua abiria mmoja aliyejikuwa tofauti. "Miongoni mwetu sisi sote, "aliandika Erasmo, "yule aliyebak ikiwa ametulia karibu kabisa alikuwa ni mwanamke mmoja kijana aliyejikuwa amempakata mtoto wake mchanga aliyejikuwa akiendelea kumnyonyesha. Yeye peke yake ndiye hakupiga makelele, hakulia, wala kujaribu kupatana na mbingu. Hakufanya kitu kingine cho chote, bali aliomba kimya kimya moyoni mwake huku akiendelea kumshikilia sana mtoto wake yule mchanga kwenye paja lake."

Saa ile, Erasmo alitambua, ilikuwa ni kuendelea na maisha yake ya sala ya kila siku. Alionekana kana kwamba amejikabidhi mwenye kwa Mungu.

GUNDUA

Meli ile ilipoanza kuzama, mama yule kijana aliweka juu ya ubao, na kupewa mhimili wa kutumia kama kasia kisha akaachiwa apate kukabiliana na yale mawimbi. Akalazimika kumshika mtoto wake kwa mkono mmoja na kujaribu kupiga kasia kwa mkono ule mwininge. Ni wachache mno waliodhani kwamba atanusurika katika mawimbi yale yaliyokuwa yameumuka.

Lakini imani yake na ule utulivu wake ulimweka katika hali nzuri. Yule mwanamke na mtoto wake walikuwa wa kwanza kufika pwani.

Tumaini kwa Mungu aliye mwaminifu linaweza kuleta tofauti kubwa sana - hata dunia yetu hii inapoonekana kana kwamba inapasuka pande zote kutuzunguka. Sisi hatuko kule nje kupiga kasia kwa kujitegemea wenyewe. Mkono mkubwa zaidi unatuongoza na kutushika.

Ukija kwa Kristo kwa kujitoa kwake kabisa, atakupa imani ambayo itakupitisha salama katika kila dhoruba. Gundua amani hii ipitayo ufahamu wote ambayo Yesu anakuahidi kukupa:

"Amani nawachieni, amani yangu nawapa..... Msifadhaike miyoni mwenu, wala msiwe na woga" - (Yohana 14:27.

Jel! unayo amani hiyo? Kama unayo, basi, mshukuru Yesu, Mwokozi wako. Kama hunayo, kwa nini usimkaribishe katika maisha yako leo hii?



YESU AJAPO KWA AJILI YAKO

Baada ya miaka mingi ya kutendewa vibaya, Armando Balladares alikuwa amekonda vibaya sana na kulemaa akiwa kama kinyago tu cha vile alivyokuwa mara ya kwanza. Alikuwa amevutiwa sana na imani yake iliyomletea mateso. Muda mfupi baada ya watu wale wawili kuoana katika sherehe ya kuwafungisha ndoa yao iliyoendeshwa kiserikali katika uwanja wa gereza lile, Martha alilazimka kuhamia Miami.

Kutengana kwao kulileta uchungu mwangi sana. Lakini Armando alifanikiwa kutuma kwa siri ahadi yake kwenda kwa mpenzi wake. Juu ya kipande cha karatasi kilichotupwa aliiandika ahadi yake hii:

"Nitakuja kwako. Singe hizo zilizo katika upeo wa mgongo wangu hazitakuwa na maana tena."

Mfungwa huyo alidhamiria kwamba kwa njia fulani yeye na Martha wangetoa ahadi zao ndani ya kanisa mbele za Mungu. Siku moja muungano wao ungekamilika. "Wewe u pamoja nami daima" alimwambia mwanamke yule.

Ahadi aliyotoa Armando ilimfanya aendelee kuishi katika miaka aliyatendewa vibaya sana ambayo ingekuwa imeivunja miyo ya wanaume wengi. Nayo ilimfanya Martha aendelee kuishi. Alifanya kazi bila kuchoka ili kuyaamsha mawazo ya umma yapate kutambua hali mbaya iliyomkabili mumewe. Yeye hakukata tamaa kamwe.

1. Ahadi

Kuna nyakati fulani sisi tunaweza kujaribiwa na kushangaa, je! hivi kweli siku moja Kristo atashuka na kuja tena katika mbingu hizo za samawi zilizo juu yetu kwa muungano ule wa ajabu pamoja nasi? Mwisho huo wenye furaha wa historia hii ndefu, yenye misiba mingi ya ulimwengu, unaweza kuonekana kama ni mzuri mno kiasi cha kufikiriwa kuwa si wa kweli kwetu sisi. Lakini kuna kitu kimoja ambacho kinawenza kulifanya tumaini letu kuwa hai miyoni mwetu. Na kitu hicho ni ahadi ya Yesu pekee alioitoa kwamba yeye atakuja tena. Muda mfupi tu kabla hajajitenga mbali na wanafunzi wake, Yesu alitoa ahadi hii:
"Yesu aliwaambia, Msifadhaike miyoni mwenu. Mwaminini Mungu; niaminini na mimi pia. Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama isingekuwa hivyo, ningekwisha waambieni. Sasa nakwenda kuwatayarishieni nafasi. Na nikienda na kuwatayarishieni nafasi, nitarudi na kuwachukueni kwangu, ili nanyi mwe pale nilipo mimi" - (Yohana 14:1-3).

Kabla Yesu hajapaa kwenda mbinguni, aliaahidi wafuasi wake, akisema "NITAKUJA TENA!" Aliahidi kurudi tena kuja kuwachukua wale wote wanaomtegemia ili awape mahali maalum alipowaandalia. Maandiko yanasema juu ya kuja kwake mara ya pili karibu mara 2,500 hivi. Ukweli kwamba Kristo anakuja mara ya pili katika ulimwengu huu ni wa hakika kama ulivyo uhakika kwamba yeye aliwahi kuishi hapa dunaini miaka elfu mbili iliyopita.

Zamani sana Mungu aliahidi kwamba Masihi angekuja, yaani Mkombozi ambaye angechukua mwilini mwake uovu wetu na kutoa msamaha wake kwa ajili ya dhambi za wanadamu. Ahadi ile ilionekana kana kwamba ilikuwa ni nzuri mno kiasi kwamba isingeweza kuwa ya kweli kwa wengi katika ulimwengu ule wa zamani amba walikuwa wakiendelea kufanya kazi zao kwa bidii katika maisha yao yote. Lakini kweli Yesu alikuja na kufa juu ya msalaba. Ahadi ilitimia kweli kwa utukufu kuliko vile watu walivyowaza kwamba uwezekano kama ule ungekuwapo. Ahadi yake ya kurudi tena pia itakuwa ni ya kweli. Sisi



GUNDUA

twaweza kumtegemea yeye atupendaye, kurudi tena na kuwakusanya wale ambao kwa ajili yao amelipa ghamama kubwa mno isiyokadirika.

Katika kipindi chote cha kufungwa kwake, Armando aliendelea kutuma kwa Martha kwa siri mashairi, ujumbe, na picha alizochora. Naye [Martha] alifanikiwa kuyachapisha baadhi ya maandiko yale. Ufasaha wake [yale maandiko] uliyavuta mawazo ya ulimwengu. Serikali zikaanza kumbana Castro ili awaachilie wafungwa wale waliofungwa kwa sababu ya kuzifuata dhamiri zao. Rais wa Ufaransa akaingilia kati na hatimaye katika mwezi wa Oktoba mwaka wa 1982 Armando alipakiwa katika ndege iliyokuwa ikienda Paris. Ilikuwa ni vigumu sana kwake kuamini kwamba alikuwa huru-hata wakati ndege ile ilipotua. Lakini basi, baada ya miongo miwili [miaka ishirini] ya mateso na shauku yake ya kungoja, Armando alikimbia na kukumbatiwa na mikono ya Martha.

Miezi michache baadaye katika kanisa la Miami la Mtakatifu Kierani wale wawili wakasimama na kurudia kutoa kiapo chao cha ndoa. Hatimaye muungano wao ukawa umekamilika. Ahadi ikawa imetimizwa: "Nitakuja kwako."

Je, waweza kufikiria ni muungano wa ajabu jinsi gani utakaokuwako hatimaye tutakapoweza kumwona Kristo uso kwa uso? Kuja kwake katika utukufu wake kutazimeza huzuni zetu zote pamoja na kuvunjika miyo kwetu kote, kutayafutilia mbali maumivu yetu yote tuliyoyaficha moyoni mwetu. Kurudi tena kwa Yesu kutakidhi shauku zetu zenye kina sana na matarajio yetu ya kusisimua sana. Kisha tutaingia katika umilele wa muungano wa karibu sana na mtu yule wa ajabu sana katika Malimwengu yote. Yesu yu aja upesi! Je, wewe unayo shauku ya kukutana naye?

2. Yesu Atakujaje?



(1) Je! Yesu atakuja kwa siri?

"Tazama, [Yesu] nimekwisha kuwaonya mbele. Basi wakiwaambia, 'yuko jangwani,' msitoke; 'yumo nyumbani,' msisadiki. KWA MAANA KAMA VILE UMEME utokavyo mashariki na KUONEKANA hata magaharibi, HIVYO NDIVYO KUTAKVYOKUWA KUJA KWAKE MWANA WA ADAMU" - (Mathayo 24:25-27).

Umeme unamulika ghafla na kuonekana wazi wazi kabisa mpaka mbali sana, hivyo ndivyo ambavyo kuja kwake Yesu hakutakuwa kwa siri ya aina fulani au kuwa tukio la kihisia tu.

(2) Je, Yesu atakuja tena kama mtu halisi?

"Walipokuwa wakikaza macho mbinguni, yeye alipokuwa akienda zake, tazama watu wawili wakasimama karibu nao, wenye nguo nyeupe, wakasema, enyi watu wa Galilaya mbona mmesimama hapa mkitazama mbinguni? HUYO YESU, aliyechukuliwa kutoka kwenu KWENDA JUU MBINGUNI, ATAKUJA JINSI IYO HIYO mlivyomwona akienda zake mbinguni" - (Matendo 1:10-11).

Siku ya kuondoka kwake kutoka katika dunia yetu hii, malaika wale waliwathibitishia wanafunzi wale kwamba "Yesu yule yule" aliyechukuliwa kwenda mbinguni - si mtu mwininge awaye yote - angerudi tena kama Mfalme wa wafalme. Yesu yule aliywaponya wagonjwa na kuyafungua macho ya vipofu. Yesu yule yule aliyezungumza kwa upole na mwanamke yule aliyekamatwa akizini. Yesu yule yule aliyeafuta machozi ya mwombolezaji yule na kuwapokea watoto na kuwalisha katika paja lake. Yesu yule yule aliyejufu juu ya msalaba ule wa Kalwari akapumzika kaburini, na kufufuka kutoka kwa wafu siku ile ya tatu.

GUNDUA

(3) Je, Yesu atakuja ili sisi tuweze kumwona?

"Tazama yuaja na mawingu, na KILA JICHO LITAMWONA" - (Ufunuo 1:7). (Sehemu ya Kwanza).

Wote walio hai wakati Yesu anakuja tena, yaani, wenye haki na waovu, watashuhudia kuyaona marejeo yake. Ni wangapi ambao Yesu mwenyewe alisema watakuona kurudi kwake tena?

"Ndipo itakapoonekana ishara ya Mwana wa Adamu mbinguni, ndipo MATAIFA YOTE YA ULIMWENGU yatakapoomboleza nao, WATAMWONA Mwana wa Adamu akija juu ya mawingu ya mbinguni, pamoja na nguvu na utukufu mwingi" - (Mathayo 24:30).

Kila mtu aliye hai katika dunia yetu hii atamwona Yesu akirudi tena.

(4) Ni nani atakayefuatana na Yesu atakapokuja?

"Mwana wa Adamu katika utukufu wake, na malaika watakatifu wote pamoja naye, ndipo atakapoketi katika kiti cha utukufu ule wake" - (Mathayo 25:31).

Fikiria jinsi itakvyokuwa Yesu atakaporudi tena katika fahari yake yote akiwa amezungukwa pande zote na "malaika wote."

(5) Je, tunaweza kutabiri wakati halisi wa kurudi kwake Yesu?

"Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana ila Baba peke yake.... Kwa sababu hiyo ninyi nanyi jiwekeni tayari; kwa kuwa katika saa msiyodhani Mwana wa Adamu yuaja" - (Mathayo 24:36,44).



Kila mmoja atakuona kuja kutukufu kwa Yesu, lakini wengine hawatakuwa tayari kwa kuja kwake huko. Je, wewe binafsi u tayari kwa kuja kwake Yesu?

3. Yesu Atafanya Nini Atakapokuja Tena?

(1) Yesu atawakusanya pamoja wote waliookolewa (wateule).

"Naye atawatuma malaika zake pamoja na sauti kuu ya parapanda, nao watawakusanya wateule wake toka pepo nne, toka mwisho huu wa mbingu mpaka mwisho huu" - (Mathayo 24:31).

Kama wewe umemruhusu Yesu akutayarische moyoni mwako na katika maisha yako, basi utampokea kwa furaha kama Mwokozi. Wako.

(2) Yesu atawaamsha watakatifu waliokufa.

"Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na kwa sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu, nao WALIOKUFA KATIKA KRISTO WATAFUFULIWA KWANZA" - (1 Wathesalonike 4:16).

Yesu anashuka kutoka mbinguni kwa sauti kuu. Sauti yake yenye nguvu nyingi inasikika ulimwenguni kote. Inayapasua makaburi katika kila eneo la makaburi na kuwafufua mamilioni ya watu waliompokea Yesu katika vizazi vyote. Hiyo itakuwa ni siku ya kusisimua sana jinsi gani!

(3) Yesu atawabadilisha wenye haki wote wakati atakapokuja - si wafu wenye haki peke yao, bali pia wenye haki walio hai.

"Kisha sisi tulio hai, tuliosalia TUTANYAKULIWA PAMOJA NAO katika mawingu ili tumlaki Bwana hewani; Na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele" - (fungu la 17).

GUNDUA

Ili kutuandaa sisi kwa maisha yale ya milele, Kristo anabadilisha miili yetu hii inayokufa kuwa miili mizuri isiyokufa.



"Angalieni nawaambia ninyi siri; hatutalala sote, lakini sote tutabadiika, kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho; Maana parapanda italia, na wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu, nasi tutabadiika. Maana sharti huu uharibikao uvae kutokuharibika, nao huu wa kufa uvae kutokufa" - (1 Wakorintho 15:51-53).

Yesu ajapo "sote tutabadiika." Hebu fikiria sasa: hakuna ugonjwa wa baridi yabisi, kupooza, wala kansa. Fungeni hospitali, na fungeni nyumba za matanga. Kristo amekuja!

(4) Yesu atawachukua wenyewe haki wote kwenda nao mbinguni.

Yesu mwenyewe alitoa ahadi hii, "Nitakuja tena na kuwachukua mpate kuwa pamoja nami" nyumbami mwa Baba yangu (angalia Yohana 14:1-3). Petro anazungumza juu ya urithi wa waliokombolewa "uliotunzwa mbinguni kwa ajili yao" (1 Petro 1:4). Tuanaweza kutazamia mbele kuweza kuyavumbua maajabu ya mji ule wa Mungu, yaani, Yerusalemu Mpya, na kumfahamu Baba yetu aliye mbinguni.

(5) Yesu atayaondoa kabisa maovu na maumivu kwa kipindi chote kitakachofuata.

Waovu - yaani, wale ambao kwa shingo ngumu wameendelea kuikataa rehema yote anayowapa Yesu - wanajihukumu kabisa wenyewe. Wanapokodoa macho yao kutazama uso wa Yesu anapokuja kwao kutoka mawinguni, fahamu zao zinazinduka ghafula na kutambua dhambi zao, tena wanaona ni vigumu kabisa kuvumilia maumivu ya dhambi zao; wanapiga makelele na kuiomba milima na miamba, wakisema, "Tuangukieni, tuisitirini mbele za uso wake ye ye aketiye juu ya kiti cha enzi, na hasira ya Mwana - Kondoo!" (Ufunuo 6:16). Wanaona ni heri kufa kuliko kusimama mbele za macho ya Yesu yaliyokazwa ambayo yanawaona wote.

Wanajua fika kwamba sauti inayounguruma sasa kutoka mbinguni iliwasih i sana zamani kwa upole ili wapate kuikubali neema ya Mungu. Wale walioamua kupotea wenyewe katika mbio za kiwendawazimu ili kutafuta fedha au anasa au cheo sasa wanatambua kwamba wamekidharau kitu kile cha pekee chenye manufaa ya kweli katika maisha yao.

Ni uvumbuzi unaowamaliza kabisa. Kwa vyovyote vile, hakuna hata mmoja wao ambaye alikuwa na haja ya kupotea. Mungu mwenyewe hakufurahii kufa kwake mtu mwovu" (Ezekiel 33:11). Yeye "hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba" (2 Petro 3:9). Yesu anatushi sana sisi, anasema, "njoni kwangu ninyi nyote msimbukao na wenyewe kulemewa na mizigo, nami nitwapumzisha" (Mathayo 11:28). Lakini basi, kwa namna isiyosadikika, wengine wanautupilia kando mwaliko huo uliojaa neema.

4. Je! U Tayari Kwa Kuja Kwake Yesu?

Ilimgharimu sana Yesu kutuhakikishia sisi yale maisha mazuri sana ya siku za mbele "nyumbani mwa Baba ya[ke]." Ilimgharimu uhai wake!

KADHALIKA KRISTO NAYE AKIISHA KUTOLEWA SADAKA MARA MOJA azichukue dhambi za watu wengi; Pasipo dhambi kwa hao wamtazamiao kwa wokovu" - (Waebrania 9:28).

Mwokozi yule aliyejuu ya msalaba ili kuzichukua dhambi zako, atatokea "mara ya pili" naye atawaleta wokovu wale wanaomngojea." Kristo alijitoa sadaka yeye mwenyewe ili kutupatia sisi wokovu, yaani, kila mmoja wetu. Lakini pasipo kuja kwake mara ya pili, msalaba ule usingefaulu kutokana na kazi yake aliyoifanya. Kristo anataka kutupatia sisi



makao salama pamoja naye milele zote. Ili jambo hili lipate kutimizwa, yatupasa sisi kumruhusu yeye ili atawale ndani ya miyo yetu kama Mwokozi na Bwana wetu kuanzia hivi sasa.

Alfajiri moja ya tarehe 16, Agosti, 1945 mvulana mdogo alikimbia kuitia katika kiwanja cha Shantung katika China ya kaskazini, akipiga makelele na kusema kwamba ameiona ndege angani. Wafungwa wote wenyi miili yenye nguvu wakakimbia na kutoka nje na kutazama juu. Wanaume hao pamoja na wanawake walikuwa wameteseka sana kwa miaka mingi ya kukaa upweke, umaskini, na wasiwasi, wakiwa wamefungwa na Wajapani kama raia wa mataifa yale ya kiadui. Kwa wengi wao kitu kimoja tu kilikuwa kimewafanya kuwa hai kiroho: tumaini kwamba siku moja vita ile ingekoma.

Mshtuko kama wa umeme vile ukaenea katika lile kundi la wafungwa 1500 waliokuwa wangali hai walipotambua kwamba ndege ile ilikuwa inakuja kwa ajili yao. Mlio wa ndege ile ulivyo zidi kuwa mkubwa zaidi na zaidi, mtu fulani mmoja akipiga kelele, akasema "Tazama, ile ni BENDERA YA KIMAREKANI imechorwa pembedi kwa rangi!" Nao wakiwa wamepigwa na bumbuazi kwa kutokuamini kwao, sauti zikapiga makelele, "Tazama, WANATUPUNGIA mikono! Wanajua sisi ni akina nani. Wanakuja kutuchukua."

Kwa wakati huo ulikuwa ni zaidi ya vile walivyoweza kumudu kuuzuia watu wale waliovaa nguo zenye viraka, waliokuwa wamechoka sana, na wenyi shauku ya kurudi nyumbani kwao ambao walikuwa wameendelea kuwa hai. Vurumai ikazagaa pote. Watu walikuwa wakikimbia katika miduara, wakipiga makelele yao kwa nguvu zao zote, wakipunga hewani mikono yao na kulia.



Ghafla kundi lile likaanza kuhema kwa mshangao na kukodoa macho kimya kimya. Sehemu ya chini ya ndege ikafunguka ghafla na watu wakaanza kueleka angani wakashuka chini kwa miavuli. Waokoaji wao walikuwa hawaji tu siku fulani moja ya baadaye; walikuwa wanakuja leo, SASA HIVI ili kuwa mionganii mwao!

Kundi lile likasonga mbele kuelekea kwenye lango la uwanja ule. Hakuna aliyesimama na kuwaza juu ya zile bunduki za rashasha zile zilizokuwa zimeelekezwa chini kwao kutoka kwenye minara ile. Baada ya miaka mingi ya kukata tamaa na upweke, wakalivunja lile lango na kutimua mbio kuelekea mahali kule walikokuwa wakitua wale askari wa miavuli.

Punde si punde gharika ya wanadamu ikarudi na kuingia kwa wingi ndani ya kambi ile - wakiwabeba wale askari mabegani mwao. Mkuu wa kambi akasalimu amri bila kupigana. Vita vilikuwa vimekwisha kweli. Uhuru ulikuwa umekuja. Ulimwengu uligeuka na kuwa mpya kabisa tena.

Upesi Mungu WETU, yaani, Mwokozi WETU, atashuka kutoka mawinguni kuja kutuokoa sisi. Kisa hiki cha kuogofya sana cha muda mrefu sana cha ukatili wa mwanadamu kwa mwanadamu mwenzake hatimaye kitakoma kabisa. Patakuwa na shangwe kuu siku ile, makelele ya furaha hatimaye tutakapoju kwamba: "Anakuja karibu sana nasi; naweza kuwaona malaika wakizipiga zile tarumbeta zao." Sauti inazidi kuwa kubwa zaidi, wingu lile lenye utukufu linazidi kung'aa zaidi na zaidi, mpaka sisi tunashindwa kustahimili kuliangalia. Lakini basi, sisi hatuwezi kuacha kuliangalia tunapotambua kwamba: "Yeye ananiona mimi! Anajua mimi ni nani." Tukiwa tumejaa furaha isiyoelezeka tutajua, tutasema: "huyu ndiye Mungu wangu. Anakuja kwa ajili yangu, sio siku fulani ya baadaye, bali leo, sasa hivi."

Je, wewe uko tayari kumpokea huyo mfalme (mtawala) katika utukufu wake wote kama siyo, basi, tafadhalii mwalike Yesu wewe mwenyewe ili aingie ndani ya maisha yako sasa hivi. Kama vile kuja kwa Yesu katika dunia yetu hii kutakavyoyatatu matatizo ya ulimwengu huu, ndivyo kuja kwake ndani ya moyo wako kutakavyokusaidia wewe kushughulika na matatizo yako ya sasa ya kila siku. Mtatuaji mkuu

GUNDUA



wa matatizo anaweza kukuokoa wewe kutokana na hatia na mzigzo wako wa dhambi na kukupa wewe uzima wa milele.

Kuja kwa Yesu katika maisha ya mtu kunaweza kuyabadilisha milele kwa namna ya kuvutia sana kama kuja kwa Yesu kutakavyoibadilisha kabisa. Unaweza kumtegemea Yesu. Atakutayarisha wewe kwa ajili ya kuja kwake na kukupa ahadi ya ajabu ya maisha yale ya milele yenye furaha.

MAKAO YAKO YA MBINGUNI

Marko Polo aliporudi kwenye mji kusafiri miaka mingi katika nchi za mashariki, rafiki zake walidhani kwamba safari zake zile ndefu sana zilikuwa zimemfanya kuwa mwehu. Alikuwa na hadithi nydingi za kusimulia zilizokuwa hazisadikiki.

Marko alikuwa amesafiri hadi kwenye mji uliojaa fedha na dhababu. Alikuwa ameayaona mawe meusi yaliyokuwa yakiungua moto, lakini hakuna hata mmoja wao aliyeokuwa amepata kuzisikia habari za makaa ya mawe. Aliona nguo iliyokataa kuwaka moto hata kama ilitupwa katika ndimi za moto, lakini hakuna hata mmoja wao aliyeokuwa amepata habari za asbestos. Aliongea juu ya nyoka wakubwa urefu wao hatua kumi na mataya yao mapana ya kutosha kumeza mtu mzima, kokwa ambazo ukubwa wake ulikuwa kama kichwa cha mtu na nyeupe kama maziwa ndani yake [nazi], na kitu fulani kilichokuwa kikibubujika kutoka ardhini ambacho kilizifanya taa ziwake kabisa. Lakini hakuna hata mmoja aliyeokuwa amepata kuona, mamba, nazi, wala yale mafuta yasiyosafishwa. Walicheka tu kusikia visa kama vile. Miaka mingi baadaye, Marko alipolala kitandani pake akiwa anakufa, mcha Mungu mmoja aliyeokuwa kando ya kitanda chake akamsihi kuzikana zile hadithi zake ngumu za kusadadiika alizokuwa amezisimulia. Lakini Marko alikataa, alisema: "Zote ni za kweli kwa kila kipengele. Kusema kweli, mimi sijasimulia nusu ya yale niliyoyaona."



Waandishi wa Biblia watuonyeshao sisi picha kidogo tu ya mbinguni ambazo huonekana kana kwamba zinatoa mwangwi wa hisia aliyokuwa nayo Marko Polo. Katika maono yao walipatazama mahali pale palipokuwa paking'aa mno, pa ajabu mno, hata waliweza kueleza sehemu ndogo tu ya yale waliyoyaona. Nasi tunakabiliwa na changamoto ifananayo na ile ya marafiki wa Marko Polo. Hatuna budi kujaribu kuwaza habari za "mamba na nazi," yaani, mambo ambayo sisi hatujapata kamwe kuyaona kwa kuwa zile picha kidogo tu tunazozipata katika Biblia zinatuonyesha kwamba mbinguni ni zaidi ya kukaa juu ya mawingu na kupiga vinubi.

1. Je, Mbinguni Ni Mahali Halisi?

Yesu anatuandalia sisi mahali halisi kabisa hivi sasa katika mbingu iliyo ya halisi kabisa.

"Msifadhaike moyoni mwenu; mniamwamini Mungu, niaminini na mimi [Yesu]. Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi kama sivyo, ningaliwaambia. Naenda KUWAANDALIA MAHALI. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, NITAKUJA TENA, niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi muwepo." - Yohana 14:1-3, KJV.

Yesu anakuja mara ya pili katika dunia yetu hii ili kutuchukua kwenda kwenye makao yaliyoandaliwa kukidhi utashi wa kila mtu katika mji wa mbinguni ulio na utukufu upitao ndoto zetu zote zilizochanganyikiwa mno; yaani, Yerusalemu mpya.

Baada ya kuishi kwa miaka elfu moja, Kristo anakusudia kuyaleta makao yetu ya mbinguni hapa katika sayari hii itwayo Dunia. Yerusalemu Mpya utakaposhuka hapa chini, moto utaitakasa dunia yote. Sayari yetu hii itakayofanywa kuwa mpya itakuwa



GUNDUA

makao ya kudumu ya waliookolewa. Ufunuo 20:7-15. mengi zaidi kuhusu suala hili yamo katika Mwongozo 22).

Je, Yohana, aliyeziandika kitabu cha Ufunuo, anatoa picha gani nyingine?

"Kisha nikaona mbingu mpya na nchi mpya; kwa maana mbingu za kwanza na nchi ya kwanza zimekwisha kupita, wala hapana bahari tena. Nami nikauona mji ule Mtakatifu, Yerusalemu Mpya ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu, umewekwa tayari, kama bibi - arusi aliyezwisha kupambwa kwa mumewe. Nikasikia sauti kubwa kutoka katika kile kitu cha enzi, ikisema, 'Tazama, maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye ataisha pamoja nao. Watakuwa watu wake, naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao na kuwa Mungu wao" - (Ufunuo 21:1-3).

Baada ya nchi hii kubadilishwa kabisa kwa moto, je! ni akina nani watakaa katika ile nchi mpya?

"Heri wenyewe upole; maana hao watairithi nchi" - (Mathayo 5:5, Angalia pia Ufunuo 21:7).

Kristo anaahidi kwamba dunia hii ambayo zamani ilikuwa kamilifu itarejeshwa katika uzuri wake ule wa Edeni, na wapole "watairithi nchi."

2. Je, Tutakuwa Na Miili Halisi Mbinguni?

Yesu alipowatokea wanafunzi wake akiwa na mwili wake uliofufuka na kutukuzwa, je, aliuelezaje mwili ule?



"Tazameni mikono yangu na miguu yangu, ya kuwa ni mimi mwenyewe. Nishikeni, mwone; kwa kuwa roho haina mwili na mifupa, kama mnavyoniona mimi kuwa nayo" - (Luka 24:39).

Yesu alikuwa na mwili halisi; alimtaka Tomaso amguse (Yohana 20:27). Wakati ule Yesu alitembea na kuingia katika nyumba halisi, na kuzungumza na watu halisi, na kula chakula halisi (Luka 24:43).

Kule mbinguni hakukaliwi na roho, bali na watu halisi wanaoyafurahia maisha ya kiroho, na ambao wana "mwili.. wa utukufu."
Nasi kwa hamu kubwa tunamngojea Mwokozi wetu kutoka kule, yaani, Bwana Yesu Kristo, ambaye, kwa uweza wake unaomfanya kuvidhibiti vitu vyote chini yake, ataibadilisha miili yetu hii minyonge ili ipate kufanana na mwili wake wa utukufu" - (Wafilipi 3:20,21).

Tunaweza kuwa na hakika kwamba miili yetu ya mbinguni itakuwa imara na ya kweli kweli kama uliviyokuwa mwili wa Kristo aliyezufukwa.

Je, tutaweza kuwatambua watu wa familia yetu pamoja na marafiki zetu kule mbinguni?

"Tuanachoona sasa ni kama tu sura hafifu katika kioo, lakini hapo baadaye tutaona uso kwa uso. Sasa ninajua kiasi fulani tu, lakini hapo baadaye nitajua yote kikamilifu, kama vile Mungu anavyonijua mimi - (1 Wakorintho 13:12).

Kule mbinguni tutajua sana." Tutaelewana na kuthaminiana kwa kina kuliko tulivyopata kufanya katika dunia ya sasa.

Wanafunzi wa Yesu walimtambua akiwa katika mwili wake wa mbinguni, ni dhahiri kutokana na sura yake walipokuwa wamezoea kuiona (Luka 24:36-43). Mariamu alimjua pale kaburini kutokana na sauti yake

GUNDUA

aliyokuwa amezoea kuisikia wakati alipomwita kwa jina lake (Yohana 20:14-16). Emau walimtambua kutoka na ishara zake fulani za mikono walizokuwa wamezoea kuziona. Walipoangalia jinsi mgeni wao alivyokibariki kile chakula, walimtambua kuwa ni Bwana kwa tabia yake (Luka 24:13-35).

Walioombolewa wanayo hakika ya kuwa na maisha ya kusisimua sana kwa kuungana uso-kwa-uso tena kule mbinguni. Fikiria furaha utakayokuwa nayo ukiitambua tabasamu ya aina yake ya mume au mke wako, au sauti inayokuita ambayo kwako inafahamika ya mtoto wako uliyemlaza kaburini zamani sana, ishara za mikono zinazoonyesha upendo kwako za rafiki yako fulani mpandwa wako. Tutakuwa na umilele utakaoimarisha vifungo vya maisha yetu kwa kina zaidi na kukuza urafiki wa karibu sana pamoja na watu wale wanaotutuvutia sana katika ulimwengu.

3. Tutafanya Nini Kule Mbinguni?

Tutakuwa na shughuli nyingi za kutupatia changamoto kule mbinguni. Vipi kama wewe utaibuni mwenyewe nyumba yako unayoiwazia?

"Tazama, mimi naumba mbingu mpya na nchi mpya... Nami nitafurahia Yerusalem, na kuwaonea shangwe watu wangu... Watajenga nyumba, na kukaa ndani yake; watapanda mashamba ya mizabibu, na kula matunda yake... Wateule wangu watafurahia kazi ya mikono yao muda wa siku nyingi" - (Isaya 65:17-22).

Tayari Yesu anaandaa nyumba zetu binafsi katika ule Mji Mtakatifu, yaani, Yerusalem Mpya (Yohana 14:1-3; Ufunuo 21). Mafungu hayo yanadokeza kwamba sisi pia tutabuni nakuzijenga nyumba nyingine - huenda zikawa ni zile nyumba zetu nzuri za mashambani, ambazo tutaziwekea mandhari nzuri sana ya mimea hai mbalimbali. Tena, basi, ni nani ajuaye ni mbinu gani za hali ya juu zinazotungojea kuzitumia katika ule ustaarabu wa juu zaidi wa Mungu? Uvumbuzi mpya wa sasa wa kisayansi, pamoja na safari ndefu zenye matukio mengi katika anga za juu zitaonekana kama mchezo wa kitoto tu tutakapoanza kufanya uvumbuzi wetu "nyumbani mwa Baba" yetu.

Je, unapenda uzuri wa maporomoko ya maji yanayounguruma, mashamba ya malisho matulivu, misitu mingi iletayo mvua, na maua mazuri yanayochanua?

"Maana BWANA ameufariji Sayuni;... amefanya jangwa lake kuwa kama bustani ya Edeni, na nyika zake kama bustani ya BWANA; furaha na kicheko zitaonekana ndani yake, kushukuru, na sauti ya kuimba" - (Isaya 51:3).

Mungu ataigeuza nchi hii itakuwa kama Bustani ya Edeni ya zamani. Hakuna tena kumwagika ovyo ovyo kwa mafuta, wala mchanganyiko wa ukungu na moshi, wala ukame; maziwa yatakuwa safi kama kioo, miti itakuwa na fahari yake, na mitelemko ya milima itakuwa bila waa lolote.

Sio tu uzuri wa dunia hii, bali pia uwezo wetu wa kuzingatia mambo utaongezeka sana. Utaonekana kama siku ya kwanza ya kutoka nije baada ya ugonjwa wa muda mrefu sana. Na zile "dakika ishirini za kuyaona mambo ya kweli" za awali zitaendelea na kuingia katika ule umilele wa kimiujiza.

Je, unafurahia kuyaona mambo mapya ? kujifunza? Kubuni vitu? "Kule, watu waishio milele watatafakari kwa furaha isiyokoma maajabu ya ubunifu wa umbaji, siri ya upendo ukomboao... Kila uwezo wa kutenda kazi utakuzwa, kila uwezo wa kukumbuka au kujifunza utaongezeka. Kujipatia maarifa hakutaichosha akili au kuzimaliza nguvu za mwili. Kule shughuli kubwa mno zitawezwa kufanya, hamu ya kuifikia hali bora kiroho itafikiwa, tamaa ya kufanya mambo makuu mno itatimizwa; na bado



GUNDUA

vilele vipyta vya kuvipita vitainuka, maajabu mapya ya kuyastaajabia, kweli mpya za kuzifahamu, vitu vipyta vitakavyohitaji kutumia nguvu za akili, roho na mwili. Hazina zote za ulimwengu zitawekwa peupe ili zipate kuchunguzwa na wale waliokombolewa wa Mungu." - Ellen G. White, The Great Controversy (Nampa, Idaho; Pacific Pres Publishing Asociation, 1950), ukurasa 677.

4. Je! Uovu Utaitishia Mbingu Tena?

"Na ndani yake hakitaingia kamwe cho chote kilicho kinyonge, wala ye ye afanyaye machukizo na uongo, bali wale walioandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo" - (Ufunuo 21:27).

Mungu ataiondoa kabisa dhambi pamoja na athari zake za kutisha; mambo hayo hayataonekana tena. Yesu atakapoonekana, "tutafanana naye" (1 Yohana 3: 2). Badala ya kuipiga misukumo iliyo ndani yetu ya kuua, kuiba, kusema uongo, au kubaka, sisi tutaendelea kuwa na zile tabia nzuri za mbinguni.

"Naye [Mungu] atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakauwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwepo, kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita"- Ufunuo 21:4.

Hata yule adui yetu wa mwisho, yaani, mauti, atatoweka kabisa. Katika nchi ile ya mbinguni yenye ujana wa mielele wale waliokombolewa wanayo "mili isiyokufa" (1 Wakorintho 15:53); hakuna mwenyeji ye yote wa nchi ile atakayeteseka kutokana na uharibifu uletwao na uzee.

Sio tu kwamba hiyo mbingu inateketeza athari za dhambi, bali pia inafanya mageuzi ya athari hizo. Hebu fikiria itakavyokuwa kwa wale amba wamepambana na ulemavu mbali mbali katika maisha yao yote:

"Ndipo macho ya vipofu yatafumbuliwa, na masikio ya viziwi yatazibulia. Ndipo mtu aliye kilema ataruka-ruka kama kulungu, na ulimi wake aliye bubu utaimba" - (Isaya 35:5,6).

5. Je, Furaha Kuu Kuliko Zote Mbinguni Ni Ipi?

Hebu fikiria kwamba wewe unamwona Bwana wa malimwengu uso-kwa-uso.

"Tazama maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atafanya maisha yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Na Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao, naye atakuwa Mungu wao" - (Ufunuo 21:3).



Mungu mwenyezi anaahidi kwamba atakuwa mwenzi na mkufunzi wetu. Ni furaha iliyoje hiyo kukaa miguuni pake! Hebu fikiria kile ambacho mwanamuziki angeweza kutoa ili kuweza kutumia dakika chache pamoja na Beethoven au Mozart. Fikiria jinsi mtaalamu wa fizikia ambavyo angeweza kuithamini sana nafasi ya kuweza kukaa chini pamoja na Albert Einstein, au ingekuwa na maana kubwa kwa kiasi gani kwa mchoraji kuweza kuongea na Michelangelo au Rembrandt.

Hebu fikiria tu jinsi wale waliokombolewa watakavyopata upendeleo mkubwa mno usio wa aina zote, sayansi yote, na sanaa yote. Watapatana kwa karibu sana na akili na moyo usio na kifani katika malimwengu yote. Na uhusiano huo utafurika na kugeuka kuwa ibada.

GUNDUA

"Na itakuwa mwezi mpya hata mwezi mpya, na Sabato hata Sabato, wanadamu wote watakuja kuabudu mbele zangu, 'asema BWANA" - (Isaya 66:23).

Katikati ya mji wa mbinguni kinasimama kiti kikuu cha enzi, cheupe, cha Mungu. Akiwa amezungukwa na duara ya upinde wa mvua wa zumaridi, uso wake unang'aa kama jua ambalo mng'aro wake unayatia macho kiwi. Chini ya miguu yake bahari ya kioo inakwenda pande zote. Katika sehemu ile ya juu inayong'aa kama kioo utukufu wa Mungu unaakisiva [nuru yake inarudishwa], waliokombolewa wanakusanyika pale ili kutoa sifa zao kwa shangwe kuu.

"Na hao waliokombolewa na BWANA watarudi, watafika Sayuni wakiimba; na furaha ya milele itakuwa juu ya vichwa vyao, nao watapatwa na kicheko na furaha, huzuni na kuugua zitakimbia" - (Isaya 35:10).

Hapa yupo mtu yule ambaye wema wake haukosi pigo hata moja. Uaminifu wake na subira yake na upendo wake huendelea tu milele zote. Na lihimidiwe jina lake takatifu!

6. Huna budi kuwa Kule!

Yesu anatamani sana kukutana nasi uso kwa uso wakati ule. Ndiyo maana yeye alipenda kukuokoa wewe kutoka katika dhambi kwa gharama kubwa kama ile. Wewe binafsi ni lazima unufaiki kwa kuipokea zawadi hiyo. Ni lazima wewe ujite kabisa kwake Kristo awe Bwana na Mwokozi wako. Unahitaji msamaha wake unaotolewa kwako kutoka katika ule msalaba, kwa sababu:

"Ndani yake kamwe hakitaingia cho chote kilicho kinyonge, wala yeye afanyaye machukizo ya uongo, bali wale walioandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo" - (Ufunuo 21:27).

Yesu anatuokoa kutoka katika dhambi [uvunjaji wa Amri Kumi], sio pamoja na dhambi [uvunjaji wa Amri Kumi]. Yatupasa kuja kwake kwa uwezo wake ulio ndani yetu na kutengwa mbali na uchafu na uovu. Yesu ni neno letu kuu la kuingilia katika ufalme wake unaokuja upesi.



Na ufalme ule unaweza kuanza sasa hivi ndani ya moyo wako. Kristo anapotuokoa sisi kutoka katika dhambi, anaiweka mbingu ndogo ndani ya moyo wetu. Anaweza kutusaidia sisi katika kushughulikia wasiwas, hasira, tamaa ya mwili, hofu, na hatia inayotusumbua. Tumaini la kwenda mbinguni si njia ya kuyakwepa matatizo yanayotukibili katika maisha yetu; linasaidia kuileta mbingu kwa wingi zaidi hapa duniani. Kura iliypigwa hivi karibuni ilionyesha kwamba "wale wanaoamini kwamba maisha yatakuwako baada ya kifo walikuwa na maisha yenye furaha na kuwa na imani na watu kuliko wale wasiosadiki hivyo."

Hakuna kitu cho chote kitakachokuwa na mvuto unaosisimua sana katika maisha yako ya wakati huu wa sasa kama kuwa na uhusiano wa imani na Yesu Kristo. Hebu sikiliza jinsi Petro anavyoeleza matokeo ya imani iliyo hai:

"Naye mwampenda, ijapokuwa hamkumwona; ambaye ijapokuwa hamwoni sasa mniamwamini; na kufurahi sana, kwa furaha isiyoneneka yenye utukufu, katika kumpokea mwisho wa imani yenu, yaani wokovu wa roho zenu" - (1 Petro 1:8,9).

Yote hayo utapata - pamoja na mbingu pia. Je! wewe umekwisha kugundua aina ile ya maisha tele ambayo Kristo anataka wewe uwe nayo? Tafadhali usigeuke na kwenda zako kwa kuukataa mwaliko wake huu wa neema.

"Na Roho na Bibi-arusi, wasema, 'Njoo!' Naye asikiaye na aseme, 'Njoo!' Naye mwenye kiu, na aje; na ye yote atakaye, na ayatwae maji ya uzima bure" - (Ufunuo 22:17).

Yesu yu pamoja nawe hivi sasa, anazungumza na moyo wako unaposoma mistari hii. Anakualika wewe, anasema, "Njoo!" "Njoo!" "Njoo!" Asingeweza kuwa na shauku kubwa zaidi ya hiyo, asingesisitiza zaidi ya hivyo alivyokwisha kufanya. Kama wewe bado hujafanya hivyo, basi, hii ndiyo dakika yako ya kukichunguza kipawa chake hicho.

Kwa nini wewe usimwambie ya kwamba unakubali kukipokea kipawa chake hicho cha neema yake na ya kwamba wewe unataka kuishi milele pamoja naye? Mwambie kwamba wewe unampenda. Umshukuru kwa yote aliyokutendea na kwa yale ambayo unapanga kwa ajili yako. Kama kuna kitu cho chote katika yako na Mungu, basi, mwombe akufanye upende kuachana nacho. Leo hii, unapoisikia sauti yake, wakati moyo wako bado unavutwa kwake, jitoe kwake wewe mwenyewe bila kuacha kitu. Inamisha kichwa chako dakika hii na kusema, "Yesu, Bwana wangu, naja kwako. Nakupa wewe vyote nilivyo navyo. Mimi nataka kuwa wako milele hata milele.

JE! NI MAPEMA KIASI GANI YESU ATARUDI?

Karibu wengi wetu tunao msukumo ambao kwa jumla ni wa kisiliwa wa kutamani mambo yale yatakayotokea baadaye. Tunataka kujua ni kitu gani kilicho mbele ya upeo wa macho yetu. Lakini utabiri uliosahihi huteleza vibaya sana. Tunao wakati mgumu wa kutosha kuweza kujaribu kubashiri hali ya hewa itakayokuwako kesho!

Lakini yuko Mmoja ambaye unabii wake umethibitika kwamba ni sahihi kwa namna ya kustaa jabisha sana. Yesu Kristo, kuititia katika Neno lake, anaweza kutuchukua mpaka siku zile za usoni; yeye ni kiongozi anayetegemewa. Katika somo hili tutaa ngalilia kile alichosema yeye juu ya kuja kwake mara ya pili. Kwa vyo vyote vile, ni nani, basi, ambaye angeweza kujua mengi sana juu ya mwisho wa dunia hii zaidi ya yule aliyeiumba pale mwanzo?

1. Ishara Zionshazo Kwamba Kristo Atarudi Katika Siku Zetu

Baada ya Yesu kuwaahidi wanafunzi wake kwamba angekuja tena katika ulimwengu huu kwa mara yake ya pili (Mathayo 23:39), je! ni swali gani walilomwuliza?

"Tuambie,' wakasema, 'mambo hayo yataokea lini, tena, patakuwa na dalili gani ya kuja kwako, na ya mwisho wa dunia?" - (Mathayo 24:3).

Yesu alijibu waziwazi na pasipo shaka lo lote. Katika sura ya 24 ya Mathayo na sura ya 21 ya Luka yeye mwenyewe aliwapa "ishara" kadhaa, au ushahidi, ambao kwa huo sisi tunaweza kujua kuja kwake kunapokaribia. Unabii mwingine wa Biblia unasa idia kuijazia picha hiyo, unaonyesha kwa kinagaubaga hali ya dunia hii itakavyokuwa kabla tu ya kurudi kwake Kristo.



Kama tutakavyoweza kuona, unabii huo unaendelea kutimia kabisa mbele ya macho yetu; unaonyesha kwamba kuja tena kwa Kristo kumekaribia sana.

Hebu na tuviangalie vibao kumi vya ishara za unabii wa Biblia vilivyo katika njia ile kuu ya kwenda mbinguni, na kuyachunguza maswali ambayo msafiri wa siku hizi anaweza kuuliza anapovisoma vibao hivyo.

Kibao-cha-Ishara ya 1 - Dhiki! Hofu Kuu Mfadhaiko!

Zaidi ya miaka elfu moja na mia tisa iliyopita Yesu alitoa maelezo ya unabii unaohusu maisha ya siku hizi yasikikayo kana kwamba yangeweza kuwa yamechukuliwa kutoka katika habari za jioni hii:

"Tena, kutakuwa na ishara katika jua, na mwezi, na nyota; na katika nchi dhiki ya mataifa wakishangaa kwa uvumi wa bahari na msukosuko wake; watu wakivunjika mioyo kwa hofu, na kwa kutazamia mambo yatayoupata ulimwengu. Kwa kuwa nguvu za mbinguni zitatikisika. Hapo ndipo watakapomwona Mwana wa Adamu akija katika wingu pamoja na nguvu na utukufu mwangi. Basi mambo hayo yaanza kutokea changamkeni mkaviiue vichwa vyenu, kwa kuwa ukombozi wenu umekaribia" - Luka 21:25-28.



Hakuna maelezo yaliyo sahihi zaidi juu ya dunia yetu ya leo kama yalivyo maneno haya: 'Watu watazimia kwa hofu, wakitazamia mambo yatakayoipata dunia hii.' Silaha kali zilizolundikana zina uwezo wa

GUNDUA

kuiteketeza sayari hii yote. Itakuwaje, basi, endapo gaidi mmoja atakipata kichwa kimoja cha nyuklia?

Yesu anatupa sisi msingi wa kuwa na tumaini katika kizazi hiki chenye maafa makubwa. Hali iliyopo sasa ya hatari inayoikabili dunia hii nzima itakayoleta "dhiki na mfadhaiko" inauilia tu nguvu ukweli usemao kwamba kuja kwake Kristo "kunakaribia." Watu siku hizi huomboleza mara kwa mara na kukata tamaa, wakisema, "Tazama ilivyo dunia hii!" Lakini mwanafunzi wa unabii wa Biblia anaweza kusema ghafla kwa sauti ilijojaa matumaini, akisema, "Tazama, NI NANI HUYO ajaye katika dunia yetu."

Kibao-cha-Ishara ya 2: Maafa katika Dunia hii

Je! maafa haya ya asili yanaingaje na kukubaliana na matukio ya siku za mwisho?

"Kutakuwa na MATETEMEKO makubwa ya nchi, na njaa na TAUNI mahali mahali, na mambo ya kutisha na ishara kuu kutoka mbinguni... Nanyi kadhalika mwonapo mambo hayo yanaanza kutokea, tambueni ya kwamba UFALME WA MUNGU U KARIBU" (Luka 21:11,31).

Hebu fikiria habari za njaa kwa dakika moja. Picha za watoto wanaokufa kwa njaa wenye matumbo yaliyovimba huendelea kutangazwa katika habari. Je! hilo si jambo la kushangaza sana kwamba dunia hii inayoweza kuwatumwa watu mwezini, HAIWEZI kuwalisha watu wake wote? Yesu alijua kwamba njaa ingeendelea kuwako, kwamba tabia ya uchoyo ya kibinadamu ingezidi kuwa mbaya zaidi na zaidi karibu na ule mwisho wa wakati.



Lakini, je! vipi kuhusu hayo matetemeko ya nchi? Kwa mujibu wa World Almanac ya 1999, karne baada ya karne za kipindi hiki cha kikristo pamekuwa na ongezeko la kustajabisha la matetemeko makubwa ya nchi: karne ya kumi na nane palikuwa na matetemeko makubwa ya nchi 6; karne ya kumi na tisa yalikuwa 7; karne ya 20 yalikuwa zaidi ya 100. Kwa hiyo ushahidi unazidi kuwa wa kuvutia zaidi na zaidi kadiri tunavyokaribia kuzifikia siku hizi zetu.

Takwimu hizo zinauthibitisha unabii ule alioutoa Yesu. Njaa na matetemeko makubwa ya nchi yanazidi kuongezeka taratibu - yakisema, "ufalme wa Mungu umekaribia!" Je! karne yetu hii ya ishirini na moja italeta matetemeko makubwa ya nchi mengi zaidi, au itakuwa ni kuja kwa yule Mfalme wa wafalme?

Kibao-cha-Ishara ya 3: Kujilimbikizia mali.

Hivi maana yake ni nini kwamba utajiri unateleza na kuingia katika mikono ya watu wachache kwa wingi zaidi na zaidi, huku watu wengi zaidi na zaidi wakizidi kuwa maskini?

"Mmejiwekea akiba katika siku za mwisho" - (Yakobo 5:3).

Licha ya ujuzi wetu wote wa uchumi, matajiri wanazidi kuwa matajiri, na maskini wanazidi kuwa maskini. Utajiri wa kuwa na mamilioni mengi ya dola [za Kimarekani] ni kibao-cha-ishara kingine kituonyeshacho kwamba "kuja kwake Bwana kunakaribia" (fungu la 8).



Kibao-cha-Ishara ya 4 - Misukosuko ya Kiraia

Kwa nini hali hii ya kutoridhika na misukosuko mionganoni mwa wafanyakazi imeongezeka kwa namna inayojionyesha wazi mno?

"Angalieni! Ujira wa wakulima waliovuna mashamba yenu ninyi mliouzuia kwa hila unapiga kelele dhidi yenu na . VILIO VYAO VYA WALIOVUNA vimeingia masikioni mwa Bwana wa majeshi..."

GUNDUA

Nanyi vumilieni mthibitishe mioyo yenu kwa maana KUJA KWAKE BWANA KUNAKARIBIA" - (Yakobo 5:4,8).

Baada ya kutabiri dhidi ya kujilimbikizia mali nyingi zisizo na idadi katika siku hizi zetu, Yakobo aliona misukosuko ya watu ikitokana na wafanyakazi wasioridhika. Migogoro iliyopo kati ya wale "walio nacho" na wale "wasio nacho" inazidi kuongezeka. Hiyo ni ishara nyingine inayoonyesha kwamba "kuja kwake Bwana kunakaribia."

Kibao-cha-Ishara ya 5: Mmomonyoko wa Maadili

Mbona uzi wa maadili ya jamii unaonekana kana kwamba unakatika vipande vipande?

"Lakini ufahamu neno hili; ya kuwa siku za mwisho kutakuwako na NYAKATI ZA HATARI. Watu watakuwa wakijipenda wenyewe, wenye kupenda fedha, wenye kujisifu, wenye kiburi, wenye kutukana, wasiowatii wazazi wao, wasio na shukrani, wasio safi, wasio wapenda wa kwao, wasiotaka suluhi, wasingiziaji, wasiojizuia, wakali, wasiopenda mema, wasaliti, wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu - wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana nguvu zake hao nao ujiepushe nao.... LAKINI WATU WABAYA NA WADANGANYAJI WATAENDELEA, NA KUZIDI KUWA WAOVU, wakidanganya na kudanganyika" - (2 Timotheo 3:1-5,13).



Je! kuna mtu ye yote ambaye angeweza kufikiria na kutoa maelezo yaliyo sahihi zaidi ya hayo kuihusu hii dunia yetu? Hebu elekeza kamera yako upande wo wote katika hizi siku tulizo nazo, nawe utapiga picha inayoonyesha ufedhuli utokanao na ile tamaa ya kupenda anasa za ulimwengu huu. Utainasa picha ya kushtua inayoonyesha ukatili wa kuwatenda vibaya watoto wadogo, pamoja na maudhi yanayoletwa kwa makusudi mazima. Utapata matukio mengi yasiyo na idadi ya vijana wasioweza kudhibitika kabisa, pamoja na watoto walio katika ule umri wa miaka ya mwanzo ya ujana wao, yaani, kuanzia miaka kumi na mitatu na kuendelea juu kidogo, ambao wanawaua watu ovyo ovyo na kuwafanya

watu vilema. Mambo hayo yote yanajenga chumba kidogo kirefu ambacho kinaonyesha picha zinazotangaza kwa sauti kuu kwamba kuja kwake Yesu kumekaribia sana.

Kibao-cha-Ishara ya 6: Kuenea kwa Dini za Siri (Kiinimacho)

Hivi kwa nini tunauona mlipuko wa kupendezwa sana na dini za siri (occult) mionganoni mwa watu?

"Kwa maana watatoka wakristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu [miujiza] wapate kuwapoteza kama yamkini hata walio wateule" -(Mathayo 24:24).

Vifungu hivi nya maneno vinatabiri kwamba wakati huu wa mwisho itaonekana miujiza ya kila namna, pamoja na ishara, yaani maonyesho ya bandia ya uwezo usio wa kawaida kwa wanadamu. Wanawake wachawi na wanaume wachawi wafanyao uchawi wa Kiafrika wataonekana katika maonyesho mbalimbali wakizungumza. Waumini wa Kizazi Kipyta (New Age) wako kila mahali, wanauzwa vijiwe vya uchawi vinyavyong'a kama kioo na maajabu hayo ya uongo hujitokeza ghafla kwa wingi. Hayo yote huyafanya mambo yawe wazi zaidi kama Yesu alivyotabiri kwamba sisi tunaishi katika kipindi cha "kuja kwake Mwana wa Adamu" (fungu la 27.)

Kibao-cha-Ishara ya 7 - Dunia Iliyozinduka


Huko kuzinduka kunakohusu mambo ya dunia hii kunamaanisha nini kwa Afrika, Mashariki ya Kati, Ulaya Mashariki, na kwa matatifa yale ya Mashariki ya Mbali?

"MATAIFA NA WAJIHIMIZE;... haya utieni mundu, maana mavuno yameiva... kwani uovu wao ni mwinci sana! Makutano makubwa, makutano makubwa, wamo katika bonde la kukata maneno [kuamua mwisho wa kila mtu]" - (Yoeli 3:12-14).

GUNDUA

Leo hii katika nchi za Asia na Afrika, Ulaya Mashariki, Muungano wa Zamani wa Kisovieti, na nchi za Mashariki ya Kati, huenda sisi tunashuhudia kuona mwamko mkubwa sana wa tatifa moja moja katika historia yote iliopata kuandikwa, "kwa maana siku ya BWANA I KARIBU."

Kibao-cha-Ishara ya 8 - Mipango ya Amani na Maandalizi ya Vita



Tunaishi katika ulimwengu huu wa ajabu. Kila mmoja anaafiki kwamba tungeipatia nafasi amani; lakini basi, zile chuki zilizokandamizwa kwa kipindi cha karne fulani zilizopita, zinalipuka na kuwa vita ya wazi. Nabii Mika na Yoeli walitabiri kwamba wakati ule ule mataifa yatakapokuwa yanasema juu ya shauku yao ya kuwa na amani (Mika 4:1-3) watalazimika kuijandaa kwa vita kutokana na shauku yao waliyo nayo dhidi ya majirani zao (Yoeli 3:9-13).

Zamani sana Biblia ilionyesha picha hii ya mgogoro wetu wa sasa wa kuwa na amani au vita, kisha ikatangaza kwamba amani ya kudumu itatawala katika dunia hii wakati ule tu Yesu atakapokuja.

Kibao-cha-Ishara ya 9 - Maendeleo ya kisasa

Mbona usafiri na mawasiliano vimeuleta ulimwengu huu kuwa karibu mno baada ya karne nyingi za historia ya wanadamu?

"HATA WAKATI WA MWISHO, wengi wataenda mbio huko na huko maarifa yataongezeka" - (Danieli 12:4).

Hapo Danieli anadokeza kwamba maarifa ya kuuelewa unabii wake yataongezeka "katika" (KJV), au "hata wakati wa mwisho." Lakini utabiri huo pia unaonekana kana kwamba unasonda kidole chake kwenye kizazi chetu hiki kilichoyaweka maarifa katika kompyuta. Maarifa ya kila namna yameongezeka kwa kasi kubwa inayolandana na umeme katika miaka hii michache iliopita. Pamekuwako na mabadiliko mengi sana katika kipindi cha miaka hamsini iliopita kuliko katika kipindi kile cha miaka elfu mbili kabla yake.

"WENGI WATAENDA HUKU NA KULE kuongeza maarifa." Kabla ya mwaka ule wa 1850, watu walisafiri kwa magari yaliyovutwa na farasi, ikiwa karibu sawa kabisa na vile iliyokuwa tangu mwanzo wa wakati. Hivi sasa tunasafiri kasi kuliko sauti na kuizunguka dunia hii kwa ndege za konkodi (concorde) hata kwa roketi za safari fupi katika anga za juu.

Ongezeko la safari na gharika ya uvumbuzi ya hivi karibuni hutoa ushahidi mwingine zaidi kuonyesha kwamba sisi tunaishi "katika siku za mwisho."

Kibao- cha- Ishara ya 10 - Injili Ulimwenguni Kote



Yesu alitabiri kwamba, muda mfupi tu kabla ya kuja kwake, injili ingefika katika ulimwengu wote:

"Tena habari njema ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote, hapo ndipo ule mwisho utapokuja" - (Mathayo 24:14).

Kwa miongo mingi [makumi mengi ya miaka] karibu nusu ya dunia hii ilikuwa imefungiwa nyuma ya pazia la chuma, ilifungiwa mbali na ile Habari Njema. Lakini baadaye, karibu kwa usiku mmoja Ulaya Mashariki iliteleza kutoka katika kubanwa na chuma cha Ukomunisti. Ukuta wa (Berlin) ukaanguka chini na kuvunjika vipande, na

GUNDUA

ile dola yenyeye nguvu nyingi ya Kisovieti ikasambaratika. Ghafla karibu nusu ya sayari hii ilikuwa ikinyoosha mikono yake ili kuipokea injili.

Injili hii inakwenda katika "ulimwengu wote" kwa namna isivyopata kufanyika katika siku zile za nyuma. Kwa njia ya Satelaiti ujumbe wa Kikristo kwa wakati uo huo unaendelea kutangazwa karibu kwa kila taifa. Tunaishi katika kipindi kile kile hasa ambacho Yesu alisema habari zake alipotangaza hivi: "Injili hii itahubiriwa katika ulimwengu wote."

2. Ni Mapema Kiasi Gani Yesu Atakuja?

Baada ya kuyaelezea yale matukio yaliyokusudiwa kuonyesha kipindi kile kinachotangulia muda mfupi tu kabla ya kuja kwake mara ya pili, Yesu anahitimisha maneno yake kwa kusema hivi,

"Amini nawaambia, kizazi hiki hakika hakitapita, hata hayo yote yatakapotimia" - (Mathayo 24:34).

Hitimisho hilo ni dhahiri - yaani, kizazi hicho kilichodokezwa kwa hivi vibao-vya-ishara za unabii ndicho kitakacho jaliwa kumwona Yesu akirudi duniani mara ya pili. Muda hautakuwa mrefu hadi hapo atakapoifagilia mbali dhambi na mateso, na kuusimika ufalme wake ule wa milele. Yesu anatutahadharisha sisi, anasema, "Hakuna aijuaye.. siku ile au saa ile" (fungu la 36.)

Tena, Yesu anaendelea kusema hivi:

"Kwa sababu hiyo ninyi nanyi jiwekeni tayari, kwa kuwa katika saa msiyodhani Mwana wa Adamu yuaja" - (Mathayo 24:44).



3. Yesu, Tumaini Pekee La Dunia Hii

Kristo ndiye tumaini bora la mwisho kwa dunia yetu hii kwa kuwa ni ye ye peke yake awezaye kukishughulikia hasa kitu kile kile kinacholivunjilia mbali hilo tumaini - yaani, ile dhambi. Yesu alikufa pale kalwari kufanya uwezekano uwepo wa kuyashinda maovu na kuwapatia ukombozi wale wote wanaoitikia na kuupokea wokovu wake.

"Atendaye dhambi [avunjaye Amri Kumi] ni wa Ibilisi, kwa kuwa Ibilisi amekuwa akitenda dhambi [akizivunja Amri Kumi - Yn. 8:44) tangu mwanzo. Sababu ya kuja kwa Mwana wa Mungu ilikuwa ni kuzivunjilia mbali kazi za Ibilisi" - (1 Yohana 3:8).



Mwokozi wetu alitayarisha njia ya kututoa kutoka katika dunia yetu hii inayovunjika-vunjika kwa kutoa kafara mwili wake na damu yake. Na Yesu yule yule, ambaye siku moja atayaponya magonjwa ya dunia hii kwa kuiteketeza dhambi, hivi sasa anakupa wewe haki yake inayofutilia mbali hatia ya dhambi katika maisha yako. Huna haja ya kungoja mpaka siku ya kuja kwake mara ya pili ili upate kuwekwa huru mbali na hatia yako na mbali na wasiwasi wako pamoja na ile tabia yako ileayo uharibifu. Yesu yu tayari sana kukupa wewe amani yake katika dakika hii hii.

Mwanamke mmoja kijana alipokuwa akiendelea kuhudhuria katika mikutano ya dini aliguswa moyo wake kiajabu na injili iliyohubiriwa pale. Aliposikia ikifunuliwa habari ya kuja upesi kwa Mwokozi, kila kitu kikaingia vizuri mahali pake. Habari ile ililetu maana kwake. Yeye katika nia yake alikuwa akitafuta upendo, furaha, na amani kutoka kila mahali palikuwa pabay. Yesu akawa jibu lake.

Siku iliyofuata wakati mwinjilisti yule na mwenzake walipokwenda

GUNDUA

kumwona, aliwasimulia habari yake yote ya maisha yake machungu na yaliyojaa uhalifu. Alikuwa amezama mpaka chini sana kama mlevi sugu, tena alikuwa akipata riziki yake kwa kufanya umalaya. Baada ya kueleza matatizo yake, alisema hivi huku akilia, "Ulikuwa unanisema mimi hasa jana usiku."

Lakini ile sauti iliyougusa moyo wake ilikuwa ni sauti ya Mungu. Naye alikuwa akisema kwa upole. Aliamua kutoa yote. Alimkaribisha Kristo kuingia moyoni mwake kama Bwana na Mwokozi wake, na kulishikilia sana lile tumaini la kuja kwake upesi.

Katika majuma yale yaliyofuata, akaanza kugundua kwamba zile hofu zake na kutokujisikia salama kwake ambako siku zote alkuwa amejitahidi sana kukuzima kwa kunywa vileo, sasa kulikuwa kumempa nafuu kiasi cha yeye akaanza kumwokoa na kumweka mbali na ile misukumo mibaya iliyokuwa ikimlazimisha kufanya mambo yale mabaya na kuyaharibu maisha yake.

Alikuwa amefanya mambo mengi sana ambayo hakuweza kujivunia. Lakini neema yake Kristo na msamaha wake vilikuwa na nguvu nyingi sana kuliko ile aibu yake. Uzoefu wa maisha aliokuwa nao yule mwizi pale msalabani ulikuwa wa maana sana kwake yule mwanamke. Katika dakika zake zile za mwisho, akitapatapa na kutaka kufa, alimgeukia yule Mteswaji Asiye na Hatia alikuwa kando yake na kumwomba, akasema, "Ee Yesu, unikumbuke mimi utakapokuja katika ufalme wako" (Luka 23:42). Yesu yule yule aliyetao msamaha wake kwa wingi kwa yule mwizi aliyekuwa akifa, hivi sasa anakupa wewe wokovu, msamaha kamili, na amani moyoni mwako. Hebu leo hii gundua hayo wewe mwenyewe.

Wewe pia unaweza kuomba pamoja na yule mwizi aliyekuwa akifa, na kusema: "Ee Yesu, unikumbuke mimi utakapokuja katika ufalme wako." Naye Yesu atakujibu hivi, "Nitakuja tena, nawe utakuwa pamoja nami katika Paradiso"

UWEZO WA AJABU KATIKA MAISHA YANGU

Katika mwaka ule wa 1929 (Frank Morris) alipanda meli iliyokuwa ikienda Uswisi. Alikuwa ametazamia kufanya safari ile kwa muda fulani. Lakini ikageuka na kuwa safari ya kumdhalilisha. Mtumishi aliyewekwa kumtunza alimfungia Frank katika chumba chake kila siku. Baada ya kupata kifungua kinywa, kwa haraka-haraka Frank aliweza kufanya mazoezi ya viungo kidogo, lakini yeye alijisikia kana kwamba alikuwa mpumbavu kuweza kuongozwa vile huku na huku juu ya sitaha ya meli ile, kama vile yeye alikuwa mnyama anayeongozwa kwa kamba. Wakati wo wote alipokutana na abiria aliyeonyesha urafiki kwake na kumwalika kwenda kutembea naye, yule mtumishi alikataa, akawaambia kwamba alipaswa kumwangalia kila wakati.



Frank alikuwa mtu mzima, mwenye hisia za kawaida za udadisi na tamaa anazopaswa kuwa nazo mtu mzima. Lakini yeye alikuwa kipofu pia. Yule mtumishi alidhani kwamba asingeweza kujitunza mwenyewe. Frank alitendewa kana kwamba alikuwa kifurushi vile, kilichopaswa kuburutwa huku na huku.

Lakini katika nchi ile ya Uswisi maisha ya Frank yalibadilika kwa namna ya kuvutia sana. Alipokuwa kule alijifunza habari za mbwa waliokuwa wamepewa mafunzo ya kuwaongoza vipofu. Aliporudi kule Marekani pamoja na kiongozi [mbwa] wake wa safari wa Kijerumani aliyeitwa Buddy, Frank alianzisha Jicho Lionel, sasa ni shirika lilioenea ulimwenguni kote.

Sasa Frank, akiwa na Buddy kando yake, aliweza kwenda ko kote, wakati wo wote, na mtu ye yote. Hatimaye alijisikia huru. Katika maonyesho yake ya kwanza kwa waandishi wa habari penye njia panda yenye magari mengi katika lile Jiji la New York, yule Buddy alimwongoza bwana wake kwa ustadi kutoka katika njia moja na kuingia katika njia nyingine wakati yale magari yalipokuwa yakiunguruma na kupita. Kwa kuwa yeye alimtumainia yule Buddy, Frank alivuka kwa urahisi mpaka upande ule wa pili. Waandishi wa habari walioonekana pale walikuwa na wakati mgumu zaidi kuvuka pale; mmoja wao alichukua kabisa teksi ili kwenda upande ule wa pili.

Katika kurasa chache zifuatazo tunakwenda kujifunza juu ya Roho Mtakatifu, kiongozi anayetaka sisi tuyakabidhi maisha yetu mikononi mwake. Sisi sote tumelemaa kutokana na asili yetu moja ya kibinadamu, tunao upofu ule ule katika mambo yale yaliyo ya maana sana kwetu. Maisha yetu hupita kasi kwa namna ambayo tunajikuta wenyewe tunayavumilia tu badala ya kwenda mahali fulani. Hata hivyo, sisi tunasita-sita kuyakabidhi maisha yetu kikamilifu kwa Kiongozi huyo. Lakini ugunduzi unaomngojea kila mmoja wetu ni huu: sisi tutapata uhuru wa kweli na uwezo kwa kumtegemea Roho Mtakatifu ktuongoza katika maisha yetu yote.

1. Mwakilishi Wa Kristo Ulimwenguni

Kristo alipokuwa tayari kupaa kwenda mbinguni, aliaahidi wanafunzi wake kwamba atawapa zawadi ya thamani kuu isiyokadirika:

"Lakini mimi nawaambia ilio kweli; yawafaa ninyi mimi niondoke kwa maana nisipoondoka huyo MSAIDIZI hatakuja kwenu; bali mimi nikienda zangu, nitampeleka kwenu. Lakini atakapokuja, HUYO ROHO WA KWELI, ATAWAONGOZA awatie kwenye kweli yote.... YEYE ATANITUZA MIMI kwa kuwa atatwaa katika yaliyo yangu na kuwapasha habari". - (Yohana 16:7,13,14).

Katika mpango wa Mungu, Yesu alihitaji kurudi mbinguni kuwa Mwakilishi wetu mbele ya kile kitie cha enzi cha Mungu ili "aonekane sasa usoni pa Mungu" (Waebriania 9:24). Wakati Bwana wetu aliyesulubiwa anapotuwakilisha sisi kule mbinguni, tunaye pia Roho Mtakatifu kama MSHAURI wetu na KIONGOZI wetu hapa hapa duniani. Yeye moja kwa moja ndiye Mwakilishi wa Yesu hapa.



Yesu alipokuwa hapa alifanya kazi zake akiwa amefungwa na mwili huu wa kibinadamu, tena yeye asingeweza kuwa kila mahali. Lakini huyo Roho Mtakatifu hana mipaka kama hiyo inayomzuia; ana weza kuhudumu kama Mshauri na Kiongozi kwa watu wasiohesabika walio mahali pengi kwa wakati mmoja. Kristo anakidhi mahitaji yetu kwa njia ya huyo Roho Mtakatifu.

2. Roho Mtakatifu Ni Nani?

Wengi wetu tunaweza kuwa na uhusiano wetu na Mungu Baba kama sisi tunatafakari habari za mzazi wetu tuliyepata kumjua ambaye alitutunza na kutulea vizuri sana. Tena mawazoni mwetu tunaweza kuona picha ya Yesu Mwanawe, kwa sababu yeye aliishi kati yetu kama mwanadamu. Lakini Roho Mtakatifu ni vigumu zaidi kuiona picha yake na kujenga uhusiano naye. Hatuna mifano rahisi ya kibinadamu ya kumlinganisha nayo. Walakini, Biblia inatoa habari za pekee zinazomhusu huyo Roho Mtakatifu:

Ni nafsi Mashuhuri. Yesu alimtaja huyo Roho Mtakatifu kama nafsi, mmojawapo katika ule Uungu, akiwa pamoja na Mungu Baba na Mungu Mwana:

"Basi enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la BABA, na MWANA, na ROHO MTAKATIFU" - (Mathayo 28:19).

Roho huyo anazo tabia za kibinaksi: yeye anayo NIA (Warumi 8:27); HEKIMA (1Wakorintho 2:10); anazo HISIA ZA UPENDO kwetu sisi (Warumi 15:30); anajisikia HUZUNI tunapotenda dhambi (Waefeso 4:30); anao uwezo wa KUTUFUNDISHA sisi (Nehemia 9:20); na uwezo wa KUTUONGOZA sisi.

Alihusika katika uumbaji. Huyo Roho Mtakatifu alishirikiana pamoja na Baba na Mwana katika kiumba dunia yetu hii.

"Hapo mwanzo Mungu alizumba mbingu na dunia... Roho wa Mungu alitembea juu ya uso wa maji" - (Mwanzo 1:1,2,KJV).

3. Kazi Za Roho Mtakatifu



(1) Huugeuza Moyo wa Mwanadamu. Katika kukutana kwake na Nikodemo, Yesu aliikazia sana kazi ya Roho Mtakatifu ya kuubadilisha moyo wa mwanadamu.

"Yesu akajibu, Amini, Amini nakuambia, mtu asipozaliwa kwa maji na kwa roho hawezi kuingia ufalme wa Mungu" - (Yohana 3:5).

Kuzaliwa kwa Roho" maana yake ni kwamba huyo Roho anatupatia sisi mwanzo mpya. Ni zaidi ya kuibadilisha kidogo hapa na pale tabia yetu. Huyo Roho anatubadilisha sisi kuanzia ndani kwenda nje, akitimiza ahadi hii, "Nami nitawapa ninyi moyo mpya" (Ezekiel 36:26).

(2) Hutuwezesha sisi kuyatambua matendo yetu mabaya na kutupatia shauku ya kuwa na utakatifu: **"Naye [Roho Mtakatifu] akiisha kuja, huyo ATAUHAKIKISHIA ULIMWENGU kwa habari ya DHAMBI na HAKI na HUKUMU" - (Yohana 16:8).**

Unaposikia kisa cha kusisimua juu ya mtu fulani anayeachana na maisha ya uasherati na kumgeukia Mungu na kuwa mwaminifu kwa mke au mume wake na kuwa mzazi anayejua kulea watoto, kumbuka kwamba kila hatua aliyochukua kuelekea kwenye uzima ilikuja kutohana na msukumo wa Roho Mtakatifu.

(3) Hutuongoza sisi katika maisha ya Kikristo. Yesu anazungumza nasi moja kwa moja kupitia kwa ile "sauti ndogo" ya huyo Roho.

GUNDUA

"Na masikio yako yatasikia neno nyuma yako, likisema, Njia ni hii ifuateni; mgeukapo kwenda mkono wa kulia, na mgeukapo kwenda mkono wa kushoto" - (Isaya 30:21).

Kwa njia ya matangazo ya Satelaiti, televisheni zetu zinatuletea daima katika sebule yetu picha na sura mbali mbali kutoka katika bara lililo mbali nasi. Roho Mtakatifu kwa kiasi kidogo anafanya kazi yake kama Satelaiti ya Mungu, akituletea kuwako kwake Kristo kutoka mbinguni kuja hapa duniani, na kumfanya awe karibu sana nasi wakati ule tunapomhitaji sana (Yohana 14:15-20).

(4) Hutusaidia sisi katika maisha yetu ya sala.

"Kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo; lakini Roho mwenyewe htuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa. Na yeye aichunguzaye mioyo aijua nia ya Roho ilivyo, kwa kuwa huwaombea watakatifu kama apendavyo Mungu " - (Warumi 8:26,27).

Tunapojitahidi sana kutafuta maneno yanayofaa, Roho anatuombea sisi. Tunapokuwa tumekata tamaa kiasi cha kuweza kupiga kite [kuguna] tu kwa Mungu, Roho anakikuza kilio chetu hicho kinyonge tunachotoa ili kuomba msaada kwake na kukifanya kiwe sala yenye nguvu mbele kabisa ya kile kiti cha enzi cha Mungu pale mahali anapoendelea kuhudumu Yesu sasa.

(5) Kukuza Sifa na Tabia ya Kikristo. Roho anawafanya watu wale walio kama jangwa kiroho kuwa kama mti ulio na rutuba, uzaao aina zote za matunda: **"LAKINI TUNDA LA ROHO ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole na kujitawala" - (Wagalatia 5:22,23).**

Kuwa na tunda la Roho huonyesha kwamba sisi tunapandikizwa katika ule Mzabibu wa kweli, yaani, Yesu (Yohana 15:5). Yesu anaweza kuishi kabisa maisha yake tele kupitia kwetu kwa njia ya uweza wa huyo Roho.



(6) Hututayarisha sisi kuwa mashahidi wake. Yesu anatoa ahadi hii:

"LAKINI MTAPOKEA NGUVU akiisha kuwajilia juu yenu Roho Matakatifu; nanyi mtakuwa MASHAHIDI WANGU.... Hata mwisho wa nchi" - (Matendo 1:8).

Wale wote wanaotaka wanaweza kufanya mashahidi wake kwa njia ya huyo Roho. Huenda sisi tusiweze kupata majibu yote, lakini huyo Roho anaweza kutupa sisi kisa fulani cha kusimulia kinachoigusa mioyo na akili za watu. Mitume wale walipata shida ya kuwasiliana na watu wale kabla ya Pentekoste, lakini baada ya yule Roho kuwajia, walimtangaza Kristo kwa uwezo uliowafanya wa "upindue ulimwengu" (Matendo 17:6, KJV).

4. Karama Za Roho

Maandiko yanaweka tofauti iliyo dhahiri kati ya kipawa cha Mungu cha Roho Mtakatifu ambacho anakitoa kwa KILA MUUMINI ili kumwezesha kuwa na maisha ya Kikristo yenye ushindi, na zile karama mbali mbali za Roho zinazotolewa kwa waumini ili wapate kutoa huduma yao kwa watu iletayo matokeo mazuri kwa kutumia njia mbalimbali.

"Hivyo husema [Kristo] alipopaa juu, aliteka mateka akawapa wanadamu vipawa. Naye alitoa WENGINE kuwa MITUME, na wengine kuwa MANABII, na wengine kuwa WAINJILISTI, na wengine kuwa WACHUNGAJI na WAALIMU, kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke hata mwili wa Kristo ujengwe" - (Waefeso 4:8, 11-12).



Si kila Mkristo anayepokea karama hizo zote, wengine wanaweza kupokea karama nyingi kuliko wengine; Roho ndiye "humpa kila mtu, kipaji tofauti kama apendavyo mwenyewe" (1 Wakorintho 12:11). Roho ndiye anayemtarisha kila muumini ili apate kufanya sehemu yake maalumu katika mpango wa Mungu. Mungu anajua ni lini na ni wapi aweze kutoa karama zitakazowaletea mibaraka mingi sana watu wake na kanisa lake.

Orodha ya karama za Roho inayopatikana katika 1 Wakorintho 12:8-10 naijumuisha hekima, maarifa, imani, karama za kuponya, unabii, kunena kwa lugha mbali mbali, na kutafsiri lugha (fungu la 8-10).

Paulo anatusisitizia kutaka sana karama zilizo kuu," halafu anaongeza kusema, "Hata hivyo nawaonesha njia iliyo bora." (1 Wakorintho 12:31). Sura ile ya upendo (1 Wakorintho 13) ambayo inakuja baada ya fungu hilo inatilia mkazo kwamba "lililo kuu kupita yote" ni upendo. Na huo upendo ni tunda la Roho (Wagalatia 5:22).

Tungejishughulisha sana kulitafuta hilo tunda la Roho, halafu kumwacha Roho atugawie karama zake kama "anavyopenda mwenyewe" (1Wakorintho 12:11).

5. Utimilifu Wa Roho Wakati Wa Pentekoste



Siku ile ya Pentekoste, Roho alimwagwa kwa kipimo kisicho na mpaka, ili kutimiza ahadi ya Yesu:

"Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu... hata mwisho wa nchi." - Matendo 1:8.

Wakati wa Pentekoste Roho aliwawezesha wale mitume kuhubiri injili wazi wazi katika lugha za watu "wa kila taifa chini ya mbingu" (Matendo 2:3-6).

Baadhi ya wanafunzi wa Biblia hulinganisha kuja kwake Roho na mvua zinazonyesha mapema katika majira ya kupukutisha (autumn) na mvua zile za mwisho katika majira ya kuchipua (spring) katika nchi ya Palestina (Yoeli 2:23). Roho yule aliyemwagwa siku ile ya Pentekoste alifanana na "mvua ya kwanza" ya majira ya kupukutisha ambayo ilizifanya mbegu kuota na kulipa lishe muhimu kanisa la Kikristo katika uchanga wake.

6. Mvua Ya Masika Ya Roho

Unabii wa Biblia unatuambia habari za siku inayokuja ambayo katika hiyo Roho wa Mungu atamwagwa kama manyunu ya mvua juu ya kanisa lake, akiwatia nguvu washiriki wa kanisa na kuwafanya mashahidi (Yoeli 2:28,29). Karne nyingi mpaka sasa zimekwisha kupita na habari ya wokovu imeenea katika sehemu kubwa ya ulimwengu huu. Sasa wakati umefika kwa "mvua ya masika" kunyesha ili kuzikomaza mbegu zilizoota, na kufanya nafaka iwe tayari kuvunwa.

Historia inapokwenda kufikia mwisho wake muda mfupi tu kabla ya Kristo kuja mara ya pili, Mungu atamfanya kila muumini aliye mwaminifu awe tayari kwenda mbinguni kwa njia ya kumwagwa kwa wingi sana kwa Roho wake. Je! wewe unaionja sasa ile "mvua ya kwanza" katika maisha yako, ambayo inaliandaa kanisa kupokea ile "mvua ya masika" ya Roho? Je! unaishi maisha yaliyojazwa Roho? Ukipewa uwezo huo na Roho, je! utamruhusu Mungu akutumie kupeleka habari ya upendo wake mwingi mno usiosadikika na habari ya kurudi kwake upesi?

7. Masharti Ya Kumpokea Roho Mtakatifu

Siku ile ya Pentekoste Roho Mtakatifu aliwagusa mioyo wale walioisikia injili hata wakapiga kelele, wakisema, "tutendeje ndugu zetu, tufanye nini sisi?" (Matendo 2:37).

"Petro akawaambia, 'TUBUNI MKABATIZWE, kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi zenu, NANYI MTAPOKEA KIPAWA CHA ROHO MTAKATIFU" - (Matendo 2:38).

Toba-yaani, kugeuka na kuiacha ile njia ya maisha ya dhambi na kumgeukia Kristo - ndilo sharti la kukipokea kipawa hicho cha Roho [wala sio kwa kunena kwa lugha]. Ili Roho apate kumwagwa juu yetu, ni lazima kwanza tutubu na kumkabidhi Kristo maisha yetu yote. Yesu alikazia pia ule utayari wa kumfuata yeye na kumtii kama sharti jingine la kupokea hicho kipawa cha Roho Mtakatifu (Yohana 14:15-17).



8. Maisha Yaliyojazwa Na Roho

Kabla hajaondoka duniani, Yesu aliwaagiza wafuasi wake, akisema:

"Wasitoke Yerusalemu, bali kingojeeni KIPAWA alichaoahidi Baba yangu kuwapa... Kwa kuwa Yohana ALIBATIZA KWA MAJI, bali, ninyi MATABATIZWA KATIKA ROHO MTAKATIFU baada ya siku chache" - Matendo 1:4,5.

Tena na tena Maandiko Matakatifu yanaonyesha kwamba Mkristo hana budi "kujazwa Roho Mtakatifu" (Matendo 2:4; 4:8; 4:31; 6:3; 6:5; 7:55; 9:17; 13:9; 13: 52; 19:6). Roho Mtakatifu anayafanya maisha ya Mkristo kuwa yenye utiifu na mazuri kwa sababu maisha yale yaliyojazwa na Roho hufikia kiwango kile kikamilifu cha maadili ambacho Kristo alikiweka kwa ajili yetu.

Akiwa anaeleza habari za maisha ya Kikristo yaliyojazwa na Roho Paulo alitoa ombi hili kwa niaba ya kila muumini:

"Naomba kwamba kutoka katika utajiri wa utukufu wake AWAFANYE IMARA KWA UWEZA WAKE KWA NJIA YA ROHO WAKE KATIKA UTUKUFU WENU WA NDANI, ili Kristo apate kukaa mioyoni mwenu kwa imani..... Basi, kwake yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyombayo au tuyawazayo, KWA KADIRI YA UWEZA WAKE UTENDAO KAZI NDANI YETU."

Kama Frank Moris, aliyejkuwa na mbwa wake mwaminifu wa kumwongoza, Basi, sisi tukiwa na kiogoz wetu Roho Mtakatifu ndani yetu, tunaweza kufanya mambo ya ajabu mno kuliko vile tulivyoweza kufanya zamani. Tukiwa na tamaa mpya na uwezo mpya tunawezeshwa naye kusonga mbele kwa imani badala ya kujaribu kuyastahimili tu matatizo ya maisha yetu.



Uzoefu wa kuwa na maisha haya yaliyojazwa na Roho unafanya kuwa mpya kila siku kwa njia ya maombi na kujivunza Biblia. Maombi yanatusogeza karibu sana na Kristo, na kule kujifunza Neno la Mungu kunatufanya tukaze macho yetu kuelekea kwenye nguvu zake. Mambo hayo yanakivunjilia mbali kizuizi cha aina yote kilichopo kati yetu na Kristo, ambacho kingeweza kumzuua asitumwagie kipawa chake cha Roho, ambacho thamani yake haikadiriki. Hivyo ndivyo tukuavyo na kuziondoa tabia zetu zile mbaya na mielekeo yetu mibaya, na mahali pake kuwekwa tabia nzuri.

GUNDUA

DISCOVER
online

Warumi 8 hutoa maelezo ya kusisimua juu ya maisha yaliyojazwa na Roho. Uisome sura hiyo kila uwazapo, na kuzingatia ni mara ngapi Paulo anasonda kidole chake kwa "Roho" wa maisha ya Kikristo.

Je! wewe umefanya ugunduzi wako wa ajabu kuhusu maisha yale yaliyojazwa na Roho? Je! unatambua kuwako kwa huyo Roho katika maisha yako? Je! unaunja ule uweza wake utiao uzima katika maisha yako? Fungua maisha yako ili ule uweza mkuu kuliko wote katika ulimwengu upate kuingia.

GUNDUA

MWOKOZI ALIYEPO DAIMA



Kijana mmoja wa Kiskoti, kwa jina Petro, alipopotea katika nyika yenye majani mengi usiku mmoja uliokuwa na giza jeusi kama wino, Mungu alimwita kwa jina lake: "Petro!" Sauti ile ya mbinguni ilipoita tena, Petro alisimama katika njia yake, akaangalia chini na kugundua kwamba alikuwa umbali wa hatua moja tu kutumbukia katika shimo la machimbo ya mawe lililokuwa limeachwa.

Je! isingekuwa ni ajabu kwetu sisi kama tungeweza kumsikia Mungu akituita kwa majina yetu? Je! yasingekuwa makubwa kwetu endapo yeye angekuwa rafiki yetu aliye karibu sana nasi-endapo tungeweza kukaa pamoja naye kabisa na kuongea naye kwa muda mrefu juu ya mapambano yetu tuliyio nayo pamoja na zile ndoto zetu?

1. Kwenda Kwa Yesu Bila Kizuizi

Amini usiamini, sisi tunaweza kwenda karibu sana na Yesu sasa kuliko vile ambavyo tungeweza endapo Yeye angeishi kabisa hapa pamoja nasi akiwa ni mtu anayeonekana kwa macho. Kuwa na Yesu kimwili katika mji wetu kwa kweli lingekuwa ni jambo la ajabu, lakini hebu fikiria juu ya yale makundi makubwa sana yatakayomsonga ili yapate kumwona kwa karibu zaidi. Fikiria juu ya muda wake mwangi ambaeo ungetakiwa kutumika. Lingekuwa ni jambo jema kuweza kupata dakika chache za kuongea naye ana kwa ana katika kipindi chote cha maisha yetu.

Kristo anapenda kujenga uhusiano wake na kila mmoja wetu. Hii ndiyo sababu moja iliyomfanya aondoke duniani humu ili kwenda mbinguni kufanya huduma ya pekee ambayo ingemwezesha kuja karibu na kila mmoja wetu kila siku. Kwa sababu Yesu hajafungwa mahali pamoja kama alivyokuwa alipokuwa hapa duniani, yeye kwa njia ya Roho Mtakatifu sasa yuko tayari kuweza kuyaongoza maisha ya kila mtu mmoja mmoja atakaye.

Je, ni ahadi gani ya kutia moyo aliyoitoa Yesu kabla hajapaa juu kwenda mbinguni?

"NAMI NIPO PAMOJA NANYI SIKU ZOTE naam, mpaka mwisho wa nyakati." - (Mathayo 28:20).

Je, Kristo anafanya kazi gani kule mbinguni ambayo inafanya uwezekano uwepo kwa yeye kuwa "pamoja nanyi siku zote?"

"Basi, tuzingatie kwa makini imani tunayoungama. Maana tunaye Kuhani Mkuu aliyeingia mpaka mbinguni; Yesu, Mwana wa Mungu. Huyu Mkuu wetu anaelewa kabisa unyonge wetu; yeye mwenyewe alijaribiwa kama sisi kwa kila namna lakini hakutenda dhambi. Basi, na tukikaribie bila hofu kitu cha enzi cha Mungu mwenye neema, tupokee huruma na neema ya kutusaidia wakati wa shida" - (Waebraania 4:14-16).

Zingatia ahadi hizi zinazotolewa kwetu tunapokuwa na Yesu kama mwakilishi wetu kila mmoja binafsi kule mbinguni: "Alijaribiwa kama sisi kwa kila namna." "Kutuhurumia sisi katika udhaifu wetu." "Kutusaidia wakati wa shida." Tukiwa na Yesu kama Kuhani wetu Mkuu hatuendelei tena kutanga mbali na mbingu iliyo mbali sana. Kristo anawenza kutukaribisha sisi kuingia kabisa mbele zake Mungu. Si ajabu, basi, kwamba tunaombwa sana tu "kikaribie bila hofu kitu cha enzi cha Mungu mwenye neema"



Je, Yesu anakaa mahali gani kule mbinguni?

"Lakini Kristo alitoa dhabihu moja kwa ajili ya dhambi milele dhabihu ifaayo kisha akaketi UPANDE KULIA WA MUNGU" - (Waebrania 10:12).

Kristo aliye hai-mmoja anayetuelewa sisi-ni mwakilishi wetu kila mmoja binafsi katika kiti kile cha enzi "mkono wa kuume wa Mungu."

Ni kwa jinsi gani maisha ya Yesu yalimwandaa kuwa Kuhani wetu?

"Ndiyo maana ilimbidi awe kama ndugu zake wa kila namna, ili awe Kuhani Mkuu wao aliye mwaminifu na mwenye huruma katika kumtumikia Mungu, ili dhambi za watu ziondolewe. Na, anaweza sasa kuwasaidia wale wanaojaribiwa na kuteswa" - (Waebrania 2:17,18).

"Ndugu" yetu aliyeshiriki katika ubinadamu wetu, na ambaye "alijaribiwa" kama sisi tunavyojaribiwa, hivi sasa yeye ni Kuhani wetu Mkuu ameketi upande wa kulia wa Mungu, "Alifanywa kama" sisi, anajua yale tunayoyapitia. Amepata kuwa na njaa, kiu, majoribu, na kuchoka sana kiasi cha kuishiwa nguvu. Alijisikia kwamba alikuwa na haja ya kuhurumiwa na kuweleka.

Lakini zaidi ya hayo yote, Yesu anazo sifa za kuwa Kuhani wetu Mkuu kwa sababu yeye alikufa ili "kufanya upatanisho" kwa ajili ya dhambi zetu. Alilipa gharama yote ya dhambi zetu kwa kufa badala yetu sisi. Hii ndiyo Injili, yaani, Habari Njema kwa wanadamu wote kila mahali na kwa wakati wote.

Mmojawapo wa Wakurugenzi wa Shule yetu ya Biblia anatusimulia kisa hiki kilichompata akisema "Binti yetu mdogo kabisa alipokuwa na umri wa miaka mitatu, alijibana kidole chake katika kiti cha kukunjwa, na kuuvunjavunja mfupa wake. Tulipomkimbiza kumpeleka kwa daktari, kilio chake kikali kutokana na maumivu yake kilituraruwa kweli mioyo yetu. Tena kikamgusa mtoto wetu wa miaka mitano kwa njia ya pekee. Sitaweba kusahau maneno yake aliyosema baada ya daktari kumshughulikia dada yake aliyejeruhiwa. Binti yule akalia kwa kwikwi, na kusema, 'Baba, natamani kingekuwa ni kidole changu mimi!'"

Wanadamu wote waliposetwa na dhambi na kuhukumiwa kufa milele, Yesu alisema, "Baba, natamani ningekuwa mimi." Naye baba akampa Yesu kile alichotamani pale msalabani. Mwokozi wetu amepitia kila aina ya maumivu makali ambayo kwayo sisi tuliteseka - na zaidi ya hayo!

2. Injili Katika Agano La Kale



Wana wa Israeli walipopiga kambi yao chini ya Mlima Sinai, Mungu alimwagiza Musa kujenga patakatifu ambapo paliweza kusafirishwa toka mahali hata mahali kwa ajili ya ibada "kama mfano wake, ulioonyeshwa [kwako Musa] mlimani "(Kutoka 25:40). Karibu miaka 500 baadaye, Hekalu kuu la mawe la mfalme Sulemani lilijengwa ili kuchukua mahali pa hema takatifu lililokuwa likichukuliwa huku na huku. Na hekalu lile lilijengwa kwa mfano ule ule kabisa kama lilivyojengwa hema takatifu lililokuwa linachukuliwa huku na huku.

3. Huduma Ya Yesu Kwetu Imefunuliwa Katika Patakatifu

Patakatifu na huduma zake hufunua kile anachofanya Yesu sasa katika hekalu la mbinguni, na anachofanya sasa hapa duniani ili kututayarisha na kutuongoza kila mmoja wetu katika maisha yetu ya kila siku.

Kwa kuwa patakatifu pale pa duniani palijengwa kwa mfano wa hekalu la mbinguni, basi, panaakisi patakatifu pa mbinguni ambako Kristo anahudumu sasa. Kutoka 25-40 huelezea habari za huduma ile na taratibu zake za kafara ya patakatifu pale pa jangwani kwa kinagaubaga sana. Muhtasari mfupi wa

GUNDUA

vyombo vya patakatifu huonekana katika Agano Jipya:



"Agano la kwanza lilikuwa na kawaida taratibu zake za ibada na maskani takatifu ya duniani. Palitengenezwa hema ambayo sehemu yake ya nje ilitwa Mahali Patakatifu. Humo mlikuwa na kinara cha taa, meza na mikate iliyotolewa kwa Mungu. Nyuma ya pazia la pili, kulikuwa hema iliyoitwa Mahali Patakatifu sana. Humo mlikuwa na madhabahu ya dhambi kwa ajili ya kufukizia ubani, na sanduku la agano, ambalo lilikuwa limepakwa dhahabu pande zote, na ndani yake mlikuwa na chungu cha dhahabu kilichokuwa na mana, fimbo ya Aroni ilikuwa imechanua majani, na vile vibao viwili vilivyoandikwa agano. Juu ya hilo sanduku kulikuwa na viumbe wenye mabawa, na mabawa yao yalitanda juu ya mahali ambapo dhambi huondolewa. Lakini sasa hatuwezi kusema kinaganaga juu ya mambo hayo" - (Waebrania 9:1-5).

Hema hilo takatifu lilikuwa na vyumba viwili, yaani, Patakatifu, na Patakatifu pa Patakatifu. Ua uliwekwa mbele ya pataktifu. Katika ua ule ilisimama madhabahu ya shaba nyeupe ambayo juu yake makuhani walitoa dhabihu zao, na birika la maji walimonawa.

Dhabihu zilizotolewa juu ya madhabahu ile ya shaba nyeupe ziliikuwa mfano wa Yesu, ambaye, kwa njia ya kifo chake msalabani alikuwa ndiye yule "Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu! (Yohana 1:29). Mwenye dhambi aliyetubu alipokuja na dhabihu yake kwenye madhabahu ile na kuziungama dhambi zake, alipokea msamaha na utakaso. Vile vile mwenye dhambi leo anapata msamaha na utakaso kwa njia ya damu yake Yesu (1 Yohana 1:9).

Katika chumba kile cha kwanza, au Patakatifu, kile kinara cha taa saba kiliwaka daima, kikimwakilisha Yesu ambaye ni "Nuru ya ulimwengu" inayowaka daima (Yohana 8:12). Meza ya mikate iliyowekwa wakfu ilimwakilisha yeye ambaye ni "Mkate wa Uzima" ambaye daima yupo kukidhi njaa yetu ya kimwili na kiroho (Yohana 6:35). Ile madhabahu ya dhahabu ya kufukizia uvumba iliwalikilisha huduma ya Yesu ya uombezi anayofanya kwa ajili yetu mbele za Mungu (Ufunuo 8:3,4).



Chumba cha pili, au Patakatifu pa Patakatifu, palikuwa na sanduku la agano liliofunikwa na dhahabu pande zote. Liliwakilisha kiti cha enzi cha Mungu. Kifuniko chake cha upatanisho, au kiti cha Rehema, kiliwakilisha uombezi wa Kristo, Kuhani wetu Mkuu, akiwaombea wanadamu wenye dhambi ambao wameivunja sheria ya Mungu ya Maadili [Amri Kuu]. zile mbaao mbili za mawe ambazo juu yake Mungu aliandika Amri Kumi zilihifadiwa chini ya kile kiti cha rehema. Makerubi wale wawili wa dhahabu wenye utukufu waliinamia kile kiti cha rehema kutoka katika kila mwisho wa lile sanduku. Nuru tukufu iliangaza katikati ya wale makerubi wawili, hiyo ikiwa ni ishara ya kuwako kwake Mungu mwenyewe.

Pazia lilipaficha pale Patakatifu ili pasionekane na watu wakati makuhani walipokuwa wakiwahudumia katika ule ua. Pazia la pili mbele ya Patakatifu pa Patakatifu lilikikinga kile chumba cha ndani kisionekane na makuhani walioingia katika chumba kile cha kwanza cha Patakatifu.

Yesu alipokufa pale msalabani, je, ni kitu gani kilitokea kwa pazia lile?
"Hapo pazia la hekalu likapasuka vipande viwili toka juu mpaka chini" - (Mathayo 27:51).



Patakatifu pa Patakatifu paliachwa wazi Yesu alipokufa. Baada ya kifo cha Yesu, hakuna pazia liwalo lote lote liwezalo kuwepo kati ya Mungu Mtakatifu na muumini aliye mnyofu wa moyo; Yesu, Kuhani wetu Mkuu, anatukaribisha na kutuingiza kabisa mbele za Mungu (Waebrania 10:19-22). Tunayo njia ya kukifikia chumba kile ambamo kimo kiti cha

GUNDUA

enzi cha Mungu kwa kuwa Yesu ni Kuhani wetu Mkuu aliye mkono wa kulia wa Mungu. Yesu ndiye anayetuwezesha sisi kuja mbele za Mungu - yaani, hadi ndani ya ule moyo wa upendo wa Baba. Basi "na tukaribie."

4. Ufunuo Wa Kristo Akifa Kutuokoa

Kama palivyotumika pale patakatifu pa kidunia kama mfano mdogo kabisa wa hekalu lile la mbinguni ambako Yesu anahudumu sasa kwa ajili yetu, huduma zile zilizoendeshwa katika patakatifu pale pa kidunia zilikuwa "mfano na kivuli cha mambo ya mbinguni" (Waebrani 8:5). Lakini ipo tofauti dhahiri ambayo inajitekeza: mkuhani wale waliohudumu katika hekalu la duniani wenyewe walikuwa hawana uwezo wa kusamehe walikuwa hawana uwezo wa kusamehe dhambi, lakini pale msalabani Yesu "alitokea mara moja tu katika utmilifu wa nyakati zile ili aziondolee mbali dhambi kwa kujitoa dhabihu yeye mwenyewe" (Waebrania 9:26).

Kitabu kile cha Mambo ya Walawi cha Agano la Kale kinaeleza kwa undani sana huduma zile zilizoendelea kufanywa katika patakatifu pale. Taratibu zile za ibada ya dhabihu ziligawanywa katika sehemu mbili: huduma za kila siku na huduma za kila mwaka. (Mwongozo 13 unazishughulikia huduma zile za kila mwaka).

Katika zile huduma za kila siku makuhani wale waliotoa dhabihu kwa ajili ya mtu mmoja binafsi na kwa ajili ya mukutano mzima. Mtu ye yote alipotenda dhambi, alitakiwa kuleta mnyama asiye na waa lolote kama sadaka yake ya dhambi, 'a[i]weka mkono wake juu ya kichwa cha hiyo sadaka ya dhambi, na kumchinja kuwa sadaka ya dhambi mahali hapo pa sadaka za kuteketezwa" (Mambo ya Walawi 4:29). Hatia ya mwenye dhambi yule ilipaswa kuhamishiwa kwa mnyama yule asiye na hatia kwa njia ya maungamo ya dhambi na kuweka mikono juu ya kichwa cha mnyama yule. Jambo hilo likuwa mfano wa Kristo akiwa amebeba hatia yetu pale Kalvari; yule mmoja asiye na dhambi alifanywa kuwa "dhambi kwa ajili yetu" (2 Wakorintho 5:21). yule mnyama wa dhabihu alipaswa kuuawa na damu yake kumwagua kwa sababu ilisonda kidole chake mbele kwenye ile adhabu kuu kuliko zote ambayo kwayo Kristo aliteswa vibaya pale msalabani.

5. Kwa Nini Damu?

"Pasipo kumwaga damu hakuna msamaha" (Waebrania 9:22). Kile kilichotokea katika patakatifu pale pa Agano la Kale kilisonda kidole chake mbele kwenye tendo lile moja kuu la wokovu alilolitenda Kristo. Baada ya yeye kufa kwa ajili ya dhambi zetu, "aliiingia patakatifu pale pawili mara moja tu kwa damu yake mwenyewe, baada ya kupata ule ukombozi wa milele" kwa ajili yetu (fungu la 12). Damu ya Yesu ilipomwagika pale msalabani kwa ajili ya dhambi zetu, "pazia lile la hekalu [kule Yerusalem] lilipasuka vipande viwili toka juu mpaka chini" (Mathayo 27:51). Kwa sababu ya ile kafara aliyoitoa Yesu pale msalabani, hapakuwa na haja tena ya kutoa dhabihu zile za wanyama.



Yesu alipomwaga damu yake kutoka katika msalaba ule, alikuwa anatoa sadaka ya maisha yake makamilifu ya utii kuwa badala ya kushindwa kwetu kwangi. Baba na Mwana walipotenganishwa kwa nguvu pale Kalvari, Baba aligeuka na kuangalia kwingine kwa utungu na Mwanawe alikufa kutokana na moyo wake uliopasuka. Mungu Mwana aliiingia katika historia yetu na kuchukua mwilini mwake athari kamili za dhambi zetu na kuonyesha wazi jinsi utendaji wa mabaya unavyoleta maafa ya kusikitisha kweli kweli. Hapo ndipo angeweza kuwasamehe wenye dhambi bila ya kuihafifisha dhambi. Kristo alifanya "amani kwa damu yake iliyomwagika pale msalabani" (Wakolosai 1:20).

6. Ufunuo Wa Yesu Akiishi Kutuokoa

GUNDUA

Je! ni kazi gani anayofanya Yesu siku-kwa-siku katika hekalu lile la mbinguni?

"**Naye kwa sababu hii aweza kuwaokoa kabisa wale wanaokuja kwa Mungu kuititia kwake, kwa sababu YU HAI SIKU ZOTE ILI AWAOMBEE**" - (Waibrania 7:25).

Yesu sasa "yu hai' ili kutoa damu yake, yaani, kafara yake, kwa ajili yetu. Sasa yeye anafanya kazi kwa bidii nyingi ili kumwokoa kila mwanadamu kutoka katika dhambi iletayo mauti. Wengine kwa kuelewa vibaya wanadhani kwamba Yesu, akiwa kama Mwombezi wetu, yuko kule mbinguni kwa madhumuni ya kumsihi sana Mungu ambaye hataki ili atusamehe sisi. Kwa kweli ni Mungu anayeikubali kwa furaha kubwa kafara ile aliyoitoa Mwanawe kwa ajili yetu.

Kama Kuhani wetu Mkuu, Kristo pia anawasihi sana wanadamu. Yeye anafanya kazi yake ili kuwasaidia wale ambao hawajali kitu ili waingalie kwa mara ya pili ile neema yake, anawasaidia wenye dhambi ambao wanakata tamaa ili walishikilie sana tumaini lao linalopatikana katika injili, na kuwasaidia katika waumini kupata utajiri mwangi zaidi katika maombi yao. Yesu anayatengeneza maisha yetu ili yapatane na amri [Kumi] za Mungu na kutusaidia kuzikuza tabia zetu ambazo zitawenza kustahimili lile jaribio la wakati.



Mungu aliyatoa maisha yake na kufa kwa ajili ya kila mwanadamu aliyepata kuishi katika dunia hii. Na sasa, yeye akiwa Kuhani Mkuu au Mpatanishi, "yu hai siku zote" ili kuwaongoza watu wakikubali kifo chake kwa ajili ya dhambi zao. Wanadamu hawatapotea kwa kuwa wao ni wenye dhambi, bali kwa sababu wanakataa kupokea msamaha ambao Yesu anawapa.

Dhambi iliharibu uhusiano wa karibu sana ambao Adamu na Hawa walifurahia kuwa nao pamoja na Mungu. Lakini Yesu, kama Mwana-Kondoo wa Mungu, alikufa ili kuwaweka huru wanadamu wote mbali na dhambi na kuwarudishia tena urafiki ule uliopotea. Je! hivi wewe umemgundua yeye kuwa ni Kuhani wako Mkuu, Mmoja aliye hai siku zote ili apate kuudumisha uhusiano huo uwe wa karibu na wa kusisimua sana?

Kifo chake Kristo kilichotolewa kama sadaka ya dhambi ni cha pekee kabisa. Huduma yake Kristo kule mbinguni haina kifani. Ni Kristo peke yake anayemleta Mungu karibu sana kando yetu. Ni Kristo peke yake anayefanya uwezekano uwepo kwa Roho wa Mungu kuweza kukaa kabisa ndani ya miyo yetu. Alijitoa kabisa yeye mwenyewe ili kutufanya sisi tutimike. Anastahili vile vile tujitoe wakfu kwake kama yeye alivyojitoa. Hebu na tumpokee kabisa kama Mwokozi na Bwana wa maisha yetu.

TOKA MDHAMBI MWENYE HATIA HADI MTAKATIFU ALIYESAMEHEWA

Hapakuwa na alama zo zote za vidole. Hakuna silaha yo yote iliyogunduliwa. Hakuna mtu ye yote aliywona mwuaji yule alipoingia katika ofisi ya yule daktari. Hakuna ye yote aliyesikia hata zilipofyatuliwa zile risasi. Lakini yule daktari alikuwa na risasi tano zimepenya shati yake.

Ilionekana kana kwamba ni uhalifu uliofanywa kwa ustadi sana. Mwanzoni Polisi hawakuweza kupata vidokezo vyo vyote. Lakini halafu waliona waya mwembamba sana uliofungwa kwenye chombo cha kuwekea kalamu ya risasi juu ya meza ya daktari yule. Waya ule ulikwenda kwenye kinasa sauti (tepurenkoda) kilichokuwa ndani ya mtoto wa meza. Chombo kile cha kuwekea kalamu ya risasi, wakang'amua, kilificha hasa ile maikrofoni aliyoitumia yule daktari kuweka kumbukumbu ya mazungumzo yake na wagonjwa aliokuwa akiwapa ushauri.



Wapelelezi waliirudisha nyuma ile tepu ya kurekodia sauti, na kwa mshangao wao, wakaanza kuisikiliza ile tepu ilipofunguliwa tena kuhusiana na uhalifu ule wenyewe. Mtu aliyeitwa Antoni alikuwa ameingia katika ofisi ile na kuanza mabishano makali na yule daktari. Risasi zikafyatuliwa. Tepu ile iliishia na sauti ya maumivu makali ya daktari yule, aliyejkuwa akifa juu ya lile zulia.

Kila habari ndogo ndogo ya kuogofya ilikuwa imerekodiwa. Yule mwuaji alidhani kwamba uhalifu wake ule ungebaki kuwa siri milele. Alikuwa mwangalifu sana kutokuacha kidokezo cho chote. Lakini ile tepu ilisimulia kisa chote.

Katika mwongozo huu tutajifunza habari za hukumu ya mwisho ya Mungu wakati wanadamu wanaendelea "kuhukumiwa sawa sawa na matendo yao kama yalivyorekodiwa katika vitabu vile" (Ufunuo 20:12). Kwa wale ambao hawajampokea Kristo kama Mwokozi wao, itakuwa ni habari mbaya kwao. Lakini hukumu hiyo ni habari njema za ajabu kwa wale waliouputa usalama wao ndani yake Kristo.

1. Unaweza Kuikabili Hukumu Hiyo Bila Kuogopa

"Tena Baba hamhukumu mtu ye yote, bali amempa Mwana hukumu yote." - Yohana 5:22.

Ni kwa jinsi gani ule msalaba ulimwandaan Kristo kuwa Hakimu wetu?

"Mungu alimtoa [Yesu] kuwa kafara ya upatanisho kwa njia ya imani katika damu yake. Alifanya hivyo ili kuonyesha wazi haki yake,... ili apate kuwa MWENYE HAKI NA MWENYE KUWAHESABIA HAKI wale wamwaminio Yesu" - (Warumi 3:25,26).



Kifo cha Kristo kama badala yetu kinamwezesha kufanya kazi yake kama Jaji mwenye haki, na Mwenye kuhesabia Haki aliye na rehema aezaye kumsamehe mwenye dhambi yule atubuye. Malimwengu yale yanayochungulia yanapouliza swali hili, "Je! yawezekanaje kwa Jaji yule asiyependelea kumtangaza mtu mwenye hatia kuwa hana hatia?" Kristo anaweza kutoa jibu lake kwa kuonyesha makovu katika viganja vyake. Amepata adhabu ya haki kwa ajili ya dhambi zetu katika mwili wake mwenyewe.

Vitabu vile vya mbinguni hutunza kumbukumbu za maisha ya kila mtu mmoja mmoja, na kumbukumbu hizo zinatumika katika hukumu hiyo

(Ufunuo 20:12). Hizo ndizo habari mbaya kwa wale wanofikiri kwamba dhambi zao za siri pamoja na uhalifu wao wanaoutenda havitarudi tena kamwe kuwasumbua. Lakini kuna habari njema za ajabu kwa

GUNDUA

wale wote waliompokea Kristo kwa moyo mnyofu kama mtetezi wao kule mbinguni. "Damu yake Yesu.... Yatusafisha dhambi yote" (1 Yohana 1:7).

Je, Yesu anatupa nini ili kubadilishana na maisha yetu ya dhambi?

"Mungu alimfanya [Kristo] aliyekuwa hana dhambi kuwa dhambi kwa ajili yetu ili ndani yake sisi tupate kuwa haki ya Mungu." - 2 Wakorintho 5:21.

Maisha yetu haya ya dhambi yanabadilishana na maisha yale makamilifu ya haki aliyokuwa nayo Kristo. Kwa ajili ya maisha yale yasiyo na dhambi na kifo chake Yesu, Mungu anaweza kutusamehe sisi na kututenda kana kwamba tulikuwa hatujapata kutenda dhambi kamwe.

Je, ni sifa gani alizo nazo Yesu ambazo zinamfanya kuwa Mtetezi na Jaji wetu?

2. Kristo Alikuja Wakati Ulipotimia

Wakati ule wa ubatizo wake, Yesu alipakwa mafuta na Roho Mtakatifu;
"Mara tu alipokwisha kubatizwa Yesu, alipanda kutoka ndani ya maji; dakika ile ile mbingu ikafunuka, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua na kutua juu ya ke. Na sauti kutoka mbinguni ikasema, "Huyu ni Mwanangu, ninayempenda; ni nayependezwa sana" - (Mathayo 3:16,17).

Baada ya kupakwa mafuta kwa Kristo na Roho Mtakatifu wakati ule wa ubatizo wake, wanafunzi wake walitangaza, wakisema:

"Tumemwona Masihi' [Kristo].'" - Yohana 1:41.

Wanafunzi wale walijua kwamba neno lile la Kiebrania "Masihi" lilimaanisha "Mpakwa Mafuta."

Luka, mwanafunzi wa Yesu, aliweka katika kumbukumbu zake mwaka wa Yesu aliopakwa mafuta kama Masihi kuwa ulikuwa ni mwaka ule wa kumi na tano wa Kaisari Tiberio (Luka 3:1). Kwetu sisi mwaka ule ungekuwa sawa na mwaka wa 27 B.K.



Zaidi ya miaka 500 kabla ya Kristo kuja hapa, nabii Danieli alitabiri kwamba Yesu angepakwa mafuta kama Masihi katika mwaka ule wa 27 B.K.

"Tangu kutolewa amri ile ya kuutengeneza na kuujenga upya Yerusalemu hata zamani zake Mpakwa Mafuta (Masihi).... Kutakuwa na majuma 'saba' na sitini na mawili jumla yake ni majuma sitini na tisa au siku 483 (7x69= siku 483). Katika mifano ya unabii wa Biblia kila siku ni sawa na mwaka mmoja (Ezekiel 4:6; Hesabu 14:34), hivyo siku hizo 483 ni sawa na miaka 483.

Danieli alitabiri kwamba amri ile ya kuutengeneza na kuujenga upya Yerusalemu ingetolewa katika mwaka ule wa 457 K.K. (Ezra 7:7-26). Kwa hiyo, ile miaka 483 ilikoma katika mwaka ule wa 457 na Kristo alipakwa mafuta mwaka wa 27 B.K., (yote hiyo miwili ikiwa ni sehemu tu ya miaka yenyewe, kwa hiyo, kipindi sahihi kingekuwa miaka 483).

Kwa wakati ule ule hasa uliowekwa katika mwaka ule wa 27 B.K. Yesu alijitokeza akiwa na ujumbe huu: "Wakati umetimia" (Marko 1:15). Kutimizwa kikamilifu kwa unabii huo wa Biblia ni uthibitisho unaovutia sana unaoonyesha kwamba Yesu wa Nazareti ni Masihi kweli, Mungu katika mwili wa kibinadamu.

Je, ni kwa muda gani Yesu alipaswa kuthibitisha ahadi ile?

"Naye alithibitisha agano [ahadi] thabiti na watu wengi kwa muda wa 'saba' moja [juma, Kiebrania].'" - Danieli 9:27, sehemu ya kwanza.

GUNDUA

Tunapoitumia kanuni ile ya mwaka mmoja siku moja, basi, "juma" hilo lingekuwa sawa na miaka saba - kuanzia 27 B.K. mpaka 34 B.K - Yesu angeweza ku "lithibitisha agano," au ile ahadi aliyokuwa ameitoa kwa Adamu na Hawa muda mfupi tu baada ya wao kutenda dhambi. Mungu alifanya agano, yaani, ahadi, kwamba angeiokoa jamii ile ya kibinadmu kutoka katika dhambi kwa njia ya yule mmoja ambaye angempeleka ili afe kwa ajili ya dhambi zetu (Mwanzo 3:5).

Je, kungetokea nini katikati ya juma hilo la sabini?

"Katikati ya hiyo "saba" [juma, Kiebrania] atakomesha sadaka na dhabihu." - Danieli 9:27, sehemu ya mwisho.



Yesu alisulibiwa katika mwaka ule wa 31 B.K. "katikati ya juma." Wakati ule wa kifo chake Kristo, Mungu akalipasua "pazia lile la hekalu... likapasuka vipande viwili toka juu mpaka chini" Mathayo 27:51. Mnyama yule wa dhabihu alikuwa karibu kuchinjwa (mfano wa Yesu "Mwana-Kondoo wa Mungu"), akaponyoka mikononi mwa Kuhani. Hii ilikuwa ni ishara ilioonyesha kwamba Mungu hakutaka wanadamu waendelee tena kutoa dhabihu za wanyama. Unabii ule ukatimizwa neno kwa neno, Yesu "akakomesha na kufanya pasiwe na haja tena ya kutoa dhabihu za wanyama. Tangu kufa kwake Kristo, watu wanamwendea Mungu si kwa njia ya dhabihu za wanyama na makuhani wa kibinadamu, bali kwa njia ya Masihi, Mwana-Kondoo wa Mungu na Kuhani wetu Mkuu.

3. Uhakika Wa Dhambi Zilizosamehewa

Kulingana na unabii wa Danieli, je, kwa nini Yesu alikuwa?

"Mpakwa mafuta huyo atakatiliwa mbali, lakini si kwa ajili yake mwenyewe." Danieli 9:26, pambizo.

Alipokufa pale msalabani, Yesu "a[li]katiliwa mbali." Alikufa, "lakini si kwa ajili yake mwenyewe," yaani, si kwa ajili ya kulipa fidia ya dhambi zake mwenyewe, bali kulipa fidia kwa dhambi za ulimwengu mzima.

Sisi twavezaje kujua kwamba Mungu amezisamehe dhambi zetu zote?

"Haki itokayo kwa Mungu huja kwa njia ya imani katika Yesu Kristo kwa wote waaminio... WOTE WAMEFANYA DHAMBI..., nao WANAHESABIWA HAKI bure KWA NEEMA YAKE, kwa njia ya ukombozi uliokuja kwa njia ya Yesu Kristo... KWA NJIA YA IMANI KATIKA DAMU YAKE" - (Warumi 3:22-25).

Pointi kuu katika mafungi hayo ni hizi: sisi "[s]ote [tu]mefanya dhambi, 'lakini kwa sababu ya "neema," ya Mungu, wote "wanahesabiwa haki" walio na "imani" katika uwezo wa kutakasa wa "damu" yake Kristo. Tunapohesabiwa haki, Mungu anatutangaza sisi kuwa hatuna hatia, anaondoa hatia inayotokana na dhambi zetu zilizopita. Na Mungu kwa njia ya imani katika Yesu Kristo.



Sisi sote tuliochakazwa na jitihada yetu ya kutaka kuwa wema kiasi cha kutosha, ili kukifiki kiwango kile kinachotakiwa kwa kutegemea uwezo wetu wenyewe, tunaweza kupata pumziko la kweli kwa kukubaliwa na Kristo kwa neema yake. Yeye anatuahidi sisi, anasema, "Njoni kwangu ninyi nyote msumbukao na wenyewe kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha" (Mathayo 11:28). Sisi sote tuliolemewa na mizigo ya makovu tuliyopata zamani, kujiona kuwa hatufai, tena tuna aibu, tunaweza kupata amani na utimilifu ndani ya Kristo.

4. Wakati Wa Hukumu Kuanza

GUNDUA

Katika sura ya nane ya Danieli malaika alimwonyesha yule nabii picha kubwa ya matukio ya siku za baadaye. Danieli alimwona (1) Kondoo mume, (2) beberu, na (3) kutoka katika mojawapo ya pembe za yule beberu, "pembe nyingine iliyokuwa ndogo mwanzoni na kukua nguvu zake" (Danieli 8:8,9); mifano hiyo inawakilisha (1)Umedi-Uajemi, (2) Uyunani (Ugiriki), na (3) Roma (Danieli 8:1-12,20-26).

Je, sehemu ya nne ya unabii huo ni ipi?

"Je, itachukua muda gani kwa maono haya kuweza kutimizwa-maono yahusuyo sadaka ya kuteketezwa ya kila siku....? Akaniambia, 'Itachukua jioni na asubuhi 2,300 [au siku, Kiebrania]; ndipo patakatifu patakapowekwa wakfu tena [patakapotakaswa]." - Danieli 8:13,14.

Danieli alizimia kabla yule malaika hajaweza kumweleza sehemu ya siku 2,300 ya unabii ule na sura ya nane inafunga bila kutoa tafsiri yake yote. Lakini baadaye yule malaika alitokea tena na kumwambia hivi: "**Yafahamu maono haya:** Saba' sabini [majuma, Kiebrania] yameamriwa [yamekatwa, Kiebrania] juu ya watu wako na mji wako mtakatifu, ili kumaliza makosa, kukomesha dhambi, na kufanya upatanisho kwa ajili ya uovu." - Danieli 9:22-24.

Kwa kweli, hizo siku 2,300 ni miaka 2,300, kila siku moja ikiwakilisha mwaka mmoja (Ezekiel 4:6). Majuma sabini, au miaka 490, ilikuwa ndiyo sehemu ya kwanza ya kile kipindi kirefu zaidi cha miaka 2,300. Vipindi vyote viwili vilianza katika mwaka ule wa 457 K.K. wakati Uajemi ilipotoa amri ya "kuutengeneza na kuujenga upya Yerusalem." Miaka ile 490 ikitolewa kutoka katika miaka 2,300, inabaki miaka 12,810. Ikiongezwa miaka hiyo 1,810 kwa mwaka 34 B.K; mwaka ambao miaka ile 490 ilifikia mwisho wake, inatufikisha kwenye mwaka ule wa 1844 B.K.

5. Patakatifu Pa Mbinguni Patakaswa - Hukumu

Malaika yule alimwambia Danieli ya kwamba katika ule mwaka wa 1844, yaani mwisho wa ile miaka 2,300, "patakatifu patatakaswa" (Danieli 8:14, KJV). Lakini hilo maana yake nini? Tangu mwaka wa 70 B.K. Waroma walipoliteketeza hekalu kule Yerusalem, watu wa Mungu hawana hekalu lo lote hapa duniani. Kwa hiyo patakatifu patakapotakaswa kuanzia ule mwaka wa 1844 ni lazima pawe ni pale patakatifu pa mbinguni ambapo hekalu lile la duniani lilikuwa nakala yake halisi.



Haya! Kutakaswa kwa patakatifu pale pa mbinguni maana yake ni nini? Israeli ya zamani iliita siku ile ya kupatakaswa patakatifu pa kidunia Yom Kippur, yaani, Siku ya Upatanisho. Kwa kweli ile ilikuwa ni Siku ya HUKUMU.

Kama tulivyogundua katika Mwongozo 12, kazi ile anayofanya Kristo kwa ajili yetu katika patakatifu pale ina awamu mbili: (1) Dhabihu za kila siku ambazo hulenga ile huduma ya Kuhani katika chumba kile cha kwanza cha Patakatifu. (2) Dhabihu ya kila mwaka ambayo inaitilia nguvu huduma ya Kuhani Mkuu katika chumba kile cha pili, yaani, Patakatifu pa Patakatifu (Walawi 16).

Katika lile hekalu la kidunia, watu walipozungama dhambi zao siku kwa siku, damu ya wanyama wale waliochinjwa ilimwagwa kwenye pembe ya madhabahu ile, kisha ilihamishiwa katika Patakatifu (Mambo ya Walawi 4 na 6). Hivyo, kwa mfano, siku baada ya siku dhambi zilizoungamwa ziliingizwa ndani ya Patakatifu na kuwekwa pale.

Halafu, kila mwaka, katika ile Siku ya Upatanisho, patakatifu pale palitakaswa kutohana na dhambi zote zilizoungamwa katika kipindi cha mwaka uliopita (Mambo ya Walawi 16). Ili kufanya utakaso huo, Kuhani Mkuu alitoa sadaka maalum ya mbuzi aliywewekwa wakfu. Kisha aliichukua damu yake na kuingia nayo mpaka Patakatifu pa Patakatifu



na kuinyunyiza damu ile ya utakaso mbele ya kile kifuniko cha upatanisho [kiti cha rehema] ili kuonyesha kwamba damu ya Yesu, Mkombozi aliyekuwa anakuja, ingeweza kulipa fidia ya dhambi ile. Kisha kwa mfano yule Kuhani Mkuu aliziondoa dhambi zile zilizoungamwa kutoka patakatifu pale na kuziweka juu ya kichwa cha mbuzi yule mwingine, ambaye alipelekwa mbali katika jangwa na kuachwa afe kule (Mambo ya Walawi 16:20-22).

Taratibu hiyo ya ibada iliyofanywa kila mwaka katika siku ya upatanisho ilipatakasa pale patakatifu kutokana na dhambi. Watu waliiona kuwa ilikuwa ni siku ya hukumu kwa kwa sababu wale waliokataa kuziungama dhambi zao walifikiriwa kuwa ni waovu, nao "walikatiliwa mbali na watu wake [Mungu]" (Mambo ya Walawi 23:29).

Alichofanya kwa mfano, yule Kuhani Mkuu, mara moja kwa mwaka, Yesu anafanya mara moja kwa wakati wote akiwa Kuhani wetu Mkuu (Waebania 9:6-12). Katika siku hii kuu ya hukumu yeze anaziondoa kutoka katika patakatifu dhambi zile zilizoungamwa za wale wote waliompokea kama Mwokozi wao. Kama sisi tumeziungama dhambi zetu, basi, yeze ataifuta kumbukumbu ya dhambi zetu wakati ule (Matendo 3:19). Huduma hiyo ni kazi ya hukumu ambayo Yesu alianza katika mwaka ule wa 1844.

Katika mwaka wa 1844 saa ya hukumu ilipoanza kule mbinguni ujumbe wa saa ya hukumu imekuja ulianza kuhubiriwa ulimwenguni kote (Ufunuo 14:6-7). GUNDUA Mwongozo baadaye litaushughulikia ujumbe huo.

6. Kukabiliana Na Kumbukumbu Ya Maisha Yako Hukumuni

Tangu mwaka wa 1844 Kristo, kama Jaji, amekuwa akiichunguza kumbukumbu ya kila mmoja aliyepeata kuishi ili kuthibitisha ni akina nani watakaokuwamo mionganini mwa wale watakaoolewa Yesu atakapokuja. Kama Jaji wetu, Yesu "anazifuta" dhambi zote za wenye haki kutoka kumbukumbu zao za maisha zilizoko kule mbinguni (Matendo 3:19).



Jina lako linapoitwa katika hukumu hiyo, itakuwa rahisi kwako kukabiliana na kumbukumbu ya maisha yako - ENDAPO wewe utakuwa umempokea Kristo kama mbadala wako. Na hukumu ya wenye haki itakapokwisha, Yesu atarudi duniani kuwalipa ujira wao (Ufunuo 22:12,14).

Je! hivi wewe u tayari Yesu akija? Au, je! kuna kitu fulani ambacho umekuwa ukimficha? Je! unao uhusiano huru na wa kweli na yule Mmoja anayetoa ahadi hii:

"Tukiziungama dhambi zetu yeze ni mwaminifu na wa haki, hata atuondolee dhambi zetu na kutusafisha udhalimu wote." - 1 Yohana 1:9.

Ungamo maana yake rahisi ni kukubali kukabiliana na dhambi zetu, kupokea msamaha wa Mungu, na kukiri kwamba tunahitaji uweza wake na neema yake.

Alipokuwa akilitembelea gereza moja katika mji wa Potsdam, mfalme Frederick William alisikiliza maombi kadhaa ya msamaha. Wafungwa wote waliapa kwamba Majaji wale walipendelea, mashahidi walikuwa wa uongo, au wanasheria walikuwa si wanyofu ambao walihusika na kifungo chao. Toka seli hata seli kisa kile kile cha kutendewa vibaya, wao wakiwa hawana hatia, kiliendelea kusimuliwa.

Lakini katika moja mfungwa mmoja hakuwa na la kusema. Akiwa ameshangaa, Frederick akamtania, "Nadhani na wewe pia huna hatia yo yote."

"Hasha, mfalme," yule mtu alijibu, "Mimi nina hatia, tena nastahili kabisa yote ninayopata."

GUNDUA

DISCOVER
online

Mfalme akamgeukia mlinzi na kumwita kwa sauti kuu, "Njoo umwachilie upesi mhuni huyu kabla hajaliharibu kundi hili zuri la watu wasio na hatia yo yote."

Je! tunajiandaaje kwa hukumu hiyo? Tunajiwekaje tayari kwa ajili ya kuja kwake Kristo? Kwa kuikiri kweli peke yake kwa moyo mnyofu: Mimi nastahili kabisa adhabu ya kifo kwa dhambi zangu, lakini yule mwingine amechukua mahali pangu na kunipa msamaha wake wa ajabu.

Amua sasa hivi kwamba chochote kile kinachotokea, wewe utadumisha uhusiano wako na Kristo ukiwa unatazamana naye jicho-kwa-jicho kwa unyofu wa moyo-kwa-moyo kwa uaminifu.

GUNDUA

SIRI YA OMBI LINALOJIBIWA



Anatoli Levitini, mwandishi na mwanahistoria wa Kirusi, alitumia miaka yake mingi katika Gulag ya Siberia, ambako dua zilizotolewa kwa Mungu zilionekana kana kwamba zimeganda ardhini. Lakini alirudi akiwa mzima kiroho. "Mwujiza mkuu kuliko yote ni maombi," aliandika. "Yanipasa tu kumgeukia Mungu kimawazo na mara moja naisikia nguvu inayoingia ndani yangu kutoka mahali fulani, inaingia katika roho yangu, na mwili wangu wote. Je! hicho ni kitu gani? Je, naweza kuipata wapi hiyo nguvu inifanyayo mimi kuwa mtu mpya na kuniokoa mimi, niliye mzee duni sana, niliyechoka na maisha, ambayo itaniinua juu ya dunia hii? Inatoka nje yangu - wala hakuna nguvu yo yote ulimwenguni humu ambyo ingeweza kuipinga."

Katika mwongozo huu tunaona jinsi maombi yanavyotusaidia kujenga uhusiano wenye nguvu zaidi pamoja na maisha ya Kikristo yenyе nguvu.

1. Kuzungumza Na Mungu

Je, tunawezaje kuwa na uhakika kwamba Mungu anatusikia tunapoomba?

"Ndipo mtaniita mimi na kwenda KUNIOMBA, nami NITA SIKILIZA. Nanyi mtanitafuta na kuniona, mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote." - Yeremia 29:12,13.

Je, ni uthibitisho gani aliota Yesu kuonyesha kwamba atasikia na kujibu maombi yetu?

"Basi nawaambia, Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, na mlango utafunguliwa kwenu." - Luka 11:9.

Maombi ni maongezi ya pande mbili. Hii ndiyo maana Yesu anaahidi anasema:

"Tazama nasimama mlangoni, nabisha. Mtu ye yote akiisikia sauti yangu, na kuufungua malngo, nitaingia na kula pamoja naye, na ye ye pamoja nami." - Ufunuo 3:20.

Kwa jinsi gani inawezekana kwetu kuketi na kuwa na maongezi mazuri wakati wa chakula cha jioni pamoja na Kristo? Kwanza, kwa kumwambia kila kitu tulicho nacho moyoni mwetu kwa njia ya maombi. Pili, kwa kusikiliza kwa makini. Tunapotafakari wakati wa maombi, Mungu anaweza kuongea nasi moja kwa moja. Na tunapolisoma Neno la Mungu kwa roho ya ibada, Mungu atawenza kuongea nasi kupitia katika kurasa zake.

Maombi yanaweza kuwa njia ya maisha kwa Mkristo.

"OMBENI BILA KUKOMA; shukuruni kwa kila jambo, maana hayo ndiyo mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu." - 1 Wathesalonike 5:16-18.

Je! sisi tunawezaje "kuomba bila kukoma?" Je, yatupasa kupiga magoti wakati wote au kurudia-rudia kusema maneno ya kumsifu au kutoa dua? La, hasha. Lakini tunapaswa kuishi karibu sana na Yesu kiasi cha kujisikia huru kusema naye wakati wo wote, na mahali po pote.

"Tukiwa katika makundi ya watu mitaani, katika shughuli ya kibashara, tunaweza kutoa dua yetu kwa Mungu na kumsiki atupe uongozi wake... Daima tungeacha wazi mlango wa moyo wetu na kuuacha



mwaliko wetu ukipanda juu ili Yesu aweze kuja moyoni mwetu na kukaa humo kama mgeni wetu wa mbinguni." - Steps to Christ, uk. 99.

Mojawapo ya njia bora sana ili kujenga uhusiano huo wa karibu sana ni kujifunza kutafakari wakati tunapoomba.

"Kutafakari kwangu na kumpendeze yeye, mimi ninapomfurahia BWANA." -Zaburi 104:34.

Unapoomba usiharakishe tu kuititia orodha ya mambo unayotaka. Ngojea. Sikiliza. Kutafakari kidogo ukiwa katika maombi kunaweza kuuboresha sana uhusiano wako na Mungu.

"Mkaribieni Mungu, naye atawakaribia ninyi." - Yakobo 4:8.

Kadri sisi tunavyozidi kumkaribia sana Yesu ndivyo kadri tunavyoweza kuonja kuwako kwake. Basi wewe unapaswa kuwa katika umbali wa kuweza kuongea na Yesu, wala usiwe na wasi wasi juu ya kusema maneno yaliyo sahihi. Ongea tu naye kwa unyofu wa moyo na bila kuficha kitu. Ongea juu ya kila kitu. Yeye amepitia maumivu makali sana ya kifo kile chenyewe ili apate kuwa Msiri wako.

2. Jinsi Ya Kuomba

Tunapoingia katika maombi, tunaweza kupenda kufuata muhtasari wa sala ya Bwana, sala ya mfano ambayo Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kuitikia ombi lao hili:

Tufundishe sisi kuomba.

"Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe, ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama huko mbinguni. Utupe leo riziki yetu. Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tulivyowasamehe wadeni wetu. Wala usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu, kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele. Amina" - (Mathayo 6:9-13).



Kulingana na mfano huo ambao Yesu aliutoa katika sala yake, sisi tunatakiwa kumwendea Mungu kama Baba yetu aliye mbinguni. Tumwombe kwamba mapenzi yake yatawale miyo yetu kama vile mapenzi yake yanavyotawala katika mbingu yote. Tunamtafuta ili atupatia mahitaji yetu ya kimwili, msamaha wake, kwa ajili ya kuwa na roho ya kuwasamehe wengine.

Kumbukeni ya kwamba uwezo wetu wa kuipinga dhambi unatoka kwa Mungu. Sala ya Kristo inahitimisha kwa maneno ya sifa kwake.

Safari nyininge Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kumwomba Baba "kwa jina langu" (Yohana 16:23) - yaani, kuomba kulingana na kanuni zake Yesu. Hii ndiyo maana Wakristo kwa kawaida hufunga sala zao kwa maneno haya: "Katika jina la Yesu, Amina." Amen (amina) ni neno la Kiebrania limaanishalo "Na iwe hivyo".

Japokuwa sala ya Bwana inatoa mwongozo juu ya mambo tunayotakiwa kuyaomba na jinsi ya kutunga sala, mawasiliano yetu na Mungu yanakuwa bora sana kama yanatoka moyoni mwetu kwa hiari.

Tunaweza kuomba juu ya kila kitu. Mungu anataka tumwombe msamaha kwa dhambi zetu (1Yohana 1:9), tumwombe atuongezee imani (Marko 9:24), tumwombe uponyaji wa maumivu na magonjwa yetu (Yakobo 5:15), na kumwagiwa kwa Roho (Zakaria 10:1). Yesu anatuthibitishia kwamba tunaweza kumpelekea yeye mahitaji yetu yote, pamoja na mashaka yetu; mno kuweza kumwomba.

GUNDUA

("Mwekeeni matatizo yenu yote, maana yeze anawatunzeni") - 1 Petro 5:7.

Mwokozi wetu anapendezwa na mambo yo yote madogo yahusuyo maisha yetu. Moyo wake huchangamka wakati inapomwendea miyo yetu kwa upendo na imani.

3. Maombi Ya Faragha



Wengi wetu tunayo mambo fulani ambayo tunasita kuwaambia hata marafiki zetu wa karibu sana. Kwa hiyo, Mungu anatalika sisi kuutta mzigo huo katika maombi yetu ya faragha: tukiwa kila mmoja peke yake na yeze. Si kwamba yeze anahitaji maelezo yote. Mwenyezi anajua vizuri sana kuliko sisi tunavyoju, makusudi yetu yaliyojificha moyoni mwetu, na chuki zetu zilizojificha ndani. Lakini tunahitaji kuifunua miyo yetu kwake yeze atujuaye mpaka ndani kabisa, na atupendaye milele. Uponyaji unaweza kuanza Yesu anapoweza kuyagusa majeraha yetu.

Tuombapo, Yesu, Kuhani wetu Mkuu, yu karibu nasi kutusaidia:
"Tunaye mmoja ALIYEJARIBIWA KWA KILA NJIA, KAMA SISI TUNAVYOJARIBIWA -lakini alikuwa hana dhambi. Basi na tukikaribie kiticha neema kwa ujasiri, ili tupate kupokea rehema na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji" - (Waibrania 4:15,16).

Je, una wasi wasi, mfadhaiko, hatia? Weka hayo mbele zake Bwana. Ndipo yeze anaweza kukidhi kila hitaji tulilo nalo.

Je, ni lazima tuwe na mahali maalumu pa maombi hayo ya faragha?
"wewe unaposali, ingia katika chumba chako, funga mlango na kumwomba Baba yako, ambaye.. atakujazi." - Mathayo 6:6.

Zaidi ya kuomba wakati wa kutembea mitaani, kufanya kazi, au kufurahia mkuutano fulani, kila Mkristo angekuwa na muda fulani uliotengwa kila siku kwa maombi yake yeze peke yake pamoja na kujifunza Biblia. Tunza miadi yako ya kila siku na Mungu wako wakati unapokuwa mchangamfu sana na wakati unapokuwa makini sana.

4. Maombi Ya Hadhara



Kujunga pamoja na wengine katika maombi huwaunganisha watu kwa kifungo maalum na kukaribisha uweza wa Mungu kwa njia ya pekee.

"Kwa kuwa wawili au watatu wanapokusanyika pamoja katika jina langu, nipo pamoja nao pale." - Mathayo 18:20.

Mojawapo ya mambo makuu kuliko yote tuwezayo kufanya sisi kama familia ni kukuza maisha ya maombi ya pamoja. Waonyesheni watoto kwamba tunaweza kupeleka mahitaji yetu kwake moja kwa moja. Watakuwa na msisimko juu ya Mungu watakapoona anajibu maombi yanayohusu mambo halisi ya maisha yao. Ifanyeni ibada ya familia kuwa wakati wa furaha na kubadilishana usoefu wa maisha katika hali ya uhuru.

5. Siri Saba Za Maombi Yanayojibiwa

Musa alipoomba, Bahari ya Shamu iligawanyika. Eliya alipoomba, moto ulishuka kutoka mbinguni. Danieli alipoomba, malaika aliyafumba makanwa ya simba wale wenye njaa kali. Biblia inatueleza visa vingi vya

GUNDUA

kusisimua nya maombi yaliyojibwa. Tena inapendekeza kwetu maombi kama njia ya kupata ule uweza kwetu maombi kama njia ya kupata ule uweza mkuu wa Mungu. Yesu anaahidi hivi:
"Mkiniomba neno lo lote kwa jina langu, nami nitalifanya" - (Yohana 14:14).

Lakini maombi mengine bado yanaonekana kana kwamba hayasikilizwi. Kwa nini? Hapa chini zipo kanuni saba zitakazokusaidia wewe kuomba kwa ufanisi zaidi:

(1) Uwe karibu sana na Kristo.

"NINYI MKIKAA NDANI YANGU, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtapewa." - Yohana 15:7.

Tunapoupa kipaumbele uhusiano wetu na Mungu na kuwa karibu naye, tutakuwa tunasikiliza na kutazamia kupata majibu kwa maombi yetu ambayo, vinginevyo, tusingeyatambua.

(2) Endelea Kumtumaini Mungu.

"MKIAMINI, mtapokea yote myaombayo katika sala zenu" - (Mathayo 21:22).

Kuamini au kuwa na imani, maana yake ni kwamba tunamtazamia Baba yetu aliye mbinguni kwamba kweli atatupa hayo mahitaji yetu. Kama wewe una wasiwasi kwamba huna imani, basi, kumbuka kwamba Mwokozi alitenda mwujiza kwa mtu yule aliyemsihi sana akiwa amekata tamaa, aliyesema:
"Naamini, nisaidie kutokuamini kwangu!" - (Marko 9:24).

Wewe kazana tu kuitumia imani ULIYO nayo; usiwe na waiswasi juu ya imani ile usiyo nayo.

(3) Jisalimishe kimya kimya chini ya mapenzi ya Mungu.

"Huu ndio ujasiri tulio nao kwake, ya kuwa, tukiomba kitu cho chote SAWA SAWA NA MAPENZI YAKE, anatusikia" - (1 Yohana 5:14).

Kumbuka kwamba Mungu anataka kutufundisha sisi, pamoja na kutupa sisi vitu, kwa njia ya maombi. Kwa hiyo, wakati mwingine anatuelekeza upande mwingine. Maombi ni njia ya kutusogezza sisi zaidi na zaidi karibu na mapenzi ya Mungu. Hisia zetu zinatakiwa ziwe kali kutambua majibu ya Mungu na kujifunza kitu kutokana nayo. Kuyafuatilia kwa karibu maombi yetu fulani fulani ya pekee pamoja na kile kinachotokea kuhusiana nayo ni msaada mkubwa kwetu.

Roho Mtakatifu atakusaidia kulenga shabaha yenyewe: "Roho anawaombea watakatifu kulingana na mapenzi ya Mungu"

(Warumi 8:27. Kumbuka kwamba mapenzi yetu yangeweza kulandana siku zote na mapenzi ya Mungu endapo sisi tungeweza kuona kama yeye anavyoona.

(4) Mngojee Mungu kwa Saburi.

"NALIMNGOJA BWANA KWA SABURI, akaniinamia akakisikia kilio changu" - (Zaburi 40:1).

Jambo kubwa hapo ni kukaza mawazo yako yote kwa Mungu, kukaza mawazo yako yote juu ya suluhisho lake. Wala usithubutu kumwomba Mungu akusaidie kwa dakika moja, na halafu kujaribu kuzizamisha shida zako kwa kujifurahisha katika anasa dakika inayofuata. Umnganje Bwana kwa saburi; tunahitaji kuwa na nidhamu hiyo vibaya sana.

(5) Usiing'ang'anie Dhambi iwayo yote.

("Kama ningalinua maovu moyoni, Mwenyezi-Mungu hangalinisikiliza")- Zaburi 66:18.



GUNDUA

Dhambi ijulikanayo hukata mara moja uweza wa Mungu katika maisha yetu; inatutenga mbali na Mungu (Isaya 59:1-2). Huwezi kuishika na kuing'ang'ania dhambi kwa mkono mmoja na kunyosha mkono mwingine kupokea msaada wa Mungu. Ungamo la dhambi litokalo moyoni hasa pamoja na toba ya kweli ndilo suluhisho la tatizo hilo.

Kama sisi hatutaki kumruhusu Mungu kutuweka huru mbali na mawazo, maneno na matendo yetu mabaya, basi, maombi yetu hayawezi kutuletea jibu lo lote.

"Hata mwaomba, wala hampati, kwa sababu mwaomba vibaya, ili mvitumie kwa tamaa zenu" - (Yakobo 4:3).

Mungu hatajibu "ndiyo" kwa maombi ya uchoyo. Acha wazi masikio yako yapate kuisikia sheria ya Mungu [Amri Kumi], yaani, mapenzi yake, naye ataacha masikio yake wazi kuzisikia dua zako.

"Yeye aligeuzaye sikio lake asiisikie sheria [Amri Kumi], hata sala yake ni chukizo" - (Mithali 28:9).

(6) Tambua Kwamba Unamhitaji Mungu.

Mungu huwajibu wale wanaoomba kuwako kwake na uweza wake katika maisha yao.

"Heri wenye njaa na kiu ya haki, maana hao watashibishwa." - Mathayo 5:6.

(7) Kuendelea Kuomba Tu.

Yesu alitoa kielelezo cha kuwapo kwa haja ya kuendelea tu kutoa dua zetu kwa kusimulia kisa kile cha mjane aliyejikuwa anaendelea tu kuomba na kuendelea kuja kwa hakimu akiwa na ombi lake lile, lile. Mwishowe yule hakimu alisema, huku akiwa ameudhika vibaya sana, "Kwa kuwa mjane huyu ananiudhi, nitahakikisha kwamba nampatia haki yake." Kisha Yesu alitoa hitimisho lake hili: "Je! Mungu hatawapatia haki wateule wake wanaomlilia mchana na usiku? Je! atazidi kuahirisha kuwapatia haki yao?" (Luka 18:5-7).

Zungumza na Mungu juu ya mahitaji yako yote, matumaini yako yote, na ndoto zako zote. Ombo mibaraka ya pekee, ombo msaada unapokuwa na shida. Endelea kutafuta, tena endelea tu kusikiliza, mpaka ujifunze kitu fulani kutokana na jibu lake Mungu.

6. Malaika Wanayahudumia Mahitaji Ya Waombao

Mtunga Zaburi alishangilia kwamba kwa njia ya huduma ya malaika wa Bwana maombi yake yalijibowi:

"Nalimtafuta BWANA akanijibu; akaniponya na hofu zangu zote... malaika wa BWANA hufanya kituo kuwazunguka wale wamchao na kuwaokoa" (Zaburi 34:4-7).

Tunapoomba, Mungu anawatuma malaika zake kujibu maombi yetu (Waebrania 1:14). Kila Mkristo anaye malaika wake mlinzi anayetembea pamoja naye:

"Angalieni msimdharau mmojawapo wa wadogo hawa. Kwa maana nawaambia ya kwamba MALAIKA WAO mbinguni siku zote huutazama uso wa Baba yangu aliye mbinguni." - Mathayo 18:10.

Kwa sababu ya maombi yetu tunayotoa:

"Bwana yu karibu. Msiwe na wasiwasi na jambo lo lote, lakini katika kila jambo kwa maombi na dua zetu pamoja na kushukuru, wekeni mambo yenu myatakayo mbele zake Mungu. Ndipo amani ya Mungu, ipitayo ufahamu wote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu." - Wafilipi 4:5-7.



7. Mtindo Wa Maisha Ya Kikristo

Biblia inaeleza wazi juu ya mtindo wa maisha ya Kikristo. Kulingana na Waefeso 4: 22-24, Mkristo anatakiwa ku"vua" mtindo wake wa maisha ya zamani uliotokana na "tamaa zenyekudanganya", na ku"vaa" mtindo mpya wa maisha ambao ume"umbwa kwa mfano wa Mungu." Katika maandiko hayo na mwongozo tuligundua kwamba wakati ule wa kuzaliwa upya sisi tuna"umbwa upya" kuwa watu tofauti ndani ya Kristo.

Mwongozo huu na miongozo sita inayofuata hutangaza upya mtindo wa maisha ya Mkristo; huifunua siri ya maisha ya Kikristo yenye furaha. Itakusaidia wewe kujenga uhusiano wenye nguvu zaidi na Kristo, ambao matokeo yake yatakuwa mtindo wa maisha ya Kikristo ulio tofauti. Kwa hiyo kaza macho yako kwa Yesu leo hii, nawe unaweza kuwa na sehemu katika sherehe ile ya mwisho ya ushindi wakati amani yake Kristo itakapotawala bila kupingwa.

SIRI YA FURAHA

Mwaka 1943, majeshi ya Uvamizi ya Kijapani yaliwaamuru wale "Wananchi Maadui" wa Kimarekani na Ulaya kwenda katika kambi la waliotekwa vitani katika lile Jimbo la china la Shantung.

Walilazimika kustahimili miezi mingi ya kuchosha sana, ya kukata tamaa, ya kusongamana pamoja na ya hofu. Watu wenye tabia tofauti waligongana, hasira zililipuka. Magomvi madogo madogo yaliongezeka sana.

Lakini mtu mmoja alielezwa na mfungwa mmoja wa kivita kwamba "bila shaka lolote alikuwa ni mtu aliyehitajika sana na kuheshimiwa sana, tena aliyependwa sana katika kambi lile." -Eric Liddell, Mmisionari kutoka katika nchi ya Waskoti (Scotland).

Malaya mmoja wa Kirusi katika kambi lile baadaye aliweza kukumbuka ya kwamba yule Liddell ni mwanaume peke yake aliyweweza kumtendea yule mwanamke jambo lolote bila kutaka kulipwa kimwili. Mwanamke yule alipokuja mle kambini kwa mara yake ya kwanza, akiwa peke yake, na mwenye kudharauliwa, ndiye aliyemtengenezea ye ye baadhi ya rafu za kuwekea vitu vyake.

Mfungwa wa vita mwingine alikumbuka kwamba, "ye ye alikuwa na mbini ya upole, na ya kuchekesha iliyozilainisha hasira zao zilizovurugika vibaya".



Katika mukutano mmoja uliojaa hasira wa wafungwa wale wa kivita, kila mmoja alikuwa akitoa madai yake kwamba mtu fulani mwingine ndiye angefanya kitu fulani kwa wale vijana watukutu wenye umri wa kuanzia miaka kumi na mitatu hadi kumi na tisa (matineja) amba walikuwa wanajitia katika matatizo. Liddell akatoa suluhisho lake. Aliandaan michezo ya kujiburudisha, ufundi wa kutengeneza vitu kwa mikono, na madarasa kwa ajili ya watoto wale, na kuanza kutumia wakati wake wa jioni pamoja nao.

Liddell alijipatia sifa na utukufu katika Michezo ya Olimpiki ya mwaka wa 192, alijinyakulia nishani ya dhahabu katika mbio za mita 400. Lakini katika uwanja ule mdogo sana wa kambi lile alijionyesha pia ya kuwa ni mshindi katika zile mbio za Kikristo, akajipatia sifa kutoka kwa wafungwa wa vita wale walioipenda sana dunia hii.

Jel! Ni kitu gani kilichomfanya kuwa mtu wa aina yake? Ungeweza kuwa umeigundua siri yake saa 12 kila asubuhi. Ule ndio wakati alipotoka kimya kimya kwa kunyatia akiwapita wenzake walialala usingizi, na kutulia kimya mezani, na kuiwasha taa ndogo ili itoe mwanga wa kumwezesha kuliona daftari lake ndogo na Biblia yake. Eric Liddell alitafuta neema na nguvu kila siku kutoka katika utajiri wa Neno la Mungu.

1. Kitabu Cha Mwongozo Wa Kuishi Mtindo Wa Maisha Ya Kikristo



Biblia iliandikwa kama kitabu cha Mwongozo kwa Mkristo. Kimejaa visa vingi vya watu halisi walio kama sisi waliokabiliwa na changamoto zile zile tunazokutana nazo kila siku. Kuwafahamu wahusika hao wa Biblia - furaha na huzuni zao, matatizo yao na nafasi zao nzuri walizopata hutusaidia sisi kukomaa kama Wakristo.

Mtunga Zaburi, Daudi aonyesha mfano wa kulitegemea Neno la Mungu kila siku kwa kulilinganisha na mwanga wa tochi (kurunzi); **"Neno lako ni taa ya miguu yangu na mwanga wa njia yangu."** **Zaburi 119:105.** (Isipokuwa pale ilipoelezwa vinginevyo, mafungu yote ya Maandiko katika GUNDUA Miongozo yanatoka katika Toleo

GUNDUA

DISCOVER
online

Jipya la Kimataifa la Biblia - New International Version (NIV).

Nuru tunayoipata kila siku kutoka katika Biblia inafunua wazi sifa zile tunazozihitaji katika maisha yetu na kanuni za kukua kiroho. Zaidi ya hayo yote, Biblia inatuonyesha Yesu, Nuru ya Ulimwengu. Maisha yetu yana maana tu anapoyaangazia Yesu kwa Nuru yake.

2. Urafiki Unaotubadilisha Kabisa



Kristo anataka Biblia kwako iwe kama barua ulioandikiwa mwenyewe itokayo kwa rafiki yako wa karibu sana.

"Ninyi nimewaita rafiki, kwa sababu kila kitu nilichokisikia kwa Baba nimewajulisheni." - Yohana 15:15.

Yesu anatutakia mema matupu. Neno lake linatuingiza sisi katika familia ile ya ndani ya Mungu; Yaani, ya wale anaowaambia siri zake na kuwafundisha yeze mwenyewe.

"Nimewaambieni ninyi mambo hayo, ili ndani yangu ninyi mweze kuwa na amani." - Yohana 16:33.

Ili kuweza kuionja amani hiyo, na uhusiano huo thabiti pamoja na Kristo, ni lazima tuzisome barua zake anazotutumia. Hivyo ndivyo Biblia ilivyo: ni barua zitokazo mbinguni. Usiziache barua hizo bila kuzifungua. Ujumbe uwezao kuyabadilisha kabisa maisha yako ambao unauhitaji umo ndani ya Neno hilo.

Hapa upo ushuhuda mmoja kamili uhusuo matokeo ya kuisoma Biblia. "Mimi nilihitaji msaada, nao niliupata ndani ya Yesu. Kila haja yangu ilitimizwa, njaa ya nafsi yangu ilishibishwa; kwangu Biblia ni ufunuo wake Kristo. Namwamini Yesu kwa sababu yeze kwangu ni Mwokozi wa Kimbingu. Naiamini Biblia kwa sababu nimeiona kuwa ni sauti ya Mungu rohoni mwangu." - The Ministry of Healing, uk. 461.

3. Miongozo Ya Kuishi Kwa Kufuata Biblia Na Zile Amri Kumi

Kuziangalia kwa kifupi tu hizo Amri Kumi kutatusaidia kuelewa kwa nini hizo pamoja na Biblia hujenga msingi muhimu sana wa maisha yaliyo manyofu.

Amri hizo kwa kawaida huangukia katika sehemu kuu mbili. Zile nne za kwanza hufafanua uhusiano wetu na Mungu, na zile sita za mwisho hufafanua uhusiano wetu na watu wengine. Zinapatikana katika Kutoka 20:3-17.

Amri mbili za kwanza zinaelezea uhusiano wetu na Mungu pamoja na ibada yake.

- I. "Usiwe na Miungu mingine ila Mimi".
- II. "Usijifanyie sanamu ya kuchongea. Usizisujidie wala kuzitumikia..."

Amri ile ya 3 na ya 4 hueleza kwa juu juu tu uhusiano wetu na jina la Mungu na siku yake takatifu.

- III. "Usilitaje bure jina la BWANA, Mungu wako..."



GUNDUA

DISCOVER
online

IV. "Ikumbuke siku ya Sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote, lakini siku ya saba ni Sabato ya BWANA, Mungu wako..."

Amri ya 5 na ya 7 inaimarisha vifungo vya familia.

V. "Waheshimu baba yako na mama yako...."

VI. "Usizini."

Amri ya 6, 8, 9 na 10 hutulinda sisi katika uhusiano wetu kijamii.

VII. Usiue."

VIII. "Usiibe."


IX. "Usimshuhudie jirani yako uongo."

X. "Usiitamani nyumba ya jirani yako. Usimtamani mke wa jirani yako..... wala chochote alicho nacho jirani yako."

Amri hizo kumi zinaweka mipaka ya uhusiano wetu kwa Mungu na kwa watu wengine. Hizo ni nguzo za kutuongoza katika mtindo wa maisha yetu ya Kikristo.

4. Aliyosema Yesu Juu Ya Hizo Amri Kumi

Siku moja Yesu alipokuwa akifundisha, kijana mmoja mwanaume mwenye ari kubwa aliharakisha kwenda kwake na kumwuliza, "Mwalimu, nitende jambo gani jema ili nipate uzima wa mielel?" (Mathayo 19:16). Yesu aliweza kuona yule kijana alikuwa akipambana na tatizo la fedha, ndipo akamshauri kuachana na mali yake na ku"zishik(a) amri" (fungu la 17).



Yule kijana mwanaume alijaribu kuukwepa utambuzi wa tatizo lake alioufanya Kristo kwa kuuliza ni amri zipi alizokuwa akiziongelea. Yesu akaorodhesha amri kadhaa katika zile Amri kumi (fungu la 18, 19).

Mwishowe, yule "mtawala kijana tajiri" aligeuka na kwenda zake kwa huzuni (mafungu ya 20-22). Kiakili ye ye alizikubali zile Amri kumi, ila hakuweza kuiti roho ya ile Sheria kwa kuachana na njia yake ya maisha ya uchoyo.

Amri kumi zinatuonyesha sisi mipaka ambayo ndani yake unaweza kukua uhusiano wenye afya pamoja na Mungu na kila mmoja wetu. Yesu alisonda kidole chake kwenye utii kuwa huo ndiyo njia ya kuipata furaha ya kweli.

"MKIZISHIKA AMRI ZANGU, mtakaa katika pendo langu, kama vile mimi nilivyozi shika amri za Baba yangu na kukaa katika pendo lake. Mimi NIMEWAAMBIA NINYI ILI furaha yangu iwe ndani yenu, na FURAHA YENU IWE KAMILI." Yohana 15:10,11.

5. Mwongozo Kwa Maisha Yenye Furaha

Kitabu cha Mhubiri ni taarifa ya utafiti wa Sulemani juu ya furaha. Anaandika kumbukumbu ya safari zake za kutafuta furaha katika utajiri wa ulimwengu huu, nyumba za kifahari, mashamba ya mizabibu izaayo sana, bustani nzuri sana, na mashamba ya miti ya matunda matamu sana yenye harufu nzuri. Aliongeza idadi ya watumishi wake. Alijikuta amezungukwa na kila kitu ambacho mtu angeweza kukitamani. Lakini furaha ikateleza na kwenda mbali naye, ndipo akaandika, akasema. **"Nilipozichunguza kazi zote**

GUNDUA

DISCOVER
online

zilizokuwa zimefanywa na mikono yangu, na kusumbuka kwangu kote katika kuzitenda, kila kitu kilikuwa hakina maana kabisa, ilikuwa ni sawa na kujilisha upemo" - (Mhubiri 2:11).

Ndipo Sulemani alipogeuka ili kuzitafuta anasa za ulimwengu huu kwa tumaini la kuipata furaha. Akatawaliwa na mvinyo, wanawake, na nyimbo. Hitimisho lake ni hili:

"Bure kabisa, bure kabisa, nakuambia mimi, Mhubiri! Kila kitu ni bure kabisa" (Mhubiri 12:8.

Zamani Sulemani alikuwa amepata kuonja na kuona ya kuwa Bwana yu mwema. Alipoyalanganisha maisha yake yale ya kwanza ya utii wake kwa Mungu na maisha yake ya kutafuta furaha katika mambo ya dhambi bila kujali kitu, wosia wake ukawa ni huu:

"Hili ndilo hitimisho la jambo hilo: Mche Mungu, na kuzishika amri zake, kwa maana huo ndio wajibu wote umpasao mtu." - Mhubiri 12:13.

Sulemani aliona angeweza kutafuta njia ya mkato ya kupata furaha kwa kuishi maisha mapotovu. Karibu na mwisho wa maisha yake, alikuwa mwanaume tosha kuweza kukiri kosa lake. Ili kuwaokoa wengine wasitende kosa lile lile, aliandika maneno haya, **"Yule aitunzaye Sheria, ana furaha."** Mithali 29:18, KJV.

6. Amri Kumi Ni Mwongozo Muhimu Sana Wa Agano Jipya

Katika Agano jipya, Yakobo alitoa ushuhuda wake huu:

"Maana yeote anayeishika sheria yote, lakini anajikwaa katika neno moja tu ana hatia ya kuivunja yote. Kwa maana yeye aliyesema; "Usizini, pia alisema, "Usiue", Usipozini, lakini ukiua, umekuwa mvunja sheria. Semeni ninyi, na kutenda kama watu wale watakaohukumiwa kwa sheria inayowapa uhuru. "Yakobo 2:10-12.

Charles Spurgeon, Mhubiri Mkuu wa Kibaptisti wa karne iliyopita alitangaza akisema." Sheria ya Mungu ni Sheria ya Mbinguni - takatifu, ya Mungu, na kamiliifu---- Hakuna amri yake hata moja iliyozidi kiasi; hakuna amri yake hata moja iliyopungua mno, lakini yenye haina kifani kiasi kwamba ukamiliwu wake ni uthibitisho wa Uungu wake." John Wesley, mmojawapo wa Waasisi wa Kanisa la Methodisti, aliandika maneno haya juu ya tabia ya kudumu ya sheria hiyo. "Sheria hiyo ya Maadili iliyo katika hizo amri kumi.... Yeye (Kristo) hakuiondoa.... Kila kipengele cha Sheria hiyo ni lazima kiendelee kuwa na nguvu juu ya wanadamu wote na katika vizazi vyote.... Sermons, gombo la 1, kurasa 221,222.



Billy Graham, Mwinjilisti wa Kiinjili wa Ulimwengu mzima aliyeheshimiwa sana, anaziheshimiwa sana Amri kumi kiasi kwamba ameandika kitabu kizima juu ya umuhimu wa amri hizo kwa Mkristo.

7. Uwezo Wa Kutii

Biblia pamoja na zile Amri Kumi ni mwongozo usiobadilika, wa muhimu sana, na mkamiliwu uletao maisha yenye furaha. Lakini, basi, mioyo ya watu bado inayo mapambano ndani yake. Mwanamke mmoja alijieleza kama ifuatavyo: "Mimi naamini kwamba hizo Amri kumi zinawafunga watu wote, nina hakika kwamba kuzishika huleta furaha. Nimejitahidi kwa nguvu zangu zote kuzishika, lakini siwezi kuzishika. Ninaanza kuamini kwamba hakuna mtu mwininge awaye yote anayeweza kuzishika."

Mwelekeo wa asili wa mtu ni kujaribu kuishi maisha hayo ya utii kwa hizo amri za Mungu. Lakini kujitahidi kama huko, tena na tena,



GUNDUA

kunakotoka katika moyo wenye dhambi wa mtuhuleta jibu hili la kukatisha tamaa, "Mimi siwezi kutii!" kwa nini? Kwa sababu.

"Nia yenyе dhambi ina uadui na Mungu. Haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii." Warumi 8:7.

Je! Kusudi la sheria hiyo ya Amri kumi ni nini?

"Kwa njia ya sheria (Amri kumi) sisi tunaitambua dhambi." Warumi 3:20.

Kazi ya sheria (Amri Kumi) ni kutufanya tutambue kabisa kwamba sisi" tu wenye dhambi tulipotea na kuwa bila tumaini, ambao tunamhitaji Mwokozi.

"Sheria (Amri kumi na Sheria ya Kafara) ilipewa madaraka juu yetu kutuongoza kwa Kristo ili tupate kuhesabiwa haki kwa imani." - Wagalatia 3:24.

Yesu ndiye jibu! Mara tu sisi tunapokuwa miguuuni pake Yesu, tukiwa hatuna uwezo wowote kabisa, tunaweza kupokea msamaha kwa ajili ya dhambi zetu, pamoja na uwezo toka kwake utakaotuwezesha kuzitii amri zake kwa njia ya imani.

8. Utii Kwa Amri Kumi Utokanao Na Upendo

Yesu anatuambia kwamba utii ni matokeo ya upendo.

"Mkinipenda, mtazishika amri zangu" - Yohana 14:15.

Tukimpenda Mungu, tutazitii amri zile nne za kwanza zinazofafanua uhusiano wetu na Mungu; na kama tukiwapenda watu, basi, tutazitii zile sita za mwisho ambazo hufafanua uhusiano wetu na wengine.

Mtu awaye yote anayezikanyaga Amri Kumi chini ya miguu yake anatenda dhambi.

"Kila mmoja atendaye dhambi anaivunja sheria (Amri Kumi); ukweli ni kwamba, dhambi ni uvunjaji wa sheria (Amri kumi)," 1Yohana 3:4.

Lakini Mungu na ashukuriwe, tunaye Mwokozi aliyejuka katika dunia hii na kufa, alifufuliwa, na sasa yu hai kwa ajili ya kusudi moja tu:

"Lakini ninyi mnajua ya kwamba alikuja ILI AZIONDOE DHAMBI ZETU."- Fungu la 5.



Ndani yetu hatuna uwezo wowote kutuwezesha kuishika hiyo sheria ya Mungu (amri kumi). Upendo wa Mungu "uliomwagwa.... Ndani ya mioyo yetu" ndilo tumaini letu la pekee.

9. Neema Ya Mungu Na Utii Wetu Kwa Sheria Yake

Wokovu ni zawadi. Hatuwezi kuufanya kazi ili tuweze kustahili kuupata. Tunaweza tu kuupokea kwa imani. Tunakupokea huko kuhesabiwa haki (kuwa katika msimamo sahihi na Mungu) kama zawadi; kwa njia ya imani peke yake kwa sababu ya neema yake Mungu.

"Kwa maana MMEOKOLEWA KWA NEEMA, kwa njia ya IMANI-na hiyo haitokani na nafsi zenu wenyewe, ni ZAWADI TOKA KWA MUNGU - Si kwa matendo, mtu ye yote asije akajisifu" Waefeso 2:8.

Hatuwezi kuzishika amri hizo kwa matendo yetu wenyewe - yaani, kwa kujitahidi kwetu. Hatuwezi kuzishika amri hizo ili tupate kuokolewa. Lakini tunapomwendea Yesu kwa imani na unyenyekevu na kuokolewa naye, hapo ndipo upendo wake unaijaza miyo yetu. Kama matokeo ya neema hiyo ya Mungu na kukubaliwa naye, sisi tunaingiwa na shauku ya kumfuata yeye na kumtii kwa njia ya uwezo wa upendo wake ulio ndani ya miyo yetu (Warumi 5:5).

Paulo anatilia mkazo wake juu ya kutokufaa kabisa kwa juhudzi za kibinadamu, naye anadokeza kwamba sisi hatuko chini ya sheria kama njia ya kujipatia wokovu wetu, bali tuko "Chini ya neema."

"Je! Tutende dhambi (tuzivunje Amri kumi) kwa sababu hatuko chini ya sheria (amri kumi) bali chini ya neema? Hasha!" - (Warumi 6:15).



Kwa nini? Kwa sababu moyo ule unaosukumwa na upendo unazaa maisha ya utii utokanao na upendo huo! (Warumi 13:10). Kumpenda Kristo ni kumtii yeye.

"Yeye aliye na amri (kumi) zangu na kuzitii, ndiye anipendaye mimi." Yohana 14:21.

Eric Liddel alidhihirisha kwamba, hata katika mazingira mabaya sana, muumini aliyepewa uweza wa Mungu unaweza kuishi maisha ya kuridhika, maisha ya utii. Liddell alionyesha wazi tabia yake iliyowavutia watu katika kipindi kile cha dhiki na hofu. Uhusiano wake wa upendo kwa Kristo ulimtia nguvu kwa njia ya Roho Mtakatifu, na kumwezesha kuyatimiza "matakwa ya haki yanayodaiwa na sheria" (Warumi 8:1-4). Uhusiano wa upendo na yule Mwokozi aliyesubiliwa na kufufuka unaweza kuzaa aina hiyo ya maisha.

Je! Hivi wewe umeigundua mwenyewe siri hii? Upendo wa Kristo kwa ajili yako ulimfanya atoe maisha yake kwa ajili ya dhambi yako. Yeye anajitolea kuutia nguvu uhusiano wako wote kwa kukupa upendo wake na kuku "fan(ya) (wewe) kuwa (m) kamilifu katika kila tendo jema ili upate kutenda mapenzi yake" (Waebirania 13:12). Jibu lako ni lipi?

SIRI YA PUMZIKO LA MBINGUNI

Miaka michache tu iliyopita wengine walikuwa wakibashiri kwamba muda si mrefu tungakuwa na muda mwingu sana wa mapumziko ambao tungeshindwa kujua tufanye nini nao. Hizi zilikuwa ndizo sababu nzuri kwa ubashiri ule wenye matumaini. Katika miji mikuu ya ulimwengu makompyuta yalikuwa yakizisaga-saga kazi ambazo zingechukua mwezi mzima kuzifanya kwa sehemu tu ya nukta moja. Na yale maroboti yalikuwa yameanza kuzifanya kazi ngumu sana za kuchosha katika viwanda nya kutengeneza mashine nzito.

Lakini baada ya makompyuta hayo kutoa mfumo wao na maroboti kufanya kazi zao, bado tunakosa hata pumzi kuzifanya kazi hizo muda wa siku hizi. Zaidi ya yote, familia zinakosa muda wa kukaa pamoja. Waume na wake zao huona vigumu kupanga "muda unaofaa" wa kuwa pamoja na watoto wao, licha ya wao wenyewe kuwa na muda mchache wa kuwa pamoja.

Utafiti mmoja uliofanywa katika jumuia moja ndogo ulionyesha kwamba wastani wa muda kila siku ambao mababa wanatumia wakiwa peke yao na watoto wao wadogo sana ulikuwa nukta 37! Familia hazina muda, wala hazina mawasiliano.



Je! Tunavezaje kupunguza hiyo kasi tuliyonayo kwa kiasi cha kutosha kuweza kuwa na uhusiano wetu tena?

1. Dawa Ya Maisha Yaliyojaa Mahangaiko

Yesu anayajua matatizo ya familia zilizo chini ya shinikizo hilo, naye anataka sisi tujue kwamba pumiziko la kiroho ni sehemu ya maisha bora; "**NJONI KWANGU, ninyi nyote mliochooka na maisha na kulemewa na mizigo, NITAWAPUMZISHA... MJIFUNZE KWANGU, kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyeketu wa moyo, nanyi mtapata RAHA NAFSINI MWENU.**" Mathayo 11:28, 29.

Biblia inatushauri kuionja hiyo raha kwa njia mbili: Kumwendea Kristo kwa kutegemea msingi huu wa aina mbili, KILA SIKU na KILA JUMA.

2. Kuungana Na Yesu Kila Siku

Makundi ya watu wakati wote yalikuwa yakidai Kristo awasikilize wao tu. Naye Kristo bado aliweza kuonyesha moyo wa amani, mtulivu, kwa kila mmoja aliyemzunguka. Hivi ilikuwaje? Alitumia muda wake kila siku kuongea na Baba yake aliye mbinguni. Alimtegemea Baba yake daima ili kupata nguvu za kumwezesha kukabiliana na changamoto za maisha (Yohana 6:57).

Endapo sisi tunataka kuishi maisha matulivu, na manyofu kama ye ye alivyoishi, basi yatupasa kumtegemea Yesu daima - turuhusu Neno lake na Roho wake kutujaza na kututengeneza. Njia bora kuliko zote ya kuzipinga nguvu zile zinazotuunguza sisi kama mtu mmoja mmoja na kututenganisha kifamilia na ile ya kutumia muda ulio bora pamoja na Kristo. Yeye anatuambia hivi:
"KAENI NDANI YANGU, nami ndani yenu.... PASIPO MIMI HAMWEZI KUFANYA NENO LOLOTE" - (Yohana 15:4,5).

Mojawapo la mahitaji yetu makuu kuliko yote kwa kipindi chetu hiki ni lile la kutega nguvu za Kiroho zipatikanazo kwa njia ya kujenga uhusiano wa siku - kwa siku na Yesu. Jambo moja la maana sana linalotakiwa kusisitizwa juu ya uhusiano wetu na Kristo ni kazi yake iliyokamilika pale msalabani pumziko la kweli,



GUNDUA

usalama halisi, mambo hayo yanaweza kuwapo tu kwa sababu ya lile jambo moja kuu alilolifanya Yesu ambalo linatajwa wakati ule alipolia kwa sauti kuu alipokuwa akifa, alisema. "Imekwisha" (Yohana 19:30). Kwa maneno mengine, ile kazi yake ya kutukomboa sisi ilikuwa imekamilika.

Maana ingalikuwa hivyo, Kristo angalipaswa kuteswa mara nyangi tangu kuumbwa ulimwengu. Lakini sasa, nyakati hizi zinapokaribia mwisho wake, ye ye ametokea mara moja tu kuondoa dhambi kwa kujitao ye ye mwenyewe dhabihu. - (Waebrania 9:26).

Yesu alipokufa, aliziondoa dhambi". Ndiyo maana yasemekana kwamba Muumini aliyeziungama dhambi zake anaweza "Kupumzika" katika kazi ile iliyokamilika ya Kristo. Sisi tunakubalika.

Hatia imejificha katika nyumba ya haraka ya kiwendawazimu tulio nayo katika maisha yetu siku hizi. Lakini Yesu alilisuluhiha tatizo hilo la hatia mara moja tu pale msalabani. Kilio cha Yesu, alichosema, "Imekwisha" kilitia muhuri ahadi yake aliyo sema "Nitawapumzisha" na kuifanya iwe ni jambo la kweli kabisa. Kristo aliikamilisha kazi yake ya kutukomboa sisi pale Kalvari (Tito 2:14), halafu akapumzika kaburini siku nzima ya Sabato, na kufufuka kaburini siku ya Jumapili asubuhi kama mshindi dhidi ya dhambi na mauti. Mkristo hawezu kuwa na ahadi kubwa kuliko hiyo ya kupumzika katika kazi ya Kristo ile iliyokwisha.

"Kwa hiyo tumkaribie Mungu kwa miyo ili yotakaswa kutokana na dhamiri mbaya, na kwa miili ili yosafisha kwa maji safi. Tuzingatie kabisa tumaini letu tunalokiri, maana Mungu aliye fanya ahadi zake ni mwaminifu." - Waebrania 10:22,23 kwa kuwa ye ye "aliyahidi ni mwaminifu," basi, sisi tunaweza kuingia katika pumziko la wokovu ambalo Yesu ametuhahidi. Uthabiti, amani, na pumziko tunaloliona ndani ya Yesu kila siku ni matokeo, sio ya neno lolote tulifanyalo, bali ya kile alichokifanya pale msalabani.

Tunaweza kupumzika ndani ya Kristo kwa sababu wokovu wetu ni wa hakika. Uhakika huo hututia moyo kutumia wakati wetu pamoja na Kristo kila siku, tukijilisha Neno lake na kuvuta hewa ya mbinguni kwa njia ya maombi yetu. Mahali pale pa kukutana na Yesu hutusaidia sisi kuyageuza maisha yetu yaliyo jaa mahangaiko na kuyafanya yawe ya amani na yenye lengo maalum.

3. Kuungana Na Yesu Kila Juma



Baada ya Kristo kuiumba dunia hii kwa siku sita (Wakolosai 1:16-17), alitoa pumziko la Sabato. Ni nafasi ya kila juma tuliyopewa ili kuuendezea mwungano wetu huo pamoja naye.

"Mungu akaona kila kitu alichofanya kuwa ni chema kabisa. Ikawa jioni ikawa asubuhi; siku ya sita. Hivyo ndivyo mbingu na dunia zilivyokamilika pamoja na vitu vyote vilivyomo. Siku ya saba Mungu akawa amemaliza kazi yake yote aliyo fanya; siku hiyo ya saba Mungu akapumzika baada ya kazi yake yote aliyo fanya. Mungu akaibariki siku ya saba na kuitakasa, kwa kuwa siku hiyo Mungu alipumzika baada ya kazi yake yote ya kuumba" - (Mwanzo 1:31-2:3).

Kama Muumbaji wao, Yesu "akapumzika" Sabato ile ya kwanza pamoja na Adamu na Hawa, naye "akaibariki" siku ya Sabato na "kuifanya takatifu". Mungu ndiye aliyeuanzisha mzunguko wa juma - la - siku - saba, si kwa faida yake mwenyewe, bali kwa faida ya Adamu na Hawa na kwa faida yetu sisi leo. Kwa kuwa aliwapenda sana watu wale aliokuwa amewaumba, alipanga kwamba kila siku ya saba katika maisha yao yote ingewekwa wakfu kwa ajili ya kutafuta kuwako kwake ye ye. Kila Sabato, kama ye ye alivyo ita, ilipaswa kuwa siku ya pumziko la kimwili na burudiko la Kiroho. Kuingia kwa dhambi katika ulimwengu wetu kulifanya haja ya pumziko la Sabato iwe kubwa zaidi.

GUNDUA

Mwokozi yule aliyemwahidi Adamu na Hawa "pumziko" lile, alimpa Musa, mnamo miaka elfu mbili baadaye, sheria juu ya ule Mlima Sinai (1Wakorintho 10:14) Yesu alichagua kuiweka amri ile ya pumziko-la-Sabato katikati kabisa ya zile amri Kumi. Amri ya nne inasomeka hivi:

"IKUMBUKE SIKU YA SABATO KWA KUITAKASA. Siku sita utafanaya kazi, na tenda mambo yako yote, Lakini siku ya saba ni Sabato ya Mwenyezi-Mungu, Mungu wako. Siku hiyo usifanye kazi yoyote, wewe, wala mwanao, wala binti yako, wala mtumwa wako wala mtumishi wako wa kike, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye nyumbani mwako. Maana, kwa siku sita mimi Mwenyezi-Mungu nilizumba mbingu na duniai, bahari, na vyote vilivyomo, kisha NIKAPUMZIKA siku ya saba. Kwa hiyo, MIMI MWENYEZI-MUNGU NILIIBARIKI siku ya Sabato na NIKAITAKASA" - (Kutoka 20:8-11).

Mungu alianzisha Sabato kama siku inayopaswa kum"kumbuk(a)" Bwana aliye "zifanya mbingu na nchi." Pumziko - la-Sabato la kila juma linatuunganisha sisi na Muumbaji wetu aliyebariki siku hiyo na kuitenga.

Yesu alipoishi hapa duniani, aliiumia vizuri kila nafasi nzuri kwa kudumisha mwungano huo na Baba yake. Alinufaika na pumziko-la-Sabato kwa kuabudu siku ya Sabato, kama Luka anavyotusimulia: "**Akaenda Nazareti, mahali alipolelewa, na SIKU YA SABATO akaingia katika singagogi, KAMA ILIVYOKUWA DESTURI YAKE.**" - (Luka 4:16).

Ikiwa Yesu aliye kuwa Mungu - Mwanadamu alihitaji kupumzika mbele za Baba yake siku ya Sabato, basi, sisi tulio wanadamu kwa hakika tunalihitaji zaidi hilo pumziko. Yesu alipozifagilia mbali sheria zile zilizoweka vizuizi vingi walivyokuwa wameviweka Wayahudi katika ile Sabato (Mathayo 12:1-12), ye ye aliwaonyesha kwamba Mungu alikuwa ameiweka Sabato kwa ajili ya kuwaletaa watu manufaa.

"Akawaambia, Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu, si mwanadamu kwa ajili ya Sabato. Basi Mwana wa Adamu ndiye Bwana wa Sabato pia" - (Marko 2:27,28).

Yesu alisitisiza sana umuhimu wa Sabato hata wakati wa kifo chake. Alikufa Ijumaa, "Siku ya Maandalio, na Sabato ikaanza kuingia "(Luka 23:54). Wakati ule alitangaza. Akasema, "Imekwisha," yaani, kazi yake ya kuja hapa duniani na kufa kama badala ya taifa zima la Kibinadamu ilikuwa imekamilika (Yohana 19:30; 4:34; 5:30). Kisha ili kusherehekeea utume wake uliokwisha, Yesu alipumzika kaburini Sabato ile nzima.

Kama Kristo alivyomaliza kazi yake ya uumbaji katika siku ile ya sita, kisha akapumzika siku ya Sabato, ndivyo kwa kufa kwake msalabani alivyomaliza kazi yake ya ukombozi katika siku ile ya sita, na halafu akapumzika siku ile ya saba.

Jumapili alfajiri Yesu alitoka kaburini kama Mwokozi Mshindi (Luka 24:1-7), Tayari alikuwa amewataka wanafunzi wake kuendelea kukutana naye siku ya Sabato baada ya ufufuo wake.

Akizungumza juu ya kuangamizwa kwa Yerusalem, ambako kulitokea karibu miaka arobaini hivi baada ya kifo chake, aliwaagiza, alisema.



"Ombeni, ili kukimbia kwenu kusiwe wakati wa baridi, wala siku ya Sabato." Mathayo 24:20.

Mwokozi wetu alitaka wanafunzi wake pamoja na waongofu wao waendelee na desturi alizokuwa amewafundisha (Yohana 15:15,6). Aliwataka wayaonje yote mawili, yaani, pumziko - la - Wokovu na pumziko - la - Sabato. Hawakumwangusha. Wanafunzi wake waliendelea kuitunza Sabato baada ya kifo chake Kristo (angalia Luka 23:54-56; Matendo 13:14; 16:13; 17:2:18:1-4).

Yohana yule aliyependwa sana alidumisha mwungano wake wa kila juma na Kristo katika siku ya Sabato. Katika miaka yake ya baadaye aliandika, akisema, "Siku ya Bwana nilikuwa katika roho" (Ufunuo 1:10).

GUNDUA

Kulingana na msimamo wa Yesu, "Siku ya Bwana" ni Sabato, "Kwa maana Mwana wa Adamu ndiye Bwana wa Sabato "(Mathayo 12:8).

Siku ya Sabato tunaadhimisha mambo makuu kuliko yote mawili aliyoyakamiisha kwa ajili yetu. Yaani, kutuumba sisi na kutuokoa. Uzoefu huo wa kuitunza Sabato utaendelea kule mbinguni:

"Kama vile mbingu mpya na nchi mpya, nitakazofanya, zitakavyokaa mbele zangu, anatangaza BWANA,... 'toka Sabato hata Sabato, wanadamu wote watakuja kuabudu mbele zangu, asema BWANA" - (Isaya 66:22,23).

4. Manufaa Ya Pumziko-la-sabato

Siku hizi watu wanakanyagana ovyo katika maisha yao ya kiwendawazimu. Watu wanateketea mmoja mmoja. Famili zinasambaratika chini ya shinikizo. Lakini Mungu anawapa Sabato yake kama njia bora zaidi ya kuishi yale maisha mema.

Hebu na tuyaangalie baadhi ya manufaa ya pekee ya hilo pumziko-la-Sabato:

1) Sabato ni kumbukumbu ya uumbaji, na kwa kuitakasa, tunamjengea kumbukumbu Muumbaji wetu. Saa zake takatifu zinatupa nafasi nzuri ajabu za kushughulikia na maisha yetu mapya tuliyoyaanza katika dunia hii iliyoumbwa na Mungu. Je! ni lini kwa mara ya mwisho wewe au familia yako mlitumia muda wenu kwa kuzama kabisa katika kutafakari ule uzuri mtulivu wa njia ile ya msituni au kijito kile kinachotiririka kuititia katika miamba ile? Sabato inatupa muda wa kutumia pamoja na Yesu na kuona kidogo tu maajabu yake aliyoyafanya kwa ajili yetu.

2) Siku ya Sabato tunaionja furaha ya kumwabudu na kushirikiana na Wakristo wengine. Kuna faida katika kumsifu Mungu tukiwa pamoja na wengine kama kundi la watu waabuduo pamoja. Sabato inatupa sisi muda wa pekee wa kukusanyika pamoja kama kundi la kanisa na kuzichajji upya betri zetu za kiroho.

3) Sabato inatupa sisi fursa ya kutenda matendo ya wema kwa kuwafikiria wengine. Je! jirani yako amekuwa mgonjwa katika juma hili ulipokuwa huna nafasi ya kumtembelea? Rafiki yako alipotaka umsikilize kwa kusikitika pamoja naye kwa kufiwa na mumewe, je! shinikizo la maisha yako ya kila siku lilitimnyima mama huyo upendo wako wa kwenda kumtazama? Yesu alitoa shauri hili: "Ni vyema kutenda mema siku ya Sabato" (Mathayo 12:12).



4) Sabato ni Siku ya kuviiimarisha vifungo vya Familia. Yesu alipoamuru hivi, "Siku hiyo (ya Sabato) usifanye kazi yoyote" (Kutoka 20:10). Asingekuwa ametoa dawa nzuri zaidi kwa mababu walio walevi wa kazi na kwa akina mama wanaosumbuka sana. Sabato ni ishara kubwa sana isemayo SIMAMA kwa familia nydingi. Simama na kuacha kuyaruhusu mambo yale ya muhimu zaidi kwako mambo yale yaliyo ya maana sana. Sabato ni siku moja ambayo katika hiyo tunaweza kuondoa shinikizo na mahali pake kuweka maombi, kuondoa kazi ngumu na kuweka kicheko badala yake, kuziondoa ratiba zenye shughuli nydingi na mahali pake kuweka tafakuri ya kimya kimya. Pumziko -la-Sabato huipa familia nzima muda wa kuungana na Kristo na kuchota nguvu za Kiroho kutoka kwake (kwa matumizi yetu).

5) Sabato ndio wakati ambapo Yesu anakuja karibu nasi zaidi kwa njia ya pekee. Kila uhusiano uliopo unahitaji muda unaofaa uwepo, na uhusiano wetu na Kristo hauna tofauti. Kuitumia siku nzima kwa ajili yake Kristo kila juma ndiyo njia kuu ya kuufanya urafiki wetu naye uwe safi na wa kufurahisha sana. Sabato inatupa muda wa ziada kwa ajili ya kujifunza Biblia na maombi, muda wa ziada wa kuwa peke yetu pamoja na Kristo mahali pa kimya na kusikiliza.

GUNDUA

Yesu "akaibariki siku ya saba na kuifanya takatifu" kwa ahadi ya kuwako kwake (Mwanzo 2:3). Unaweza kuelewa kwa nini ni jambo la maana kuitunza Jumamosi, siku ya saba ya juma, kama Kristo aliitenga wakati ule wa uumbaji ili apate kuitumia kwa kuwasiliana nasi kwa njia ya pekee.

Yesu alipoifanya Sabato yaonekana kabisa kwamba alikuwa anakifikiria kizazi chetu mawazoni mwake. Ndiyo tunayoihitaji hasa katika mazingira yetu ya maisha yaliyojaa shinikizo. Ni siku ambayo inatutenga kweli mbali kabisa na mambo mengine yote. Ni siku ya kumwabudu Mungu, kuwasiliana tena na uumbaji wake, na kuuimarisha uhusiano wetu badala ya kuvishuhulikia vitu.

5. Ni Kilionja Mapema Pumziko La Mbinguni

Tunaweza kufanya muhtasari wa manufaa tunayoweza kupata kwa kuijunganisha na Kristo kwa njia ya kukutana naye KILA SIKU na KILA JUMA kwa kutumia neno moja tu - pumziko. Neno hili "Sabato" linatoka katika neno la Kiebrania limaanishalo pumziko, basi, si jambo laajabu ya kwamba Maandiko yanaiita hiyo siku ya saba kuwa ni "Sabato ya kupumzika kabisa" (Mambo ya Walawi 23:3).

"(Mungu) amesema juu ya siku ya saba kwa maneno haya: Siku ya saba Mungu alipumzika na kuacha kufanya kazi yote aliyofanya.... BASI LIMESALIA PUMZIKO-LA-SABATO KWA WATU WA MUNGU.... Basi, na tufanye bidii kuingia katika pumziko lile" - (Waebraania 4:4-11).

Kulionja hili "Pumziko-la-Sabato" kila juma hutuwezesha sisi kuionja mapema ile furaha tutakayoipata katika lile pumziko kamilifu kule mbinguni. Pumziko lile sikukaa tu kivivu, linamaanisha kujisikia u salama moyoni, una hali ya amani na hali njema ya maisha iliyo katika shina lile la maisha tele ya kweli. Aina hiyo ya pumziko la kiroho inaweza kuthaminiwa tu kwa kulionja. Ushuhuda wa wale walloonja pumziko-la-wokovu pamoja na hilo pumziko-la-Sabato unajulikana kote. "Kama wewe umeingia katika pumziko la Yesu kwa njia ya kuungana naye kila siku na kila juma, basi, utaigundua furaha kuu kuliko zote katika maisha yako."

Je! ungependa kumshukuru Yesu kwa zawadi yake hiyo ya pumziko? Je, ungependa kumshukuru kwa ahadi yake ya pumziko-la-wokovu analokupa kila siku ili kukabiliana na changamoto za maisha, na kwa ahadi yake ya kukupa pumziko-la-Sabato kila juma ili kuifanya imara uhusiano wako pamoja naye? Endapo wewe hujapata kamwe kufanya hivyo, Je! ungependa kuupokea wokovu anaokupa? Je, ungependa kumwambia kwamba unatamani kuitunza Sabato yake kila juma? Je! ungependa kumwambia, "Ndiyo, Bwana! Natamani kuipata furaha yangu katika siku ile uliyoiweka? Kwa nini usitoe ahadi yako kwake sasa?

(Huenda wewe unashangaa: Ni nani aliyeibadili Sabato kutoka Jumamosi kwenda Jumapili, siku ya kwanza ya juma? Badiliko hilo lilifanyika lini? Je! hivi Mungu alitoa idhini yake kwa badiliko hilo? Maswali haya yatajibiwa katika Mwongozo 21.)



SIRI YA UKUAJI KWA KUSHUHUDIA

Larry alikuwa akifurahia maongozi yale mazuri, chai ya kijapani, wali mkavu, nyumbani kwa Bwana Komari wakati wageni wengine walipoanza kuzitoa Biblia zao. Wote wakamtazama na kumngojea. "Tafadhalii tupe somo letu sasa?" Bwana Komari aliomba.

Larry alikuwa karibu amepaliwa na chai yake. Alikuwa amedhani kwamba mukutano ule wa dhifa (Karamu) ulikuwa wa kujifurahisha tu. Na sasa hakuweza kufikiri juu ya kitu chochote cha kusema.

Kwa kweli Larry alikuwa amefundisha madarasa mengi ya Biblia katika shule ya Kikrsito ya Lughya ya Kiingereza katika nchi ya Japan alikokuwa akifanya kazi. Lakini yalikuwa yameandaliali vizuri. Aliweza kutoa maelezo juu ya Biblia kwa wepesi. Lakini kuweza kuzungumza habari za Mungu papo hapo bila kuijandaa vizuri... hilo lilikuwa ni jambo tofauti.

Larry alikuwa amezisikia hadithi zote za Biblia tangu utoto wake. Lakini hazikuwa na maana sana kwake kwa msingi wa kibinagsi. Alikuwa anafanya mambo aliyojua kwamba yalikuwa mabaya machoni pake Mungu. Angeweza basi, kuwaambia wengine habari za Mungu ambaye ye ye mwenyewe alikuwa hamjui kwa kweli?

Basi, akiwa ameketi pale kwenye kochi lile, amezungukwa na watu waliokuwa wakimngojea, mchezo wake wa viigizo bubu ulikuwa karibu kuperomoka. Katika saa ile ya hofu yake, fungu likapita kasi mawazoni mwake lililosema kwamba roho Mtakatifu aweza kutupa sisi maneno ya kusema tunapoletwa mbele ya watu kutoa ushuhuda wetu (Luka 12:12). Alitoa sala yake ya kufa na kupona kuomba msaada, kisha akaking'ang'ania kisa kile kinachojulikana sana ambacho aliweza kukifikiria: yaani, kisa cha mwana mpotevu.



Alipoeleza jinsi Mungu anavyowapenda sana hata wale amba wananatangatanga mbali naye, Larry akajikuta anaongea moja kwa moja toka moyoni mwake. Maneno yake yalikuwa yakiwaingia wale watu. Kwa mara ya kwanza katika maisha yake Larry alitambua jinsi Mungu alivyopenda sana.

Usiku ule Larry alipiga magoti kando ya Kitanda chake na kutoa maisha yake kwa Mungu ambaye hatimaye alikuwa ni wa kweli kwake. Kushuhudia juu ya upendo wa Mungu kulifanya jambo hilo kuwa zaidi ya jambo la kawaida la kuwazia tu. Sasa likawa ni jambo la kweli lililomshinda nguvu.

1. Yesu Anatupa Changamoto Ya Kukua Kwa Njia Ya Kushuhudia

Wanafunzi walikuwa wametumia miaka mitatu na nusu wakiyazingatia maneno na matendo yake Kristo, na hatimaye kifo na ufufuo wake. Yesu alipokuwa karibu kurudi mbinguni, aliwateua wanafunzi wake kuwa wawakilishi wake.

"MTAPOKEA NGUVU akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu, NANYI MTAKUWA MASHAHIDI WANGU... hata mwisho wa nchi." Matendo 1:8. (Isipokuwa pale ilipoelezwa vinginevyo, mafungu yote ya maandiko katika GUNDUA Miongozo yanatoka katika Toleo jimpya la Biblia la Habari Njema.)

Wafuasi wake Kristo waliitoa miyo yao kwake bila kuacha kitu katika ile siku ya pentekoste, Kristo, yule aliyefufuliwa alikuwa ameyabadilisha maisha yao kwa uwezo wa Roho. Wakawa mashahidi, sio tu wa kufufuka kwake kimwi na kupaa kwake, bali pia wa uweza wake wa ufufuo uliokuwa umeyabadilisha maisha yao.

GUNDUA

Sisi kama Wakristo tu mashahidi pia wa ufufuo wake Yesu katika maisha yetu wenyewe kwa kuwa tumeupokea uwezo wake utufanyao sisi kuwa wapya.

"Kuna mwili mmoja na Roho mmoja, kama vile tumaini mliloitiwa na Mungu ni moja. Kuna Bwana mmoja, imani moja na ubatizo mmoja; kuna Mungu mmoja na Baba wa wote, ambaye yuko juu ya wote, afanya kazi katika yote na yuko katika yote. Kila mmoja wetu amepewa neema kadri ya kipimo alichojaliwa na Kristo" - (Waefeso 2:4-7).



Tumehuisha pamoja na Kristo, kwa hiyo, tunaweza ku "udhihirish(a) wingi wa neema yake." Naye anatutaka sisi tuzipeleke habari hizo njema kwa ulimwengu mzima kuhusu kile awezacho kufanya ndani ya maisha ya mwanadamu, kisha anatuahidi kwamba atakwenda pamoja nasi tukifanya hivyo (Mathayo 28:19-20).

H.M.S. Richards, muasisi wa huduma ya Redio ya Sauti ya Unabii, siku moja alitoa ushuhuda huu. "Mimi nimekwisha kuona badiliko ndani ya miyo ya watu waliosikia hiyo injili ya Kristo. Nimesafiri kwenda katika nchi ambako jina la Mungu na la Kristo lililokuwa halijulikani kabisa mpaka kanisa lake lilipoipeleka injili kule. Nimewaona watu hao

wakibadilika kutoka katika uchafu kwenda katika usafi, kutoka katika magonjwa kwenda katika afya, kutoka katika hofu ya daima ya mapepo na kuingia katika furaha ile itokanayo na kuishi maisha ya Kikristo. Nimekwisha kuona badiliko katika hadhi walionyayo wanawake. Nimeziona nyumba za kweli za Kikristo zikijitokeza kutoka katika giza la kipagani. Katika kila nchi niliyotembelea nimeona maisha ya watu yakibadilika. Mimi najua kwamba injili yake Kristo... ni uweza wa Mungu uletao wokovu (Warumi 1:16). Najua kwamba kanisa linapoutangaza ujumbe huo wa injili, mabadiliko hutokea ndani ya miyo ya wanadamu, nayo yanaonekana kwa macho katika maisha ya wale wanaoitikia mwito wake."

Mungu ametupa sisi wanadamu tulio dhaifu sehemu yetu maalum ya kufanya katika kazi hiyo inayosisimua sana kwa sababu kule kutoa ushuhuda wetu ni sehemu muhimu sana ya kukua kwetu. Ili imani yetu iendelee kuwa na afya, ni lazima itangazwe. Kama yule Larry alivyogundua kwa njia ya kuvutia sana, kugawa imani yetu kunatusaidia sisi kuwa nayo kwa utimilifu zaidi, na kutufanya sisi tukue.

2. Tunamshuhdua Kristo Kwa Namna Tuishivyo

Kijana mmoja mwanaume, aliyekulia katika nyumba iliyojaa matusi, siku moja alitoa maoni yake haya. "Niliwaangalia wazazi wangu ambao kwa kielelezo chao walinipa picha mbaya ya Mungu; sikuona kamwe kielelezo cha mtu ye yeyote mwenye ngozi juu ya mwili wake anayenipenda mimi." Watu wale wanaotuzunguka. Wanamhitaji sana mtu fulani atakayewapa picha nzuri ya Mungu. Wanamhitaji mtu fulani "mwenye ngozi juu ya mwili wake" ambaye atawaonyesha tabia nzuri ya dini. Kwa kawaida hubiri letu lenye nguvu nyingi kuliko yote mara nyingi ni namna sisi tunavyoishi. Kabla watu hawajayazingatia yale unayoyajua, ni lazima wajue kwamba wewe unawajali kwa kiasi gani. Petro anatusihii, anasema.

"MWE NA MWENENDO WENU kati ya watu wasiomjua Mungu unapaswa kuwa mwema kabisa, ilihata watakawasingizieni kwamba mnatenda mabaya, waweze kutambua matendo yenu mema na hiyo wamtukuze Mungu kila siku ya kuja kwake. HAYO NDIYO mliyoitiwa; maana Kristo mwenyewe aliteseka kwa ajili yenu, akawaachieni mfano, ili mfuate mwenendo wake" 1Petro 2:12,21.

Kwa kuwa "Kristo aliteswa" kwa ajili yetu pale Kalvari, basi, tunacho kielelezo cha upendo wake wa kujitoa mhanga ambacho ki karibu sana nasi. Upendo ule, ukijitokeza ndani yetu kama matendo ya upendo ambayo sisi tunawatendea



GUNDUA

wengine, unaweza kuwa uwezo wenyewe nguvu nyingi kiasi cha kuwavuta wasioamini kuja mikononi mwake Kristo.

3. Tunamshuhudia Kristo Kwa Njia Ile Tunayofikiri

Ibilisi alipomshambulia Yesu kule nyikani kwa vishawishi vyake vya kuamsha tamaa ya kula chakula, majivuno, na kiburi cha makusudi, Yesu alipigana naye na kushinda kwa kunukuu Maandiko (Mathayo 4:4,7,10). Kristo alikuwa amejiandaa kwa sababu alikuwa ameujaza moyo wake na zile kweli za Biblia. Humo ndimo vita hii inamoupata ushindi wake au kushindwa kwake-yaani, ndani ya mioyo yetu.

"Maana kama vile mtu afikirivyo moyoni mwake, ndivyo alivyo" (Mithali 23:7).

Wakristo wanaokua hufikiri mambo yale ya mbinugni. Wanaweka nguvu zao zote katika kujenga tabia zile nzuri wanazojitahidi kuwa nazo.

"Furahini katika Bwana siku zote,... katika kila neno kwa KUOMBA na kutoa dua zenu, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, ITAWAHIFADHI MIOYO YENU NA NIA ZENU katika Kristo Yesu. Hatimaye, ndugu zangu, mambo yoyote yaliyo ya KWELI, yoyote yaliyo ya STAHA, yoyote yaliyo ya HAKI, yoyote yaliyo SAFI, yoyote yenye KUPENDEZA, yoyote yenye SIFA NJEMA - iwapo kitu chochote ni KIZURI SANA ua KINA SIFA NZURI- yatafakarini mambo kama hayo.... Na Mungu wa amani atakuwa pamoja nanyi." - (Wafilipi 4:4-9).

Kile tunachoilisha mioyo yetu kinaleta tofauti kubwa sana. Ukiweka uchafu ndani yako, utatoa nje uchafu. Ukiweka Neno la Mungu ndani yako, utatoa nje maisha yake Mungu.

4. Tunamshuhudia Kristo Kwa Namna Sisi Tunavyoonekana

Akiwa mwakilishi wa Kristo, Mkristo atakuwa na adabu hata kwa namna anavyoonekana kwa nje, akiepuka kuzidi kiasi kwa njia yoyote ile.

"Inanyi wake, jiwekeni chini ya mamlaka ya waume zenu, ili kama wako waume wo wote wasioamini neno la Mungu, wapate kuamini kwa kuuona mwenendo wenu. Haitakuwa lazima kwenu kusema neno, kwani wataona jinsi mwenendo wenu ulivyo safi na wa kumcha Mungu. Katika kujipamba kwenu msitegemee mambo ya nje nje, kama vile mitindo ya kusuka nywele, kujivalia vitu vya dhahabu na nguo maridadi. Bali uzuri wenu unapaswa kutokana na hali ya ndani ya utu wa kweli, uzuri usioharibika wa wema na utulivu wa roho, ambaao ni wa thamani kubwaa mbele za Mungu. Ndivyo walivyojipamba hapo kale wanawake waadilifu waliomtumainia Mungu; walijiweka chini ya mamlaka ya waume zao"- (1Petro 3:1-5).



Kuva mavazi na mapambo ya kawaida kumedhihirisha daima uzuri ule wa kufanana naKristo. Kwa mfano ulio mkamilifu, wengine wangeweza kuvutwa kuja kwetu kwa kuwa sisi tu Wakristo, sio kwa sababu ya maneno yetu tunayosema juu ya mitindo ya kisasa, bali kwa maneno ambayo maisha yetu yanamtangaza Yesu.

5. Tunamshuhudia Kristo Kwa Namna Tutendavyo

Mwanahistoria Edward Gibbon anatuambia sisi kwamba Galerio (Galerius) alipoliteka kambi la Waajemi, mfuko wa ngozi unaong'aa uliojazwa lulu uliangukia mikononi mwa askari mmoja aliyejewa akiteka

GUNDUA

nyara. Mtu yule aliutunza kwa uangalifu sana mfuko ule wenyewe manufaa, lakini lulu zile za thamani akazitupilia mbali.

Watu wale wanaozing'ang'ania furaha za juu juu tu ambazo ulimwengu huu unaweza kuwapa - huku wakimtupa Yesu mbali, Lulu ya Thamani kuu - wako katika hali mbaya sana kuliko yule askari aliyeteka nyara zile. Si mali tu iwezayo kuteleza mikononi mwetu, bali na uzima wa milele. Kwa hiyo Maandiko yanatuonya, yanasema:

"Msiipende ulimwengu, wala cho chote kilicho cha ulimwengu. Mtu anayeupenda ulimwengu, upendo wa Baba hauwezi kuwa ndani yake. Vitu vyote vya ulimwengu - tamaa mbya za mwili, vitu wanavyoviona watu na kuvitamani, majivuno yasababishwayo na mali - vyote hivyo havitoki kwa Baba, bali vyatoka kwa ulimwengu. Ulimwengu pamoja na vitu vyake vyote vyenye kutamanika unapita; lakini mtu atendaye atakalo Mungu, anaishi milele" - (1 Yohana 2:15-17).



Shetani anafanya kazi yake kwa bidii nyingi sana kupaka dhahabu nije ya dhambi zile zinazoangamiza watu sana na yale mazoea mabaya kabisa. Matangazo ya vimeo huwaonyesha tu watu wale amba ni vijana, wazuri, wachapa kazi, na wenyewe furaha nyingi sana. Hatumwoni mtu ye yote anayetoka katika duka la vimeo akichechemea kama kinyago na kuwa na kisalfeti (gunia) mkononi mwake.

Tunapaswa kuwa waangalifu kuhusu marafiki wale tunaoshirikiana nao ili tusije tukaziacha kanuni zile za Kikrsito (2 Wakorintho 6:14). Kwa kweli, Kristo anatutaka sisi kuendelea kuwatemblea marafiki zetu hao wasiokuwa Wakristo. Uhusiano wetu na mtu mmoja mmoja ndizo njia za msingi ambazo kwanza imani yetu inagawanywa kwa wengine hakikisha tu kwamba rafiki zako hao hawakuvuti kukurudisha katika mwenendo wako ule wa zamani.

Kile tunachokiingiza katika maisha yetu, hata burudani tunayoichagua, vinalo shinikizo lake juu ya maisha yetu ya Kikristo. Tunahitaji kukitambua kile tunachoilisha mioyo yetu.

"Sitaweka mbele yangu neno la uovu" - (Zaburi 101:3).

Tukiilisha mioyo yetu kile kilicho bora kabisa, basi, kile kilicho kiovu kabisa hakitaweza kutuvutia chini ili tupate kufanana nacho. Kule kuzishikilia sana zile kanuni za juu zaidi katika vitu vile tuviletavyo nyumbani na miyoni mwetu hakutayafanya maisha yetu kubanwa sana. Mkristo anayo mengi ya kumfanya awe na furaha kuliko mtu mwingine awaye yote.

("Wanionyesha njia ya kufikia uhai; kuwako kwako kunijaza furaha kamili, katika mkono wako wa nguvu mna mema ya milele") (Zaburi 16:11).

6. Tunamshuhudia Kristo Kwa Utoaji Wetu



Alipokuwa karibu kumbatiza muumini mmoja mpya, hayati Mchungaji H.M.S. Richards aligundua kwamba yule mtu alikuwa na pochi ya fedha iliyokuwa imjeaa vizuri katika mfuko wake. Richards akamwuliza endapo alikuwa amesahau kuiacha fedha yake ile katika chumba cha kubadilishia nguo. "Mfuko wangu huu na mimi tutabatizwa pamoja," alieleza yule mtu. Alikuwa ameipata roho halisi ya Ukristo - yaani, kutoa ili kuwasaidia wengine. Wakristo hukua kwa kutoa na ndiyo maana "Yesu mwenywewe alisema. "Ni heri kutoa kuliko kupokea". (Matendo 20:35). Kile tutoacho ili kuendeleza ufalme wa Mungu kinaendelea kuwa na thamani ya milele.

"Msijiwekee hazina zenu duniani, nondo na kutu viharibupo, na wezi huvunja na kuiba. Bali JIWEKEENI HAZINA ZENU MBINGUNI. Kwa kuwa hazina yako ilipo, ndipo utakapokuwapo na moyo wako"- (Mathayo

6:19-21).

"Unapotoa kumbuka" Dunia ni mali ya BWANA, na vyote viijazavyo" (Zaburi 24:1), hii ni pamoja na fedha na dhahabu (Hagai 2:8). Sisi wenyewe tu mali ya Mungu,. Kwa sababu alituumba na kwa sababu yeye alituokoa kutoka katika dhambi zetu kwa kulipa fidia ya dhambi zetu kwa damu yake (1Wakorintho 6:19-20). Kila kitu tulicho nacho ni mali ya Mungu, kwa sababu yeye ndiye "a(tu)paye nguvu za kupata utajri" (Kumbukumbu la Torati 8:18).

Ni kiasi gani anachotaka tutoe, huyo Bwana wetu aliyesulibiwa na kufufuka, ili tupate kushirikiana naye katika kuipeleka injili kwa wengine?

**"Je! mwanadamu atampora Mungu? Lakini ninyi mnanipora mimi. Lakini ninyi mwasema,
"Tumekupora kwa namna gani?**

"Mmenipora ZAKA NA SADAKA...

**Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu. Mnijaribu kwa njia hiyo,'
asema BWANA wa majeshi; Mwone kama SITAWAFUNGULIA MADIRISHA YA MBINGUNI na
kuwamwagieni baraka hata hamtaweza kuwa na nafasi ya kutosha kuiweka hiyo baraka" - Malaki
3:8-10.**

Zaka ni "Sehemu ya kumi" ya mazidio" yote (Kumbukumbu la Torati 14:22, KJV; Mwanzo 28:22). Kwa mkulima au mfanyabiashara mazidio hayo ni mapato baada ya kutoa gharama za biashara (mtaji). Kwa mfanyakazi, ni mshahara wake kamili. Kanuni ya kutoa zaka ni kanuni ya kimaadili kwa sababu inahusu tabia ya mtu. Tunaposhindwa kutoa zaka huwa tuna "mwibia" Mungu. Zaka ni ya Mungu, nayo inatakiwa kutumika kwa ajili ya kuwapa riziki yao wachungaji wake Kristo peke yao (1Wkorintho 9:14), na kuimaliza kazi yake duniani ili yeye apate kurudi (Mathayo 24:14).

Yesu alipokuja hapa kuishi kati yetu, alitoa idhini yake ya kulipa zaka katika nyakati za Agano Jipy (Mathayo 23:23).

Je! hivi tutoe kiasi gani kama sadaka? Sadaka ni mtu mwenyewe anavyoamua kutoa. Kila mtu anatakiwa "atoe kama alivyokusudia kutoa moyoni mwake" (2Wakorintho 9:5-7). Wewehuwezi kumpita Mungu katika utoaji.

**"Toeni, nanyi mtapewa. Kipimo cha kuja, na kushindiliwa, na kusukwa-sukwa hata kumwagika,
ndivyo mtapewa mapajani mwenu" - (Luka 6:38).**

H.M.S. Richards siku moja alisimulia kisa hiki.

"Mpiga kamari mmoja aliyebolea katika maisha yake yote alihudhuria mikutano yangu kule Los Angeles, wala sitasahu kamwe wakati ule nilipozungumza naye tukiwa peke yetu nyuma ya ukumbi wa mikutano. Alitoa bunda la noti mfukoni mwake, Dola za Kimarekani 500, na kunipa mimi zote, huku akisema, "Hii ndiyo zaka yangu ya kwanza!"

"Yule mtu hakuwa mzima, naye alikuwa hajafanya kazi nyininge yoyote isipokuwa kupiga kamari kwa miaka 30 au 40 hivi, basi mimi nikamwuliza, utaishije kuanzia sasa?

"Alijibu, Nimebakiwa na dola tano au sita hivi, lakini hizo nyininge ni mali ya Bwana. "Kisha nikamwuliza, utafanya kazi gani, basi?

"Sijui, alijibu, ila najua kwamba ni lazima nitoe zaka yangu kwa Mungu, yeye atanitunza.!

"Na kwa hakika Mungu alimtzunza. Toba ya mtu yule ilikuwa ya kweli. Alikwenda njia yote katika kujitoa wakfu kwake, naye alikuwa na furaha katika maisha yake ya Kikristo. Na Mungu hatoi ahadi kwamba waumini wote waaminifu watakuwa matajiri. Lakini tunayo ahadi kwamba Muumabaji wetu atatupatia mahitaji yetu ya maisha.



GUNDUA



Kristo alitoa kila kitu kwa ajili yetu. Hebu sasa na tumpe kabisa miyo yetu. Hebu na tuwaambie wengine habari zake Kristo kwa namna sisi tuishivyo, tufikirivyo, tuonekanavyo kwa nje, tutendavyo, na tutoavyo. Kwa nini sisi tusiigundue furaha hii ya kuwaambia wengine habari za Kristo na kuendelea kukua katika neema yake ya ajabu?

SIRI YA MTINDO WA MAISHA ULETAO AFYA

Watafiti wanaoishi katika kipindi hiki tulicho nacho wamejitahidi sana kuithibitisha ile kweli iliyothibitishwa kwanza na Biblia kwa kutoa maelezo haya: Wanadamu ni viumbe kamili. Mara nyingi kile tunachokigawa katika sehemu za kimwili, kiakili, na kiroho ni sehemu za mtu zilizo na uwiano unaoingiliana, wala hazitenganishiki. Kwa maneno mengine, kinachoidhuru akili, kinaudhuru mwili. Hali yetu ya kiroho ina shinikizo lake juu ya hali yetu ya kimwili, na kinyume chake. Sisi ni watu kamili.



Kwa mfano watafiti wa kisayansi katika uchunguzi wao uliodhibitiwa wamegundua kwamba kicheko kile kitokanacho na furaha na shangwe huleta mabadiliko yanayoweza kupimwa katika mfumo wa kinga mwilini mwa mtu. Unaweza kabisa kuusaidia mwili wako kupigana na ugonjwa kwa vizuri zaidi ukiwa na furaha! Uchunguzi huo huonyesha jinsi akili na mwili vinavyofanya kazi yao kwa pamoja kwa ushirikiano wa karibu sana.

Katika maelfu ya miaka iliyopita Neno la Mungu lilidokeza kuwapo kwa uhusiano huo wenyewe nguvu kati ya akili na mwili amba ni hivi karibuni tu umekubaliwa na kuingizwa katika nadharia ya kiganga:

"Moyo uliochangamka ni dawa nzuri, bali roho iliyopondeka huikausha mifupa"
- (Mithali 17:22)

Kulingana na mtume Yohana, Je, Ni kwa karibu jinsi gani uhusiano huo uliopo kati ya akili na mwili unaathiri usitawi wetu wa kiroho?

"Mpenzi wangu, nakutakia mafanikio mema ya kila aina; nakutakia afya njema ya mwili kama ulivyo nayo rohoni" - (3 Yohana 1:2).

Muumbaji wetu anataka sisi tupate " kufurahia kuwa na afya njema " Neno la Mungu linaweza kutumika kama chemchem yetu ya afya, pamoja na kuwa chemchem yetu ya uzima wa milele.

Kwa kuwa usitawi wetu kimwili na kiakili na kiroho unakwenda bega kwa bega, Paulo anatoa kwetu ombi hili:

"Mlapo mnywapo au mtendapo neno lolote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu" - (1 Wakorintho 10:31).

Injili inajumuisha mambo yote mawili, uponyaji wa mwili na uponyaji wa roho. Mtindo wa maisha uletao afya unaweza kutusaidia sisi kuwa Wakristo wenyewe uchangamfu mwingi.

Hapa zipo kanuni nane za kufuata endapo wewe kweli unataka kuishi maisha yenye afya na yenye manufaa mengi zaidi.

1. Hewa Safi

Hewa safi ya nje, ni ya lazima kwa afya nzuri. Wakati wa mchana na wakati wa kulala usiku, kuingiza na kuitoa hewa kwa njia inayofaa katika nyumba zetu na mahali petu pa kazi hutuhakikishia kwamba damu yetu daima itagawa oksijeni ya kutosha kila sehemu ya mwili wetu. Kuvuta pumzi nyingi wakati wa matembezi ya asubuhi ni njia kuu ya kuupatia mwili wako oksijeni.

Aina ya hewa tuivutayo ni dhahiri kwamba ni ya maana. Jihadhari usikae mahali penye moshi au mvuke mwingi, penye hewa mbaya au hewa inayochukua vijimea vidogo sana (bacteria) kutoka mahali fulani palipojificha.

Kuvuta tumbako huichafua sana hewa na ni mojawapo ya wauaji wakuu wa siku hizi. Utafiti wa sayansi umethibitisha kuwapo kwa uhusiano unaoleta madhara kati ya tumbako na kansa ya mapafu, ugonjwa wa kuvimba mapafu na kupumua kwa shida (emphysema) na ugonjwa wa moyo. Mazoea ya mwili kuhusiana na hiyo sumu ya nikotini katika sigareti hufanya uvutaji huo wa sigara (tumbako) uwe mmojawapo wa mazoea magumu kabisa kuachana hayo. Kuvuta tumbako kutaweza kuwaa watu milioni 12 kwa mwaka kufukia mwaka wa 2020 endapo mwendo huu wa sasa utaendelea

2. Mwanga Wa Jua

"Faida za mwanga wa jua ni nydingi:

1. Dakika kumi na tano hadi 30 za kupata mwanga wa jua kila siku katika ile sehemu ya mwanzo ya asubuhi au baadaye mchana alasiri husaidia mwili kukusanya pamoja au kutengeneza Vitamini D yake wenyewe, kirutubisho muhimu/homoni ndani ya ngozi. Vitamini D huisaidia damu kutengeneza kalisi (calcium) na fosforasi, inayojenga na kuitengeneza mifupa.
2. Mwanga wa jua unafanya kazi yake kama dawa ya kuvika viini vya maradhi na kuua vijimea vidogo sana (bacteria)
3. Jua linatoa nguvu ambayo kwa hiyo mimea inaweza kuigeuza kaboni dioksidi na maji kuwa kabohidreti [chakula cha wanga]... Bila ya njia hiyo wanyama na wanadamu wangekuwa kwa njaa
4. Jua pia linamsaidia wanadamu kujirekebisha na kukabili ana kazi ya usiku na kupunguza unyong'onyevu (depression) unaotokana na siku za giza wakati majira ya baridi kali yanapotokea.



Neno la tahadhi: Mwanga wa jua unaweza pia kuleta madhara kukaa kwa muda mrefu kwenye mwanga wa jua kunaweza kuiunguza ngozi, kunaweza kuongeza hatari ya kupatwa na kansa ya ngozi kunaweza kuharakisha kuzeeka, kunaweza kuyaharibu macho, na kusababisha mtoto wa jicho (cataracts). " [Madondoo yote katika Mwongozo huu yamenukuliwa kutoka katika Look up and Live: A Guide to Health, Lesoni ya Watu Wazima, Robo ya kwanza ya mwaka wa 1993, (Nampa, Idaho: Pacific Prexss Publishing Association). Mambo mengi katika Mwongozo huu ambayo hayajawekwa katika Alama za kunukuu yamefundishwa kutoka katika lesoni hiyo hiyo]

3. Kupumzika

Mwili huu ni lazima upumzike ili upate kujitengeneza upya wenyewe. Yatupasa kuwa na muda wa burudani na wa kupumzika ili kupunguza msongo utokanao na kazi pamoja na majukumu ya kifamilia. Bila kuwa na muda wa kutosha kupumzika mara nydingi watu wanakuwa na wasiwasi, mfadhaiko na hasira kali. Msongo huo wa moyo unaweza kuleta ugonjwa ambao utatulazimisha kuchukua pumziko letu ambalo miili yetu ilikuwa inataka kwa muda wote. Hakuna kitu cha badala cha kuweka mahali pa usingizi mzuri wa usiku.

Kuzichaji upya betri zetu za kiroho kwa kuweka utaratibu wa kila siku ni muhimu pia kwa afya yetu ya kimwili. Muda wa kila siku anaotumia Mkristo katika kutafakari, kusoma Biblia, na maombi utawezza kuuponya mwili pamoja na roho. Tunakuhitaji pia kupata pumziko ili kuuvunja mzunguko wa kazi, yaani, kuwa na siku ya kupumzika kila juma, na likizo ya mwaka au nusu mwaka.

4. Mazoezi Ya Mwili

GUNDUA



Mazoezi ya mwili ni ya muhimu sana kwa afya yetu:

1. Mazoezi ya mwili husaidia kulirekebisha shinikizo la damu.
2. Mazoezi ya mwili huiruhusu damu nyingi zaidi kuzifikia sehemu zote za mwili na kuifanya mikono na miguu ipate joto.
3. Mazoezi ya mwili yanaondoa mambo yote mawili. Yaani mkazo wa mwili na mfadhaiko wa moyo, na kukusiadia wewe kujisikia vizuri zaidi katika maisha yako. Mazoezi ya mwili kwa kawaida ni tiba bora kabisa ya wasiwasi na msongo (stress).
4. Mazoezi ya mwili hutupatia nguvu ya umeme kwa ajili ya ubongo wetu pamoja na seli za neva. Yanaongeza afya kwa kuuamsha mfumo wa kinga mwilini (immune system). Mwili unapowekwa katika hali ya afya kwa kufanya mazoezi yanayofaa. Ubongo unakuwa na uwezo wa kufikiri kwa ubunifu na ufanisi zaidi.
5. Yanaweza kukusaidia kuiweka vizuri rangi ya uso wako na kukuweka katika hali nzuri kabisa kimwili.
6. Mazoezi ya mwili hukufanya uwe na nguvu nyingi zaidi, hivyo kuchelewesha kupatwa na uchovu kimwili na kimawazo
7. Yanausaidia ubongo wako kutengeneza dawa inayokupa wewe hali ya kujisikia vizuri na kukuongezea uwezo wa kustahimili maumivu.

Endapo wewe ulikuwa hufanyi mazoezi, basi anza taratibu (polepole) na kuongeza nguvu yake hatua kwa hatua upatapo uwezo wa kustahimili. Laweza kuwa ni jambo la busara kumwona mganga wako kabla ya kuanza mazoezi hayo. Lengo lako na liwe kujishughulisha na kila aina ya mazoezi hayo ya mwili ambayo yanaweza kulinganishwa na kutembea maili moja kwa dakika kumi na tano mara nne au zaidi kwajuma.

5. Maji

Kwa vile maji ni ya lazima kwa kila seli mwilini, basi, ingetupasa kunywa maji mengi.

1. Kwa uzito, mwili wetu karibu asilimia sabini ni maji...
2. Mwili wetu unahitaji takribani visaga (quarts) viwili na nusu vy ya maji kila siku ili uweze kufanya kazi zake zote. Baadhi ya kazi hizo ni pamoja na mzunguko wa damu mwilini, kuondoa uchafu mwilini, kusafirisha virutubisho vy chakula mwilini, na kukiyeusha chakula mwilini
3. Mtu wa kawaida anazo seli za ubongo kati ya billioni 15 na 40 hivi. Kila moja ya hizo ina maji asilimia 70 hadi 85. Maji ya kutosha kuweza kuzigawa seli hizo hukufanya uwe na akili iliyochangamka, halafu husaidia kuzuia mfadhaiko (depression) na hasira kali.
4. Si maji yale tu unayokunywa ambayo ni ya muhimu. Kuoga maji ya baridi kidogo au vuguvuvugu kila siku au kwa kutumia bafu ya manyunu (shower) huboresha mzunguko wa damu mwilini, hivyo kuupa mwili na ubongo wako nguvu. Bafu ya manyunu au kuoga kwa njia ya kawaida huweza pia kutuliza mishipa ya fahamu iliyochachamaa, ambayo inaweza kuleta ugonjwa kwa kudhoofisha mfumo wa kinga mwilini. Kuoga pia kunaondo uchafu kutoka juu ya ngozi, pia kunaweza kupunguzahoma.



6. Lishe Ifaayo



Wakati ule wa uumbaji Mungu alimwagiza Adamu na Hawa kula chakula cha kokwa, nafaka na matunda (Mwanzo 1:29). Baada ya Adamu na Hawa kutenda dhambi, ziliongezwa mboga za majani katika lishe yao (Mwanzo 3:18). Baada ya ile gharika, Muumbaji aliongeza nyama ya wanyama "safi" katika lishe yao (Mwanzo 7:2-3, 9:1-6)

Nyama ya wanyama ina mafuta ya majimaji (saturated fat) na mafuta mazito kolesterolo [cholesterol], ambayo yote huongeza hatari ya kupatwa na shinikizo la damu, kupooza (stroke), ugonjwa wa moyo, kansa, unene usio wa kawaida, kisukari na magonjwa mengineyo. Leo matabibu wengi wanawashauri wale wanaokula nyama kula mnofu ule tu usiokuwa na mafuta, uliopikwa vizuri, pamoja na kula samaki na kufanya hivyo kwa nadra sana.

Kwa vile watu wanaokula chakula cha mimea wana afya bora zaidi, tena wanaishi kwa muda mrefu zaidi, wataalamu wengi wa lishe na afya wanatushi sana sisi ili tupate kufikiria kukirudia chakula kile cha awali walichopewa wanadamu cha kokwa, nafaka na matunda pamoja na mboga za majani zilizoongezwa.

Ukitaka kuanza kula vyakula vya mimea, hakikisha kwamba unelewa kwanza namna ya kuandaa lishe bora bila kutumia nyama. Ule kiasi cha chakula kinachomtsha mtu kula kwa siku (migawo [serving] mitano au sita hivi) ya aina mbalimbali za matunda, pamoja na kokwa [karanga n.k.] nafaka, maharage, kunde, mbaazi na mboga za majani. Mboga za majani za kijani na za njano, pamoja na machungwa ni za muhimu sana. Tumia unga wa nafaka isiyokobolewa na mchele mwekundu (brown rice) badala ya ule mweupe. Ulaaji wako wa wanga na sukari za mchanganyiko ungekuwa katika migawo (servings) sita au zaidi kwa siku moja. Badilisha matumizi yako ya mafuta ya wanyama (samli, siagi, mafuta ya nguruwe, shahamu izungukayo figo, n.k.) kwa kutumia mafuta ya mimea. Lishe hiyo juu inatosha bila kutumia nyama kama wewe unatumia vitu vinavyotokana na maziwa.

Wale wanaochagua kula nyama kama sehemu ya chakula chao, wangepaswa kuzila nyama zile tu ambazo Biblia inasema ni "safi" au zile zinazofaa kuliwa na wanadamu. Mungu alipowaruhusu wanadamu kula nyama baada ya gharika (Mwanzo 7:2-3) (Mambo ya walaei 14:47), alibainisha nyama za wanyama gani zilikuwa safi, na zipo zilikuwa najisi na zilikuwa hazifai kuliwa.

Soma katika Mambo ya Walawi 11 na Kumbukumbu la Torati 14 orodha ya ndege, wanyama, na samaki ambaeo Mungu alisema hawafai kuliwa. Kwa mujibu wa sura hizo, wanyama safi ni lazima kwato zao zigawanyike na pia wacheue. Samaki safi ni lazima wawe na magamba na mapezi, vyote viwili. Ndege wanaokula uchafu ni marufuku kuliwa.

Miongoni mwa wanyama najisi, kwa namna ya pekee nguruwe wanatajwa kwa kulaaniwa (Kumbukumbu la Torati 14:8) Asilimia ya juu ya miili ya wanadamu inayofanyiwa uchunguzi na waganga imejaa minyoo isiyokufa ya trikina (trichinae). Minyoo hiyo midogo sana inahamishiwa kwa wanadamu wale wanaokula nguruwe walioambukizwa minyoo hiyo. Utafiti wa kisanyansi wa siku hizi unazidi kufunua sababu zinazoonyesha kwa nini Mungu alitangaza nyama za wanyama fulani kuwa ni najisi. Sababu moja huenda ikawa ni yale matokeo yanayoleta uharibifu mkubwa kutokana na mafuta ya wanyama ya majimaji katika mfumo wa mwili wa kibinadamu wa kuyeyusha chakula.

7. Epuka Vitu Vinavyoleta Madhara

Je, ni maonyo gani ambayo Biblia inatoa kuhusu vinywaji vyenye alcohol ndani yake?

"Mvinyo hudihaki na kileo huleta ugomvi; Na akosaye kwa vitu hivyo hana hekima" - Mithali 20:1

Wala wezi wala watamanio, wala WALEVI, wala watukanaji hawataurithi ufalme wa Mungu" - (1 Wakorontho 6:10).

Alkoholi huathiri mifumo ya mwili ifuatayo:

1. Mfumo wa kinga mwilini - Alkoholi inapunguza uwezo wa chembechembe nyeupe wa kupigana na ugonjwa, hivyo kuzidisha hatari ya kupatwa na nimonia (pneumonia), kifua kikuu, homa ya manjano, na kansa za aina kadhaa.
2. Mfumo wa tezi (endocrinesystem) zinazotoa majimaji mwilini - Vinywaji viwili tu au vitatu kwa siku huzidisha hatari ya kuharibika mimba, kuzaa watoto



waliokufa, na watoto waliozaliwa kabla ya wakati wake.

3. Mfumo wa mzunguko wa damu mwilini Matumizi ya alkoholi huzidisha hatari ya kupatwa na ugonjwa wa moyo, hupunguza sukari katika damu, na kuzidisha kiwango cha mafuta katika damu na kuongeza mapigo ya moyo, hivyo kuzidisha shinikizo la damu.

4. Mfumo wa kuyeyusha chakula - Alkoholi inaleta kuwashaa tumboni, na kwa njia hiyo kusababisha kutoka damu katika tumbo hilo... Mazoea ya kutumia alkoholi huzidisha hatari kwa ini kuwana mafuta mengi, homa ya manjano, na ugonjwa wa ini (cirrhosis).

Alkoholi inahusika na asilimia kubwa ya watu wanaojua wenyewe, vifo vinavyosababishwa na magari, kuwatendea vibaya watoto, na ukatili uliomo nyumbani.

8. Kuutumainia Uweza Wa Mungu

Mtu anayesumbuliwa mara kwa mara na hofu au hatia ataona vigumu kwake kupata manufaa kamili kutokana na mazoea hayo ya afya tuliyotoka kuyaeleza muda mfupi tu uliopita. Lakini mtu yule mwenye imani isiyo na shaka kwa Mungu atapata chimbuko hili la mwisho litakalomletea hali njema katika maisha yake.

"Ee nafsi yangu umhimidi BWANA, wala usizisahau fadhili zake zote - yeye anayekusamehe dhambi zako zote na KUKUPONYA MAGONJWA YAKO YOTE, ANAYEUKOMBOA UHAI WAKO na kaburi" - Zaburi 103:2-4.



David Larson, mshauri wa Taasisi ya Taifa ya Afya ya Akiliki kule Marekani, alifanya utafiti wake mpana juu ya uhusiano wa moja kwa moja uliopo kati ya dini na afya. Uchunguzi wake ulionyesha wazi kwamba upo uhusiano wa moja kwa moja kati ya Mkristo aliyejitoa na afya. Alishangaa kujua kwamba, wale wanaohudhuria kanisani wanaishi kwa muda mrefu kuliko wale wasiohudhuria. Wale wanaokwenda kanisani wana upungufu wa kupatwa na mshtuko wa moyo, Mishipa ya arteri kuwa migumu, shinikizo la damu, na magonjwa mengine. Wale wanaomwamini Mungu huishi maisha yenye manufaa zaidi kwa sababu hawapatwi kirahisi na mfadhaiko, hawageuki na kuwa walevi sugu, kufungwa kama

wahalifu wanaorudia mle tena na tena, na kunaswa katika ndoa isiyo na furaha. Kuutumainia uweza wa Mungu ndio msingi wa ustawi wa kweli na maisha ya afya yenye furaha.

Waadventista, Wasabato wapatao 50,000 hivi walichunguzwa, hasa kule California kwa kipindi cha zaidi ya miaka 30. Matokeo yalionyesha kwamba Waadventista wanaume wanaishi miaka 8.9 na wanawake miaka 7.5 kuliko

watu wengine wote kwa jumla. Uchunguzi huo wa Waadventista kule Uhlanzi, Norway na Polandi huonyesha matokeo yanayofanana na hayo. Watafiti wanaona kwamba sababu ya kipindi kirefu cha kuishi kwa Waadventista inatokana na kuzifuata kwao baadhi au kanuni zote nane za afya zilizoleezwa katika mwongozo huu. Wale wanaozifuata kanuni hizi sio tu kwamba wana maisha mrefu zaidi, bali pia wana maisha yaliyo bora sana.

Tukiutumia mtazamo wa Biblia katika maisha yetu tutakuwa tofauti katika aina zote za njia za utendaji wetu na kutoa ushahidi unaovutia kuonyesha kwamba katika ulimwengu mzima Ukristo ni dini inayoweza kuwekwa katika vitendo. Inawabadilisha watu - yaani, fikra zao na matendo yao na kujenga mtindo mpya wa maisha.

Kutokana na uhusiano wa karibu sana uliopo kati ya akili, mwili na maisha yetu ya kiroho, Wakristo wale wanaoishi kwa Neno la Mungu watataka kuzifuata kanuni hizo za mtindo wa maisha uletao afya wanapojiandaa kwa ajili ya marejeo yake Yesu (1 Yohana 3: 1-3). Sio tu kwamba Kristo anataka sisi tuwe

GUNDUA



tayari kukutana naye atakaporudi, pia anataka kuyaboresha maisha yetu ya sasa. Tunaweza kushirikiana naye kwa kuzifuata hizo kanuni za afya za Mungu.

Yesu anaahidi kutuokoa sisi mbali na kila tabia iletayo uharibifu mwilini kwa " kadri ya nguvu [yake] itendayo kazi ndani yetu" (Waefeso 3:20). Endapo wewe unajitahidi kuishinda tabia fulani inayokuathiri mwili wako kama vile kutumia tumbaku au kunywa vimeo, basi, maazimio yako hayo mazuri sana ya kutaka kuacha tabia hiyo mara nyingi yanageuka na kuwa kwako kama kamba za mchanga. Lakini kwa kuuchota uwezo wa Mungu unaotenda kazi ndani yako Mungu aweze kukupa wewe nguvu za kukuwezesha kushinda. Neno la Mungu linaahidi hivi: " Naweza kufanya mambo yote kwa njia yake Kristo anitiaye nguvu" (Wafilipi 4:13)

KUINGIA KATIKA MAISHA YA KIKRISTO

Hapa ni barua ya kusimua sana toka kwa mmojawapo wa wawakilishi wa Shule yetu ya Biblia katika Afrika.

" Miaka mitano iliyopita nilipokea ombi toka kwa sauti ya Unabii ili nimtembelee mfungwa mmoja ambaye alikuwa mwanafunzi wa Shule ya Biblia kwa Posta. Nilionyesha ombi lile kwa wakuu wa gereza lile ambao kwa hisani yao walinipa ruhusa. Kwa kuwa mwanafunzi yule alikuwa na hamu kubwa sana ya kujifunza Biblia, basi, nilimtembelea mara kwa mara.

"Karibu miezi sita baada ya kumtembelea mara ya kwanza, aliomba kubatizwa na kujiunga na kanisa. Wakuu wale walikubali kuandaa mahali ili ubatizo ule ufanyike ndani ya gereza lile. Wasimamizi wao pamoja na wafungwa wengine walikusanyika pale kushuhudia ubatizo ule niliopata kuufanya ambao uliigusa mioyo yao.

"Muda mfupi baada ya tukio lile, ndugu yetu yule alifunguliwa toka kifungoni, ingawa bado alikuwa na muda mrefu wa kutosha kutumikia kifungo chake. Nilipoulika imekuwaje, niliambiwa kwamba maisha yake yalikuwa yamebadiliaka kabisa, naye akawa shahidi aliyemshuhudia Mwokozi wake, na dini yake hata hakuweza tena kufikiriwa kama mfungwa wala kutendewa kama mfungwa. Mtu yule akaungana na familia yake na sasa ni kiongozi katika mojawapo ya makanisa yenye watu wengi."



1. Ubatizo Maana Yake Nini?

Mfungwa yule alipogeuka na kuwa Mkristo na maisha yake yalipobadilika kabisa, kwa nini ilikuwa ni lazima kwake kubatizwa? Katika mazungumzo yake na Nikodemo, Yesu anaonyesha umuhimu na maana ya huo ubatizo:

"Hakuna mtu ye yote aezaye kuuona ufalme wa Mungu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho" - Yohana 3:3,5.



Basi kulingana na Yesu ni lazima sisi tuzaliwe " kwa maji na kwa Roho." Katika maisha mapya kuititia katika badiliko la mawazo na moyo. Kwa kuwa kuingia katika ufalme wa Mungu kunataka maisha mapya kabisa, si yale maisha ya zamani yaliyotiwa viraka, ndio maana yanaitwa kuzaliwa upya. Ubatizo wa maji ni ishara ya nje inayoonyesha badiliko hilo la ndani. Mwakilishi wetu alimbatiza yule mfungwa kama ishara ya kutambua kujitoa kwake kwa Kristo na ishara ya badiliko kamili ambalo Roho Mtakatifu alikuwa ameanza kufanya katika tabia yake.

2. Kwa Nini Mimi Nibatizwe?

Wokovu wetu unayazunguka matendo makuu matatu ya Kristo.

"Kristo ALIKUFA kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo Maandiko, ... ALIZIKWA, ... ALIFUFUKA siku ya tatu, kama yanenavyo Maandiko" - (1 Wakorintho 15:3,4).

Kristo alifanya wokovu huo uwezekane kwa njia ya kifo chake, kuzikwa kwake, na kufufuka kwake.

"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu TULIBATIZWA KATIKA MAUTI YAKE? Basi TULIZIKWA PAMOJA NAYE KWA NJIA YA UBATIZO katika mauti yake, kusudi KAMA

GUNDUA

DISCOVER
online

KRISTO ALIVYOFUFUKA KATIKA WAFU kwa njia ya utukufu wa Baba, VIVYO HIVYO NA SISI TUPATE KUISHI MAISHA MAPYA." - Warumi 6:3,4.

Kristo alikuwa kwa ajili ya dhambi zetu, alizikwa, kisha alifufuka katika kaburi ili kutupa sisi maisha mapya ya haki. Kwa kubatizwa sisi tunashiriki kabisa katika kifo, kuzikwa, na kufufuka kwake Yesu. Ubatizo una-maanisha kwamba sisi tumeifia dhambi pamoja na Kristo, kisha tunafufuka na " Kuishi maisha mapya" ndani ya Kristo. Kifo chake Kristo ufufuo wake huwa ni Kifo chetu na ufufuo wetu. Mungu anaweza kutufanya sisi kuwa hai katika mambo yale ya Roho kana kwamba sisi tulikuwa tumefufuliwa katika wafu. Tendo la kimwili la ubatizo kwa picha huwakilisha hatua za kuongoka.



Kwanza, tunaingizwa ndani ya maji, yaani, tunazamishwa majini kabisa, sawasawa tu na watu ambao wamekuwa wanavyoshushwa kaburini na kufunika na udongo. Hii ni kusema kwamba sisi tunapenda kuwa pamoja na Kristo na kuyazika maisha yetu yale ya zamani. Ubatizo ni mazishi (maziko), ni kuyaaga rasmi maisha yale ambayo yalitawaliwa sana na dhambi. Halafu, tunanyanyuliwa juu kutoka ndani ya maji na yule anayebatiza, sawasawa tu na mtu anayefufuliwa kutoka kaburini. Hii ni kusema kwamba sisi ni "[vi]jumbe vipyä" tumejitoa kabisa kuishi hayo maisha mapya anayotupa Mungu.

Ni kuzamishwa ndani ya maji peke yake kunakoweza kuonyesha kielezo sahihi cha maana halisi ya ubatizo - yaani, kifo, kuzikwa na kuzaliwa upya. "Ubatizo" kwa njia ya kunyuniiza maji kidogo kichwani hauonyeshi kwa utoshelevu mfano huo wa kuzaliwa upya.

Je! Kufa pamoja na Kristo maana yake ni nini hasa?

"Tukijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena" - (Warumi 6:6)

Ubatizo unawakilisha kwa nje kile anachopaswa mtu kufanya ndani yake: yaani, kusalimisha kila kitu kwa Kristo. Tukizua kitu chochote kwa Mungu, huenda tutaendelea kuwa "Watumwa wa dhambi" Tunapojisalimisha kabisa kwa Kristo, tamaa zetu za dhambi zinafanya kuwa bila nguvu yoyote na badiliko kamili linaanza kutokea.

Je! Ni nani ahusikaye na mabadiliko yanayotokea?

Nimesulubiwa pamoja na Kristo wala mimi si hai tena, lakini KRISTO ANAISHI NDANI YANGU. Na maisha haya ninayoishi katika mwili huu, NAISHI KWA KUMWAMINI MWANA WA MUNGU, aliyenipenda na kujitoa nafsi yake kwa ajili yangu" - (Wagalatia 2:20).

Ninapoifananisha na kusulibiwa kwake Kristo kwa njia hiyo ya ubatizo nakaribisha uwezo wenye nguvu nyangi katika maisha yangu - yaani, "Kristo anaishi ndani yangu". Ili upate kuyaweka maisha yako mikononi mwa Kristo kabisa kwanza huna budi kumtazama Kristo akifa pale msalabani. Usiiangalie ile dhambi inayokutishia wewe, usiingalie kumbukumbu yako ya zamani na kuomboleza mtazame Yesu. Kukitazama kifo chake Kristo kilichojaa neema na ujasiri pale Kalvari, unaweza kuonyesha mshikamano wako ulio nao pamoja naye, kwa maneno haya: "Kwa nguvu ya msalaba nadai kwamba mimi ni mfu kwa zile tabia zangu za zamani, na Mungu. Naamua kusimama pamoja na Kristo. Kuanzia sasa na kuendelea mimi nita"ishi kwa kumwamini aliyenipenda na kujitoa nafsi yake kwa ajili yangu"

Tunapoichota ile nguvu itokanayo na kifo na ufufuo wake Kristo, tunaziona sifa za tabia yake zikijitokeza zaidi na zaidi na kuchukua mahali pa tabia zetu zile za zamani:

"Mtu awaye yote akiwa NDANI YA KRISTO, amekuwa KIUMBE KIPYA: ya Kale yametoweka, MAPYA yamekuja!" - (2 Wakorintho 5:17).

Kwa njia hiyo ubatizo sisi tunaonyesha tamaa yetu tuliyonayo ya kushikana mikono na Yesu na kuishi hayo maisha mapya yaliyo bora tukiwa ndani ya Kristo" Yesu anafanya ndani yetu kile ambacho sisi tusingeweza kamwe kujifanya wenyewe. Tunapanda kutoka ndani ya maji tukiwa " [vi]umbe [vi]pya" anatupa uwezo wa kuishi hayo "maisha mapya".

3. Hivi Kwa Nini Yesu Alibatizwa?

Wakati ule wa Pentekoste, Petro aliwaambia wale walioataka kuwekwa huru mbali na dhambi kwamba wanapaswa kutubu na kubatizwa ili Kristo aweze kuwasamehe "dhambi zenu" (Matendo 2:38) Kwa kuwa Yesu hakutenda kamwe dhambi hata moja, basi kwa nini alijachia mwenyewe kubatizwa?

"Wakati huo YESU AKAJA kutoka Galilaya MPAKA YORDAN ILI ABATIZWE na Yohana ... KUITIMIZA HAKI YOTE" - Mathayo 3:13,15.



Yesu alikuwa hana dhambi. Hakuwa na haja ya kutubu dhambi yoyote. Alibatizwa kutokana na sababu nydingine: "Kutimiza haki yote" kwa kubatizwa kwake, Yesu alitoa kielelezo chenye nguvu kwa ajili yetu sisi wanadamu dhaifu na wenyewe dhambi. Kristo kamwe hawaombi wafusi wake kwenda mahali kokote ambako yeje hajapata kufika. Kwa hiyo waumini wanapozamishwa ndani ya maji ya ubatizo, wanafuata nyayo za bwana wao.

Kwa vile Kristo alikuwa kwa ajili ya dhambi zetu, anaweza kutupa sisi haki yake.

Mungu alimfanya yeje asiyejewa na dhambi kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili ndani yake sisi tupate kuwa haki ya Mungu" 2 Wakorintho 5:21.

Tukiwa tumebadilishwa kabisa kutoka katika hali yetu ya kuwa wenyewe dhambi na kuwa watakatifu machoni pake Mungu, tunakuwa ndani ya ile "haki" na kwa njia hiyo tunaishi maisha mapya ndani ya Kristo.


4. Kwa Nini Nizamishwe Ndani Ya Maji?

Kristo alizamishwa ndani ya maji wakati wa ubatizo wake. Hakunyuniyiziwa maji kidogo kichwani. Yohana alimbatiza ndani ya mto wa Yordani "kwa sababu huko kulikuwa na MAJI TELE" (Yohana 3:23) Yesu alipobatizwa alikwenda na kuingia ndani ya maji, kisha "mara tu Yesu alipokwisha kubatizwa [alipokwisha kuzamishwa , Kigiriki] AKAPANDA KUTOKA NDANI YA MAJI" (Mathayo 3:16)

Tunapoilewa maana halisi ya ubatizo, hatuna shida sana kuutambua mfumo sahihi wa ubatizo. Neno lenyewe hasa la "ubatizo"linatokana na neno la Kigiriki baptizo " ambalo linamaanisha kuchovya au kuzamisha, kuweka chini ya).

Wakati wa ziara yake moja John Wesley kule Amerika katika mwaka wa 1737, baraza la wazee wa mahakama ya kanisa wapatao wanaume 34 walimhukumu yeje kwa shtaka la ajabu la "kukataa kumbatiza mtoto wa Bwana Parker, isipokuwa kwa njia ya kumzamisha ndani ya maji." Ni dhahiri kwamba baba huyo wa Kimethodisti aliwabatiza waongofu wake kwa kuwazamisha ndani ya maji.

Mwanamatengenezo ya kanisa John Calvin alieleza hivi: "Ni jambo la hakika ya kwamba kuzamisha majini ilikuwa ndiyo desturi ya Kanisa lile la kale" - Institute of the Christian Religion, Kitabu cha 4, Sura ya 15, Sehemu ya 19.



Historia ya kanisa lile la kwanza inadhahirisha kwamba ubatizo ulimaanisha kuzamishwa ndani ya maji.

Mkuu wa makasisi Stanley, wa Kanisa la Anglikana, aliandika maneno haya: "Kwa karne kumi na tatu za mwanzo, desturi ya ubatizo iliyoenea sana mahali pote ilikuwa ni ile tuisomayo katika Agano Jipy, na ambayo ndiyo maana halisi ya neno "batiza" - kwamba wale waliobatizwa walitumbukizwa, yaani walifunikwa kabisa na maji, walizamishwa ndani ya maji" - Christian Institutions, Uk. 21

Mashimo ya kubatizia ndani ya maji yanaonekana katika makanisa mengi yaliyojengwa kati ya karne ya nne na karne ya kumi na nne kule Ulaya na Asia, makanisa kama vile kanisa Kuu la Pisa, Italiana la Mtakatifu Yohana, kanisa kubwa kuliko yote mjini Roma.

Kanisa Katoliki halikuukubali ubatizo wa kunyunyizia maji kichwani kuwa ni wa halali kama ule wa kuzamishwa majini mpaka lilipokaa Baraza la Ravenna mapema katika karne ile ya kumi na tano. Katika masuala yale yanayohusu desturi za kanisa, hatutakiwi kufuata kile anachofundisha mwanadamu, bali kile ambacho Kristo na mitume wake wanafundisha.

Wakristo wengi waliowanyofu wa moyo wanayapenda sana yale mapokeo yahusuyo ubatizo wa watoto wachanga, na kule kuwatoa watoto wetu kwa Mungu kuanzia mwanzo kabisa wa maisha yao ni jambo linalopendeza hakika. Walakini, Biblia inaeleza wazi ya kwamba ni lazima mtu afundishwe ile njia ya wokovu kabla ya ubatizo wake (Mathayo 28:19,20) kwamba ni lazima mtu amwamini Yesu kabla ya kubatizwa (Matendo 8:35-38) na ya kwamba ni lazima mtu atubu dhambi zake na kusamehewa kabla ya kubatizwa (Matendo 2:38) Mtoto mchanga hana uwezo kabisa wa kuamini, kutubu au kuungama dhambi zake, mambo ambayo ni lazima yatangulie kabla ya ubatizo.

5. Kwa Nini Ni Muhimu Kubatizwa?

Kulingana na Yesu, ubatizo ni wa lazima kwa wale wanaotaka kuingia mbinguni.

"Hakuna mtu ye yote auezaye kuingia katika ufalme wa Mungu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho"- Yohana 3:5.

Yesu anatoa walakini mmoja tu. Yule mwizi pale msalabani ali "zaliwa kwa Roho" ingawa kwake ilikuwa haiwezekani kabisa hata kuondoka tu pale msalabani na kwenda kuzamishwa ndani ya maji kama ishara ya badiliko lake la moyo. Naye Yesu alimwahidi kwamba angekuwa pamoja naye [Kristo] katika ufalme wake (Luka 23:42,43) Kwa yule mwizi, kuzaliwa kwa maji na kwa Roho" kuliwakilishwa na damu ya Yesu iliyomwagika pale kumtakasa dhambi zake. Agostino (Augustine) alichunguza na kusema "Kuna tukio moja la toba ya mtu mmoja aliyeokuwa akifa kitandani pake ambalo limewekwa katika kumbukumbu, yaani lile la mwizi yule aliyetubu, ili asiwepo mtu hata mmoja wa kukata tamaa, naye alikuwa ni yule mmoja tu ili asiwepo hata mmoja anayethubutu kufanya hivyo"

Yesu mwenyewe alitoa onyo hili zito:

Aaminiye na kubatizwa ataokoka, asiyeamini [na kwa sababu hiyo habatizwi]atahukumiwa " - Marko 16:16



Alipokuja badala yetu pale Kalwari Yesu alionyesha mbele ya wanadamu wote upendo wake alionao kwetu sisi. Tunahitaji kuitikia kwa kufanya ungamo letu bila haya mbele ya watu kuhusu kujitua kwetu kwa Kristo kwa njia ya ubatizo. Je! Hivi wewe umeanza maisha hayo mapya ndani ya Kristo? Je! Umebatizwa ? Kama sivyo kwa nini wewe usijjandae kwa ubatizo katika siku za karibuni?

6. Ubatizo Ni Mwanzo Tu

Ubatizo unawakilisha kujitoa kwetu ili tupate kuishi mtindo wa maisha ya Kikristo. Lakini kule kujisalimisha kwetu wakati wa ubatizo hakujidhesi kwenyewe kama mashine katika kipindi chote cha maisha yetu.

Mtoto anapozaliwa, kufanya sherehe ni sawa. Baada ya siku ya kuzaliwa kupita na msisimko kupungua, yule mtoto mchanga anahitaji kulishwa kila siku, kuogeshwa kila siku, na kuwa makini kila siku kuangalia afya yake.

Ni sawasawa na ubatizo. Paulo alisema hivi kuhusu uzoefu wake wa maisha "Ninakufa kila siku" (1 Wakorontho 15:31) Kwa kubadiliwa kila siku na kuachana na ubinafsi wetu, tunakuwa wepesi kuvutwa na zaidi kwa Kristo.



Taratibu ya ibada ya ubatizo, kama sherehe ya kufungisha ndoa, ilikusudiwa kuwa uthibitisho rasmi uonyeshao kwamba uhusiano wa ajabu ambao unakuwa umekwisha kuanza. Ili kuweza kukua daima tunahitaji kujitoa sisi wenyewe kila siku kwa Kristo kupokea kila siku maisha hayo mapya kwa njia ya maombi na kujifunza Biblia.

7. Sababu Ya Kushangilia

Ubatizo ni sababu iletayo kushangilia sana kwa sababu wale wanaomwamini Kristo wanayo ahadi ya uzima wa milele. Yeyote aaminye na kubatizwa ataokoka (Marko 16:16) Tunapokwisha kubatizwa tunaingia katika njia ile iendayo juu ambayo inatupeleka kwenye ile furaha ya milele.

Ubatizo pia unasherehekea furaha yetu tuliyo nayo sasa pamoja na Kristo. Anaahidi kuwapa zawadi ya thamani kubwa mno ya Roho Mtakatifu wale waliobatizwa (Matendo 2:38) Pamoja na huyo Roho huja lile "tunda la Roho" - yaani upendo ambao unayajaza maisha yao na "uvumilivu, utuwema, fadhili, uaminifu, upole na kujitawala nafsi" (Wagalatia 5:22,23)

Kuwa na Yesu anayeishi ndani yetu kwa njia ya Roho Mtakatifu hutupa sisi hisia kubwa sana ya kuwa na hakika. Kwa maana " Roho Mwenyewe hushuhudia ... ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu" (Warumi 8:15,16)

Uhusiano huo imara pamoja na Mungu unatuletea manufaa mengi, lakini hautoi dhamana kwetu ya kutupatia maisha yasiyokuwa na matatizo yoyote.

Kwa kweli, adui yetu mara nyingi anajitahidi sana kuwatupia shida nyingi sana wale waliokwisha kujitoa sasa kwa Kristo. Walakini tunapokuwa mikononi mwake Mungu tunaweza kujua kwamba atatumia kila jambo linalotupata sisi, liwe jema au baya, ili kutufundisha na kutusaidia kukua (angalia Warumi 8:28)

Mwanamke mmoja kijana alikata shauri kutoa maisha yake kwa Kristo na kubatizwa licha ya vitisho vyakupwa talaka toka kwa mume wake. Yeye hakutaka sehemu yoyote ya imani yake ile mpya lakini mwanamke yule akamng'ang'ania Yesu na kujitahidi kuwa mwenye upendo kuliko alivyokuwa kabla yake. Kwa kipindi fulani yule mume alifanya mambo kuwa magumu mle nyumbani. Lakini hatimaye alishawishiwa kwenda upande wa mkewe kutokana na hoja aliyoshindwa kujibuu: yaani, maisha ya mkewe yaliyobadilika kabisa. Mtu huyo akasalimisha maisha yake kwa Kristo, naye akabatizwa pia.

Kule kung'ang'ania kwetu kusimama karibu na Kristo "kwa heri na kwa shari" [katika hali iwayo yote ile] kutatufanya kuwa vyombo vyenye nguvu nyingi mikononi mwake. Tunaweza kumkabidhi maisha yetu bila masharti yoyote kwa sababu yeye kimsingi tayari amekwisha kujitoa kwetu alipolipa fidia kwa ajili ya dhambi zetu pale msalabani. Ni heshima kubwa iliyopewa sisi kuweza kumpa upendo na utii wetu

GUNDUA

DISCOVER
online

mbele ya watu! Endapo wewe bado hujafanya hivyo, kwa nini usisalimishe maisha yako kwa Kristo sasa hivi. Mwombe ye ye akupe maisha mapya ndani yako kwa njia ya Roho wake Mtakatifu halafu batizwa na kuingia ndani ya Kristo.

SIRI YA KUKUA KWA USHIRIKIANO

Mapema katika miaka ile ya kuanzia 1960 na kuendelea, Ndugu Andrew, mtu wa Uholanzi, aliingiza kwa siri mzigo wa Biblia katika gari lake la Volks Wagen (Folks Vageni) na kuvuka mpaka wa Romania na kuwapita walinzi wa kikomunisti. Alipanga katika hoteli moja na kuanza kuomba kwamba Mungu amwongoze kwenda kwenye makundi ya Kikristo yanayofaa - yaani wale ambao wangeweza kuzitumia vizuri sana zile nakala zake za Maandiko.

Mwisho wa juma lile Andrew alitembea kwenda kwa karani wa hoteli ile na kumwuliza angeweza kulipata wapi kanisa.

Yule karani akamwangalia kwa njia isiyo ya kawaida kidogo na kujibu, "Hatunayo mengi ya hayo, unajua. Isitoshe, usingeweza kuielewa lugha yetu"

"Je! Wewe hukujua?" akajibu Andrew, "ya kuwa Wakristo wanazungumza lugha ya ulimwengu mzima."

"Ehee! Ni lugha gani hiyo?"

"Inaitwa Agape [Upendo]"

Yule karani alikuwa hajapata kuisikia kamwe, lakini Andrew alimhakikishia kwa kusema hivi, "Ni lugha nzuri kuliko zote ulimwenguni"

Andrew aliweza kuyapata makundi kadhaa ya kanisa katika eneo lile na kufanikiwa kupanga kuonana na mwenyekiti na katibu wa dhehebu fulani. Kwa bahati mbaya, ingawa Andrew na watu hao walijua lugha kadhaa za Ulaya, wakajikuta hawana lugha hata moja waliyoijua wote. Basi, wakakaa pale wakikodoleana macho tu. Andrew alikuwa amesafiri maili nyingi za hatari na ule mzigo wake wathamani, lakini ikaonekana ya kwamba hapakuwa na njia yoyote ya kujua iwapo watu wale walikuwa ni ndugu Wakristo wa kweli au makachero wa Serikali.

Hatimaye akaiona Biblia ya Kiroma juu ya meza katika ofisi ile. Andrew akaingiza mkono wake katika mfuko wake na kuichomoa Biblia ya Kiholanzi. Alifunua 1 Wakorintho 16:20, na kuishika Biblia akiwa amenyosha mkono wake akisonda kidole chake kwenye jina la Kitabu kile waliweza kilitambua. Mara moja nyuso zao zikang'aa kwa meru. Upesi wakaipata sura ile ile na fungu lile lile katika Biblia zao za Kiromania, Kisha wakasoma maneno haya: "Ndugu wote hapa wanawasalimu. Salimianeni kwa busu takatifu."

Watu wale wakatabasamu na kumwangalia Andrew. Kisha mmoja wao akapekua katika Biblia yake na kupata Mithali 25:25.

Andrew akalipata fungu lile na kulisoma "kama vile maji baridi yalivyo kwa mtu mwenye kiu, ndivyo ilivyo habari njema itokayo katika nchi ya mbali "

Watu wale walitumia nusu saa wakiongea na kupeana habari - kwa kuititia tu katika maneno ya Maandiko. Walikuwa na furaha nyingi sana kwa urafiki wao huo uliovuka mipaka yote ya utamaduni hata wakachecha mpaka machozi yalipowatoka.

Andrew alijua kwamba amewapata ndugu zake. Alipowaonyesha mzigo wake wa Biblia, Waromania wale walitekwa nao wakamkumbatia tena na tena.

Jioni ile katika ile hoteli, yule karani alikuja karibu na Andrew na kusema kwa mshangao, 'Aisee, nilitafuta 'agape' katika kamusi. Hakuna lugha ya jina lile. Hilo ni neno la Kigiriki limaanishalo upendo.



GUNDUA

Andrew akajibu "sawasawa. Mimi nilikuwa nazungumza kwa kutumia neno hilo mchana kutwa".

Je! Wewe umeigundua lugha hiyo nzuri? Katika mwongozo huu utajifunza juu ya jinsi Mungu anavyoweza kutuleta sisi sote katika jamii yake kubwa ya upendo.

1. Kanisa Lilianzishwa Kwa Ajili Ya Ushirika

Yesu alilianzisha kanisa ili kukidhi hitaji la msingi la kibinadamu la malezi na kusaidiana. Sisi sote tunayo mahitaji yetu. Na hivyo ndivyo kanisa linavyohusika na mambo hayo yote. Hapo ni mahali tunapokuja ili kushirikiana na kusaidiana. Maandiko yanalidhihirisha kanisa lile lenye nguvu la Mitume ambalo liliwaita wanaume na wanawake kuja katika ushirika uliojaa furaha ambaa ulikwenda juu ya njia yote hadi kwa Mwenyezi:

"Tulichokiona na kukisikia ndicho tunachowatangazieni nyinyi pia, ili nanyi mpate kuijunga nasi katika umoja tulio nao na Baba na Mwanae Yesu Kristo. Tunawaandikia nyinyi mambo haya kusudi furaha yetu ikamilike" - 1 Yohana 1:3,4.

Miyo yenye mawazo sawa iliyofungwa pamoja kwa njia ya mawasiliano na Yesu na mawasiliano ya wao kwa wao, huionja "furaha kwa kiwango chake chote! Wote wanaongea lugha moja, lugha ile ya upendo.

Wakristo wanakuwa sehemu ya familia iliyotandaa. Wanakuwa ndugu na dada katika Kristo kwa kuwa wote wanayo roho ya undugu. Kadiri unavyozidi kupanuka umoja huo wa imani, ndivyo kadiri vifungo vyenye nguvu zaidi vinavyokuwepo mionganoni mwa Wakristo.

Washiriki wa makanisa yale yaliyoanzishwa na mitume wa Yesu walifungwa pamoja wakiwa na itikadi zao zinazofanana, kwa upendo wao waliokuwa nao kwa Mungu na kwa shauku yao ya kumtumikia na kuugawia ulimwengu huu neema yake. Kifungo hicho cha ushirika wao wa karibu sana kilikuwa kimojawapo ya sababu zilizowafanya watu wale wachache wasiokuwa na nguvu, ambaa walikuwa wakiteswa, kuupindua ulimwengu wa wakati ule.

2. Kanisa Aliloanzisha Kristo

Je! Hivi Kristo analo kanisa, au wazo zima juu ya shirika la dini ni mavumbuzi tu ya wanadamu? Yesu anajibu hivi:

"Juu ya MWAMBA huu nitalijenga kanisa langu, wala milango ya kuzimu haitalishinda" - (Mathayo 16:18).



Yesu ndiye ule Mwamba wa kutia nanga zetu, Jiwe la pemberi la kanisa lake.

Je! Ni kusudi gani ambalo lilikuwa sehemu ya msingi wake?

"Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye Kristo mwenyewe ni jiwe la pemberi" - Waefeso 2:20.

Je! Injili ile ilipohubiriwa, Bwana alifanikiw akufanya nini?

"Na Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa" - (Matendo 2:47, KJV).

Yesu alipoanzisha kanisa lile, aliahidi kwamba "milango ya kuzimu haitalishinda"(Mathayo 16:18), na kanisa la Kikristo mpaka sasa linaendelea kuwapo. Limepata kuwa na maadui wenye nguvu nyingi kabisa kuanzia na wafalme wale wa Dola ya Kiroma hadi kwa madikteta wa Kikomunisti lakini damu ya wafiadini imelifanya lizidi kuwa na nguvu nyingi. Mkristo mmoja alipochomwa moto kwenye mti wa kuchomea au alipotupwa kwa simba, wengine kadhaa walijitekeza kuchukua nafasi yake. Watu wenye nadharia ya kushuku mambo ya Mmungu

wamefanya kila waliloweza kujaribu kutoa sababu zao na kulipotosha kanisa. Lakini ile kweli ya Kikristo inashindana nao kwa usafaha sana kuliko hapo kwanza katika kizazi hiki cha sayansi na kinachopenda mambo ya ulimwengu.

Mojawapo ya changamoto kuu kuliko zote kwa kanisa ilikuja mara tu baada ya kukubalika kwake kama dini rasmi ya Dola ya Roma. Kanisa likapata utajiri mwingu - na hatimaye likaharibika. Likaonekana limekuwa kiroho katika zile zama za giza. Lakini siku zote Bwana alihifadhi sehemu ya maana ya waumini waliokuwa wajasiri na waaminifu ambao katikanyakati zile zisizokuwa na matumaini na ngumu, waling'aa sana kama nyota wakati wa usiku usiokuwa na mbalamwezi.

Paulo analinganisha uhusiano uliopo kati ya Kristo na Kanisa lake na uhusiano ule wa upendo, unaotunza, wa mume kwa mke wake (Waefeso 5:23-25). Kanisa ni familia, kila mshiriki akifanya uhusiano wake na washiriki wengine wa familia hiyo na kuchangia katika usitawi wao (Waefeso 2:19)

Paulo pia analionyesha kanisa kama mwili hai, Kristo mwenyewe akiwa ndiye kichwa chake (Wakolosai 1:18).

Tunapokuwa tumebatizwa, tunatoa ushuhuda wa imani yetu ndani ya Yesu na kuwa washiriki wa ule "mwili" yaani kanisa.

"Maana sisi, tukiwa Wayahudi au watu wa mataifa mengine, watumwa au watu huru, sote TUMEBATIZWA kwa Roho mmoja KATIKA MWILI HUO MMOJA; na sote tukanyweshwa Roho huo mmoja" - (1 Wakorintho 12:13).

Kitabu cha ufunuo kinaonyesha picha ya Kristo aliyefufuka akitembea katikati ya makanisa akionyesha ulinzi wake alionao juu yake (Ufunuo 1:20,12,13). Kristo hajawaacha watu wake kamwe, wala hatawaacha kamwe.

3. Kanisa Lenye Kusudi Maalum

Kuhudhuria kanisani ni kwa maana sana kwa Mkristo. Tunahitaji msaada wa wengine kuifanya imani yetu iwe hai na iendelee kukua.

Kanisa pia lina wajibu wa maana wa aina tatu:

1) Kanisa linalinda kweli.

Likiwa ni "nguzo na msingi wa kweli" (Timotheo 3:15), kanisa linatetea na kulinida kweli ya Mungu mbele ya ulimwengu.

Tunahitaji hekima ya pamoja ya waumini wengine ili kutusaidia kukuza mawazo yetu juu ya kweli zile zilizo za muhimu za maandiko.

2) Kanisa ni kielelezo cha jinsi neema ya Mungu iwezavyo kuwatendea wenyе dhambi. Mabadiliko aliyoafanya Kristo katika maisha ya waumini humtangaza Mungu atuitaye sisi "Katika nuru yake ya ajabu" (I Petro 2:9).

3) Watu wa Mungu ni mashahidi wake kwa ulimwengu huu wenyе shida. Kabla tu hajarudi mbinguni, Yesu aliwaahidi wanafunzi wake, alisema.

"Lakini mtapokea nguvu Roho Mtakatifu akiisha kuwajilia juu yenu, nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalem, na ktika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi" - (Matendo 1:8).

Ni heshima kubwa kwa kanisa kuupeleka huo ujumbe wa pendo kuu la Mungu ulimwenguni kote.



4. Limeanzishwa Kwa Ajili Ya Kutiana Nguvu

GUNDUA

DISCOVER
online

Kanisa lile alilolianzisha Kristo lilikuwa na mfumo halisi. Mtu aliweza kuingizwa au kutoingizwa katika ushirika wake (Mathayo 18:15-18). Kanisa la Mungu liliwachagua viongozi, tena lilikuwa na makao makuu ya ulimwengu pamoja na sehemu za kukutania za kila mahali (Matendo 8:14;14:23;15:2 1Timotheo 3: 1-13) Walipokwisha kubatizwa, waumini walijiunga na kundi lililokuwa limeanzishwa. (Matendo 2:41 na 47).

Kanisa lipo kwa ajili ya kutiana moyo.

"Hebu na tufikirie jinsi tuvezavyo kuhimizana katika upendo wa kazi nzuri. Tusiache kukusanyika pamoja, kama wengine walivyozoea kufanya, bali TUTIANE moyo sisi kwa sisi - na kuzidi kufanya hivyo kadiri mwonavyo. Siku ile (ya kuja kwake Kristo) kuwa inakaribia. "-Waebrania 10:24,25.



Kwa kifupi, hayo ndiyo mambo yafanywayo na kundi la Kanisa lenye afya. Washiriki wake wanajengana katika imani, wanatiana moyo wao kwa wao. Mungu alilianzisha Kanisa lake ili kuwatia nguvu watu wa Mungu na pia kutoa huduma kwa ulimwengu huu. Twaweza kufanya mambo mengi sana tukiwa pamoja kuliko tuvezavyo kufanya mambo mengi sana tukiwa pamoja kuliko tuvezavyo kufanya kama mtu mmoja mmoja hapa na pale. Chukua mfano mmoja tu. Kanisa la Waadventista Wasabato. Sisi tunaendesha kazi ya uganga katika eneo kubwa sana ulimwenguni kote - kuanzia yale magari ya afya yaliyo ndani kabisa ya mji mkuu kwenda kwenye kliniki zilizo katika visiwa vilivyojijenga mbali katika bahari ya Pasifikasi ya Kusini. Taasisi zetu za elimu zimewaletea makumi ya maelfu ya vijana maarifa ya maisha bora ndani ya Kristo - kuanzia Chuo kikuu cha Loma Linda, kinachoongoza katika kazi ya kupandikiza miyo, kwenda kwenye shule ndogo kabisa za misheni zilizotawanyika ndani ya nchi zote za Afrika. Sisi tunashughulika na njaa na maafa kupidia ADRA. Makanisa yaliyo katika maeneo mbali mbali yanawavika nguo na kuwalisha maskini na wasio na kwao katika maelfu ya vituo vya huduma kwa jamii. Nayo makundi ya waumini wa Kiadventista wanahubiri ujumbe wa wokovu katika nchi zaidi ya 200. Ni lile kundi la Wakristo waliojitoa wakfu tu lililoundwa ambalo lingeweza kuleta matokeo hayo kwa ulimwengu mzima.

Kristo na mitume walilifananisha Kanisa na mwili, na kuonyesha kwamba sehemu zote za mwili zinahitajika (1Wakorintho 12:21-28). Sehemu zote za mwili hazifanani kabisa, lakini zote ni za muhimu na zote hazina budi kufanya kazi pamoja kwa ushirikiano.Jicho lililoitenga na mwili haliwezi kuona.

Mkono uliokatwa hauna faida ye yeyote. Si kitu kama sisi tu jicho, mkono, au kidole tu, hatuwezi kutenda kazi yetu kwa ajili ya Kristo kwa ufanisi kama kila mmoja wetu anajitegemea mwenyewe kabisa. Kuwa mshiriki wa kanisa, kuungika na viungo vingine vya mwili hututua nguvu sisi kama wakristo.

5. Furaha Ya Kuabudu

Ndani kabisa ya mioyo yetu imo shauku ya kumwabudu Mungu, na haja hiyo yaweza kufilia au kutoweza tusipoiruhusu kufanya kazi yake. Je! Mtunga Zaburi alijisikiae alipofikiria kwenda mahali pale pa ibada? **"NALIFURAH! pamoja na wale walioniambia, "Na twende nyumbani mwa BWANA" - (Zaburi 122:1).**

Je! Muziki una sehemu gani katika ibada ya watu wote?
"Mwabuduni BWANA kwa furaha, "Njoni mbele zake kwa nyimbo za furaha"
- (Zaburi 100:2).

Biblia inatuambia kwamba kutoa sadaka ni sehemu murua ya ibada ya Mungu.



GUNDUA

"Leteni sadaka mkaziingie nyufa zake. Mwabuduni BWANA kwa uzuri wa utakatifu" - (Zaburi 96:8-9).

Maombi nayo pia ni sehemu ya maana ya ibada ya watu wote.

"Njoni tusujudu katika ibada tupige magoti mbele za BWANA MUUMBAJI wetu' - Zaburi 95:6

Kujifunza Biblia na kuhubiri ni kitovu cha ibada ya Agano Jipy. Kuanzia na lile hubiri la Petro katika ile siku ya Pentekoste, ambalo linapatikana katika Matendo 2, na kuanzia katika nyakati zile za wanamatengenezo ya kanisa wale wakiporotestanti hadi katika hizi siku zetu, kila uamsho mkuu wa kidini umejengwa juu ya mahubiri yatokanayo katika Biblia. Hivi kwa nini? Kwa sababu "Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu. Lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili" - (Waebrania 4:12-13).

6. Je Kitu Gani Ni Chema Kuhusu Kanisa?

Wengine hupinga na kusema kwamaba kanisa limejaa watu amba si wakamilifu. Lile alilolisema Henry Ward Beecher ni la kweli:

"Kanisa sio nyumba ya sanaa ya maonyehso ya Wakristo maarufu, bali ni shule kwa ajili ya kuwaelimisha hao wasio wakamilifu.

Kwa kuwa hakuna hata mmoja mionganii mwetu aliye mkamilifu, basi kanisa halitakuwa kamilifu pia.

Katika mmojawapo wa mifano yake Yesu alitukumbusha sisi kwamba magugu huota pamoja na ngano (Mathayo 13:24-30). Tunapozisoma nyaraka za Paulo za Agano Jipy, tunagundua kwamba kanisa lile la mitume lilikuwa na matatizo makubwa sana. Na kanisa la leo mara nyinyi lina upungufu mkubwa. Lakini, Tafadhalii, kumbuka kwamba hakuna washriki wenye makosa wawezao kuliharibu au kulivuruga lile Jiwe kuu la Pembeni la kanisa - yaani, Yesu Kristo mwenyewe. Basi, ndani ya makanisa yasiyo makamilifu yatupasa kukaza macho yetu juu ya Mwokozi wetu anayetuhudumia na kulipa jambo hilo umuhimu wa kwanza. Licha ya makosa yake, kanisa ni mali yake, basi, ninyi kazeni macho yenu juu ya Kristo.

"Nanyi waume, wapendeni wake zenu kama Kristo alivyolipenda kanisa, akajitoa mwenyewe sadaka kwa ajili yake. Alifanya hivyo ili kwa neno lake, aliweke wakfu kwa Mungu, baada yakulifanya safi kwa kulioshatika maji, kusudi ajipatie kanisa lililo takattifu na safi kabisa, kanisa lisilo na doa, kasoro au cho chote cha namna hiyo" (Waefeso 5:25 - 27).

Kanisa ni la maana sana kwa Yesu hata akajitoa nafsi yake kwa ajili yake alipokufa kwa ajili ya kila mmoja wetu na kanisa kwa jumla. Kwa hiyo, ushirika wa kanisa kwako wewe ungeswaswa kuwa wa maana. Je ! hivi wewe ni mshiriki wa mwili wa Kristo?

7. Kulipata Kanisa Hilo

Je! Ni imani ngapi za kweli alizonazo Yesu uliwenguni humu?

"Kuna mwili (kanisa) mmoja , na roho mmoja.... Bwana mmoja, Imani Moja, Ubatizo mmoja" - (Waefeso 4:4,5).

Kwa vile Kristo anayo "iman moja" tu, je! Twawezaje sisi kujua ni imani ipi hiyo? Yesu anatupatia sisi ufunguo wake huu:

"Mtu anayependa kufanya yale anayotaka Mungu, atajua kama mafundisho yangu yametoka kwa Mungu, au mimi najisemea tu mwenyewe" - Yohana 7:17. (Angalia pia Yohana 8:31,32).

Tunapojitoa wenyewe kufanya mapenzi ya Mungu, atatusaidia sisi kujua endapo mafunzo hayo yanatoka kwa Mungu, au ni mapokeo tu ya



GUNDUA



wanadamu. Tunapolitafuta hilo kanisa jambo kuu ni kuchunguza jinsi linavyoliheshimu na kulitii Neno la Mungu. Ushirika wa kweli umejengwa juu ya maandiko, sio juu ya kiongozi mmoja mwenye uwezo wa ajabu au taasisi moja kuu.

Endelea kufanya ugunduzi wako mwangi katika miongozo hii, tembea katika nuru anayokufunulia Mungu kutoka katika Biblia, naye atayafunua mapenzi yake kwako. Mkristo anayekua ni mtu anayeufungua moyo wake na akili yake ili kuipokea ile kweli kama Mungu anavyoifunua kutoka katika Neno lake.

JE! WENGI WANAWEZA KUKOSEA?

Katika Mwongozo 16 tuligundua kwamba kulionja pumziko la Sabato ni tiba muhimu kwa maisha ya siku hizi yaliyojaa msongo mwingi. Kwa kuwa Mungu anaelewa kila haja tuliyonayo , aliiweka kila siku ya saba kwa ajili ya pumziko letu la kimwili na burudiko letu la kiroho. Baada ya kiumba dunia yetu kwa siku sita, yeche "akapumzika" katika siku ile ya saba, "akaibariki" na "kuifanya takatifu" (mwanzo 2:1-3).

Mungu alipowapa watu wake Amri kumi, yaani, wana wa Israeli, aliiweka amri ya kuitunza Sabato ya siku ya saba katikati ya sheria yake (Amri kumi) (Kutoka 20:8-11). Kulingana na amri hiyo, Sabato ni ukumbusho wa uweza wa Mungu wa Uumbaji, ni siku ya kutulia na kutafakari juu ya uzuri na maajabu ya kazi zake alizozumba, ni siku ya kustarehe na kumkaribisha sana Muumbaji wetu, siku ya kuchunguza kwa kina zaidi uhusiano wetu na yeche.



Katika kipindi kile cha maisha ya kibinadamu ya Yesu aliyoshi hapa duniani, yeche pia aliitunza Sabato (Luka 4:16) na kuiidhinisha kama siku inayowaletea Wakristo manufaa (Marko 2:27,28.) Mafungu kadhaa katika kitabu cha Matendo yanaonyesha wazi kwamba wanafunzi wake Kristo waliabudu katika siku ya Sabato baada ya ufufuo wake (Matendo 13:14, 16:13, 17:2, 18: 1-4, 11).

1. Suala Lenye Utata

Hiyo inatufikisha sisi kwenye somo ambalo wengi huliona kuwa lina utata kwao. Kwa kipindi fulani ulimwengu wa Kikristo umekuwa ukizitunza siku mbili tofauti. Kwa upande mmoja, Wakristo wengi sana kwa unyofu wa moyo wanaitunza Jumapili, siku ya kwanza ya juma, ambayo wao wanaamini kwamba ndio ukumbusho wa ufufuo wake Kristo. Kwa upande ule mwengine, kundi kubwa la Wakristo, nao vilevile wakiwa ni wanyofu wa moyo, wanaamini kwamba Biblia inaipa heshima siku ya saba peke yake kama ndio Sabato na ya kwamba hakuna mahali popote inapothitisha utakatifu wa Jumapili.

Je! inaleta tofauti yeoyote juu ya siku gani tunayoitunza kama Sabato? Sisi kama watu walio wanyoofu wa moyo na wenyewe ari tunaotaka kujua kweli, ni lazima tujilize wenyewe swali hili. "Je! Ni jambo gani ambalo ni maana kwa Yesu? Hivi Yesu anataka mimi nifanye nini?

Katika kufikiria uamuji wa jambo hilo, mambo kadhaa ya maana hayana budi kuwekwa wazi, je ni nani aliyebadili Sabato kutoka Jumamosi siku ya saba ya juma, kwenda Jumapili siku ya kwanzia ya juma? Je! Hivi Biblia inatoa idhini kwa badiliko kama hilo? Kama jibu ni ndio, Je, Mungu, Kristo, au labda wale mitume ndio waliofanya badiliko hilo?

Tutaendelea mbele kwa kuangalia uwezekano wo wote uliopo

2. Je! Ni Mungu Aliyebadili Siku?

Je! Kuna tamko lolote toka kwa Mungu ambalo linaibadilisha Sabato kutoka siku ya saba kwenda siku ya kwanza ya juma?

Wakristo wengi sana wanazikubali Amri kumi kama mwongozo halali ambao kwa huo sisi tunpaswa kuishi. Huu ni ujumbe wa pekee ambao Mungu mwenyewe amepata kuandika kwa ajili ya wanadamu. Ni za muhimu sana, alizandika juu ya mbao za mawe kwa kidole chake mwenyewe (Kutoka 31:18).



GUNDUA

Katika ile amri ya nne Mungu anatuagiza sisi anasema:

"Ikumbeke siku ya Sabato uitakase. Siku sita fanya kazi na kutenda mambo yako yote, lakini **SIKU YA SABA NI SABATO YA BWANA, MUNGU WAKO**. Siku hiyo usifanye kazi yoyote, ... maana kwa siku siku sita **BWANA** alifanya mbingu, na nchi, na bahari na vyote vilivyomo, lakini **AKAPUMZKA** siku ya saba. Kwa hiyo **BWANA AKAIBARIKI** siku ya Sabato **AKAITAKASA**" - Kutoka 20:8-11.

Mungu alipowapa watu wake zile Amri kumi, pia alieleza wazi kwamba maagizo yale yaliyotoka kinywani mwake asiwepo mwanadamu yeyote wa kuyafanya marekebisho yeyote ili kuyafanya yawe bora zaidi au kuondoa maneno yake yeyote anapofanya uhariri wake.

"MSIONGEZE neno lolote katika yale niwaamuruyo, wala MSIPUNGUZE neno lolote, bali zishikeni amri (kumi) za BWANA, Mungu wenu ninazowapa ninyi" - (Kumbukumbu la Torati 4:2).


Mungu mwenyewe anatoa ahadi kwamba hawesi kuzibadili amri zake [kumi]:

"MIMI SITALIVUNJA agano langu, wala SITABADILI NENO LILILOTOKA MIDOMONI (MWANGU) - (Zaburi 89:34).

Biblia inaeleza waziwazi kwamba Mungu hakubadili Sabato kutoka siku ya saba kwenda ile ya kwanza ya juma.

3. Je! Yesu Aliibadili Sabato?

Kulingana na maneno ya Yesu, Amri kumi haziwezi kubadilika kamwe:



"Msidhani ya kuwa nimekuja kutangua sheria na mafundisho ya manabii. Sikuja kutangua bali kukamilisha. Kweli nawaambieni, mpaka hapo mbingu na dunia zitakapopita, hakuna hata nukta moja au sehemu ndogo kabisa ya sheria itakayoondoka mpaka yote yametimia" - (Mathayo 5:17-18).

Katika Mwongozo 16 tuligunda kwamba desturi ya Yesu ilikuwa ni kwenda kuabudu katika sinagogi siku ya Sabato (Luka 4:16). Pia tuligunda kwamba Yesu alitaka wanafunzi wake waendelee kuionja raha ya kuitunza ile Sabato ya kweli (Mathayo 24:20)

Ni dhahiri, basi, kwamba kutokana na mafundisho ya Yesu na kielelezo chake sisi bado tunayo haja ya hilo pumziko la Sabato, yaani, kustarehe na kuutumia wakati wetu pamoja na Mungu.

4. Je! Wale Mitume Waliibadili Sabato?

Yakobo, kiongozi wa kwanza wa kanisa lile la mwanzo, aliandika maneno haya kuhusu zile Amri kumi:

"Anayevunja amri mojawapo ya sheria, atakuwa na hatia ya kuivunja

sheria yote. Maana yule yule aliyesema: "USIZINI, "alisema pia"

"USIUE." Kwa hiyo, hata ikiwa hukuzini, lakini umeua, wewe umeivunja sheria - (Yakobo 2:10, 11).

Luka, tabibu na mwinjilisti katika kanisa lile la kwanza, anatoa taarifa hii.

"Siku ya Sabato tukatoka nje ya mji, tukaenda kando ya mto, ambapo tulidhani kuwa mahali pa kusali. Tuliketi, tukiongea na wanawake waliokusanyika mahali hapo" - (Matendo 16:13).



GUNDUA

Kitabu cha Matendo cha Agano Jipya kinataja mara 84 ilipotunzwa. Sabato hiyo na wafiasi wa Kristo, zote hizo zilikuwa zikitunzwa zaidi ya miaka 14 baada ya ufuluo wa Yesu: Sabato 2 pale Antioquia (Matendo 13:14,42,44); 1 pale Filipi (Matendo 16:13), 3 pale Thesalonike (Matendo 17:2,3), Sabato 78 pale Korintho (Matendo 18:4,11).

Yohana, wa mwisho kufa miongoni mwa wale mitume kumi na wawili, aliiunza Sabato. Aliandika hivi:
"Siku ya Bwana nilikuwa katika Roho" - (Ufunuo 1:10).

Kulingana na maneno ya Yesu, siku ya Bwana ni Sabato:

"Mwana wa Adamu ndiye Bwana wa Sabato" - (Mathayo 12:8).

Uchunguzi wa ushahidi wa maandiko unaoonyesha wazi kwamba wale mitume hawakufanya jaribio lolote la kuibadili siku ya Mungu ya mapumziko kutoka siku ya saba kwenda ile siku ya kwanza ya juma. Agano jipya, linaitaja siku hiyo ya kwanza ya juma mara nane tu. Katika mifano hiyo yote hakuna ambapo siku ya kwanza ya juma inatajwa kuwa ni takatifu, wala hata kudokezwa kuwa tunapaswa kuitenga kama siku ya ibada. Uchunguzi uliofanywa kwa makini sana wa hayo mafungu manane yanayoitaja siku ya kwanza ya juma huonyesha matukio haya yaliyotokea Jumapili:

- (1) Wanawake walikwenda kaburini siku ile ya kwanza ya juma (Mathayo 28:1).
- (2) "Hata Sabato ilipokwisha" wanawake wakaanza tena kufanya shughuli zao za kidunia katika siku ile ya kwanza ya juma (Marko 16:1,2).
- (3) Yesu alimtokea kwanza Mariamu Magdalena mapema siku ile kwanza ya juma (Marko 16:9).
- (4) Wafiasi wa Yesu walianza tena kufanya shughuli zao katika ile siku ya kwanza juma (Luka 24:1).
- (5) Mariamu alikwenda kwenye kaburi lile la Yesu na kulikuta kaburi liko tupu katika ile siku ya kwanza (Yohana 20:1).
- (6) Wanafunzi wale walikusanyika mahali pamoja "kwa hofu ya Wayahudi" (si kwa ajili ya kuendesha ibada) Katika ile siku ya kwanza ya juma (Yohana 20:19).
- (7) Paulo aliwaomba washiriki wa kanisa kufanya mahesabu ya fedha zao walizopata katika ile siku ya kwanza ya juma, na "kuweka kando kiasi fulani cha fedha" kwa ajili ya maskini kule Yerusalem (I Wakorintho 16:1,2). Kifungu hicho hakitaji mkutano wowote wa dini ambaa ulifanyika.
- (8) Katika Matendo 20:7 Luka anaongea habari za hotuba (mahubiri) ya Paulo aliyoitoa katika ile siku ya kwanza ya juma wakati wa mkutano ule wa kuagana ambaa haukutazamiwa kufanyika. Kusema kweli, Paulo alihubiri kila siku, na mitume wale walimega mkate kila siku (Matendo 2:46).

Hakuna hata moja kati ya mafungu hayo linalodokeza ya kwamba wale mitume waliazimu kuacha kuitunza Sabato ya siku ya saba. Mitume wale hawakulitaja badiliko lolote la Sabato kutoka siku ya saba kwenda ile ya

kwanza ya juma. Hakuna ushahidi wowote ulio wazi katika Agano Jipya unaoonyesha badiliko hilo la Sabato kutoka Jumamosi, siku ya saba ya juma, kwenda Jumapili, siku ya kwanza ya juma. Badiliko hilo lilikuja baada ya siku zile za Yesu na mitume wake, kwa hiyo, yatupasa sisi kuigeukia historia ili kuona ni lini na kwa jinsi gani badiliko hilo lilitokea.

5. Jumapili Ilitoka Wapi?

Mitume wale wanatuonya sisi waziwazi kwamba Wakristo fulani wangetangatanga na kwenda mbali na mafundisho ya Ukristo ule wa Agano Jipya: "Iweni macho " (Matendo 20:29-31). Na ndivyo ilivyotokea hasa. Wanahistoria wanaoaminika wanaandika waziwazi kuonyesha jinsi Wakristo walivyoanza kupotea na kuuacha usafi ambaa kanisa lile la mitume lilikuwa nao. Mapokeo na mafundisho ambayo hayakuungwa mkono kamwe na Paulo, Petro na waasisi wale wengine wa kanisa lile la Kristo, yakaanza kuingia taratibu ndani ya kanisa.



Badiliko lilofanyika kutoka katika utunzaji wa Sabato kwenda kwenye utunzaji wa Jumapili lilitokea baada ya kukamilika kuandikwa kwa Maandiko ya Agano jipya na baada ya kufa mitume wale wote. Historia inaandika katika kumbukumbu zake ya kwamba hatimaye Wakristo wakahama kutoka katika kufanya ibada yao na kupumzika siku ya saba kwenda katika siku ile ya kwanza ya juma. Lakini, kwa kweli, waumini hawakuacha kuitunza Sabato ile ya siku ya saba mwishoni mwa juma fulani lililowekwa na ghafila kuanza kuitunza Jumapili kama siku ya Bwana. Mfano mmoja uliothibitishwa ambao ultioka mapema sana wa utunzaji wa Jumapili na Wakristo ultioka katika nchi ya Italia, katikati ya karne ile ya pili baada ya pale Wakristo wengi walizitunza siku zote mbili, ambapo wengine bado waliendelea kuitunza Sabato peke yake.



Tarehe 7 Machi, 321 B.K Konstantino Mkuu alitoa amri ya kwanza ya Kiserikali ya Jumapili, akawalazimisha wote, isipokuwa wakulima, katika Dola ya Kiroma kupumzika Jumapili. Hivyo pamoja na sheria nyingine zipatazo tano za kiserikali zilizoamriwa na Konstantino kuihusu Jumapili, ziliweka mfano wa sheria zote za Jumapili kuanzia wakati ule mpaka leo. Katika ile karne ya nne Baraza la Laodikia liliwakataza Wakristo wasiache kufanya kazi siku ya Sabato, huku likiwashurutisha kuiheshimu Jumapili kwa kuacha kufanya kazi endapo uwezekano ulikuwapo wa kufanya hivyo.

Historia inaonyesha kwamba ibada ya Jumapili na utunzaji wake ni desturi iliyowekwa na wanadamu. Biblia haitoi kibali chochote ili kuifutilia mbali Sabato ya siku saba ya amri ile ya nne. Nabii Danieli alitabiri kwamba katika kipindi kile cha Kikristo mamlaka fulani yenye hila ingejaribu kuibadili sheria ya Mungu (Amri Kumi) (Danieli 7:25)

6. Ni Nani, Aliyefanya Badiliko?

Jel! Ni nani aliyeihamisha rasmi Sabato kutoka siku ya saba kwenda siku ya kwanza ya juma? Kanisa Katoliki linadai kwamba limefanya badiliko hilo. Katika jitihada ya kutaka kuiokoa Dola ya Roma iliyokuwa inavunjika, viongozi wa kanisa waliokuwa na kusudi zuri wakafanya maridhiano na kujaribu kubadili siku ya ibada kutoka Jumamosi kwenda Jumapili.

Katekismo ya kanisa Katoliki la Roma inasomeka hivi:

"Swali: Ipi ndiyo siku ya Sabato?

"Jibu: Jumamosi ndiyo siku ya Sabato.

"Swali: Kwa nini sisi tunaitunza Jumapili badala ya Jumamosi?

"Jibu: Tunaitunza Jumapili badala ya Jumamosi kwa sababu kanisa Katoliki Lilihamisha ibada toka Jumamosi kwenda Jumapili".

- Peter Geirmann, The Convert's Catechism of Catholic Doctrine (toleo la 1957). Uk. 50.



Kwa majivuno kanisa Katoliki linatangaza kwamba viongozi wa kanisa amba ni wanadamu tu ndio waliofanya badiliko hilo.

"Siku ile takatifu, yaani, Sabato, ilibadilishwa kutoka Jumamosi kwenda Jumapili... si kutohana na maagizo yo yote yaliyoonekana katika Maandiko bali kutohana na hisia ya kanisa kwamba linao uwezo wake lenyewe... watu wale wanaofikiri kwamba Maandiko ndiyo yangetuwa mamlaka peke yake, kwa mantiki hiyo, ingewapasa kuwa Waadventista Wasabato , nao wangeitakasa Jumamosi." - Cardinal Maida, Askofu Mkuu wa Detroit, Saint Catherine Catholic Church Sentine, Algonac, Michigan, Mei 21, 1995.

7. Je! Makanisa Ya Kiprotestanti Yanasemaje?

Hati rasmi zinazotoa muhtasari wa itikadi za madhehebu kadhaa ya Kiprotestanti zinakiri kwamba Biblia haitoi kibali cho chote cha kuitunza Jumapili.

Martin Luther, mwasisi wa kanisa la Kilutheri, aliandika katika ungamo la Augusiburgi (Augusburg Confession), sharti la imani la 28, aya ya 9, maneno haya: "Wao [Wakatoliki wa Roma] wanadai kwamba Sabato ilibadilishwa na kuwa Jumapili, siku ya Bwana, kinyume na ile sheria ya Amri kumi,.. wala hakuna mfano wanaojivunia sana kama huo wa kuibadili siku ya Sabato. Ni mkuu, wasema wao, uwezo na mamlaka ya Kanisa, kwa kuwa liliiondoa mojawapo ya zile Amri kumi."

Wanatheolojia wa Kimethodisti Amosi Binney na Danieli Steele walitoa maoni yao haya:
"Ni kweli, hakuna amani dhahiri ya ubatizo wa watoto wachanga....wala hakuna yo yote ya kuitakasa siku ya kwanza ya juma." Theological Compend (New York: Methodist Book Concern, 1902), Kurasa 180,181.

Dk. N. Summerbell, mwanahistoria wa wanafunzi wa Kristo (Disciples of Christ) au Kanisa la Kikristo (Christian Church), aliandika, alisema:
"Kanisa la Roma lilikuwa limeasi kabisa.....Liliigeuza Amri ya Nne kwa kuiondoa Sabato ile ya Neno la Mungu, na kuiweka Jumapili kama siku takatifu" A True History of the Christian and the Christian Church, kurasa za 417,418.

8. Suala Lenyewe hasa ni lipi?

Jambo hilo linatuleta ana kwa ana kupambana na maswali haya: kwa nini Wakristo wengi sana huitunza Jumapili bila kuwa na idhini ya Biblia? La maana zaidi ni hili, Je! Niitunze siku gani? Je! Niwfuate wale wasemao, "Sidhani kwamba inaleta tofauti yoyote kuhusu siku gani ninayoitunza mradi tu mimi naitunza moja katika zile saba"? Au, Je! Nihihesabu kuwa ni ya maana ile siku ambayo Yesu, Muumbaji wetu, alianzisha alipouimba Dunia yetu hii, tena ni siku ile alioiteua Mungu na kuiweka katika zile Amri kumi: yaani, kwamba "siku ya saba ni Sabato"?

Hapa tunashughulika zaidi ya utunzaji wa nje tu, bali juu ya siku ipi yaonekana kibiblia kuwa ni sahihi. Hoja muhimu inayohusu hapa ni ile ya utii kwa Yesu. Muumbaji wetu alitienga Sabato kama siku "Takatifu," kama ndio wakati uliowekwa kwa ajili yetu na familia zetu kumkaribia yeye zaidi ili tupate kupewa nguvu na burudiko. Nitamtii nani? Je! Nimitii Kristo, mwana wa Mungu, au mapokeo ya wanadamu katika suala hili la siku ninayoitakasa? Uchaguzi uko wazi: mafundisho ya wanadamu au amri za Mungu. Neno la wanadamu au Neno la Mungu. Siku mbadala iliyowekwa na wanadamu au amri ya Mungu.



Nabii Danieli anatoa onyo kwa wale ambao wange "jaribu kubadili majira yaliyowekwa pamoja na sheria" (Danieli 7:25,NIV) ["azimu kubadili majira na sheria" (Daniel 7:25, NKJV)]. Mungu anawaita watu wake warudi na kumtii yeye. Anawaita ili wapate kuitunza Sabato kama ishara ya Utii na upendo wao kwake yeye.

Yesu alisema, "Mkinipenda, mtakishika kile niwaamurucho" (Yohana 14:15). Tena yeye anaahidi kuwapa furaha kamili wale wampendao hata kuweza kuzitii amri zake (Yohana 15:9-11). Tunaye Mwokozi wa ajabu. Anayo shauku nydingi kwa ajili yetu ili sisi tupate kuuonja upendo wake kwa utimilifu wake wote. Moyo ule ulio na utii wa hiari unafungua mlango wazi ili kuupokea upendo huo.

Katika ile bustani ya Gethsemane Kristo alijinyenyekeza kikamilifu chini ya mapenzi ya Baba yake - licha ya kukabiliwa na msalaba na dhambi za ulimwengu mzima zilizokuwa zikiyaangamiza maisha yake. Alipomlilia Mungu, na kusema, "Uniondolee kikombe hiki," alikuwa amejinyenyekeza katika maombi yake, kisha akaongeza kusema hivi "Walakini, si kama nitakavyo mimi, bali utakavyo wewe" (Marko 14:36).

GUNDUA

DISCOVER
online

Kristo anatamani sana kwamba sisi tupate kuuonja utimilifu ule uletwao na maisha yaliyosalimishwa kweli kweli. Pia anataka sisi tuionje furaha ya pumziko la Sabato. Anataka sisi tumtumainie yeye kiasi cha kutosha kumtii katika mambo yote ya maisha yetu. Endapo wewe utaitika anapokuita na kuzitii amri zake zote [kumi], basi, wewe utaweza kuionja ahadi ya Yesu isemayo kwamba furaha yake itakuwa "ndani yenu" na "furaha yenu" ita "timizw[a]" (Yohana 15:11).

JE! MUNGU ANA HAKI?

Mvulana mmoja ndani kabisa ya mji anauawa kwa risasi zilizofyatuliwa ovyo na majambazi wakati anafanya kazi yake ya shulenii akiwa ameketi nyumbani kwao katika meza ya familia yake.

Mama mmoja kijana katika viunga vya mji anagundua kwamba mtoto wake amepatikana na Ukimwi kutokana na damu alioongezewa mwilini mwake.

Misiba inazidi kuendelea tena na tena katika ulimwengu wetu huu. Nasi tunatamani sana kujua jibu kwa mambo hayo yote. Hivi Mungu huyo yuko wapi katika ulimwengu wetu huu uliojaa mateso na vifo visivyo na maana? Mtunga Zaburi anatuhakikishia sasa kwamba "dunia hii imejaa upendo wake usio na mwisho" (Zaburi 33:5).

Lakini, basi, kama hilo ni jambo la kweli, mbona hayakomeshi mateso hayo pamoja na misiba? Sura ya 20 ya Ufunuo inatuonyesha sisi ni kwa ajili gani na lini Mungu atakapo komesha dhambi na mateso.



1. Miaka Ile Elfu Moja Yafunuliwa

Ufunuo 20 huelekeza mawazo yetu yote kwenye kipindi kile cha miaka 1,000 ambacho kinakuja baada ya Kristo kuja mara ya pili. Matukio yale yanayokizunguka kipindi hicho cha mika 1,000 ni lile tendo la mwisho katika pambano ambalo limekuwa likiendelea kati ya Kristo na Shetani tangu dhambi ilipoingia katika ulimwengu huu.

Mfululizo wa matukio hayo ya kuvutia macho ulianza kule mbinguni wakati Lusifa alipomuonea vivu Kristo, akaanzisha vita kule dhidi ya malaika wale ambao hawakuanguka [dhambini] alifukuzwa kule, na kukimbilia katika dunia yetu. Matukio hayo yaliendelea hapa duniani katika ile Bustani ya Edeni, halafu kuititia katika Karne zote na kushuka hadi yalipofikia kilele chake cha kwanza wakati ule Ibilisi alipowachochea wanadamu kumsulibisha Kristo. (Ukipenda waweza kukipitia tena kisa hicho cha kusikitisha katika Mwongozo 3.) Matukio hayo yatafikia kilele chake cha mwisho kitakapokwisha kipindi kile cha miaka 1,000 wakati dunia yetu hii yenye dhambi itakapotakaswa na kuwekwa chini ya utawala wa Kristo. Ufunuo 20 unatuonyesha sisi kwamba kipindi hicho cha miaka 1,000 kimetenganishwa na ufunuo wa aina mbili.



Je! Ni akina nani hao ambao Mungu anawafufua kutoka kwa wafu katika ufufuo wa kwanza unaotokea mwanzo wa ile miaka 1,000?

"Wameneemeka sana, heri yao wote wanaoshiriki ufufuo huu wa kwanza. Kifo cha pili hakitakuwa na nguvu juu yao; watakuwa makuhani wa Mungu na wa Kristo, na watatawala pamoja naye kwa miaka elfu moja"- (Ufunuo 20:6).

Wale walio "heri na watakatifu," yaani, wale waliompokea Kristo kama Mwokozi wao wanatoka katika ule ufufuo wa kwanza wa wenye haki na hawana budi kutawala pamoja na Kristo katika kipindi cha miaka 1,000 basi, ni lazima wafufuliwe mwanzo wa ile miaka 1,000.

Je hao ni akina nani wanaofufuliwa katika ufufuo wa pili utakaotokea mwisho wa kipindi cha miaka elfu moja?

GUNDUA

Hao wafu Waliosalia hawakuwa hai mpaka ilipokwisha ile miaka elfu moja - (Ufunuo20:5).

Maneno haya "hao wafu waliosalia" yanaweza tu kuwataja waovu wale waliokufa kwa sababu wale wenye haki amba ni heri na watakatifu wanaofufuliwa mwanzo wa ile miaka 1000.

Kwa hiyo, hicho kipindi cha miaka 1,000 kimetenganishwa na ufufuo wa aina mbali : yaani, ufufuo wa wenye haki unatokea mwanzo wake, na ufufuo wa waovu unaotokea mwisho wake.

2. Kufufuliwa Wakati Wa Marejeo Ya Kristo

Ufufuo wa kwanza, yaani, ule wa wenye haki unatokea wakati wa kuja mara ya pili kwa Kristo.



"Maana patatolewa amri, sauti ya tarumbeta ya Mungu, naye Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni. Ndipo wale waliokufa wakiwa wanamwamini Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai wakati huo tutakusanywa pamoja nao katika mawingu kumlaki Bwana hewani. Na hivyo tutakuwa daima pamoja na Bwana" (1Wathesalonike 4:16,17)

Yesu anapokuja katika dunia hii anawafufua wale "waliokufa katika Kristo" na kuwachukua kwenda nao mbinguni pamoja na wenye haki wale walio hai. Kwa kuwa wale waovu bado wanaendelea kung'a ng'ania dhambi, hawawezi kuendelea kuwa hai mbele zake Mungu, nao wanaangamizwa wakati ule wa kuja kwake Kristo (Luka 17:26-30). (Unaweza kupenda kupitia tena Mwongozo 8 uhusu matokeo yale yanayoambatana na kurudi kwa Yesu).

3. Shetani Afungwa Mnyororo Hapa Duniani Kwa Miaka Elfu Moja

Miaka hiyo elfu moja inapoanza, wenye haki wote watakuwa wamekwisha kwenda zao mbinguni, na waovu watakuwa wamekufa wote. Je! hivi kutatokea nini juu ya dunia hii katika hiki kipindi cha miaka 1,000?

"Kisha, nikamwona malaika mmoja anashuka kutoka mbinguni akiwa na ufunguo wa kuzimu na mnyororo mkubwa mkononi mwake. Akalikamata lile joka - nyoka wa kale, yaani Ibilisi au Shetani - akalifunga kwa muda wa miaka elfu moja. Malaika akalitupa kuzimu, akaufunga mlango wa kuingilia huko na kuutia mhuri ili lisiweze tena kuyapotosha mataifa mpaka hapo miaka elfu moja itakapotimia. Lakini baada ya miaka hiyo ni lazima lifunguliwe tena, lakini kwa muda mfupi tu " Ufunuo 20:1-3.

Wakati wa kuja kwake Yesu Shetani anafungwa, naye atabaki na mnyororo yake katika kipindi kile cha miaka 1,000. Je! Ni wapi atakafungwa Shetani? Atafungwa "kuzimu" (Abyss), hili ni neno la Kigiriki limaanishalo "kilindi kirefu" au "shimo la kuzimu" katika Mwanzo 1:2 tafsiri ya Kigiriki ya Agano la Kale inatumia neno hili "vilindi" (Abyss) kuiielezea dunia hii ilipokuwa katika hali yake isiyotengenezwa vizuri kabla ya siku zile za uumbaji kuanza. Kwa hiyo dunia yetu hii ndiyo iitwayo kuzimu (Abyss), ni mahali ambapo Mungu anamfunga Shetani kuwa amefungwa "na mnyororo halisi? La, ni mfano, ni mnyororo wa mazingira. Shetani angependa sana kuendelea kuwadanganya wanadamu katika kipindi kile cha miaka 1,000. Lakini, basi, ye ye hawezu kuwapata wenye haki wowote wa kuwajaribu, kwa sababu wote wako kule mbinguni. Wala hawezu kuwapata waovu wa kuwaongoza, kwa kuwa wote wamekufa, wamelala usingizi wa mauti katika mavumbi ya ardhi. Akiwa hana uwezo wowote wa kuwadanganya au kuwajaribu, anatangatanga katika dunia hii tupu akilazimishwa kutafakari huzuni kubwa na misiba aliyoisababisha.



4. Wenye Haki Wanawahukumu Waovu

GUNDUA

Kipindi kile cha miaka elfu moja ni kipindi cha hukumu pia. Lakini kumbuka kwamba hukumu hiyo ina hatua kuu nne:

- (1) Hukumu ya wenze haki kabla ya kuja kwa Kristo mara ya pili.
- (2) Thawabu ya wenze haki wakati ule wa kuja mara ya pili kwa Kristo.
- (3) Hukumu ya waovu katika kipindi kile cha miaka elfu moja.
- (4) Thawabu ya Shetani na waovu mwishoni mwa kipindi kile. (ukipenda waweza kuupitia tena Mwongozo 13 amba unashughulika na hatua ya 1 na ya 2 ya hukumu hiyo, yaani, upelelezi na thawabu ya wenze haki.)

Tumekwisha kuona ya kwamba wenze haki waliokufa amba unashughulika, pamoja na wenze haki wale walio hai wananyakuliwa kwenda mbinguni wakati ule wa kuja kwake Kriso mara ya pili. Wao wako nyumbani kwao kule mbinguni katika kipindi kile cha miaka 1,000. Je, watakuwa wakifanya nini huko?

"Je! hamjui kwamba watu wa Mungu watauhukumu ulimwengu? Ikiwa basi, ulimwengu utahukumiwa nanyi kwa nini hamstahili kuhukumu hata katika mambo madogo? hamjui kwamba, licha ya kuhukumu mambo ya kawaida ya kila siku, tutawahukumu hata malaika?" - (1 Wakorintho 6:2-3).

"Kisha nikaona viti vyta enzi na watu walioketi juu yake; watu hao walipewa mamlaka ya hukumu. Niliona pia roho za wale waliokuwa wamenyongwa kwa sababu ya kumshuhudia Yesu na kwa sababu ya neno la Mungu. hawa hawakumwabudu yule mnyama na sanamu yake, wala hawakupigwa alama yake juu ya paji ya nyuso zao, au juu ya mikono yao. Walipata tena uhai, wakawatawala pamoja na Kristo kwa miaka elfu moja "- (Ufunuo 20:4).



Katika kipindi kile cha miaka 1,000, wenze haki watazichunguza kesi za wanadamu wale waovu pamoja na malaika wale walioanguka, akiwamo na kiongozi wao Shetani. Ni jambo lifaalo jinsi gani kwa wafia dini, washindi, na wale walio na makovu ya vita walioifuata injili kuweza kuichunguza na kuielewa ile hukumu ya Mungu aliyotoa dhidi ya waovu.

Kwa neema yake nyingi Mungu amewapa wanadamu waliokombolewa nafasi ya kutathmini alivyowashughulikia waovu. Tunaweza kuwa na maswali mengi kama haya: "mbona shangazi yangu hayupo hapa? Alionekana kana kwamba alikuwa mtu mzuri" Tutakapozipitia kumbukumbu zile na kuwahukumu wale wafu "

kulingana na matendo yao kama yalivyoandikwa katika vitabu vile" (fungu la 12), tutajionea wenyeve ya kwamba katika kushughulika kwake kote kule na wanadamu, Mungu amekuwa wa haki wala hana upendeleo kwa kila mtu. Tutaona jinsi Roho Mtakatifu alivyowapa wanadamu nafasi baada ya nafasi ili wapate kujitoe kabisa kwa Mungu, na haki ya kila hukumu itaonekana wazi.

5. Shetani Afunguliwa Mwisho Wa Ile Miaka Elfu Moja

Mwisho wa ile miaka 1,000 Biblia inatangaza hivi:

"Nikaona mji Mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka kwa Mungu mbinguni. Ulikuwa umetayarishwa vizuri kama bibi harusi aliyepambwa tayari kukutana na mumewe" - (Ufunuo 21:2).

Mji huu wa ajabu umekuwa makao yetu kwa miaka elfu moja. Sasa Mji huu Mtakatifu - ndani yake ukiwa na Kristo na watu wote aliowakomboa - unashuka kutoka mbinguni kuja katika dunia mpya.

Je! Shetani anafanya nini mwisho wa mika hiyo 1,000?

GUNDUA

"Wakati miaka elfu moja itakapotimia, Shetani atafunguliwa kutoka gerezani mwake. Basi, atatoka nje, ataanza kuyapotosha mataifa yote yaliotawanyika kila mahali duniani, yaani Gogu na magogu. Shetani atawakusanya pamoja kwa ajili ya vita; nao watakuwa wengi kama mchanga wa pwani. Walipita katika nchi yote, wakaizunguka kambi ya watakatifu na mji wa Mungu aupendao. Lakini moto ulishuka kutoka mbinguni, ukawaangamiza" - (Ufunuo 20: 7-9).

Waovu wanafufuliwa katika ufufuo wa pili mwisho wa ile miaka 1,000 (fungu la 5). Wenye haki wanaposhuka duniani wakiwa ndani ya huo mji Mtakatifu, na waovu wanapofufuliwa, Shetani ata "funguliw[a] kwa muda mchache" (fungu la 3). Yeye anao tena wale waovu ili kuwaongoza na shabaha yake ni wale wenye haki. Bila kupoteza hata dakika moja, anaanza mara moja, kuwapanga waovu katika jeshi kubwa sana. Shetani anatoa amri ya kusonga mbele dhidi ya mji huo. Waovu wanapoipanga mahali pao kuuzunguka Yerusalem Mpya (fungu la 9), mara moja wanaingwa na hofu kuu ya kupotea - yaani kupotea milele.



6. Mandhari Ya Hukumu Ya Mwisheso

Hapo, kwa mara ya kwanza, wanadamu wote wanakutana pamoja ana kwa ana. Yesu anawaongoza wana wa Mungu waliokombolewa ambao wamo ndani ya mji huo. Shetani anaongoza akiwa mbele ya hilo kundi kubwa sana lililosongamana la waovu ambao wako nje ya kuta hizo. Katika wakati huu wa hatari sana, Mungu anatekeleza hatua ya mwisho ya hukumu na waovu wanapokea siku yao katika mahakama hiyo.

"Kisha nikaona kiti cha enzi, kikubwa, cheupe, na yule aketiye juu yake. Dunia na mbingu vikatoweka mbele ya macho yake, na havikuonekana tena. Kisha nikawaona watu wakubwa na wadogo, wamesimama mbele ya kiti cha enzi, na vitabu vikafunguliwa. Halafu kitabu kingine, yaani kitabu cha uhai, kikafunguluwa pia. Wafu wakahukumiwa kadri ya matendo yao, kama ilivyoandikwa ndani ya vitabu hivyo" - (Ufunuo 20:11,12).

Waovu wanaposimama mbele ya hicho kiti cha enzi cha hukumu, maisha yao yote yanaonyeshwa mbele yao. Kutoka katika zile kumbukumbu zilizoko kule mbinguni, Yesu, Jaji mwenye haki, anakifunua rasmi kisa chake kamili kuhusu jinsi aliyowashughulikia wanaume, wanawake, na malaika walioanguka.



Malimwengu yote yanaangalia kwa hamu kubwa. Akisimama mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, Yesu anamwonyesha kila mmoja picha kamili ya kazi yake ya ukombozi. Anawaonyesha kwamba ye ye aliukua kuwatafuta na kuwaokoa wale waliopotea. Aliingia katika dunia yetu akiwa na mwili wa kibinadamu, aliishi maisha yasiyo na dhambi katikati ya mapambano na majoribu, alitoa kafara yake ya mwisho pale msalabani, na kuhudumu kama Kuhani wetu kule mbinguni. Mwisheso, Yesu anapopiga hatua kuja mbele kwa huzuni na kutamka hukumu dhidi ya wale walioendelea kwa ukaidi kuikataa neema yake, kila kiumbe katika malimwengu hayo atakiri kwamba tendo hilo la mwisheso la hukumu ya Mungu ni la haki, tena ni la lazima.

"Sisi sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu. Imeandikwa: 'Kama niishivyo,' asema Bwana, kila goti litapigwa mbele zangu; na kila ulimi utamkiri Mungu!" - (Warumi 14:10-11).

"Kristo Yesu akawa mtii hata mauti - naam, mauti ya msalaba!. Ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, mbinguni na duniani.. kila ulimi ukiri ya kuwa Yesu Kristo ni Bwana, kwa utukufu wa Mungu Baba" - (Wafilipi 2:5-11).

GUNDUA

Tangu dhambi ilipoanza, Ibilisi amekuwa akiielezea vibaya tabia ya Mungu, akimshtaki kwamba hatendi haki. Lakini sasa maswali yote yamejibiwa, utata wote umeondolewa. Sasa kila kiumbe aliye katika hayo malimwengu anakiri kwamba Yesu, Mwana-Kondoo wa Mungu, anastahili kupewa upendo wetu na kuabudiwa.

Mpango wote na kusudi la Mungu sasa vimefunuliwa kikamilifu, na tabia ya Mungu inasimama ikiwa imethibitishwa kuwa ni ya haki.

Si wale tu waliokombolewa, bali pia wale malaika waovu pamoja na Shetani mwenyewe watakiri kwamba njia ya Shetani imekuwa na makosa na ya kwamba njia za Mungu ni za haki na za kweli. Wote wanaona wazi kwamba uovu na uchoyo vimeleta huzuni tu na kutokuridhika, na kwamba mambo hayo hayafai kuendelea.

7. Dhambi Yaufikia Mwisho Wake

Ingawa Shetani na kundi lile kubwa sana liliosongamana la watu wale waovu wanakiri kwamba njia ya Mungu haijabadilika, tabia zao bado zina dhambi. Na baada ya hukumu ile kutamkwa wale waovu:

"Wakatembea kijeshi kupitia katika mapana ya nchi, wakaizingira kambi ya watu wa Mungu, mji ule aupenda. Lakini moto ukashuka kutoka mbinguni na kuwateketeza kabisa. Na yule Ibilisi, aliyekuwa, anawapotosha katupwa ndani ya ziwa linalowaka moto wa kiberiti.... Kisha kifo na kuzimu vikatupwa ndani ya ziwa la moto. Ziwa hili la moto ndicho kifo cha pili. Mtu ye yote ambaye jina lake halikupatikana limeandikwa katika kitabu kile cha uhai, alitupwa katika ziwa la moto" - (Ufunuo 20:9-15).

Katika hukumu ya mwisho moto wa milele wa Mungu utateketeza dhambi pamoja na wale ambao kwa ukaidi wao wanaing'ang'ania. Shetani na wote waliopotea wanaangamia katika hicho "kifo cha pili," yaani, wanapatikana na kifo cha milele ambacho katika hicho hawataamshwa kamwe.

Mwenendo wao wa uasi umewaacha waovu hao wakiwa hawafai kuingia katika furaha ya kweli, kisha wanateketeza pamoja na Ibilisi na malaika zake. Moto ule utokao mbinguni unaitakasa dunia kabisa kutokana na uharibifu wa dhambi; hatimaye Mungu anakuwa na ulimwengu safi, usioweza tena kutiwa makovu ya uovu. Pambano hilo la kishujaa kati ya wema na uovu, kati ya Kristo na Shetani, sasa limekomma, na Kristo anatawala. Pazia linayafunika matokeo ya dhambi ya zamani yaliyofuatia, kasha linafunuliwa ili kuuonyesha ulimwengu mpya wenye utukufu usiokuwa na kikomo.



8. Dunia Inatakaswa Na Yafanywa Upya

Kutoka katika majivu yale ya maangamizi makuu ya mwisho, Mungu ataiumba dunia mpya:

"Kisha nikaona mbingu mpya na nchi mpya; kwa maana mbingu za kwanza na nchi ya kwanza zimekwisha kupita... Nami nikauona mji ule mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu.. "Tazama, maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye fanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao. Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena, wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu, hayatakuwapo tena kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita... Tazama, nayafanya yote kuwa mapya" - (Ufunuo 21:1-5).



Itakapokuwa imerudishwa katika uzuri wake wa awali, dunia hii itakuwa makao ya waliokombolewa milele hata milele. Ikiisha kukombolewa mbali na choyo, magonjwa, na maumivu, tutayachunguza na malimwengu yote na tutakuwa na uhusiano wa ajabu na kuukuza, na umilele wa kuketi miguuni

GUNDUA

DISCOVER
online

pake Yesu na kusikiliza, kujifunza, na kupenda. (Kwa maelezo kamili ya dunia mpya, ukipenda waweza kusoma tena Mwongozo 9.)

Je! wewe unapanga kuwa wapi siku hiyo? Je! umeamua kuwa pamoja na Kristo ndani ya mji ule na kuokolewa milele? Au utakuwa nje ya ule mji bila Kristo na kupotea milele?

Kama wewe umeyakabidhi maisha yako mikononi mwake Yesu, basi, huna haja ya kuionja ile hofu isiyoneneka ya wale walio nje ya mji amba wanatambua kwamba wamepotea milele. Haidhuru maisha yakuletee kitu gani, kama wewe unayaweka maisha yako mikononi mwake Yesu hivi sasa, basi, unaweza kuwa ndani ya mji ule pamoja na Kristo na pamoja na wale waliokombolewa. Endapo wewe hujafanya hivyo, basi mpe Yesu moyo wako sasa, naye atakuzungushia upendo wake na msamaha. Hii ni nafasi yako ya pekee. Hii ndiyo siku yako ya wokovu kwako.

JEHANAMU NI NINI NA IKO WAPI?

Kufyatua risasi kipumbavu kulitokea wakati mwanafunzi mmoja alipoingia katika shule yake na kuwaua wanafunzi wenzake kadhaa. Mwanaume mmoja mwenye chuki, ambaye alikuwa amefukuzwa kazi, alingia mahali pale alipokuwa akifanya kazi zamani na kumpiga risasi mkuu wake wa kazi. Mama mmoja alisukuma gari lake dogo na kulitumbukiza ziwani likiwa na watoto wake wawili ndani yake na kuwazamisha.



Kwa uchache katika mabara mawili maelfu wamechinjwa katika mauaji ya safisha-safisha ya kikabila. Uhasama wa muda mrefu uliochukua karne nyingi kati ya makundi mawili au zaidi ya makabila hayo ndicho chanzo chake. Wanaume, wanawake, watoto, na hata watoto wachanga wamepigwa risasi, wamekatwa-katwa, wamepigwa, na kubakwa.

Kutoa adhabu ya kifo kwa uhalifu huo wa kishenzi, hata kwa wauaji wale walio wakatili sana, kunashutumiwa na wengi. Makundi yaliyo kinyume na hukumu ya kifo yanapinga kwa makelele mengi, wakiita hukumu hiyo kuwa sio ya kibinadamu ati ni "mfumo wa ibada ya kipagani." Wanauliza hivi, je! wauaji hao hawarekebishi?

Je! njia sahihi ya kibinadamu ya kuwaua wahalifu waliohukumiwa kuuawa ni ipi? Je! ni kile kiticha umeme? Wengine wanadhani kudungwa sindano yenye sumu ya kufisha ingekuwa ni njia isiyo na maumivu kabisa. Wengine wanatetea kwamba uhai wa mtu ungekoma kwa upesi zaidi kwa kumnyonga.

Lakini katika majadiliano hayo yote yaliyojaa harara juu ya adhabu ya kifo, upo uchaguzi mmoja ambao hakuna mtu anayefikiria. Hakuna anayependekeza kwamba wale wauaji wakatili, ambao kwa ukatili wamekomesha maisha ya mtu mwengine, wapatilizwe kwa kuteswa vibaya sana kimwili mpaka wafe. Kwa mfano, hakuna aliyependekeza kwamba wauaji hao wachomwe moto polepole mpaka wafe.

Lakini, basi Wakristo wengi waaminifu wanadhani kwamba Baba yetu aliye mbinguni atatenda vibaya kuliko hivyo. Wao wanasma, waovu ni lazima wateswe vibaya ili kubatilizwa kwa ajili ya dhambi zao. Tena, zaidi sana ya hayo, wanafikiria kwamba maeneo ya Mungu anayoyatumia kuwailia wahalifu ni mahali pa mateso yasiyo na mwisho.

Ni kitu gani hasa kinachowapata waovu? Je! maangamizi yao yanapatanaje na upendo na haki ya Mungu? Hebu na tuangalie Biblia itupe jibu.

1. Huzuni Kubwa Ya Mwisho Ya Yesu

Kwa miaka 6,000 Mungu amekuwa akiwasihii sana wanaume na wanawake:

"Kama mimi niishivyo, mimi Bwana Mwenyezi-Mungu...mimi sikufurahii kifo cha mtu mwovu, bali napenda mtu mwovu aachane na mwenendo wake mbaya, apate kuishi" - (Ezekiel 33:11).



Msalaba ulidhihirisha ni kwa kiwango gani Mungu anataka kuwaokoa wanadamu walioanguka [dhambini]. Yesu alipopaza sauti pale msalabani, akisema, "Baba uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo," aliufunua wazi moyo wake uliokuwa ukimwuma (Luka 23:34). Muda mfupi baada ya hapo Yesu akakata roho, na kama wengine waaminivyo, akafa kwa kupasuka moyo wake (Yohana 19:30,34).

Lakini hata pamoja na udhihirisho huo wenye nguvu ya upendo wa Mungu, watu wengi bado hawamgeukii Yesu. Na kadiri dhambi inavyoendelea kutawala

GUNDUA

katika dunia hii, ndivyo itakavyozidi kuongeza misiba ya wanadamu. Kwa hiyo ni lazima dhambi iteketezwe kabisa. Je! hivi Mungu anapanga kufanya nini ili kuikomesha hiyo dhambi?

"Siku ya Bwana itakuja.... mbingu zitatoweka kwa kishindo kikuu; na vitu vyake vya asili vitateketezwa kwa moto, nayo dunia itatoweka..." - (2Petro 3:10).

Hatimaye ni lazima Mungu aitakase dunia hii kutokana na uovu wake na kuikomesha dhambi kabisa. Wale wanaoendelea kung'ang'ania dhambi hatimaye watateketezwa kwa moto huo ulioandaliwa kwa ajili ya kumteketeza Iblisi, malaika zake, na dhambi katika dunia yetu hii. Ni wakati wa kuhuzunisha jinsi gani kwa Yesu anapouangalia moto ukiwateketeza wale aliokuja kuwafia ili kuwaokoa.

2. Wapi Na Lini Utakapowaka Moto Wa Jehanamu?

Kinyume na dhana zinazopendwa sana na watu wengi, Mungu hana moto unaowaka sasa mahali paitwapo "jehanamu" ambapo wafu huenda wanapokufa. Jehanamu hutokea wakati ule dunia hii itakapogeuka na kuwa ziwa la moto. Mungu anangojea kutekeleza hukumu hiyo dhidi ya waovu mpaka hapo hukumu ya mwisho itakapotolewa mwisho wa ile miaka 1,000 (Ufunuo 20:9-15).



"Bwana anajua jinsi ya kuwaokoa katika majaribu watu wanaomcha Mungu, na jinsi ya kuwaweka waovu katika adhabu hadi siku ile ya hukumu" - (2 Petro 2:9).

Pia anaitakasa dunia yetu kwa moto huo utakasao.

"Lakini Mbingu na nchi za sasa zimehifadiwa kwa neno la Mungu kwa ajili ya kuharibiwa kwa moto. Zimebekwa kwa ajili ya siku ile ambapo watu wasiomcha Mungu watahukumiwa na kuangamizwa." - (2 Petro 3:7).

Kamwe Mungu hakupanga kwamba mwanadamu awaye yote amalizie maisha yake katika mioto ile ya jehanamu. Lakini watu wanapokataa katakata kuachana na Shetani, halafu wanaoendelea kuzing'ang'ania dhambi zao, basi, ni lazima wapokee hatimaye matokeo ya uchaguzi wao.

"Kisha atawaambia wale walio upande wake wa kushoto, 'Ondokeni mbele yangu enyi mliolaaniwa! nedeni katika moto wa milele aliotayarishiwa Ibilisi na malaika wake" Mathayo 25:41.

Kulingana na maneno hayo ya Kristo, je! ni lini jehanamu itakapowaka moto?

"Kama vile magugu yanavyokusanywa na kuchomwa moto, ndivyo itakavyokuwa mwisho mwa nyakati; Mwana wa Mtu atawatuma malaika wake wawakusanye kutoka katika ufalme wake wale wote wenye kusababisha dhambi, na wote wenye kutenda maovu, na kuwatupa katika tanuru ya moto, na watalia na kusaga meno. Kisha, wale wema watang'ara kama jua katika ufalme wa Baba yao. mwenye masikio na asikie!" - (Mathayo 13:40-42).

Magugu, yaani, wale watendao maovu, hawachomwi moto mpaka utakapofika ule mwisho wa dunia. Kabla haijatekelezwa hiyo hukumu, malimwengu yote hayana budi kuthibitisha kwamba Mungu ni mwenye haki katika kumshughulikia kila mwanadamu. Kama ilivyoelezwa kwa kinaganaga katika Mwongozo 22, katika pambano kuu linaloendelea kati ya Kristo na Shetani, Shetani amekuwa akijaribu kuyathibitishia hayo malimwengu kwamba njia ya dhambi ndiyo njia bora; Yesu amekuwa akionyesha wazi kwamba njia ya utii ndiyo ufunguo wa maisha yanayoridhisha zaidi.

GUNDUA



Mwisho wa miaka ile 1,000, udhihirisho huo utaishia katika hukumu ya Shetani, malaika zake, na waovu. Baada ya kufunguliwa vitabu vya kumbukumbu ambavyo vinafichua sehemu aliyofanya kila mtu katika mfululizo wa matukio hayo ya kusisimua, ndipo Mungu atakapomtupa Shetani, mauti na kaburi [kuzimu], pamoja na kila mmoja ambaye jina lake "halikuonekana limeandikwa katika kitabu cha uzima.... Katika ziwa la moto" (Ufunuo 20:15). Kulingana na fungu hili lifuatalo, yaani, Ufunuo 21:1, baada ya Mungu kuitakasa nchi hii kwa moto kutokana na dhambi, anaumba, "mbingu mpya na nchi mpya."

3. Jehanamu Itawaka Kwa Muda Gani?

Waumini wengi wanalikubali wazo hili lisemalo kwamba mioto ile ya jehanamu inawaka milele na milele. Hebu na tuangalie kwa makini mafungu yale yanayoeleza jinsi Mungu anavyoishughulikia dhambi pamoja na wenye dhambi.

"Na miale ya moto huwaadhibu wale wanaomkataa Mungu na wale wasiotii Habari njema ya Bwana ya Yesu. Adhabu yao itakuwa kuangamizwa milele na kutengwa mbali na utukufu wake mkuu" - (2 Wathesalonike 1:8,9).

Tafadhalii zingatia kwamba hayo "maangamizi ya milele" sio sawa na "mateso makali ya milele." Maana yake tu ni kwamba hayo ni maangamizi yanayoendelea milele. Matokeo yake ni mauti ya milele. Petro alizungumza juu ya siku ya hukumu na ya "kuangamizwa kwao wanadamu wasiomcha Mungu" (2Petro 3:7).

Kulingana na Yesu, maneno yote mawili, yaani, "roho na mwili" huangamizwa katika Jehanamu (Mathayo 10:28). Katika hotuba yake ya mlimani, Yesu alizungumza juu ya mlango ulio mwembamba "uendao uzimani," na njia ile pana "iendayo kwenye maangamizi" (Mathayo 7:13,14). Katika Yohana 3:16, Yesu anaeleza kwamba Mungu "akamtoa Mwanawe pekee," bali wawe na uzima wa milele." Yesu anailinganisha miisho miwili: uzima wa milele au kuangamia sio kuchomwa moto milele na milele.

Tunapaswa kuhitimisha kwa kusema kwamba ni dhahiri ya kuwa jehanamu ina mwisho wake; mwisho wake ni mauti na maangamizi ya waovu.

Semi zinazoleweka wazi katika maandiko yote zinatuambia kwamba waovu wataangamizwa. "Waovu wataharibiwa" (Zaburi 37:28), "wataangamizwa" (2Petro 2:12), "watautoweka kama moshi" (Zaburi 37:20). Moto ule utawateketeza kabisa hadi watakuwa majivu (Malaki 4:1-3). "Mshahara wa dhambi ni mauti, "sio uzima wa milele katika jehanamu; (Warumi 6:23).

Kusudi la adhabu ya mwisho katika moto ule wa jehanum ni kuiondoa dhambi kabisa ulimwenguni humu, sio kuiendeleza dhambi milele na milele. Ni vigumu kabisa kumwazia Kristo aliyeulilia mji ule mkaidi kutokana na ajali yake, na ambaye aliwasamehe wale waliomwua, kwamba atumie umilele wake wote kuyaangalia maumivu yale makali ya waliolaaniwa.



Ni dhahiri kwamba jehanamu ina mwisho wake. Mwisho wa miaka 1,000, Mungu ananyesha moto chini kutoka mawinguni na kumwangamiza kabisa Ibilisi, malaika zake, pamoja na waovu wanaoendelea kuzing'ang'anira dhambi zao. "Moto" huo una "shuka kutoka mbinguni" na kuwateketeza kabisa (Ufunuo 20:9).

Kulingana na maneno yake Kristo, moto huo ni "moto usiozimika" (Mathayo 3:12). Hakuna zima moto iwayo yote iwezayo kuuzima mpaka umalize kazi yake ya kuteketeza kabisa.

Mungu anaahidi kwamba, kutokana na moto huo utakasao, yeye ataiumba "nchi mpya," ambayo ndani yake "taabu zote zilizopita zitakuwa zimesahaulika," na "sauti ya kuomboleza na kulia haitasikika tena ndani yake" (Isaya 65:16-19).


Ile ni siku ilioje! Kila chanzo kiletacho huzuni kubwa kitakuwa kimetoweka kabisa. Mungu atayafutilia mbali kabisa majeraha ya dhambi kutoka katika kila moyo, ndipo furaha yetu itakuwa imetimilika.

4. "Milele" Katika Maandiko

Katika Mathayo 25:41 Yesu anazungumza juu ya "moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake." Je, neno hili "milele" linadokeza kwamba jehanamu hiyo ni ya milele? Yuda 7, anaeleza habari za Sodoma na Gomora kuwa "imewekwa kuwa mfano wa wale watakaopata adhabu yao katika ule moto wa milele." Ni dhahiri kwamba miji ile haiendelei kuteketezwa kwa moto ule. Lakini moto wenyewe ULIKUWA wa milele kwa maana kwamba ulisababisha maangamizi ya kudumu.

Katika 2Petro 2:6 tunasoma mara moja tena habari za moto wa milele. Lakini maandiko hayo pia huonyesha wazi kwamba Mungu "akaihukumu miji ya Sodoma na Gomora, akiiteketeza kabisa kwa moto na kuifanya majivu, akaifanya iwe mfano wa kile kitakachowapata wale wasiomcha Mungu." Wale wasiomcha Mungu waliokuwa Sodoma na Gomora hawaendelei kupata maumivu makali; waliteketezwa kabisa kuwa majivu zamani sana. Na, hata hivyo, moto ule uliowateketeza ni "wa milele' kwa kuangalia matokeo ya kazi yake - yaani, maangamizi yale ya kudumu. Milele maana yake ni adhabu ya kudumu, sio kuendelea tu kuadhibiwa.

Kwa kuwa kile kitabu cha Ufunuo kinatumia lugha ya mifano dhahiri kama ile, baadhi ya vifungu vyake vya maneno vimeeleweka vibaya. Kwa mfano, Ufunuo 14:11 husema maneno haya juu ya wale waliopotea, "moshi wa maumivu yao hupanda juu hata milele na milele." Maneno haya yanasiyika kana kwamba ni mateso yasiyo na mwisho. Lakini, tena, hebu na tuliache Andiko kulitafsiri Andiko.



Kutoka 21:6 katika toleo la KJV huzungumzia habari za mtumishi kutobolewa sikio lake kama ishara ionyeshayo kwamba yeye angeendelea kumtumikia bwana wake "milele." Katika mfano huu neno hili "milele" lingemaanisha kadiri uhai wa mtumishi yule ambavyo ungeendelea kuwapo. Yona, aliyekaa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la yule nyangumi (Mathayo 12:40), anatoa taarifa yake kwamba alikuwa ndani mle "milele" (Yona 2:6). Bila shaka zile siku tatu na lile giza lisilokuwa na matumaini kwake vilionekana kana kwamba ni milele.

Basi hatuna budi kuwa waangalifu kuelewa ni jinsi gani na lini maandiko yanapotumia lugha ya mafumbo, ya mashairi. Moshi ukipanda juu milele kutoka katika ziwa lile la moto ni njia dhahiri ya kuonyesha maangamizi ya milele. Ufunuo 21:8 hutuambia waziwazi kwamba ziwa lile linalowaka moto na kiberiti "ni mauti ya pili." Jehanum ina mwisho wake. Waovu wanateketezwa kwa moto; yaani, wanaangamizwa kabisa.

5. Kwa Nini, Iweko Hiyo Jehanamu?

Hapo mwanzo Mungu aliiumba dunia hii ikiwa kamilifu. Lakini dhambi ikaja na kuleta misiba, uharibifu, na mauti. Kama jioni moja ungerudi nyumbani kwako na kuikuta nyumba yako imepekuliwa na kuharibiwa, je! ungeiacha katika hali ile milele? Hasha. Ungefagia takataka na uchafu, ungesafisha



GUNDUA

mahali pale kabisa, na kuitupilia mbali samani [fanicha] iliyoharibiwa kiasi cha kutoweza kutengenezeka tena. Mungu atafanya vivyo hivyo. Ataushughulikia uharibifu na uchafuzi wa dhambi kwa mara moja tu, na kuiumba dunia mpya mahali pake. Kusudi la Mungu kuitakasa dunia hii kwa moto ni kutayarisha njia ya kupatikana dunia kamilifu kwa ajili ya kuishi ndani yake wale waliookolewa.

Lakini Mungu anakabiliwa na tatizo zito kwa sababu dhambi hiyo haikuharibu tu dunia hii, bali pia imewaambukiza watu. Dhambi iliharibu uhusiano wetu naye na kati yetu sisi kwa sisi. Wanadamu wanaedelea kusumbuliwa na watoto wanaoteswa, ugaidi, picha za wanawake walio uchi zinazoamsha ashiki, na maelfu ya kansa nyininge za kiroho. Siku moja Mungu atalazimika kuiangamiza dhambi kabisa, kwa sababu dhambi ndiyo inayowaangamiza watu. Tatizo la Mungu ambalo ni gumu kulitatu ni hili; jinsi gani akiteketeze kile kirusi cha dhambi kiletacho mauti kutoka katika dunia hii na wakati huo huo asiweze kuwaangamiza watu wote walioambukizwa nacho? Suluhisho lake lilikuwa ni lile lakukichukua kirusi hicho cha dhambi ndani ya mwili wake mwenyewe; akairuhusu ile kansa ya dhambi kumwangamiza yeye kabisa pale msalabani. Matokeo yake ni haya:

"Tukiziungama dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki, naye atatusamehe dhambi zetu na KUTUSAFISHA UDHALIMU WOTE." - (1 Yohana 1:9).

Mungu anampa bure kila mmoja suluhisho lake kwa hilo tatizo la dhambi. Lakini ukweli wa kusikitisha ni kwamba wengine wanaung'ang'ania ugonjwa huo wa dhambi kwa nguvu zao zote. Na Mungu hatatumia nguvu kuwalazimisha watu hao ili wapate kuichagua njia yake ya uzima wa milele. Wale wanaolikataa suluhisho lake hatimaye wataangamizwa kabisa pamoja na ugonjwa huo. Sababu ya kweli ya kuwako hiyo jehanamu ni hii:

"Kwa sababu mimi nilipoita ninyi hamkuitika, niliponena hamkusikia. Mlitenda yaliyo mabaya machoni pangu, mlitchagua mambo nisiyoyafurahia mimi" - (Isaya 65:12).

Wakiwa wametengwa mbali na Yesu kwa uchaguzi wao wenyewe, waovu watagundua kwamba kumbe njia pekee iliyobaki kwao ni kukabiliwa na ile mauti ya milele.

6. Nini Gharama Ya Kupotea?

Ijapokuwa maandiko hayafundishi kwamba moto ule wa jehanamu unasababisha maumivu yasiyo na mwisho, yanatupa picha ya haraka kuonyesha ni jambo la kutisha jinsi gani kupotea. Waovu wataukosa uzima wa milele. Litakuwa ni jambo la kuogofya jinsi gani kutambua kwamba furaha ile ya kuishi milele pamoja na Mungu imeteleza mikononi mwao, ya kwamba hawatauonja kamwe uhusiano ule wenyefuraha kamilifu na upendo milele hata milele.



Kristo alipoangikwa pale msalabani, dhambi za ulimwengu mzima zikimtenga na Baba yake, bila shaka alipata wale watakapotea milele. Waovu wanapoliangalia lile giza jeusi, lenye ukiwa, mbele yao, wanaona tu maangamizi yao ya milele. Hawana budi kufa bila kuwa na tumaini la kufufuliwa mara ya pili. Wakati huo huo wanaona jinsi walivyomsukumia mbali huyo Kristo mara kwa mara alipokuja karibu nao akiwa na maneno ya upendo ya kutaka kufanya amani nao. Mwisho watapiga magoti yao na kukiri kwamba Mungu ni mwenye haki na upendo (Wafilipi 2:10,11).

Si ajabu, basi, kwamba waandishi wa Biblia wanasisitiza sana juu yetu kuhusu uzito wa uchaguzi wetu tunaofanya pamoja na madai ya Kristo kwetu.

"Basi, tukiwa wafanyakazi pamoja na Mungu, tunawasihi msikubali ile neema mliyopokea kutoka kwa Mungu ipotee bure, Mungu asema hivi: "Wakati wa kufaa nimekusikiliza, wakati wa wokovu nikakusaidia". Basi, sasa ndio wakati wa kufaa, sasa ndiyo siku ya wokovu" - 2 Wakorintho 6:1,2.

GUNDUA

DISCOVER
online

Siwezi kufikiria juu ya msiba mkubwa kuliko ule wa mtu fulani anayeitumia vibaya kafara ya Yesu kwa kuchagua kupotea. Njia zilizobaki mbele yetu ziko dhahiri kabisa: yaani, yale maangamizi ya milele - kutengwa milele mbali na Mungu, au urafiki wa milele pamoja na Kristo ambao unakidhi shauku yetu ya ndani kabisa ya moyo wetu. Je! wewe unachagua ipi? Kwa nini wewe usiugundue mwisho wako kwa kukaa ndani ya Kristo leo?

MTU AKIFA, KUNA NINI BAADAYE?

Tunajikunyata mtoto mdogo anapouliza kwanza swali hili, "kufa maana yake nini? Tunaywea kuzungumza au hata kufikiri juu ya mtu fulani tumpendaye anapokaribia kufa. Mauti ni adui wa watu wote kila mahali.

Je! majibu ni yapi kwa maswali magumu yahusuyo kifo? Je! kuna maisha baada ya kufa? Je! tutawaona tena wapendwa wetu waliokufa?

1. Kukikabili Kifo Bila Hofu

Sisi sote kwa wakati fulani, labda baada ya kufa rafiki yetu au mpendwa wetu, tumejisikia kana kwamba tumbo liko tupu, yaani, kuwa na hisia ile ya upweke inayopita ndani yetu tunapoangalia kwa haraka kuona mwisho wa uhai wa mtu.

Katika jambo hili la maana sana, liliojaa hisia nyingi, ni wapi basi, tunakoweza kujifunza habari za kile kinachotokea tunapokufa? Kwa bahati nzuri, sehemu ya utume wa Kristo hapa duniani ilikuwa ni "kuwaweka huru wale ambao katika maisha yao yote walikuwa katika hali ya utumwa kwa hofu ya mauti" (Waibrania 2:15). Na katika Biblia, Yesu anatoa ujumbe wenye faraja, kisha anajibu maswali yetu yote juu ya mauti na yale maisha ya baadaye kwa njia inayoleweka wazi.



2. Jinsi Mungu Alivyotuumba

Kuelewa kutoka katika Biblia ukweli halisi juu ya kifo, hebu na tuanze mwanzo na kuona jinsi Mungu alivyotuumba.

"BWANA MUNGU AKAMFANYA MTU (ADAMU, KIEBRANIA) KWA MAVUMBI YA ARDHI (ADAMAH, KIEBRANIA), AKAMPULIZIA PUANI PUMZI YA UHAI, NA MTU YULE AKAWA NAFSI HAI [ROHO, KIEBRANIA]." - (MWANZO 2:7).



Wakati ule wa uumbaji, Mungu alimfinyanga Adamu kutoka katika "mavumbi ya ardhi." Alikuwa na ubongo kichwani mwake ulio tayari kufikiri; damu katika mishipa yake iliyo tayari kuzunguka mwilini mwake. Ndipo Mungu alipompulizia puan "pumzi ya uhai," na Adamu akawa "nafsi hai" [Kiebrania, "roho hai"]. Zingatia kwa makini, Biblia haisemi Adamu alipokea roho; bali inasema tu kwamba "mtu akawa roho hai." Mungu alipompulizia Adamu pumzi puan mwake, uhai ukaanza kuingia ndani yake kutoka kwa Mungu. Mwungano huo wa mwili na "pumzi ya uhai" ulimfanya Adamu kuwa "nafsi hai," tunaweza kundika mlinganyo (equation) wa kibinadamu kama hivi:

"Mavumbi ya Ardhi" + "Pumzi ya Uhai" = "Roho Hai"

Mwili Usio na Uhai + Pumzi toka kwa Mungu = Nafsi Hai.

Kila mmoja wetu anao mwili na akili inayofikiri. Kwa kadiri sisi tunavyoendelea kuvuta pumzi, tutaendelea kuwa nafsi hai, yaani, roho hai.

3. Kunatokea Nini Mtu Akifa?

GUNDUA

Mtu anapokufa kinyume cha hatua zile za uumbaji zilizolezwa katika Mwanzo 2:7 hutokea "**Nayo MAVUMBI huirudia ardhi yalikotoka, nayo ROHO [PUMZI YA UHAI] humrudia Mungu aliyeitoa.**" - (Mhubiri 12:7).

Mara nyingi Biblia hutumia maneno ya Kiebrania yamaanishayo "pumzi" (breath) na "roho" (spirit) kwa kubadilishana. Watu wanapokufa, mwili wao unageuka na kuwa "mavumbi" na "roho ("pumzi ya uhai") humrudia Mungu aliyeitoa. Lakini, je! kunatokea nini kwa ile roho hai (living soul)?

"Kama mimi niishivyo, atangaza Bwana Mungu,... Kila ROHO ILIYO HAI (LIVING SOUL) ni mali yangu;... ROHO YULE ATENDAYE DHAMBI NDIYE ATAKAYEKUFA." - Ezekiel 18:3-4.

Roho inakufa! Kwa sasa haina uwezo wa kuishi milele - inaweza kuangamizwa. Mlinganyo ule ulioupata kutokana na Mwanzo 2:7, Mungu alipotuumba sisi, unajipindua wakati ule wa kufa.

"Mavumbi ya Ardhi" - "Pumzi ya Uhai" = "Roho Iliyokufa"

"Mwili usio na uhai - Pumzi toka kwa Mungu = Nafsi Iliyokufa.

Mauti ni kukoma kabisa kwa uhai. Mwili unavunjika-vunjika na kugeuka kuwa mavumbi, na ile pumzi, au roho, humrudia Mungu. Sisi ni roho hai tunapoendelea kuishi, lakini tunapokufa tunakuwa maiti tu, yaani, roho Iliyokufa, nafsi Iliyokufa. Kwa hiyo wafu hawana fahamu zo zote. Mungu anapoiondoa kwetu pumzi yake ya uhai aliyatupa, roho yetu hufa. Lakini kama tutakavyoona baadaye katika somo hili, tukiwa na Kristo tumaini liko.

4. Mfu, Anajua Kiasi Gani?

Baada ya kufa ubongo unaharibika; hauwezi kujua, wala kukumbuka kitu cho chote. Hisia zote za moyo za kibinadamu hukoma kabisa mtu anapokufa.

"Upendo wao, chuki yao na wivu wao, vimetoweka siku nyingi sana..." - (Mhubiri 9:6).

Wafu hawana fahamu zo zote, hivyo hawana habari na kitu cho chote kinachotokea hapa. Hawana mawasiliano yo yote na wale walio hai:

"Kwa sababu walio hai wanajua ya kwamba watakufa, lakini WAFU HAWAJUI CHO CHOTE." - (Mhubiri 9:5).

Kifo ni kama usingizi usio na ndoto - kwa kweli, Biblia inakiita kifo kuwa ni "usingizi" mara 54. Yesu alifundisha kwamba kifo ni kama usingizi., alisema hivi kwa wanafunzi wake:

Yesu alipomaliza kusema maneno hayo, akawaambia, **"Rafiki yetu Lazaro amelala, lakini mimi nitakwenda kumwamsha".** **Wanafunzi wake wakamwaabia, "Bwana, ikiwa amelala, basi atapona".** **Wao walidhani kwamba alikuwa amesema juu ya kulala usingizi, kumbe alikuwa amesema juu ya kifo cha Lazaro. Basi, Yesu akawaambia waziwazi, Lazaro amekufa;-** (Yohana 11:11-14).



Lazaro alikuwa amekufa yapata siku nne kabla Yesu hajafika pale. Lakini Yesu alipokwenda kwenye kaburi lake, alithibitisha kwamba kwa Mungu ni rahisi kuwafufua wafu kama ilivyo rahisi kwetu kumwamsha mwenzetu aliylala usingizi.

Ni faraja kubwa kwetu kujua kwamba wapendwa wetu waliokufa wame "lala usingizi," yaani, wanapumzika salama salimini ndani ya Yesu. Shimo lile refu la mauti, ambalo sisi wenywewe tutalipitia siku moja, ni kama kulala usingizi mtulivu wa amani.

5. Je! Mungu Anawasahau Wanaolala Usingizi Wa Mauti?

GUNDUA

DISCOVER
online

Usingizi huo wa mauti sio mwisho wa kisa hiki. Pale kaburini, Yesu alimwambia Martha, dada yake Lazaro, maneno haya: "**MIMI NDIMI HUO UFUFUO, na uzima. YEYE ANIAMINIYE MIMI ATAKUWA ANAISHI, HATA KAMA ATAKUFA.**" - (Yohana 11:25).

Wale wanaokufa "katika Kristo" wanalala usingizi makaburini mwao lakini wao bado wanalo tumaini zuri la kupata maisha yale ya baadaye. Yeye anayeuhesabu kila unywele juu ya vichwa vyetu na kutushika katika kiganja cha mkono wake hatatusahau sisi. Tunaweza kufa na kurudi mavumbini, lakini kumbukumbu ya utu wetu bado i wazi katika mawazo ya Mungu. Na Yesu atakapokuja, atawaamsha wenye haki waliokufa kutoka katika usingizi wao, kama vile alivyofanya kwa Lazaro.

"Ndugu, twataka mjue ukweli kuhusu wale ambao wamekwisha fariki dunia, ili msipatwe na huzuni kama watu wengine wasio na matumaini. Maana patatolewa amri, sauti ya malaika mkuu, sauti ya tarumbeta ya Mungu, naye Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni. Ndipo wale waliokufa wakiwa wanamwamini Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai wakati huo tutakusanya pamoja nao katika mawingu kumlaki Bwana hewani. Na hivyo tutakuwa daima pamoja na Bwana. Basi, farijaneni kwa maneno haya" - (1 Wathesalonike 4:13, 16-18).

Siku ile ya ufufuo lile shimo refu la mauti litaonekana kana kwamba ni pumziko letu la muda mfupi sana. Wafu hawana habari na muda unaopita. Wale waliompokea Kristo kama Mwokozi wao, wataamshwa kutoka usingizini kwa sauti yake ya ajabu ikishuka kuja hapa duniani.



Tumaini hilo la ufufuo linaye mwenzake; yaani, tumaini la kuwa na makao yale ya mbinguni ambako Mungu "atafuta kila chozi katika macho yao." Mauti haitakuwapo tena, wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu" (Ufunuo 21:4). Wale wanaompenda Mungu hawana haja ya kuogopa mauti. Ng'ambo yake kuna umilele wa maisha yale matimilifu pamoja na Mungu. Yesu anazo "funguo za mauti" (Ufunuo 1:18). Bila Kristo, mauti ingekuwa ni njia ya moja kwa moja inayoishia katika hali ya usahafulifu kabisu, lakini tukiwa pamoja na Kristo, basi, kuna tumaini linalong'aa, lenye furaha.

6. Je! Tuna Miili Isiyokufa Sasa?

Mungu alipomwumba Adamu na Hawa, waliumbwaa wakiwa na miili inayokufa, yaani, walikabiliwa na kifo. Laiti kama wangaliendelea kuwa watii kwa mapenzi yake Mungu, wasingeweza kufa kamwe. Lakini walipotenda dhambi, walipoteza haki yao ya uzima. Kwa uasi wao ule wakakabiliwa na mauti. Dhambi yao iliwaambukiza wanadamu wote, na kwa kuwa wote wamefanya dhambi, basi, sisi sote tuna miili inayokufa, yaani, tunakabiliwa na mauti (Warumi 5:12). Wala hakuna dokezo hata moja katika Biblia lisemalo kwamba roho ya mwanadamu inaweza kuishi peke yake kama kitu kilicho na fahamu.



Kamwe Biblia haijaeleza hata mara moja kwamba roho kama ilivyo sasa ina hali hiyo ya kutokufa kamwe - yaani, kwamba haiwezi kufa. Maneno ya Kiebrania na Kigiriki ya neno hili "roho" (soul), na "roho" (spirit), na "pumzi" (breath) hutokea mara 1,700 katika Biblia. Lakini hakuna hata mara moja ambapo roho ya binadamu (soul), roho (spirit), au pumzi (breath) inatajwa kuwa haiwezi kufa. Kwa wakati huu wa sasa ni Mungu peke yake ambaye ana hali hiyo ya kutokufa kamwe.

"Mungu.... PEKE YAKE HAPATIKANI NA MAUTI." - I Timotheo 6:15,16.

Maandiko yanaeleza wazi kwamba katika maisha haya wanadamu wana hali ya kufa: yaani, wanakabiliwa na kifo. Lakini Yesu ajapo, mwili wetu utafanyiwa mabadiliko makubwa.

GUNDUA

"Sikilizeni, nawaambieni siri sisi hatutakufa sote, ila sote tutageuzwa, wakati wa mbiu ya mwisho, kwa nukta moja, kufumba na kufumbua. Maana tarumbeta ya mwisho itakapolia, wafu watafufuliwa katika hali ya kutokuweza kuwa tena, na sisi tutageuzwa. Maana ni lazima kila kuharibikacho kijivalie hali ya kutoharibika, mwili uwezao kuwa ujivalie hali ya kutokufa"- (1Wakorintho 15:51-53).

Sisi, kama wanadamu, hatuna miili isiyokufa sasa. Lakini ahadi inayotolewa kwa Mkristo ni kwamba sisi tutakuwa na miili isiyoweza kuwa kamwe wakati Yesu atakapokuja tena kwa mara yake ya pili. Uhakika wa ahadi ya uzima wa milele ulionyeshwa wazi Yesu alipolipasua kaburi lake na:

"Lakini imefunuliwa kwetu sasa kwa kuja kwake Mwokozi wetu, Yesu Kristo. Yeye amekomesha nguvu za kifo, na kwa njia ya Habari Njema akadhihirisha uhai usio na kifo" - 2Timotheo 1:10.

Mtazamo wa Mungu kuhusu mwisho wa wanadamu uko wazi: yaani, mauti ya milele kwa wale wanaomkataa Kristo na kuzing'ang'ania dhambi zao, au hali ya kutokufa kamwe kama zawadi kwa wale waliompokea Yesu kama Bwana na Mwokozi wao wakati ule atakapokuja.

7. Kukikabili Kifo Cha Mpandwa Wetu

Hofu zile ambazo kwa kawaida sisi tunapambana nazo tunapokabiliana na kifo zinakuwa kali sana wakati ule anapokufa mpandwa wetu. Upweke pamoja na ile hisia ya kupotelewa, mambo hayo yanaweza kutulemea sana. Suluhisho pekee kwa utungu huo uliosababishwa na kutengana na mpandwa wetu ni ile faraja tu atupayo Kristo. Kumbuka kwamba huyo mpandwa wako amelala usingizi, na wapendwa wako wanaopumzika katika Kristo watafufuliwa katika ule "ufufuo wa uzima Yesu atakapokuja."



Mungu anapanga maajabu yake ya kuwaunganisha tena wale waliotengana. Watoto wadogo watarejeshwa kwa wazazi wao waliojaa furaha kubwa. Waume na wake zao watakumbatiana. Utengano wa kikatili uliotokea katika maisha haya utakwisha. "Mauti imemezwa kwa ushindi"- (1 Wakorintho 15:54).

Wengine wanajisikia vibaya sana kutengwa na mpandwa wao kiasi kwamba wanajaribu kufanya mawasiliano na wapendwa wao waliokufa kuitia kwa mjumbe wa mizimu (spiritualist medium) au kwa mtu yule anayeunganisha mawasiliano kama hayo wa Kizazi Kipyra (New Age Channeler). Lakini Biblia kwa njia ya pekee inatuonya sisi dhidi ya kujaribu kupunguza maumivu yetu yanayotokana na kufiwa kwa njia hiyo:

"Baadhi watawaambieni "Nendeni mkatake shauri kwa mizimu na mizuka iliayo kama ndege; kwani ni kawaida watu kutaka shauri kwa miungu yao; na kutaka shauri kwa wafu kwa ajili ya walio hai" - (Isaya 8:19).

Ndiyo, Hivi kwa nini? Biblia inaeleza waziwazi kwamba wafu hawana fahamu yo yote. Suluhisho la kweli kwa huo uchungu uliosababishwa na kutengwa na mpandwa wetu ni ile faraja ambayo ni Kristo tu aewzaye kutupa. Kutumia muda wetu kuwasiliana na Kristo ni njia bora kabisa kiafya ya kukua kuitia katika hatua hizo za kuhuzunisha.

Kumbuka siku zote kwamba, kule kuzipata fahamu tena kwa wale walalao katika Kristo kutawajia wakati ule zitakapopigwa kelele za kuja mara ya pili kwa Kristo ambazo zitawaamsha wafu!

8. Kukikabili Kifo Bila Hofu

Kifo kinatunyang'anya sisi karibu kila kitu. Lakini kitu kimoja ambacho hakiwezi katuondolea ni Kristo, na Kristo anaweza kukirudisha kila kitu mahali pake tena. Mauti haitatawala daima katika dunia hii. Ibilisi,

waovu, mauti na kaburi vitaangamizwa kabisa katika lile "ziwa la moto" ambalo ni "mauti ya pili" (Ufunuo 20:14).

1. Hapa yapo mapendekezo manne rahisi juu ya kukikabili hicho kifo bila hofu: Uishi maisha ya kuwa na matumaini kwa kumtegemea Kristo, ndipo utakuwa tayari kufa dakika yo yote.
2. Kwa uweza wa Roho Mtakatifu, uwe mtiifu kwa amri zake Kristo, nawe utakuwa umejandaa kwa yale maisha ya pili, ambayo ukiwa nayo hutawenza kufa kamwe.
3. Ifikirie mauti kama usingizi wa muda mfupi ambao kutoka katika huo sauti ya Yesu itakuamsha atakapokuja mara ya pili.
4. Itunze ile ahadi atupayo Yesu ya kutupa sisi makao yetu kule mbinguni kuishi pamoja naye milele hata milele.
Kweli ya Biblia humweka mtu huru mbali na ile hofu ya mauti kwa sababu inamfunua Yesu, ambaye hata mauti haikuweza kumshinda. Yesu anapoingia katika maisha yetu, anaigharikisha miyo yetu na amani:
"Amani nawaachieni; amani yangu nawapa... Msifadhaike moyoni mwenu , wala msiwe na woga."
- (Yohana 14:27).

Yesu pia anafanya uwezekano uwepo kwetu wa kukabiliana na msiba unaotokana na kumpoteza mpendwa wetu. Yesu alitembea katika lile "bonde la uvuli wa mauti;" anaujua usiku mnene tunaoupitia.

"Basi, kwa vile watoto hao, kama awaitavyo, ni watu wenye mwili na damu, Yesu mwenyewe akawa kama wao na kushiriki ubinadamu wao. Alifanya hivyo ili, kwa njia ya kifo chake, amwangamize Ibilisi ambaye ana mamlaka juu ya kifo, na hivyo awaokoe wale waliokuwa watumwa maisha yao yote kwa sababu ya hofu yao ya kifo" - (Waebrania 2:14,15).



Dk. James Simpson, tabibu mkuu aliyetengeneza ile dawa ya nusu kaputi [ya usingizi wakati wa upasuaji], alipatikana na hasara ya kutisha mtoto wake mkubwa kuliko wote alipokufa. Alihuzunika vibaya sana kama mzazi mwingine ye yote auezavyo kufanya. Lakini baadaye akaiona njia iliyomletea matumaini. Juu ya kaburi la mtoto wake yule mpendwa aliweka jiwe la kuonyesha alama na juu yake aliandika kwa kukata maneno haya ambayo Yesu alisema kuhusu ufufuo wake: "Na tazama, mimi ni hai."

Hayo ndiyo yote. Msiba wa mtu mmoja wakati mwingine unaweza kuonekana kana kwamba unaifutilia mbali ile mbingu; hata hivyo, Yesu yu hai! Miyo yetu huenda ikawa ina huzuni nytingi sana; hata hivyo, Yesu yu hai!

Ndani ya Kristo tunalo tumaini la kuishi baada ya kifo chetu. Yeye ndiye "huo ufufuo, na uzima" (Yohana 11:25), naye anatoa ahadi hii kwetu, "kwa kuwa mimi ni hai ninyi pia mtakuwa hai" (Yohana 14:19). Kristo ndiye tumaini letu la pekee la kuwa hai kwetu baada ya kifo chetu. Na Kristo atakapokuja tena atatupa sisi uzima wa milele. Kamwe hatutaishi tena chini ya uvuli wa mauti, maana tunao uzima wa milele. Je! wewe umeligundua tumaini hili kuu ambalo tunawenza kulihifadhi moyoni mwetu katika zile nyakati zetu za giza nene kabisa? Kama wewe hujapata kumpokea Yesu kama Bwana na Mwokozi wako, je! utafanya hivyo sasa?

JE! NAWEZA KULIPATA KANISA LA MUNGU LEO?

Mara kwa mara Mungu ametoa ujumbe wa pekee kukidhi mahitaji ya vizazi tofauti mbali mbali: ujumbe wa kumsaidia Adamu na Hawa baada ya dhambi kuiharibu dunia yao, ujumbe kwa ulimwengu uliokuwako kabla ya gharika ile kuu ya maji, ujumbe kwa Israeli wakati Ashuru au Babeli ilipowatishia. Yesu alikuja na ujumbe maalum kwa siku zetu. Sura ya 12 na 14 ya Ufunuo hutoa muhtasari wa ujumbe wa Mungu wa pekee kwa ajili yetu leo. Katika GUNDUA Mwongozo huu na mwongozo ule unaofuata, tutauangalia ujumbe huo.



1. Kanisa Lilianzishwa Na Yesu

Maisha na mafundisho ya Yesu yalianzisha umoja wa imani na ushirika wa karibu sana katika kanisa lile la mitume walilolianzisha. Mitume wale walikuwa na uhusiano wa karibu kabisa na Kristo yule aliyefufuka. Paulo alitoa picha ya kifungo hicho cha karibu sana na kukilinganisha na uhusiano wa ndoa:

"Naliwaposea Mume mmoja, yaani, Kristo, ili niwalete ninyi kwake mkiwa bikira safi." - 2 Wakorintho 11:2.

Kulingana na maneno ya Paulo, kanisa la Kikrsto ni mwanamke safi, ni bibi-arusi wa Kristo, ishara inayofaa kabisa kwa kanisa lake Kristo alipendalo. Katika Agano la Kale mithali iyo hiyo inatumika kuielezea Israeli, yaani, wateule wa Mungu. Mungu aliwaambia Israeli: "wewe kama bibi-arusi ulinipenda mimi" (Yeremia 2:2); "Mimi ni mume wenu" (Yeremia 3:14).

Kitabu cha Ufunuo pia kinazungumza juu ya kanisa kama mwanamke:

"Ishara kuu na ya ajabu ilionekana mbinguni: mwanamke aliyevikwa jua, na mwezi ulikuwa chini ya miguu yake, na taji ya nyota kumi na mbili juu ya kichwa chake" - (Ufunuo 12:1).



Mwanamke huyo ame "vikwa jua". Maneno hayo yanadokeza kanisa linalong'aa kama jua, kwa sababu ya kuvikwa utukufu wa kuwako kwake Kristo. Yesu, "Nuru ya Ulimwengu" (Yohana 8:12), anaangaza kupitia kwa washiriki wa kanisa lake, nao kwa upande wao wanapaswa kuwa "nuru ya ulimwengu" (Mathayo 5:14).

Mwanamke huyo ana "mwezi chini ya miguu yake." Mwezi huo unawakilisha nuru ya Injili iliyoakisiwa [iliyoangaza] katika dhabihu na taratibu za ibada ya watu wa Mungu katika Agano la Kale. Mwezi huo ukiwa "chini ya miguu yake" unadokeza kwamba nuru ya Injili iliyoakisiwa imepitwa na huduma anayofanya Kristo.

Mwanamke huyo anayo "taji ya nyota kumi na mbili juu ya kichwa chake." Nyota zinawakilisha vizuri sana mitume wale kumi na wawili, watu waadilifu ambao ushuhuda wao juu ya Yesu unang'aa sana mpaka siku hii ya leo.

Ni dhahiri, basi, kwamba maelezo yamhusuyo mwanamke huyo yanaonyesha kwamba Yohana katika mawazo yake analiona badiliko lililotokea kutoka kwa watu wa Mungu, Israeli, katika Agano la Kale kwenda kwenye kanisa lile la Kikrsto la Agano Jipy a lilolianzisha Yesu. Jua, mwezi, na nyota huitilia mkazo huduma ya kupeleka nuru inayofanywa na kanisa hilo la Kikrsto kwa kuzitangaza hizo Habari Njema.

2. Matukio Yanayofuatana Ya Kushindwa Kwa Shetani

GUNDUA

Kuingia kwa mwanamke huyo kunaweka jukwaa kwa matukio haya makuu yanayofuatana: "Alikuwa mja mzito, naye akapaaza sauti kwa maumivu na uchungu wa kujifungua mtoto. Kisha, ishara nyininge ikatokea mbinguni: joka mkubwa jekundu na lenye pembe kumi na vichwa saba; na kila kichwa kilikuwa na taji. Joka hilo liliburuta kwa mkia wake theluthi moja ya nyota za anga na kuzitupa duniani. Nalo liliSIMAMA mbele ya huyo mama aliyeKUWA karibu kujifungua mtoto, tayari kabisa kummeza mtoto, mara tu atakapoZALIWA. Kisha, mama huyo akajifungua mtoto wa kiume ambaye atayatawala mataifa yote kwa fimbo ya chuma. Lakini mtoto akanyakuliwa na kupelekwa kwa Mungu na kwenye kiti chake cha enzi" - Ufunuo 12:2-5.

Wakuu watatu wanashiriki katika mfululizo wa matukio haya:

Mwanamke, huyo tayari ametambulishwa kama kanisa lake Mungu.

Mtoto wa kiume aliyezaliwa na mwanamke huyo ana "nyakuliwa hata kwa Mungu na kwenye kiti chake cha enzi," na siku moja "atayatawala mataifa yote." Yesu ndiye mtoto peke yake aliyePATA kuzaliwa katika ulimwengu huu ambaye alinyakuliwa kwenda kwenye kiti cha enzi cha Mungu na ambaye siku moja atayatawala mataifa yote.

Joka anamwakilisha Ibilisi, au Shetani.

"Kisha kukazukaa vita mbinguni: Mikaeli na malaika wake walipigana na hilo joka, nalo likawashambulia pamoja na malaika wake. Lakini joka hilo na malaika wake walishindwa, na hatimaye hapakuwa tena na nafasi mbinguni kwa ajili yao. Basi, joka hilo kuu likatupwa nje. Joka hilo ndiye yule nyoka wa kale ambaye huudanganya ulimwengu wote. Naam, alitupwa duniani, na malaika wake wote pamoja naye." - Ufunuo 12:7-9.



Picha hiyo inakuwa dhahiri mara tu tunapoifahamu mifano hiyo.

Ibilisi na malaika zake "wa[li]po] poteza mahali pao mbinguni,"

wali "tupwa duniani." Yesu alipozaliwa katika dunia hii, Ibilisi

alijaribu kumwua Yesu, mwana yule wa kiume, mara tu alipokwisha kuzaliwa. Alishindwa, kisha Yesu "akanyakuliwa" kwenda kwenye kiti cha enzi cha Mungu.

Ndipo Shetani akaondoka kwenda kuliangamiza kabisa kanisa la Kristo alilolianzisha Kristo. Mtume Yohana, aliyeKIANDIKA kitabu cha Ufunuo, aliliona kidogo tu pambano hilo kuu kati ya Kristo na Shetani likipiganwa vikali sana juu ya dunia hii. Vita hiyo ilipofikia kilele chake wakati ule wa kusulibiwa kwake Kristo, Yohana alisikia sauti ikipiga kelele kutoka mbinguni, ikisema:

"Kisha nikasikia sauti kubwa kutoka mbinguni ikisema: Sasa umefikia mkombozi na nguvu na ufalme wa Mungu wetu, na mamlaka ya Kristo wake! Maana yule aliyweshtaki ndugu zetu mbele ya Mungu ametupwa chini. Naam, ametupwa chini huyo anayeweshtaki usiku na mchana" - Ufunuo 12:10. (Linganisha na Yohana 12:31 na Luka 10:18).

Yesu alipata ushindi dhidi ya Shetani pale msalabani. Wakati ule ndipo alipothibitisha uhakika wa mpango ule wa "wokovu" na kutoa "uwezo" wa kuzipinga hila za Shetani. "Ufalme wa Mungu" ukaimarishwa, na "mamlaka" ya Mwokozi ya kuwa Kuhani wetu Mkuu na Mfalme wetu ikawa imethibitishwa.



"Sasa umekuja wokovu" ni tangazo linaloonyesha kwamba tendo lile la kilele la historia limefika. Kuzaliwa kwake Kristo, Mwokozi wa ulimwengu, kumekwisha kutokea (fungu la 5). Licha ya majaribu makali ya Shetani, Yesu aliishi maisha yasiyo na dhambi, alikuwa na kufufuka akiwa mshindi dhidi ya dhambi na mauti (fungu la 10). Shetani ameshindwa milele (fungu la 7-9). Msalaba umetukuzwa katika uwezo wake wote.

Tangazo hili, "Sasa umekuja wokovu," halimpendezi Yohana tu, bali malimwengu yote:

GUNDUA

"Kwa hiyo shangilieni, enyi mbingu, na ninyi mkaao humo! Ole kwa nchi na bahari, kwa sababu Ibilisi ameshuka kuja kwenu! Amejaa ghadhabu nyngi, kwa sababu anajua kwamba ana wakati mchache tu." - (Ufunuo 12:12).

Mbingu yote ilisherehekea ushindi wa Kristo. Kristo aliyavunjilia mbali madai ya aina yo yote ile aliyokuwa nayo Shetani zamani kuhusu kuwa na mahali pake kule mbinguni, na yule Shetani aliyeshindwa akapoteza milele madai yake aliyosema dunia hii ni yake.

3. Kanisa La Kikristo Katika Mapambano Dhidi Ya Shetani

Kabla Yesu hajapaa kwenda mbinguni alilianzisha kanisa la Kikristo (ambalo linafananishwa na mwanimke). Kifo chake pale msalabani kililipa hilo kanisa la Kikristo uwezo wa kumshinda Shetani.

"Nao [Kanisa la Kikristo] wakamshinda [Shetani] kwa damu ya Mwana-Kondoo na kwa neno la ushuhuda wao; hawakuyapenda sana maisha yao kiasi cha kuogopa kufa." - (Ufunuo 12:11).

Kristo anaweza kulipa kanisa lake uwezo wake sasa, yaani, kulipa lile tunda la ushindi wake. Yesu alimshinda Shetani kabisa kwa njia ya kanisa lake. Sifa tatu zinalitambulisha kanisa hilo lenye kushinda katika karne zilizokwu zikiendelea kupita za kipindi hiki cha Kikristo: "Wakamshinda [Shetani] kwa damu ya Mwana-Kondoo." Yesu alinyakuliwa hadi kwenye kiti cha enzi cha Mungu ili apate kuifanya damu yake iwe na matokeo mema katika maisha ya wafuasi wake. Yeye anaweza kuiondoa kumbukumbu ya dhambi zetu, anaweza kutuoka kwa njia ya damu yake iliyomwagika (1Yohana 1:7), na kutupa uwezo wa kuishi maisha yenye afya ya Kikristo siku kwa siku. "Hawakuyapenda sana maisha yao kiasi cha kuogopa kufa." "Damu ya Mwana-Kondoo" iliwafanya wawe tayari kufa kwa ajili ya kazi yake Kristo; hawa "kuogopa kufa." Mungu alikuwa ameteseka sana, kwa hivyo Wakristo wale wafia dini walikuwa tayari kuteswa na kuuawa. Hata watoto wadogo walijitao mhanga hatimaye. Kisa kinasimuliwa cha mama mmoja Mkristo aliyetupwa kwa



Simba katika uwaniwa wa michezo wa Kiroma kwa kuwa alitoa utii wake kwa Kristo, wala si kwa serikali. Binti yake mdogo, badala ya kujikunyata kwa hofu kuu, alisikia ari ya kujitoa wakfu ikijaa ndani yake. Wale simba walipomshambulia mama yake, alisimama na kupiga kelele, "Mimi pia ni Mkristo." Maafisa wa Kiroma wakamkamata na kumtupa kwa nguvu kwa wanyama wale wenye njaa. "Wakamshinda [Shetani]... kwa neno la ushuhuda wao." Sio maneno, bali neno la ushuhuda wao yaani, ushuhuda wa maisha yao, ushuhuda wao hai kwa uweza wa Yesu na injili yake. Katika zile saa za giza nene kabisa la kipindi kile cha Kikristo, jeshi la Wakristo - kuanzia kwa mababa wale wa kwanza wa kanisa hadi kwa wanamatengenezo wa

kanisa la Kiprotestanti - waliyashinda mambo yote mabaya mno, ambayo Ibilisi aliweza kuwatupia kwa nguvu, kwa njia ya ushuhuda wao tu wenye nguvu wa maisha yao.

Ufunuo 12:11 huonyesha picha ya kanisa linaloshinda ambalo limejaa washindi: mitume, wafia dini, wanamatengenezo ya kanisa, na Wakristo wengineo waaminifu. Upole, uaminifu, ujasiri, na ushindi wao umenguruma kushuka katika karne nyngi na kuupindua ulimwengu.

Kwa kuwa Shetani alishindwa kumwangamiza Yesu alipoishi hapa duniani, sasa anajitahidi sana kumwangamiza Kristo anayeishi ndani ya kanisa lake.

"Joka lilipotambua kwamba limetupwa chini duniani, likaanza kumwinda yule mama aliyekuwa amejifungua mtoto wa kiume. Lakini mama huyo akapewa mabawa mawili ya tai apate kuruka mbali sana na hilo joka, mpaka mahali pake jangwani ambapo angehidhiwa salama kwa muda

GUNDUA

wa miaka mitatu na nusu. Basi, joka likatapika maji mengi kama mto, yakamfuata huyo mama nyuma ili yamchukue. Lakini nchi ikamsaidia huyo mama: ikajifunua kama mdomo na kuyamezaa maji hayo yaliyotoka kinywani mwa hilo joka - (Ufunuo 12:13-16).

Kama vile ilivyotabiriwa, katika zama zile za giza za kipindi kile cha Kikristo, Shetani alitoa "mtu" wa mateso ili kufanya kanisa li"chukuliwe na mkondo ule wa mto." Shetani anataka kuufutilia mbali mvuto wa Kristo kwa kulifutilia mbali kanisa lake, tena anatumia kila hila ambayo akili yake nyingi iliyojaa uovu inaweza kubuni. Kimsingi Joka anamwakilisha Shetani. Lakini kumbuka kwamba Shetani anazitumia taasisi za wanadamu katika utendaji wake kama joka ili kuwashambulia watu wa Mungu. Alimtumia mfalme wa Kiroma Herode katika jaribio lake la kumwua mtoto Kristo mara tu alipokwisha kuzaliwa. Alifanya kazi yake kupitia kwa viongozi wa dini wenye husuda na wenye kuwania madaraka waliomnyemelea na kumsumbuu Mwokozi, na hatimaye kumwua juu ya ule msalaba. Lakini ule ulionekana kama ni ushindi mkubwa usio na kifani wa Kristo.



Akiwa amekasirika vibaya sana dhidi ya kushindwa kwake pale msalabani, Shetani akaielekeza ghadhabu yake dhidi ya Kanisa lile alilolianzisha Yesu. Katika miongo [miaka kumi-kumi] iliyofuata baada ya kusulibowiwa kwake Kristo, maelfu waliuawa katika ule uwanja wa duara uliojengwa mijini Roma (Colosseum), maeneo tupu ya pembe mraba yaliyokuwa mijini, magereza yale ya chini ya ardhi, na katika maficho ya jangwani.

Mwanzoni wale wenye mamlaka [serikali] ya kidunia walianzisha hayo mateso. Lakini baada ya kufa wale mitume badiliko lilitokea taratibu ndani ya kanisa lile. Katika kipindi kile cha karne ya pili, ya tatu, na ya nne, wengi ndani ya kanisa lile walianza kuzibadili kidogo zile kweli zilizokuwa zimefundishwa na Kristo pamoja na mitume wake. Viongozi fulani, walioasi hata wakaanza kuwaresa Wakristo wale waliosisitiza kuwa na usafi wa itikadi [imani] za Agano Jipy.

Wataalam wa Biblia wanakadiria kwamba takriban milioni 50 ya wale waliokuwa waaminifu walieuawa. Katika jitihada yake ya kulizamisha na kuliangamiza kanisa, Ibilisi alitoa "mtu" wa mateso ili kulifanya "lichukuliwe [lile kanisa] na mkondo ule wa mto." "Lakini nchi ikamsaidia yule mwanamke kwa... kuumeza ule mto" wa mateso na mafundisho ya uongo.

Katika kipindi cha mateso ya Zama za Kati [1100-1500], kanisa la kweli lilijiondoa kutoka katika uongozi ule ulioasi na kujificha "Nyikani, mahali alipoandaliwa na Mungu, ili wamlishe muda wa siku 1,260" (fungu la 6). Utabiri huo ultimizwa katika kipindi cha miaka 1260 ya mateso kuanzia mwaka wa 538 hadi mwaka wa 1798 B.K. (siku moja mara nyingi husimama badala ya mwaka mmoja katika unabii wa mifano wa Biblia, angalia Ezekiel 4:6).

Katika kipindi cha karne za giza Wakristo waaminifu walioiamini Biblia walipata kimbilio lao po pote walipoweza kupapata kwa mfano, katika mabonde ya Wawaldensia wa Italia magharibi na Ufaransa mashariki, na katika kanisa la Kikeltiki [Waskoti Waairishi, Waweishi] la visiwa vyaya Uingereza.


4. Kanisa La Mungu Katika Siku Hizi Zetu

Jambo hilo linatufikisha katika siku hizi zetu - yaani, kwenye kanisa la kweli la Kristo tangu mwaka wa 1798. Kama ambavyo ingeweza kutarajiwa, yule joka bado amewakasirikia watu wa Mungu. Vita kuu isiyoonekana kwa macho inaendelea. Kwa kweli, Shetani anafanya shambulio lake kubwa kabisa dhidi ya kanisa hilo muda mfupi tu kabla ya kuja kwake Yesu.

GUNDUA

"Ndipo yule Joka [Ibilisi] akamkasirikia sana yule mwanamke [Kanisa la Mungu], akaenda zake afanye vita dhidi ya wazao wake waliosalia - wale wanaozitii amri za Mungu na kuwa na ushuhuda wa Yesu." - (Ufunuo 12:17).

Unabii huu unalenga katika siku zetu hizi. Shetani amekasirika sana; anafanya vita dhidi ya wazao wa mwanamke waliosalia" - yaani, dhidi ya watu wa Mungu wa siku hizi. Angalia alama zao zinazowatambulisha:



- (1) Waumini hao wa siku za mwisho wanao "ushuhuda wa Yesu." Kwa uaminifu wakiyang'ang'ania mafundisho safi ya Neno la Mungu, wanamshuhudia Yesu kwa njia ya maisha yao yenye nguvu nyingi ya Kikristo.
- (2) Wakristo hao wa siku za mwisho ni watu wa unabii. Kuupokea ule "ushuhuda wa Yesu Kristo" kulimwezesha Yohana kukiandika kitabu kile cha Ufunuo (Ufunuo 1:1-3). Kundi hilo la mwisho la waumini linapokea karama ile ile: yaani, ushuhuda wa moja kwa moja toka kwa Mungu kupitia kwa mjambe wa kibinadamu. Karama yao ya unabii inalenga juu ya ufunuo wa Mungu kuhusu utume wao na mwisho wao.
- (3) Wakristo hao wa siku hizi za mwisho wanatambulikana pia kama "wale wanaozitii Amri [kumi] za Mungu." Hawatetei tu ukamilifu wa hizo Amri Kumi, bali wanazitii pia. Upendo wa Mugu ulio miyoni mwao unawaletea utii unaotolewa kwa moyo wa furaha (Warumi 5:5; 13:8-10).

Wakristo hao wa siku hizi za mwisho wanakifuata kielelezo cha Kristo na cha kanisa lile la kwanza kwa kuzitii amri [kumi] za Mungu. Jambo hilo linamkasirisha vibaya sana yule Joka - yaani, yule Ibilisi. Naye anapigana vita dhidi ya "wazao" wa mwanamke "waliosalia" kwa sababu wanatoa ushuhuda kwamba upendo wao kwa Mungu unawafanya wafuasi wake hao kuwa watii. Kama vile Kristo alivyoagiza, aliposema:

"Mkinipenda, mtazishika amri zangu" - Yohana 14:15.

Maisha ya Wakristo hao wa siku hizi za mwisho yanaonyesha kwamba uwezekano upo wa kumpenda Mungu kwa miyo yetu yote na kuwapenda wenzetu kama sisi tunavyojipenda wenywewe. Kulingana na maneno ya Yesu, sifa hizo za tabia, yaani, upendo kwa Mungu na upendo kwa watu, hufanya muhtasari wa Amri kumi za Mungu (Mathayo 22:35-40).

Ya nne katika hizo amri inatutaka sisi kuitunza Jumamosi, siku ya saba ya juma, kama Sabato. Kwa kuwa upendo wao kwa Yesu umezitia ndani ya miyo yao amri zote kumi [Ebr. 8:10; Kut. 20:3-17; Yak. 2:10-12], basi, Wakristo hao wa siku hizi za mwisho ni Wasabato.


Sabato ndicho kiini cha ujumbe wa mwisho wa Mungu kwa watu wake katika kitabu cha Ufunuo, sura ya 12 na 14:6-15. Nguvu zote za mbinguni zinajipanga nyuma ya Wakristo hao wa siku hizi za mwisho walioelezwa katika sura hizo. Mwokozi wao aliye hai ndiye rafiki yao daima, na Roho Mtakatifu anafanya kazi yake "kuwafanya imara kwa nguvu katika utu wao wa ndani." Ahadi yake ni ya hakika. WATAmshinda Shetani "kwa damu ya Mwana-Kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao" (Ufunuo 12:11).

Je! unataka kuwa mmoja wa Wakristo hao wa siku hizi za mwisho ambao "wanazitii amri [kumi] za Mungu" tena wa "na ushuhuda wa Yesu"? Kwa nini usikate shauri sasa hivi?

JE! MUNGU ANAO UJUMBE WA PEKEE KWA AJILI YA SIKU ZETU?

Ramon Umashankar alizaliwa katika tabaka ya juu ya Kihindu (Brahmin). Wakubwa wake kwa umri walimfundisha akiwa na umri ndogo ya kwamba yeye alikuwa mungu, na ya kwamba ili kuufikia uungu wake ni lazima afanye mazoezi ya yoga na kutafakari. Yeye kama kijana mbichi [tineja], Ramon alianza kushangaa kama kweli angempata Mungu kuititia kwa sanamu zile mbali mbali zilizoabudiwa katika mahekalu ya Kihindu [Kibanian].

Ramon akaanza kuichunguza Biblia na madai ya Kristo. Yeye alikuwa amemheshimu Yesu siku zote kwa unyenyekevu wake aliokuwa nao, lakini sasa Ramon akasikia kwamba huyo Yesu alidai kwamba alikuwa ndiye Mwana pekee wa Mungu. Tena aligundua kwamba Wakristo wengi walionekana wanayo amani ambayo kutafakari kwa miaka mingi kulikuwa kumeshindwa kuifikia. Lakini, Ramon bado alikuwa amedhamiria kuipata kweli katika dini yake ya Kibanian.



Lakini baadaye alionna filamu iliyooynesha maisha yake Kristo. Kwa mara yake ya kwanza alitambua kwamba Yesu alikuwa amepatikana na mateso na hofu kama mwanadamu. Kabla ya hapo alikuwa amedhani kwamba Yesu kwa njia fulani alikuwa ametumia uweza wake wa Uungu kuyakwepa maumivu yale yaliyotokana na kusulubiwa kwake. Lakini sasa, alishindwa kueleza habari za msalaba ule. Alishangaaa na kujuliza-uliza: Hivi ilikuwa-kuwaje huyo Yesu aliweza kuyapitia mateso makubwa kama yale - kwa ajili ya wanadamu wenye dhambi?

Ramon alipoendelea kutafakari juu ya kifo cha Kristo, alizidiwa nguvu kwa kudhihrishwa kwa upendo kama ule. Aliamua kukitupilia mbali cheo chake kinachotamaniwa sana na watu wa Brahmini [tabaka la juu la Kibanian] na kutoa maisha yake kwa Yesu, Mwokozi wake. Alipoyalinganisha mambo yote na ule upendo wa kujitoa mhanga wa Kristo, Ramon alisema hivi, "Kila kitu cho chote kingine kikasambaratika."

Mbrahmini huyo kijana alikigundua kiini cha ile kweli ya Ukristo: yaani, Yesu Mwokozi wa ulimwengu.

1. Dini Ipi Inaokoa?

Yesu ndiye Njia - njia pekee - ya wokovu.

"Wokovu haupatikani katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo." - Matendo 4:12.

Biblia inafundisha wazi kwamba sisi tumepeotea katika dhambi, na hivyo tunakabiliwa na adhabu ya dhambi: yaani ile mauti (Warumi 6:23). Wote wametenda dhambi (Warumi 3:23), kwa hiyo wote wanakabiliwa na hiyo mauti. Na Yesu ndiye yule mmoja - mmoja pekee aezaye kutuokoa sisi kutoka katika laana ya dhambi.

"Kila mmoja amtazamaye Mwana na kumwamini yeye atapata uzima wa milele, nami nitamfufua siku ya mwisho" - (Yohana 6:40).

Kuna dini moja tu ya kweli:

"Bwana mmoja, IMANI MOJA, ubatizo mmoja" - (Waefeso 4:5).

2. Je! Mungu Anao Ujumbe Wa Pekee Kwa siku zetu?

GUNDUA

Ndiyo! Ujumbe huo wa aina tatu unaonekana katika Ufunuo 14:6-16. kutangazwa kwa ujumbe huo uliotolewa na malaika hao watatu kunafikia kilele chake wakati ule wa kuja mara ya pili kwa Kristo (fungu la 14-16).

Ujumbe wa Malaika wa Kwanza.

"Kisha nikamwona malaika mwengine, akiruka juu ya anga akiwa na Habari Njema ya milele ya Mungu, aitangaze kwa watu waishio duniani, kwa mataifa yote, makabila yote na watu wa lugha zote na rangi zote. Naye akasema kwa sauti kubwa, "Mcheni Mungu na kumtukuza! Maana saa imefika ya kutoa hukumu yake. Mwabuduni yeye aliyeumba mbingu na nchi, bahari na chemchemi za maji" - (Ufunuo 14:6,7).



Ingawa Maandiko yanaonyesha picha ya kuvutia ya ujumbe huo wa aina tatu kwa njia ya mfano wa hao malaika watatu, watu wa Mungu ndio wajumbe hasa wautangazao kwa ulimwengu mzima. Hawahubiri injili mpya, bali "injili ya milele" kwa ulimwengu mzima- yaani, kwa kila taifa na kabilia na lugha na jamaa. "Injili ya milele" ya Kristo ni ujumbe ule ule wa wokovu ambaa watu katika kipindi kile cha Agano la kale waliupokea " kwa imani" (Waebrania 3:16-19; 4:2; 11:1-40); ni mafundisho yale yale aliyoyatangaza Yesu mwenyewe; ni injili ile ile iliyounguruma katika karne zile zote za kipindi cha Kikristo.

Injili hiyo rahisi, iokoayo, ya Yesu Kristo ilikuwa karibu imetoweka kabisa katika Kanisa kwa zaidi ya miaka elfu moja katika kipindi cha zama za giza (Dark Ages), lakini matengenezo ya Kanisa (Reformation) yaliifufua, na watu wa Mungu wanaihubiri ulimwenguni kote leo. Malaika wa kwanza anatangaza ujumbe wa injili iyo hiyo, lakini inahubiri katika mwelekeo mpya - yaani, wa ulimwengu mzima - kwa ajili ya watu wanaoishi kabla tu ya kuja Yesu mara ya pili.

Wale wanaoupokea ujumbe huu wanajikuta wanaitwa ku "mch[a] Mungu na kumtukuza [kuakisi tabia yake]." Wanaonyesha ulimwengu tabia ya Mungu ya upendo, sio tu kwa maneno yao, bali pia kwa maisha yao yenye ushuhuda wenye nguvu. Wanatoa ufunuo wa kusimua wa kile Mungu awezacho kufanya kuititia kwa watu waliojazwa na Roho wa Kristo.



Hivi ni lini utakapotangazwa huo ujumbe wa malaika hao watatu katika ulimwengu mzima? Wakati saa ya "hukumu yake [Mungu] imekuja." Mwongozo 13 unaeleza kwamba Yesu alianza kazi ya hukumu inayotangulia kabla ya kuja kwake katika mwaka ule ule, yaani, 1844, Yesu aliwavutia watu ulimwenguni kote kuanza kuhubiri ujumbe huo wa Ufunuo 14.

Ujumbe huo unatuagiza sisi ku "msujudi[a] yeye aliyezfanya mbingu, [na] nchi" [Ufunuo 14:7]. Mungu anatutaka sisi ku "ikumbuk[a] siku ya Sabato [t]uitakase" kwa sababu "kwa siku sita Bwana alifanya mbingu na nchi" (Kutoka 20:8-11). Katika mwaka ule wa 1844 Darwin alipokuwa anaitoa nadharia yake ya evalusheni [kutokea vyenyewe tu vitu vyote], Mungu alikuwa anawaita watu wake kurudi na kumsujidia yeye kama Muumbaji wao. Wakati ule ule hasa, wale waliokuwa wakiuhubiri ujumbe huo wa malaika watatu waliigundua Sabato ya siku ya saba ya neno la Mungu, nao wakaanza kuitunza kwa kumheshimnu Muumba wa Mbingu na Nchi.

(2) Ujumbe wa malaika wa pili.

"Malaika wa pili akafuata, akasema, 'Umeanguka! Umeanguka Babeli Mkuu, uliowafanya mataifa yote kunywa mvinyo wa usherati wake unaowafanya kuwa vichaa.!! - ufunuo 14:8.

GUNDUA

Malaika wa pili anaonya anasema, "Umeanguka Babeli Mkuu." Ufunuo 17 unaonyesha picha ya "Babeli" ya kiroho - yaani, Ukristo ulioasi - kama mwanamke kahaba (fungu la 5). Anasema akiwa tofauti na mwanamke safi wa Ufunuo 12 anayeliwakilisha kanisa la kweli la Kikristo. Mwanamke anayewakilisha Babeli ni mwanamke aliyeanguka [aliyeasi] ambaye aliwafanya "mataifa yote kunywa mvinyo wa uasherati wake unaowafanya kuwa vichaa." Mvinyo wa mafundisho ya uongo umeenea kote katika mfumo potofu wa Ukristo. Ujumbe huo wa malaika wa pili unawaita watu wa Mungu kuyapinga mafundisho hayo ya uongo ya Ukristo huo ulioasi.



Babeli unawakilisha mseto wa mifumo mingi ya Ukristo ulioasi. Ni wa hatari mno kwa sababu unaipotosha picha ya Mungu na kuifanya kama vikaragosi [sanamu za kuchekesha]: yaani, unamfanya Mungu kuwa ni mlipiza kisasi na mwenye madai mengi, unamfanya Mungu kama babu yetu mwenye upendo ambaye ni mwema mno kuweza kumsumbuu mtu awaye yote juu ya dhambi zake. Kanisa lenye afya litatoa picha yenye uwiano mzuri wa sifa zote za Mungu, kisha litaonyesha jinsi haki na rehema yake inavyofungamana na kweli isemayo kwamba Mungu ni upendo.

Mungu anawaita watu wake anasema "tokeni" Babeli (Ufunuo 18:4), anataka wayakatae mafundisho yale yasiyotoka katika Biblia, kisha wayafuate mafundisho ya Kristo.

(3) Ujumbe wa malaika wa tatu

"Na malaika wa tatu aliwafuata hao wawili akisema kwa sauti kubwa, Yeyote anayemwabudu yule mnyama na sanamu yake na kukubali kutiwa alama yake juu ya paji la uso wake au juu ya mkono wake, yeye mwenyewe atakunywa divai ya ghadhabu ya Mungu ambayo imemininwa katika kikombe cha ghadhabu yake bila kuchanganywa na maji. Mtu huyo atateseka ndani ya moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu na mbele ya Mwanakondoo. Moshi wa moto unaowatesa hupanda juu milele na milele. Watu hao waliomwabudu huyo mnyama na sanamu yake na kutiwa alama ya jina lake, hawatakuwa na nafuu yoyote usiku na mchana. Hivyo lazima watakatifu, yaani watu wanaotii amri ya Mungu na kumwamini Yesu, wawe na uvumilivu" - (Ufunuo 14:9-12).

Ujumbe wa malaika wa tatu unaugawa ulimwengu wote katika makundi mawili. Upande mmoja wanasmama Wakristo waasi [yaani, wasiofuata mafundisho ya Biblia] amba hu "msujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea alama yake katika kipaji cha uso wake au katika mkono wake." Upande ule mwingine wanasmama wale wanaoikataa mamlaka ya mnyama, yaani. Wale "watakatifu wanaozitii amri [kumi] za Mungu na kuendelea kuwa waaminifu kwa Yesu."

Zingatia tofauti iliyopo kati ya makundi hayo mawili yanayopingana. Wale wanaoipokea alama ya mnyama ni waabudu wanaoyalegeza masharti ya imani amba wanafuata mawazo yaliyotungwa na wanadamu yaonekanayo kama yanafaa pamoja na kuzifuata desturi zao. "Watakatifu wanatabia hizi zinazowatambulisha: "uvumilivu" utii kwa "Amri za Mungu" kisha "wanaendelea kuwa waaminifu kwa Yesu."

Baada ya ujumbe huo wa aina tatu kutangazwa ulimwenguni kote, Yesu atakuja ku "vun[a] wale walookolewa:

"Kisha, nikatazama, na kumbe palikuwapo wingu jeupe hapo. Na juu ya wingu hilo aliquwako aliye kama Mwana wa Mtu. Alikuwa amevaa taji ya dhahabu kichwani, na kushika mundu mkononi mwake. Kisha malaika mwingine akatoka hekaluni, na kwa sauti kubwa akamwambia yule aliyekuwa amekaa juu ya wingu, "Tafadhali, tumia mundu wako ukavune mavuno, maana wakati wa mavuno umefika; mavuno ya dunia yameivaa". Basi, yule aliyekuwa amekaa juu ya wingu akautupa mundu wake duniani, na mavuno ya dunia



yakavunwa" - (Ufunuo 14:14-16).

3. Kanisa La Kristo La Siku Za Mwisho

Je! umevutiva sana na Mkristo mwenye nguvu, aliye imara, na kushangaa kuiona bidii aliyo nayo katika kumwabudu Mungu, uvumilivu wake, na imani yake, na kutamani sana kuwa na uzoefu wa kiroho unaofanana na huo? Mungu alitoa ujumbe wake wa pekee kwa ajili ya siku zetu katika Ufunuo 14 kwa sababu unaweza kuleta uzoefu wa maisha kama huo.

Kama tulivyojadili katika Mwongozo 25, Ufunuo 14:17 unawatambulisha Wakristo wa siku hizi za mwisho kuwa ni "wanaozitii amri [kumi] za Mungu na kuwa na ushuhuda wa Yesu." Ufunuo 14:12 unaeleza habari za kundi hilo kuwa ni la "watakatifu kwa Yesu."

Hebu na tufanye muhtasari wa sifa za tabia ya Wakristo wa siku za mwisho.

1. Wana"kuwa na ushuhuda wa Yesu." Hata Shetani anapoionyesha hasira yake dhidi yao, wao "wanaendelea kuwa waaminifu kwa Yesu." Imani yao haitokani na nafsi yao wenyewe ni kipawa toka kwa Mungu (Waefeso 2:8). Kanisa la Mungu la siku hizi za mwisho linamwona Kristo katika tabia yake halisi na kwa neema kwa njia ya imani wanakuwa minara hai ya ukumbusho inayoshuhudia uweza wa Kristo anayekaa ndani yao.

2. Wanayo "imani.... Ya Yesu" (Ufunuo 14:12, KJV). Imani aliyokuwa nayo Yesu, yaani, imani aliyoifundisha, imani aliyoiweka katika maisha yake, sasa inaijaza miyo yao. Hawanayo tu kweli, wanai"tunza" kweli - yaani, wanaifuata. Kwao dini ni maisha, imani yao inafungamana na matendo yao, tena imani hiyo inafungamana na utii wao. Katika maisha yao ya nje wanaionyesha "imani ya Yesu." Wamekwisha kugundua ya kwamba mafundisho makuu ya Biblia, yakitumiwa katika maisha yao ya kila siku, yanawapa maisha ya Kikristo yenye nguvu. Wamegundua kwamba kweli hizo kuu za Biblia zinaamsha upendo na kicho chao kwa Kristo, mambo ambayo hukidhi haja na shauku zote za moyo wa kibinadamu.

3. "Wanazitii amri [kumi] za Mungu" - Amri zile Kumi, yaani, sheria ya maadili ya Mungu. Juu ya mambo hayo yote mengine wanataka kutii kila alipendalo Mungu, kutii kila amri yake. Wanauionyesha upendo wao kwa Mungu na upendo wao kwa watu wengine kwa kuzifuata amri zote [kumi] za Mungu, pamoja na ile ya nne inayotuamuru kumwabudu Muumbaji wetu kwa kuiheshimu Jumamosi, yaani, Sabato ya siku ya saba.

4. Wanautangaza ujumbe wa "injili ya milele" ulimwenguni kote (Ufunuo 14:6). Injili hutangaza kwamba Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, halafu alifufuka kutoka kaburini ili sisi tupate kuwa na kanisa la Kristo la siku hizi za mwisho limekuwa likiwaita watu kila mahali kutoka katika machafuko ya kidini na kujenga uhusiano pamoja wa ile kweli ya Biblia peke yake.

5. Wanasukumwa na hisia ya kuharakisha mambo kwa sababu "saa ya mavuno imekuja, kwa kuwa mavuno ya nchi yamekomaa" (Ufunuo 14:15), na mamilioni bado hawajamwona Kristo.

6. Wanajitoa kabisa kutekeleza utume waliopewa na Mungu. Kwa sababu "Babeli Mkuu" umeanguka, wao wanaendelea kuwasih wale wanaoishi katika machafuko hayo ya kidini, wakiwaambia "Tokeni kwake, enyi watu wangu" (Ufunuo 18:4). Wanatamani kuwaeleza wengine juu ya uhusiano wa ajabu walio nao pamoja na Kristo, na furaha waliyo nayo wao kwa wao.



GUNDUA

Yote hayo na zaidi yanaiunganisha mioyo ya mamilioni ya Wakristo wa siku hizi za mwisho walioitwa na ujumbe huo wa malaika hao watatu ili watoke. Maisha yao yenye furaha yanawafanya kijiunga na mtume Yohana kutangaza kote mwaliko huu:

"Tulichokiona na kukisikia ndicho tunachowatangazieni nyinyi pia, ili nanyi mpate kijiunga nasi katika umoja tulio nao na Baba na Mwanae Yesu Kristo. Tunawaandikia nyinyi mambo haya kusudi furaha yetu ikamilike" - (1 Yohana 1:3,4).

Kwa njia ya Roho wake na kwa njia ya kanisa lake, Yesu anakualika wewe pia ili uje kwake na kusalimisha kila kitu kwake yeye:

"Roho na bibi-arusi [kanisa] wasema, Njoo! Naye asikiaye na aseme, 'Njoo!' ye yote mwenye kiu na aje; na ye yote atakaye, na atwae zawadi hii inayotolewa bure ya maji ya uzima." . - Ufunuo 22:17.

4. Mavuno Ya Aina Mbili

Ujumbe wa malaika hao watatu unafikia mwisho wake Yesu anaporudi duniani kuwavuna waliookolewa wa vizazi vyote (Ufunuo 14:14-16). Yesu

anawakusanya wote waliookolewa na kuwachukua kwenda nao kule kwenye "makao mengi" mbinguni (Yohana 14:1-3, KJV). Anafutilia mbali dhambi, magonjwa, huzuni na mauti. Watakatifu wanaanza kuishi maisha mapya mazuri sana pamoja naye milele hata milele (Ufunuo 21:1-4).



Yesu atawa "vuna pia waovu wakati wa kuja kwake".

"Kisha, malaika mwingine akatoka katika hekalu mbinguni akiwa na mundu wenye makali. Kisha malaika mwingine msimamizi wa moto, akatoka madhabahuni, akamwambia kwa sauti kubwa yule malaika mwenye mundu wenye makali, "Nawe tia huo mundu wako mkali ukakate vichala nya mizabibu ya dunia, maana zabibu zake zimeiva!" Basi, malaika huyo akautupa mundu wake duniani, akakata zabibu za dunia, akazitia ndani ya chombo kikubwa cha kukamulia zabibu chombo cha ghadhabu ya Mungu. Zabibu zikakamuliwa ndani ya hilo shinikizo lililoko

nje ya maji, na damu ikatoka katika shinikizo hilo mtiririko wenye kina kufikia hatamu za farasi na urefu upatao kilometra mia tatu" -(Ufunuo 14:17-20).

Huo utakuwa ni wakati wa kuhuzunisha sana wa maangamizi ya milele tukio la kuhuzunisha mno kwake Kristo, kwa sababu atalazimika kuwaangamiza wale wanaokataa kuokolewa. Yesu "huvumilia kwa ajili yenu, hapendi mtu ye yote aangamie, bali kila mmoja aifikilie toba" (2 Petro 3:9).

Yesu anapokuja kuvuna mavuno ya nchi, je! wewe utakuwa katika mavuno yapi? Je! utasimama mionganini mwa nafaka iliyokomaa pamoja na waliokombolewa wa vizazi vyote (Ufunuo 14:13-16)? Au utakuwa mionganini mwa zile zabibu zilizoiva sana za ghadhabu pamoja na wale waliopotea? (mafunku 17-20).



Jambo hilo limewekwa wazi. Upande mmoja, Yesu anasimama mikono yake iliyotobolewa kwa misumari ikiwa imenyoshwa kwako, akikusihii wewe ili upate kusimama pamoja na "watakatifu wanaozitii amri [kumi] za Mungu na kuwa na imani ya Yesu" (fungu la 12). Upande ule mwingine ni sauti za wanadamu tu, zinazokusihii sana zikikuambia kwamba utii wako kwa mafundisho yote ya Biblia na kwa zile amri zote [kumi] za Mungu hauna maana.

GUNDUA

Siku moja kundi lililokuwa katika ukumbi wa hukumu wa Pilato lilikabiliwa na jambo ambalo linafanana ajabu na hilo. Upande mmoja alikuwako Yesu, mwenye hali ya uungu-ubinadamu, yaani, Mungu-mwanadamu. Upande ule mwingine alikuwako Baraba, mtu asiye na uwezo wo wote, yaani, asiyeweza kujisaidia mwenyewe, wala waliokuwa katika kundi lile ambao walishuhudia tukio la kuhuzunisha sana. Lakini, basi, yale maneno ya Pilato yenye amri yalipovuma katika kundi la watu wenye tabia mbalimbali, yakisema, "Ni yupi kati ya hawa wawili mnayetaka niwafungulie?" sauti nyingi za watu wale zikaunguruma kwa hasira, "Baraba!"

"Basi," akauliza Pilato nimtendeje Yesu aitwaye Kristo?"

Kwa sauti moja lile kundi likapiga makelele, "Na asulubiwe!"

Na hivyo ndivyo Yesu, asiye na hatia yo yote, alivyosulibiwa; na Baraba, mwenye hatia, akaenda zake akiwa huru. (Angalia Mathayo 27:20-26).

Je! wewe unamchagua nani leo hii, Baraba au Yesu? Je, unachagua kufuata mawazo na mafundisho yaliyotungwa na wanadamu ambayo yanagongana na amri [kumi] za Mungu, tena yanagongana na injili ya milele ya Yesu? Au wewe unataka ku"zitii amri [kumi] za Mungu na kuendelea kuwa [m]waminifu kwa Yesu?" kumbuka, Yesu ndiye anayeahidi kumtuma Roho wake Mtakatifu kutatua matatizo yako yote, kuiponya kila huzuni kubwa uliyo nayo moyoni mwako, na kuitosheleza kila shauku uliyo nayo.